

6 MEI, 2013

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Kumi na Tisa – Tarehe 6 Mei, 2013

(Mkutano Ullanza Saa 3.00 Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tukae.

Waheshimiwa, mtakuwa mmepeata *Supplementary Order Paper*, halafu na ile *paper* ya kwanza *Supplementary* hiki ni Kikao cha 19, wameandika 18 ni Kikao cha 19. Kwa hiyo, mtakuwa na *Supplementary Order Paper*. Katibu tuendeleee?

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatayo Ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

6 MEI, 2013

MHE. AUGUSTINO M. MASELE (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA ULINZI NA USALAMA):

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

MHE. GRACE S. KIWELU (K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI):

Taarifa ya Msemadi Mkuu wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 145

Wajibu wa Wenyeviti wa Mitaa na Vijiji

MHE. MARIAM R. KASEMBE (K.n.y. MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA) aliuliza:-

Msingi mkubwa wa Maendeleo ya Jamii huanzia kwenye ngazi ya Mitaa na Vijiji ambapo hutegemea ubunifu na utendaji wa Viongozi wa ngazi husika.

Je, Serikali, inawezaje kuwashakikishia wananchi kwamba, Wenyeviti wa Mitaa na Vijiji wanajua wajibu wao?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (*TAMISEMI*) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anastazia James Wambura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana kwamba, msingi wa maendeleo ya jamii unaanza katika ngazi za chini za Serikali za Mitaa. Wasimamizi wa maendeleo katika ngazi hiyo ni Wenyeviti wa Vitongoji, Vijiji na Mitaa. Aidha ni kweli, kwamba, ili Viongozi hawa waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi ni lazima wapatiwe mafunzo ya kuwajengea uwezo.

Mheshimiwa Spika, Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa wana wajibu wa kusimamia Ulinzi na Usalama katika maeneo yao, kuwakilisha wananchi wao katika Vikao vya Kamati za Maendeleo za Kata na ya Wilaya na kuitisha na kuongoza Mikutano ya Vijiji na Mitaa, kushirikiana na Maafisa Watendaji katika kuhakikisha mapato yanakusanywa na kudhibitiwa. (*Makofii*)

Aidha kuwahamasisha wananchi kushiriki katika shughuli za kijamii na maendeleo, kutunza *registrya* wakazi wote wa Vijiji na takwimu nyingine za maendeleo ya Vijiji, ikiwa ni pamoja na kumbukumbu za vizazi na vifo. Kusimamia masuala ya kislasa katika maeneo yao na kutekeleza kazi nyingine watakazopangiwa na Halmashauri za Wilaya.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa zinazoikabili Serikali, hasa katika kutekeleza Sera ya Ugatuaji wa Madaraka kwa wananchi ni ushiriki mdogo wa jamii katika shughuli za kijamii na maendeleo. Mahudhurio hafifu ya wananchi katika vikao vya maamuzi na ukusanyaji na usimamizi dhaifu wa mapato.

Aidha, katika ngazi ya Vijiji na Mitaa kumekuwa na tatizo la utunzaji wa vitabu vya mahesabu, uandaaji wa Taarifa za Mapato na Matumizi na Taarifa ya Utekelezaji wa majukumu ya Kijiji na Mtaa.

Pia masuala ya utawala bora, hasa uwazi na uwajibikaji, uadilifu ni miongoni mwa maeneo yanayolalamikiwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto hizi ni wazi kwamba, upo umuhimu mkubwa wa kuendelea kuwajengea uwezo Wenyeviti na Watendaji wengine wa Vijiji na Mitaa. Serikali, imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali kuhakikisha kuwa Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa wanajengewa uwezo, ili kujuu majukumu yao. Mara baada ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2009, kila Halmashauri ilioa mafunzo kwa Viongozi hao kuhusu majukumu yao.

Aidha, Serikali, imekuwa ikipeleka 40% ya fedha za kujenga uwezo katika Vijiji na Mitaa, ambapo 50% ya fedha hizo hutumika kwa ajili ya kujenga uwezo wa Wenyeviti na Watendaji wa Vijiji na Mitaa. Pamoja na jitihada hizi za Serikali, baadhi ya Halmashauri kuitia mapato ya ndani, zimekuwa zikitenga fedha kwa ajili, ya kuwajengea uwezo Wenyeviti wa Vijiji na wale wa Mitaa.

Mheshimiwa Spika, Serikali, itaendelea kuwajengea uwezo Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa, kadiri hali ya kifedha itakavyokuwa inaruhusu. (*Makofii*)

MHE. MARIAM R. KASEMBE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Kwa kuwa, katika majibu ya msingi Mheshimiwa Waziri, amesema kwamba, imekuwa ikipeleka 40% katika Halmashauri zetu kwa ajili, ya mafunzo ya Viongozi wetu wa Vijiji.

Je, Wizara imekuwa ikifuatiliaje kuhakikisha kwamba, 40% hii inayokwenda ni kweli, Wenyeviti wa Vijiji pamoja na Wenyeviti wa Vitongoji wamekuwa wakipatiwa mafunzo hayo? Kwa sababu, nina uhakika katika Halmashauri nyingine, mafunzo haya Wenyeviti huwa hawapewi.

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa nini, sasa, kwa kuwa, suala hili la kupewa mafunzo hawa Wenyeviti wa Vijiji ni la msingi sana.

Kwa nini sasa Serikali, isiziruhusu Halmashauri kutenga fedha kwenye Bajeti yetu kutokana na makusanyo tunayokusanya, ili mafunzo haya ya Watendaji wa Vijiji, Vitongoji, waweze kuyapata kwa uhakika, kulikoni hali ilivyo hivi sasa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kasembe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu ambao tumeweka katika Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, na kwa sasa tunapozungumza hapa, na nimshukuru sana dada yangu Kasembe, kwa hili analozungumza. Tumeimarisha Sekretarieti zetu. Tunachofanya sisi ni kwamba, tunaye hapa mtu anayesimamia masuala ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika Sekretarieti.

Pale kwa Mkuu wa Wilaya, Katibu Tawala na yeye anahusika katika jambo hili, lakini sisi kama *centre*, kwa maana ya Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, mmetuona tunakwenda mpaka kule chini Kijijini.

Mheshimiwa Spika, na kuitia katika Taarifa za CAG, ambaye huwa anaangalia kama zimetengwa hizi hela zinazozungumza hapa 40%, ambayo Mheshimiwa Kasembe anazungumzia, tunakwenda mpaka kule na tumefika mahali tunaanza hata kuchukua hatua kwa wale ambao wameacha kupeleka hii 40% inayozungumzwa hapa. Na 40% inayozungumzwa hapa ni ile ya kujenga uwezo ndio inazungumza hapa.

Mimi nataka nikuthibitishie, mimi mwenyewe hapa, Mheshimiwa Waziri wa Nchi pamoja na Waziri Mkuu na mwenzangu, tumekuwa tunakwenda katika Halmashauri kufuatilia, kuhakikisha kwamba, zinakwenda hizi hela.

Sasa nataka nikubaliane na Mheshimiwa kwamba, inawezekana kabisa kwamba, kuna maeneo mengine haziendi. Waheshimiwa Wabunge, tunaomba mtupatие orodha ya Halmashauri ambazo hazipeleki hizi hela kule, halafu sisi tutachukua hatua; hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili. Hili la kupewa mafunzo; jana tulikuwa na Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na wako hapa wanajua, tumetoka Hombolo, tumetoka kwenda kuzungumzia jambo hili. Halmashauri zinatakiwa zitenge hela, zichukue hawa watendaji wetu wa Vijiji na Wenyeviti wa Vijiji, wawapeleke mpaka Hombolo kule, waende wakasome.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu, ya hali hii inayosemwa, tunachokifanya, tumefanya semina. Baada ya kumaliza Uchaguzi Mkuu, tulijua kwamba, walio wengi pale uwezo wao ni mdogo kwa hiyo, tukapanga semina. Nawaomba Wabunge, kama mnafahamu kwamba, kuna semina ambayo haikufanyika katika ngazi hiyo tunayozungumza hapo, mtusaidie.

Mheshimiwa Spika, jana tumetoa maelekezo, tumesema Halmashauri zote ambazo hazijalipia kule Hombolo, tumeomba tupewe orodha yao. Na leo nimeomba saa 7.00 iwe pale Ofisini, ili tushuke na hawa ambao hawapeleki hizo hela kule Hombolo. (*Makofii*)

MHE. JEROME D. BWANAUSI: Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa kunipa nafasi. Nianze ku-*declare interest* kwamba, mimi nimeshawahi kuwa Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri, amejaribu kueleza kwa undani na kwa kirefu juu ya hatua za Serikali. Lakini nataka nimwulize Mheshimiwa Waziri kwamba, ni lini kweli kabisa, Serikali, itaamua kwa dhati kabisa kutekeleza majukumu ya kuwawezesha Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa na Vitongoji kwa kuwapa vitendea kazi, posho pamoja na kuhakikisha kuwa, mafunzo haya yanafanyika?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Bwanausi. Sio tu kwamba, amekuwa Mwenyekiti wa Mtaa, amekuwa Mstahiki Meya wa Temeke kule kwa hiyo, anajua. Huyu anayezungumza hapa anajua sana haya mambo yanayozungumzwa hapa.

Mheshimiwa Spika, mimi nitoe picha kidogo hapa na wala hapa sitaki ku-*dismiss* kwamba, Wenyeviti wa Vitongoji na Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa, wamefanya kazi kubwa sana katika nchi yetu. Hizi shule tunazozungumza hapa zilizojengwa wao ndio wamejenga, hizi barabara tunazozungumza hapa ndio wanaosimamia; Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, inatambua juhudii zinazofanywa na Wenyeviti wetu wa Vijiji na Vitongoji na tunawapongeza kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Spika, sasa tunaulizwa habari ya posho hapa; ni kweli tumezungumza na juzi tulijibu hapa. Nataka nitoe picha, Vitongoji tulivyonavyo katika Tanzania hapa, tunavyo Vitongoji 60,000 Vijiji tunavyozungumza hapa 12,500 Mitaa tunayozungumza hapa tunazungumza habari ya Mitaa 2,500 *on average* na mingine imekuwa ina-*develop*.

Hii yote tulipopiga hesabu tukakuta kwamba, ili uweze kupeleka ni bilioni 21 unahitaji *with assumption* kwamba, imelipa kati ya 10,000/= na 20,000/= au kwenye manufaa 30 kwenda 50. Katika *General Purpose Grant* ambayo tulipitisha hapa, zimepitishwa bilioni 63, ndizo zimepitishwa hapa. (*Makofii*)

6 MEI, 2013

Haujazungumza mambo ya maendeleo, haujazungumza vitu vingine vinavyofanyika kule na kila kitu.

Mheshimiwa Spika, nataka nikwambie, tumetoa maelekezo hapa tunapeleka 20% inayorudishwa kutokana na *nuisance taxes*, tumeamua kwamba, ziende kule Kijiji na juzi tulijibu hapa. Hizi ni hela zile ambazo zilikuwa zinatolewa kwa ajili ya vitumbua, walikuwa wanatoza kwa ajili ya maandazi, kwa ajili ya samaki wa kukaanga, na kadhalika. Hizi zote tukasema warudishieni kule, wamepelekewa 20%. Katika 20% Utawala 3% tu, 17% yote itumike kwa ajili ya kulipia posho na tukasema watumie pia na mapato ya ndani.

Mheshimiwa Spika, sisi rai hii, sauti hii unihurumie mama yangu, mimi ni msisitizo tu nafanya hapa, wala sio kwamba, nataka kuwagombeza Wabunge. Mimi ninachosema ni kwamba, mpango upo na tumesema kwamba, mapato ya ndani pamoja na hizo nilizozieleza zote zitumike, zielekezwe kwa Wenyeviti wa Vijiji kwa ajili ya kulipa posho zao na Wenyeviti wa Vitongoji; Watendaji, wanalipwa mshahara. (*Makofii*)

SPIKA: Nashukuru. Tatizo langu sio sauti, ila muda wangu; umechukua dakika 15, swali moja.

Tunaendelea na Mheshimiwa Moza Abeid Saidy. Swali lingine?

Na. 146

Kupandiasha Hadhi Mji wa Kondoa

MHE. MOZA A. SAIDY aliuliza:-

"Hakuna sababu za msingi zinazosababisha mji wa Kondoa usipandishwe hadhi ukilinganisha na miji mingine iliyokishapandishwa hadhi kwa kujifunza kutoka mji wa Kondoa."

Je, Serikali, haioni inachelewesha maendeleo ya mji huo kwa kukosesa ruzuku ya maendeleo ambayo ingesaidia kuharakisha maendeleo ya mji huo wa Wilaya ya Kondoa?"

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (*TAMISEMI*) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Moza Abeid Saidy, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mji Mdogo wa Kondoa, ilianzishwa mwaka 1990 pamoja na Mamlaka nyiningine za Tangazo la Serikali (*Government Notice No. 137 of 8/6/1990*) na kwa mujibu wa Sheria za Serikali za Mitaa (*The Local Government (District Authorities) Act 1982, No. 7 of 1982*). Tarehe 1/5/2000 Mamlaka ya Mji Mdogo wa Kondoa, ilipata cheti cha kuanzishwa rasmi (*Certificate of Establishment of Kondoa Township Authority*). Aidha, mchakato wa kupandishwa hadhi Mamlaka ya Mji Mdogo wa Kondoa kuwa Halmashauri ya Mji wa Kondoa, uko katika hatua nzuri.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu – *TAMISEMI*, kwa kuititia barua yenye *Kumb Na. HA. 118/395/01/29* ya tarehe 28 Julai, 2011, ilitoa maelekezo kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Kondoa kuhusu hatua na vigezo vyta kuzingatia katika mchakato wa kupandisha hadhi Mamlaka hiyo, kuwa Halmashauri ya Mji. Vikao vyta Kisheria ambavyo ni Baraza la Madiwani, Kamati ya Ushauri ya Wilaya na Kamati ya Ushauri ya Mkoa, vilikaa na kuitisha pendekezo hilo.

Mheshimiwa Spika, tarehe 11/5/2013, Kikao cha *RCC* (*Regional Consultative Committee*) Mkoa wa Dodoma, kitathibitisha Muhtasari wa Kikao cha tarehe 5/6/2012 na ombi hilo kuwasilishwa rasmi Ofisi ya Waziri Mkuu – *TAMISEMI*, kwa ajili ya kulifanyia kazi zaidi. Aidha, Ofisi ya Waziri Mkuu – *TAMISEMI*, baada ya kupokea maombi hayo itatuma Wataalamu kwa ajili, ya uhakiki wa vigezo vinavyozingatiwa katika uanzishwaji wa Halmashauri za Miji nchini.

Baada ya Mamlaka ya Mji Mdogo wa Kondoa kukidhi vigezo, kufuatia uhakiki utakaofanywa na Wataalamu hao, Mamlaka hiyo itaunganishwa na Mamlaka za Miji Midogo mingine ambazo zimekidhi vigezo hivyo, ili iweze kuanzishwa kuwa Halmashauri ya Mji wa Kondoa.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Mamlaka ya Mji Mdogo, inaendelea kuhudumiwa kwa kupitia Bajeti ya Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa, mpaka hapo itakapokuwa imepandishwa rasmi kuwa Halmashauri ya Mji wa Kondoa, ambapo itakuwa na Bajeti yake yenye.

MHE. MOZA A. SAIDY: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kumuuliza maswali mawili, Mheshimiwa Waziri, ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Na kwa kuwa, Mji wa Kondoa ni Mji Mkongwe, takribani sasa ni miaka 87. Je, Wataalamu hawa watafika lini Kondoa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Pamoja na Serikali, kutoa Wataalamu hao. Je, mchakato huo utakwisha lini?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (*TAMISEMI*): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Moza, kwa pamoja yote mawili, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hawa watakapokuwa wamemaliza huu mchakato, mambo yote yatakuwa, tutamaliza tu kama nilivyoeleza. Labda kwa ajili ya kuwasaidia kidogo waheshimiwa Wabunge, vigezo tunavyovitumia hapa ambavyo mkishatuletea, mkiishapitia hatua hizo zote ni kama ifuatavyo; kuwe na watu wasiopungua 30,000 eneo liwe na uwezo wa kujitegemea angalao kwa 50% ya Bajeti yake.

Tatu kuwe na huduma za jamii zifuatazo; Hospitali na Shule za Sekondari, kuwe na Kituo Cha Polisi, leo tunazungumza habari ya Polisi hapa. Kuwe na maduka ya reja-reja lenye leseni yasiyopungua 50 na mwisho liwe ni eneo la Makao Makuu ya Tarafa.

Mheshimiwa Spika, sasa haya yote akishayaangalia ataangalia, sehemu hii tunaweza tuka-*ignore* na nini, mwisho anaamua kwamba tu. Kwa hiyo, ni lini tutakwenda kule, ni baada ya kukamilika kwa mchakato huo na tukishaupata, tutatuma watu waende wakahakiki kule kwa sababu, huwezi ukatwambia Kondoa kuko hivi, tunakwenda ku-*check* sisi wenyewe, kuhesabu na watu na kujua kila kitu.

MHE. HENRY D. SHEKIFU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Kama ilivyo mji wa Kondoa, iko Miji ilianzishwa zamani, Miji Midogo, tangu wakati wa ukoloni, ukiwemo Miji wa Lushoto; taratibu zote za kuomba Miji hii iwe Miji Kamili, zimefanywa.

Mheshimiwa Spika, Waziri anatamka nini muda unaochukuliwa katika kufanya maamuzi, wakati mchakato wote umekamilika?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shekifu mjomba wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, juzi tu hapa tumepitisha wazo la kuwa na Halmashauri ya Bumbuli hii inayozungumzwa ni sehemu ya hiyo Halmashauri ya Bumbuli na ndiyo shughuli inayoendelea pale mimi najua kabisa kwamba Mheshimiwa Shekifu amekuwa anafuatilia sana suala la hili la mji wa Lushoto.

6 MEI, 2013

Sasa sisi tukishamaliza hiyo tutakwenda tena kuangalia kama hakikidhi kama tulivyosema hapa wala hatuna tatizo na ni kweli kama anavyosema kwamba walishaleta haya sasa maamuzi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kupiditia kwa Waziri wa nchi yalikuwa ni haya kwamba tuna-deal/kwanza na Bumbuli tumalize sasa tutakwenda kuangalia na haya mengine.

Lakini pia nataka niseme hapa siyo kila mji utakaoombewa kwamba uwe Halmashauri ya mji tutasema sawa namwona Mheshimiwa Ntukamazina ananiangalia pale nilikwenda kule kwake yeye kweli anakidhi na nini lakini nataka siyo kila mtu atakayekuja hapa akileta itakuwa ni hivyo mpaka tujiridhishe tufike pale tupeleke na wataalam na mimi mwenyewe watanituma hawa wakuu wangu nitakwenda kule ku-chechhalafu baadaye nasema barabara.

SPIKA: Tunaendelea na Wizara inayofuata Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim atauliza swali hilo, Mheshimiwa Kombo eeh?

Na. 147

Mashirika ya Ndege Nchini

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO (K.n.y. MHE. MASOUD ADALLA SALIM) aliluliza:-

Usafiri wa anga haukidhi mahitaji ya Watanzania Walio wengi katika Mikoa mbalimbali.

Je, kuna Mashirika/Kampuni ngapi za ndege hapa nchini zinazofanya kazi ndani na nje ya nchi kwa mchanganuo wa idadi ya ndege?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim, Mbunge wa Mtambile, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa usafiri wa anga haukidhi mahitaji kwa Watanzania walio wengi katika mikoa mingi nchini kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo ukosefu wa miundombinu imara na ya kutosha katika baadhi ya mikoa. Miundombinu hiyo ni pamoja na viwanja vya ndege ambavyo vingetumika wakati wote wa mwaka na mitambo ya kuongozea ndege hususani wakati wa usiku. Aidha ukosefu wa makampuni ya ndege yenye uwezo wa kutoa huduma za usafiri ndani ya nchi kwa ufanisi na ushindani na kutoa nafuu kwa mtumiaji ni moja ya sababu ya usafiri wa anga nchini kutoridhisha.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa za mamlaka za usafiri wa anga hadi tarehe 31 Machi mwaka huu idadi ya kampuni za ndege zinazotoa huduma ya usafiri wa anga hapa nchini zilikuwa arobaini na sita na kati ya kampuni hizo 20 zinatoa huduma za usafiri wa ratiba na kampuni 26 zinatoa huduma zisizo na ratiba. Aidha kampuni mbili *Precision Air na Air Tanzania* zinatoa huduma nje ya nchi katika vituo vya Nairobi, Entebbe, Lubumbashi, Hahaya, Lusaka na Kigali. (*Makofii*)

MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO: Mheshimiwa Spika, asante sana, bei ya usafiri wa ndege ni kubwa mno na zinatofautiana sana baina ya kampuni moja na kampuni nyingine hasa kwa usafiri wa ndani.

Je, kuna utaratibu gani wa angalau kupunguza bei za usafiri wa ndege ili kuwawezesha Watanzania walio wengi kutumia usafiri huu?

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, jambo muhimu la kuzingatia ni usalama wa abiria wanaosafiri kwa kutumia ndege lakini nimeshuhudia kwa macho yangu mara nyingi ndege hizi zinakuwa na rubani mmoja.

Je, kufanya hivyo Mheshimiwa Spika si kuona kwamba tunahatarisha maisha ya abiria kwa kutumia rubani mmoja kusafirishia abiria kwenye ndege zetu?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kombo, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, bei zinazotumika katika kukatisha tiketi za ndege hazipangwi na mamlaka ya usafiri wa anga. Hili ni eneo ambalo nilikwisha toa jibu la namna hii hapa Bungeni kwamba soko ndilo linaloelekeza bei za tiketi katika usafiri wa anga ziweje na hii ndiyo taratibu ya Mataifa yote duniani. Hakuna Taifa ambalo linasafirisha watu angani mwanachama wa /CAO ambalo kumeweke utaratibu huu wa kudhibiti ndege ndiyo maana utaona unaweza kwenda asubuhi katika shirika fulani ukununua tiketi kwa shilingi 200,000/=, ukaenda baada ya nusu saa ukaambiwa 400,000/= au 500,000/= huo ndiyo utaratibu uliopo. Soko lenyewe tukiwa na huduma ya kutosha litazifanya bei ziteremke kama ambavyo tumeona. Ujio wa *Fast Fet* umefanya nauli za ndege kwenda maeneo ambayo ndege hiyo inakwenda kupungua kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la usalama wa abiria wanaosafirishwa na ndege zenye rubani mmoja mamlaka ya usimamizi wa usalama wa anga wanaruhusu jambo hilo kwa aina kadhaa za ndege. Aina nyingine za ndege hairuhuswi ndege kusafiri na *pilot* mmoja lakini zipo ndege hizi ndogo ndogo usalama wa anga wanaruhusu kuwa na *pilot* mmoja kwa sababu pia hata safari zenyewe zinakuwa ni fupi fupi kutokea mahali wanapoanzia. (*Makofii*)

MHE. SAID A. ARFI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa mahitaji ni pamoja na kuwepo na kiwanja ambacho kinakidhi kwa wakati wote kwa maana ya kipindi cha mvua na kiangazi. Serikali imewekeza Mpanda kujenga kiwanja kizuri na cha kisasa.

Je, Serikali itasaidia vipi ili kiwanja hicho kiweze kutumika na huduma za ndege ziweze kufika Mpanda?

SPIKA: Kama swali jipya lakini haya.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Arfi kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli uwanja wa ndege wa Mpanda unatumika kwa sasa na tunaendelea kuukamilisha kwa kuweka huduma za msingi ambazo zinatakiwa kuwepo katika uwanja wa ndege. Moja ya huduma hizo ni mnara wa uongozaji wa ndege, mafuta au matanki ya mafuta na baadaye nadhani tuko katika utaratibu tunaweza kuweka taa kwa ajili ya uwanja ule uanze kutumika usiku.

Mheshimiwa Spika, mambo haya yanahitaji fedha kwa hiyo tunakwenda na kadiri fedha zinazopatikana.

Na. 148

Kupanua Kiwanja cha Ndege cha Arusha

MHE. CATHERINE V. MAGIGE aliuliza:-

Kiwanja cha ndege cha Arusha kilichopo eneo la Kisongo ni muhimu sana katika kukuza uchumi wa Mkoa wa Arusha na Taifa kwa ujumla.

Je, Serikali ina mpango gani wa kukipanua kiwanja hiki au kujenga kiwanja kikubwa cha Kimataifa kinachoendana na mji wa Arusha?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Catherine Magige Mbunge wa viti maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge ya kuwa kiwanja cha ndege cha Arusha kina umuhimu mkubwa katika kukuza Mkoa wa Arusha na Taifa letu kwa ujumla. Hatuwezi kuongelea utalii Tanzania hususani Mkoa wa Arusha bila kuhusisha kiwanja cha ndege cha Arusha. Kwa kutambua umuhimu huo Serikali iliongeza eneo la kiwanja ili kutoa fursa ya upanuzi wa kiwanja hicho. Kufuatia kupatikana kwa eneo hilo Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege iliandaa mpango kabambe wa kuendeleza kiwanja ulioainisha miradi mbalimbali ya uwekezaji. Ili kupata mahitaji ya ujumla ya ukarabati na upanuzi wa uwanja Serikali inafanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ambao ulihusisha pia viwanja vya ndege vya Bukoba, Mafia, Kigoma, Shinyanga, Sumbawanga na Tabora chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imekamilisha urefushaji wa njia ya kurukia na kutua ndege kwa kiwango cha lami na hivyo kukidhi hadhi ya kuwa kiwanja cha Mkoa chenye uwezo wa kuhudumia ndege zinazobeba abiria 70. Kwa sasa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imeshampata mshauri mwelekezi wa kufanya usanifu wa jengo jipya la abiria pamoja na miundo mbinu yake. Aidha Mamlaka ya Viwanja vya Ndege inafanya mazungumzo na Benki ya Rasilimali Tanzania kwa ajili ya kupata mkopo wa fedha za ujenzi wa jengo hilo na mkataba wa mkopo yaani *loan agreement* unatarajiwa kusainiwa mwezi Juni mwaka huu.

MHE. CATHERINE V. MAGIGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza:-

Kwa kuwa Serikali inakiri kuwa kiwanja cha Arusha ni muhimu kwa Mkoa wa Arusha na Taifa kwa ujumla. Je, Serikali ahioni sasa ni wakati muafaka wa kuboresha miundombinu katika kiwanja hiki ili ziweze kutua ndege kwa masaa 24 badala ya sasa hivi ambapo mwisho wa kutua kwa ndege ni saa kumi na mbili na nusu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili kwa kuwa Serikali imesema kuwa ilifanya upembuzi yakinifu. Je, wananchi wa Mkoa wa Arusha wategemee ukarabati huu wa kiwanja hiki ni lini hasa utaanza?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi naomba kujibu kwa haraka haraka maswali mawili ya Mheshimiwa Magige kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, miundombinu ni pamoja na *runway* yenyewe na uboreshaji ndio kama huo tuliuofanya na unaendelea. Nimesema katika jibu la msingi kwamba sasa hivi tuko katika majadiliano na *TIB Development Bank* ambapo mkataba wa uendelezaji wa jengo la abiria utasainiwa mwezi Juni mwaka huu hiyo ni sehemu ya miundombinu ya uwanja huo. Fedha zikipatikana tunaendelea na aina nyingine ya miundombinu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukarabati wa uwanja huo, ukarabati ndio huo huo, miundombinu tunayoizungumzia ndio ukarabati wenyewe tunapotengeneza jengo ndio tumetengeneza miundombinu, tunapotengeneza uwanja ndio tumekarabati *runway* na kadhalika.

SPIKA: Mheshimiwa taa za usiku.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, taa za usiku ni sehemu ya miundombinu ninayoisema kwa sababu tukishakarabati jengo, tukishakarabati *runway* tukipata fedha tunajenga tunaweka taa, tukipata fedha tunaweka vituo vya kuongezea ndege na kadhalika. Kwa hiyo, yote haya yako katika *package* na tunavyopata pesa ndio tunatengeneza hicho ambacho tunauwezo nacho kwa fedha inayopatikana.

MHE. MARIA I. HEWA: Mheshimiwa Spika, ahsante wakati Serikali inapanua viwanja hivi mara nyingi huwa wanajisahau kuboresha majengo yanayozunguka kiwanja hicho ikiwemo Mwanza wanatengeneza viwanja vikubwa.

Je, Serikali katika hili, inaweza kututamkia nini kwamba kiwanja kinapoboreshwa na majengo yanayostahili kuweko hapo ikiwemo uchukuzi wa mizigo wa abiria wanapotua?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Maria Hewa, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli ukarabati au uboreshaji wa viwanja haukomei katika kuongeza au kupanua barabara ya kuruka na kutua ndege. Moja ya miundombinu ya msingi ni pamoja na jengo la abiria na majengo ya mizigo pamoja na vitu vingine ambavyo vinakuwepo hapo. Lakini pia tunachofanya sasa hivi hata maeneo ambayo yako kwenye siyo ndani ya eneo lenyewe la uwanja lakini karibu na viwanja vyta ndege. Tungependa sana tuwe tunayachukua na kuyawekea uwekezaji mzuri ili mandhari ya eneo hilo kwa ujumla iwe nzuri.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano Mbeya eneo la uwanja tumekwisha lichukua lakini tunalipa fidia hata kwa eneo lillo nje ya uwanja ili tuweze kuweka pale majengo ambayo yatakuwa yanavutia kwa watu wanaotua au kuitia kwenye viwanja vyetu wanaotoka nje au ndani ya nchi, kwa hiyo majengo haya ya kupokelea mizigo ya kuondokea abiria yote yanafanyiwa ukarabati mara tu tunapokuwa tumeputa fedha za kufanya hivyo.

Na. 149

Matengenezo ya Barabara ya Mbinga Mbamba Bay

MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA aliuliza:-

Kwa muda mrefu Serikali aliahidi kutengeneza barabara ya Mbinga – *Mbamba Bay* kwa kiwango cha lami.

- (a) Je, barabara hii itaanza kutengenezwa rasmi lini?

(b) Je, ni lini awamu ya tatu ya ujenzi wa daraja la Mto Ruhekei katika barabara hiyo itakamilika?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa *Capt. John Damiano Komba*, Mbunge wa Mbinga Magharibi, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepanga kuanza ujenzi wa barabara ya Mbinga – Mbamba Bay yenye urefu wa kilomita 67 katika mwaka wa fedha 2013/2014 ambapo shilingi milioni 2,600 zimeombwa kwa ajili kuanza ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, illi kuwapunguzia kero wananchi wanaotumia barabara ya Mbinga – Mbamba Bay Wizara ya Ujenzi kuitia wakala wa barabara *TANROADS* tayari imekamilisha ujenzi wa madaraja mawili yaani Ruhekei C lenye urefu wa meta 60 na Ruhekei B lenye urefu wa meta 15.6 na kuyaunganisha kwa lami. Daraja liliobaki la Ruhekei A lenye urefu wa meta 20 limetengewe shilingi milioni 577 katika mwaka wa fedha 2012/2013 ambapo ujenzi wa nguzo za daraja hilo umekamilika. Kazi iliyobaki ni kujenga sehemu ya juu ya daraja (*deck*) na barabara za maingilio kazi ambayo imepangwa kukamilika katika mwaka 2013/2014.

MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, shilingi bilioni 2.6 inajenga barabara ya urefu gani?

Kwa utaratibu huu wa Serikali kutenga bilioni 2.6 kwa mwaka hii barabara itajengwa kwa muda gani?

SPIKA: Nashukuru kwa maswali yako mafupi na yapate majibu mafupi.

6 MEI, 2013

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Komba kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, shilingi billioni 2.6 tunasema tunaanza kujenga barabara ya Mbinga – Mbamba Bay kitu cha muhimu hapa ni kumpata mkandarasi tutatangaza tenda atapatikana mkandarasi tutaweka mkataba fedha hii inatosha kulipa ile fedha ya kuanzia kazi. Kwa mwaka unategemea mkandarasi ambaye anafanya kazi kwa nguvu sana anaweza kwenda labda kilomita 15 mpaka 25 sasa inategemeana na *speed* ile na mkataba ambao tutakuwa tumeuweka kwa hiyo usiwe na wasiwasi na kilomita 67 tunategemea angalau katika muda wa miaka miwili mpaka miaka miwili na nusu barabara ile inakuwa imekamilika.

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Vita Kawawa zile barabara za Mbamba Bay Kigoma mnatokea wapi?

MHE. VITA R. M. KAWAWA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Serikali kupitia mradi wake wa MCC imejenga barabara ya kutoka Songea – Namtumbo kwa kiwango cha lami vizuri sana na sasa iko mwishoni kukamilika. Lakini barabara hiyo hiyo kipande kutoka Namtumbo kwenda Tunduru Serikali ilifanya vizuri kumsimamisha Mkandarasi aliyekuwa anafanya kazi hiyo kwa kutofanya kazi yake vizuri.

Je, ni lini mkandarasi mwingine atapatikana ili aje kuanza kazi kukamilisha barabara hiyo kuondoa tabu wanayopata wananchi wanapolala njiani kwenye barabara ambayo ina pori kubwa na wanyama wakali?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vita Kawawa kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli hii barabara ya Namtumbo – Tunduru ilikuwa imepata mkandarasi *package* tatu na mkandarasi yule kulingana na mkataba tuliokuwa tumekubaliana ameshindwa kutekeleza na Serikali imesitisha mkataba wake. Sasa baada ya kusitisha mkataba tuko kwenye hatua za kupata mkandarasi mwingine mkandarasi yule kaenda mahakamani. Kwa hiyo suala hilo mpaka mahakama itakapotoa uamuzi ili tuweze kuona namna gani hatua za kuchua aweze kupatikana mkandarasi mwingine.

Na. 150

Msongamano wa Magari- Barabara ya Ali Hassan Mwinyi

MHE. IDDI M. AZZAN (MHE. ABAS Z. MTEMVU) aliuliza:-

Kumekuwa na msongamano mkubwa wa magari katika barabara ya Ali Hassan Mwinyi (zamani *Bagamoyo Road*) ambapo watumiaji wa barabara hiyo hutumia takribani saa moja na nusu kutoka *Oysterbay Police* hadi Salenda *Bridge* hususan wakati wa asubuhi, saa moja hadi saa tatu.

Je, Serikali inaweza kutoa ufanuzi juu ya ufumbuzi wa matatizo la msongamano huo?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abas Zuberi Mtemvu, Mbunge wa Temeke, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa jiji la Dar es salaam lina tatizo la msongamano wa magari na Serikali inayo miradi mingi inayolenga kutatua tatizo hilo. Kwa kiasi kikubwa msongamano wa magari unatokana na uwezo mdogo wa miundombinu ya barabara ambayo haitoshelezi kuhimili kiasi kikubwa cha magari cha sasa ukizingatia kuwa asilimia kubwa ya magari yote nchini yako Dar es salaam na yanaongezeka kwa kasi kila mwaka.

Kwa upande mwingine, shughuli nyingi za kibiashara na Serikali zinafanyika katikati ya Jiji na hivyo kufanya magari mengi kuingia na kutoka katikati ya Jiji kwa pamoja nyakati za asubuhi na jioni. Hali hii inachangia kuwa na msongamano mkubwa wa magari Jijini Dar es salaam.

Mheshimiwa Spika, katika kutafuta ufumbuzi wa tatizo hili, Serikali inatekeleza miradi ya kupunguza msongamano wa magari katika jiji la Dar es salaam yenye thamani ya shilingi bilioni 876.336 kama ifuatavyo:-

(a) Barabara ya Kimara – Kivukoni(*fire*), *Fire* –Kariakoo na Magomeni – Morocco (shilingi bilioni 240);

(b) Karakana na vituo vya mabasi yaendayo kwa haraka (*BRT*) pamoja na kuhamisha nguzo za umeme (shilingi bilioni 47.90);

(c) Barabara ya Mwenge – Tegeta (shilingi bilioni 88.00);

(d) Barabara ya Kilwa (*Kilwa Road*) Bendera Tatu – Mbagala Rangi Tatu, (shilingi bilioni 35.16);

(e) Daraja la Kigamboni, (Shilingi bilioni 214.64);

(f) *Flyover* ya TAZARA, Serikali ya Japan imetoa msaada wa fedha kwa ajili ya usanifu;

(g) Barabara ya Gerezani (Bendera- Tatu – KAMATA), Serikali ya Japan imetoa msaada wa fedha kwa ajili ya ujenzi;

(h) Barabara ya Mandela (Shilingi bilioni 61.25); na

(i) Barabara ya *Wazo Hill* – Bagamoyo – Msata (Shilingi bilioni 89.61).

Kukamilika kwa ujenzi wa Barabara ya mabasi yaendayo haraka (*BRT*) kutoka Morocco kwenda Magomeni hadi Kivukoni na Kimara kutapunguza msongamano wa magari kati ya *Oysterbay* Polisi na Daraja la *Salender*.

Mheshimiwa Spika, katika mipango ya baadaye, Serikali itaangalia uwezekano na kujenga barabara ya juu (*viaduct*) pande zote za daraja la *Salender*, kupanua barabara kwenye maingilio (*approaches*) ya daraja lingine pembedi mwa daraja la *Salender* au kujenga njia mbadala (*Salender Bridge Bypass*) kutokea *Kenyata Drive* kuunganisha na *Ocean Road*.

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Iddi Azzan swali la nyongeza.

MHE.IDDI M.AZZAN: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Ujenzi wa barabara ambayo ameizungumza ni barabara zile kubwa, lakini ili kuondoa msongamano ni lazima barabara za mitaani ziimalishwe. Je, Serikali itakuwa tayari sasa kuzlongezea Fedha za mfuko wa Barabara Halamashauri za Jiji la Dar es salaam, hususan Halamashauri ya Manispaa ya Kinondoni na itoe pesa hizo kwa wakati ?

Baada ya usanifu wa *flyover TAZARA* Serikali iko tayari kutumbia ujenzi wa *flyover* hiyo itaanza lini?

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Iddi Azzan, kama ifuatavyo:-

Kwanza nakuomba Mheshimiwa Iddi Azzan tutakapokuwa tukileta Mpango wetu wa Maendeleo ya barabara, naomba upitishe Bajeti katika Mpango huo. Tuna Mpango wa kuongeza kiwango cha *Road Fund*, fedha hizo zitaongezwa katika barabara za Halamashauri.

Pili, kutohana na makubaliano yetu na Serikali ya Japan, ni kwamba *flyover* ya Tazara inatakiwa ianze katika mwaka wa fedha 2013/2014.

6 MEI, 2013

SPIKA: Mheshimiwa James F. Mbatia swali la nyongeza.

MHE. JAMES F. MBATIA: Kwa kuwa utafiti uliofanyika mwaka 2009 kuhusiana na msongamano wa Jiji la Dar es salaam unaonyesha Taifa linaingia hasara ya shilingi bilioni 4 kila siku kutohana na muda wa zaidi ya asilimia 30 wa kufanya kazi unaopotea barabarani, Mafuta yanayochomwa, uharibifu wa mazingira na msongo wa mawazo ambao haujajumuishwa. Suala la *parking facility* maeneo ya Ubungo na maeneo mengine ambayo ni muhimu na suala la msingi nalouliza ni maeneo ya *Oysterbay* kwenda katikati ya Jiji. Je, mpango wa kuanzisha usafiri wa haraka kupitia majini kuanzia Bagamoyo kuja katikati ya Jiji ambao utaondoa msongamano maeneo ya *Oysterbay* umefikia wapi?

SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Nalbu Waziri wa Ujenzi, majibu?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa James Mbatia kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Ni kweli tunatambua kwamba Serikali inapoteza fedha nyingi kulingana na msongamano huo. Ndiyo maana kwenye jibu langu la msingi nimesema tumewekeza zaidi ya bilioni 800 ili kupunguza msongamano, msongamano hautaweza kuisha kama hatuta *develop facilities* nyingine nje ya katikati ya jiji la Dar es salaam. *As long as tutaendelea kujenga kila kitu katikati ya Jiji hata tukimaliza hii miradi bado msongamano huu utakuwepo.*

Sasa hivi tuna *encourage* wawekezaji wote wafanye maendeleo mengine nje ya katikati ya jiji ili msongamano uweze kupungua. Sambamba na hilo, tunajaribu kupunguza zile barabara za *ring roads* ambazo ziko kwenye hatua mbalimbali za manunuzi zaidi ya hizi nilizozielezea. Kwa hiyo, zote zitakapokuwa zimekamilika, na uhakika kwa kiasi kikubwa msongamano utakuwa umepungua. (*Makof!*)

SPIKA: Nasikitika na dakika 15 na nina maswali manne, siwezi kuyamaliza kwa muda huo. Wizara ya Kilimo chakula na Ushirika, Mheshimiwa Grace S. Kiwelu atauliza swali linalofuata.

Na. 151

Kilimo cha Kahawa Kilimanjaro

MHE. GRACE S. KIWELI aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani madhubuti na mahsus wa kufufua kilimo cha kahawa Mkoani Kilimanjaro ambacho kwa miaka mingi kimekuwa tegemeo kwa wananchi wa Kilimanjaro na mhimili mkubwa kwa uchumi wa Taifa?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Grace S. Kiwelu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Serikali kuitia Bodi ya Kahawa nchini na kwa kushirikiana na wadau wa sekta ya kahawa imeandaa Mkakati wa kuendeleza Tasnia ya Kahawa (*Tanzania Coffee Industry Development Strategy 2012-2022*) kwa lengo la kuendeleza kilimo cha kahawa nchini kwa kuongeza uzalishaji tija na ubora wa kahawa kitaifa ili kuboresha mapato ya wakulima wa kahawa katika mikoa mbalimbali inayolima kahawa ukiwemo Mkoa wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, Malengo mahsus ya mkakati huo ni pamoja na kuongeza uzalishaji wa kahawa safi kutoka wastani wa sasa wa tani 50,000 kwa mwaka hadi kufikia tani 100,000 ifikapo mwaka 2022 na kuongeza ubora wa kahawa ili kupata bei ya ziada katika masoko ya nje kutoka wastani wa asilimia 35 hadi kufikia wastani wa asilimia 70 ifikapo mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, maeneo muhimu katika mkakati huo ni pamoja na:-

(a) Kuimarisha huduma za ugani ili wakulima wazingatie kanuni bora za kilimo cha kahawa?

(b) Kushirikiana na taasisi ya utafiti wa Kahawa (*TACRI*) ili kuhakikisha upatikanaji wa miche bora ya kahawa?

(c) Kuongeza matumizi ya viwanda vyta kati vya kutayarisha kahawa ili kuongeza ubora wa zao hilo na hivyo wakulima kunufaika na bei nzuri?

Mheshimiwa Spika, kama sehemu ya utekelezaji wa kamati huo, wadau wa Tasnia ya Kahawa wameanzisha Mfuko wa Wakfu wa kuendeleza Sekta ya Kahawa (*Tanzania Cofee Development Trust Fund*) ambao utakuwa na jukumu la kugharamia majukumu ya pamoja (*Shared Functions*) uendelezaji wa kilimo cha zao la kahawa hapa chini ukiwemo Mkoa wa Kilimanjaro. Aidha, Wizara yangu imeshasisitiza kuhusu umuhimu wa kipekee wa kuzingatia kanuni bora za kilimo cha kahawa ikiwa ni pamoja na kuondoa mibuni iliyo mingi ambayo ina umri wa ziadi ya miaka 40 ikilinganishwa na umri wa miaka 25 inayoshauriwa matumizi ya dawa sahihi na ushauri bora wa Maafisa Ugani. Katika Wizara yangu inategemea ushirikiano wa wadau wote ili kuwa na uhakika wa mafakanikuo makubwa.

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Nina maswali madogo mawili ya nyongeza. Hivi sasa wakulima wa Kahawa wamekata tamaa. Je, Serikali iko tayari kuongeza ruzuku ya zao hili la Kahawa ili iwe kichocheo na kuongeza uzalishaji kwa wakulima hawa?

Swali la pili, bei ya zao la kahawa imeshuka sana. Je, Serikali iko tayari kuanzisha mfuko ambao utafidia hasara wanazopata wakulima hawa kutokana na bei kushuka?

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri wa Nchi majibu. Waheshimiwa Wabunge, mnapokuwa humu ndani si mahali pa kuongea kwa sauti, wengine nitawataja kwa majina.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU): Mheshimiwa Spika, mpaka ninapoongea sasa, Serikali imekuwa ikitoa ruzuku kwa ajili ya miche bora inayozalishwa na kituo cha *TACRI* pale Kilimanjaro kwa ajili ya wakulima wa kahawa. Hii ndiyo ruzuku pekee ambayo sasa hivi inatolewa na inasaidia sana, kwa sababu inamuwezesha mkulima kuweza kubadili na kung'oa miche ya zamani na kuweka miche ya kisasa, jambo hili linafanyika kwa nchi nzima. Tunaweza kuongeza ruzuku kwa ajili ya zao la kahawa, ila inategemea na uwezo wa fedha, lakini nia ipo.

Kuhusu suala la kushuka kwa bei. Hili ni tatizo ambalo linakabili mazao yote ya kilimo nchini, kwani huwa bei inashuka na kupanda. Sera ambayo tunaisisitiza ni kwamba hatimaye tuanzishe mifuko ambayo inaitwa *price stabilization fund* ambayo inaweza ikamfidla mkulima wakati bei inaposhuka sana, ili asiweze kukatishwa tamaa. Wakulima kuititia vikao vyao wameanzisha mfuko na Serikali ipo tayari kushirikiana nao katika jambo hili.

MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Chama Kikuu cha Ushirika *KNCU* kipo Moshi kinanunua kahawa ya mkulima kwa mkopo, na wakulima wanadai madai ya miaka miwili mitatu bila kulipwa, na pia nyongeza hawajapata. Serikali inatoa kauli gani ili kuwapa moyo wakulima wa Kilimanjaro wa *KNCU* ili kuweza kufufua zao la kahawa.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwanza utaratibu unaotumika katika ununuzi wa kahawa ambaou naitwa stakabadhi ghalani, ndiyo utaratibu ambaou kusema kweli umekuwa unatumika na umewapa manufaa makubwa sana wakulima wa kahawa. Inapotokea kwamba wakulima hawalipwi mabaki ni udhaifu wa vyama vya ushirika ambavyo kusema kweli vinakusudia kumhudumia mkulima na siyo kumkatisha tamaa.

6 MEI, 2013

Kwa hiyo, kauli ya Serikali ni kwamba vyama vyama ushirika ambavyo vimenunua kahawa kwa mfumo ule lazima viwalipe wakulima mabaki ili kuhakikisha kwamba wakulima wanaendeleza kilimo cha zao la kahawa na wanapata manufaa yanayotokana na kazi yao.

SPIKA: Tunaendelea na swali linalofuata Tuna dakika kumi na maswali yamebaki matatu! Mheshimiwa Ezekiel M. Maige, kwa niaba yake Mheshimiwa James D. Lembeli atauliza.

Na. 152

Kuimarisha Kilimo cha Umwagiliaji Mkoani Shinyanga

MHE. JAMES D. LEMBELI (K.n.y. MHE. EZEKIEL M. MAIGE) aliliza:-

Mkoa wa Shinyanga una ukosefu mkubwa wa chakula japo kuna mabonde mengi yanayofaa kwa Kilimo cha Umwagiliaji.

- (a) Je, Serikali inachukua hatua gani kuimarisha usalama wa chakula mkoani humo?
- (b) Je, Serikali imechukua hatua gani za kuwekeza katika kilimo cha Umwagiliaji hasa katika jimbo la Msalala lenge mabonde yanayofaa kwa umwagiliaji?
- (c) Je, Serikali itatembelea lini mabonde ya Chela, Ngaya, Bugile, Ntobo na Segesa ambayo yote yanafaa kwa umwagiliaji na kushauri juu ya matumizi yenyeye tija ya mabonde hayo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ezekiel M. Maige, Mbunge wa Msalala, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo.

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inachukuwa hatua mbalimbali ili kuimarisha usalama wa chakula mkoani Shinyanga. Hatua hizo zinajumuisha: Kutoa chakula cha msaada pale ambapo pamekuwa na uzalishaji mdogo wa mazao ya chakula kutohana na hali mbaya ya hewa; kutoa ruzuku ya mbegu za mazao yanayochukua muda mfupi au yanayostahimili ukame zikiwemo mbegu za mtama na alizeti; kujenga mabanio ya kuchepua maji na kuyaelekeza mashambani kwa kutumia teknolojia ya kuvuna maji ya mvua na kujenga mabwawa pale inapowezekana kutohana na sura ya ardhi (*land topography*) ili kuhifadhi maji kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji.

Aidha, wakulima wameshauriwa kuwa baada ya kuvuna mazao ya msimu wa mvua, unyevunyevu wa maeneo ya umwagiliaji utumike kupanda mazao yasiyohitaji maji mengi kama vile dengu, jamii za kunde na mboga.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikiendeleza kilimo cha umwagiliaji mkoani Shinyanga kupitia *program* mbalimbali kwa kutumia teknolojia ya kuvuna maji ya mvua (*Rain Water Harvest Technology*) kwa kujenga mabanio ya kuchepusha maji wakati wa mvua. *Program* hizo ni pamoja na Programu iliyoghamariwa kwa pamoja na Serikali na Mfuko wa IFAD katika miaka 1993 – 2006 iliyotekeleza miradi ya kuvuna maji ya mvua katika mikoa kame – SDPMA/PIDP na sasa kupitia *program* ya ASDP na mradi wa DASIP.

Mheshimiwa Spika, katika jimbo la Msalala, Skimu ya Kahanga (450 ha) yenye kunufaisha kaya 500 imetengewa fedha za ujenzi kupitia mradi wa DASIP Tsh. 635 milioni na mkandarasi amekabidhiwa *site* kwa ajili ya kuanza ujenzi.

Aidha juhudzi za Serikali za kufanya upembizi yakinifu katika bonde la Manonga kupitia mradi wa '*Tanzania irrigation and Watershed Management*' uliopata fedha kutoka *Nile Basin – NELSAP* zimeonyesha kuwa hakuna maeneo yanapoweza kujengwa mabwawa kutohana na sura ya ardhi kuwa na tambarare. Serikali itaendelea kuainisha maeneo yanayofaa kuendelezwa kwa kuvuna maji

ya umwagiliaji kwa kutumia mabanio na kutenga fedha za utekelezaji katika mabonde ya jimbo la Msalala.

(c)Mheshimiwa Spika, kama sehemu ya kuimarisha kilimo cha umwagiliaji Wizara imemwagiza Mhandisi wa Umwagiliaji Kanda ya Mwanza kwa kushirikiana na wataalamu wa Kilimo wa Wilaya ya Kahama kuyatembelea mabonde ya chela, Ngaya, Bugile, Ntobo na Segese na kuyaanisha maeneo yanayofaa kwa umwagiliaji na kuwasilisha ushauri wa kitaalam juu ya matumizi yenyе tija ya mabonde hayo.

MHE. MHE. JAMES D. LEMBELI: Mheshimiwa Spika, nina swali moja la nyongeza. Kwa mujibu wa jibu katika swali la msingi kwamba Wizara imemwagiza Mhandishi wa Maji, kutembela maeneo yale aliyoyataja na yako katika sehemu moja tu ya Wilaya ya Kahama wakati Wilaya ya Kahama ni kubwa na maeneo yanayoweza kutumika kwa ajili ya umwagiliaji yako mengi. Je, Serikali inasema nini kuhusu kumwelekeza Mhandisi wa Maji kutembelea maeneo yanayofaa kwa umwagiliaji ambayo yapo katika Jimbo la Kahama pia?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU): Mheshimiwa spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Kwa kweli jitihada za Serikali ni kuhakikisha kwamba mabonde mengi ambayo yanastahili kuingizwa katika mpango wa umwagiliaji yanashughulikiwa. Kwa hiyo, katika maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge anayazungumzia Mkoa wa Shinyanga, Tabora, Igunga – Nzenga. Mikoa yote ile ambayo ina ukame, suala la umwagiliaji linatakiwa lipewe nafasi kubwa zaidi kwa sababu ndiyo njia peke yake inayoweza kufanya maeneo yale yakajitegemea kwa chakula na vilevile kuongeza uchumi wa wananchi wa maeneo hayo.

Hivyo tutazungumza na Mheshimiwa Mbunge ili atueleze ni maeneo gani ambayo angependa tutoe

maelekezo ili maelekezo yetu yawe *specific* kwa maeneo ambayo anafikiri yakifanyiwa uchunguzi yanaweza kuleta manufaa kwa mpango huo wa umwagiliaji.

SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Mawasialino Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Deo H. Filikunjombe atauliza swali linalofuata.

MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Ludewa naomba sasa swali hili lipate majibu.

SPIKA: Inabidi utaje namba.

MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE: Namba hiyo hiyo, namba 153.

SPIKA: Haiwezekani ikawa hiyo hiyo. Haya Mheshimiwa Naibu Waziri!

Na. 153

Uhaba wa Mawasiliano ya Simu- Ludewa

MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE aliuliza:-

Maeneo mengi katika Wilaya ya Ludewa yana uhaba wa mawasiliano ya simu za mkononi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka minara ya simu katika eneo la Mwambao kule Ziwa Nyasa na Milimani?

NAIBU WAZIRI OFISI YA MAKAMU WA RAIS alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Deo H. Filikunjombe, Mbunge wa Ludewa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote inaendelea na jitihada zake kuhakikisha maeneo yote nchini, hususan vijijini yanapata

huduma za mawasiliano ya simu. Juhudi hizo ni pamoja na kuhakikisha kuwa maeneo yasiyofikiwa na watoa huduma yanafikiwa kwa kutumia mbinu mbalimbali zikiwemo ruzuku inayotolewa na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote kushawishi kampuni za simu kupeleka mawasiliano katika maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, aidha, maeneo ya Jimbo la Ludewa yasiyofikiwa na huduma mawasiliano ya simu, vikiwemo vijiji Chanjale, Lumbila na Nkanda, Kata ya Lumbila; vijiji vya Kata ya Madilu na Viji vya Lupingu, Mtumbati na Nindi Kata ya Lupingu pamoja na vijiji vya Kata za Kilondo, Makonde na Madope vimejumuishwa kwenye zabuni ya awamu ya kwanza (A) ya ujenzi utakaogharamiwa kuititia fedha za Benki ya Dunia ambayo itatangazwa mwezi Mei, 2013.

SPIKA: Mheshimiwa Filikunjombe swali la nyongeza, huku wote muwe mkiangalia saa.

MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE: Mheshimiwa Spika, napenda niwashukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Serikali kwa ujumla kwa kuwakumbuka wananchi wa Ludewa hasa maeneo ya Ziwa Nyasa ambako wanapata shida sana. Kule maeneo ya Mangalanyeye na Madope kwa mfano wanapanda kwenye miti kuitafuta *network*.

Sasa minara hii ni ukombozi mkubwa sana kwetu. Swali langu la kwanza, Je, ujenzi huu wa minara ya simu Madope, Makonde na Lupingu utaanza lini na lini utakuwa umekamilika. Ujenzi utakapokuwa umekamilika Mheshimiwa Waziri yupo tayari kuja madope pamoja na Lupingu kwa ajili ya uzinduzi wa minara hiyo?

SPIKA: Nilifikiri unawakaribisha wakapande mtini. Mheshimiwa Naibu Waziri Majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU YA RAIS: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolijia, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Deo Filikunjombe, kama ifuatavyo:-

Kwanza nimhakikishie tu kwamba, mchakato wa *Tenderukishaanza* unachukua muda wa kutosha, lakini tuna uhakika kwamba mara tu mchakato wa kumpata Mkandarasi utakapokamilika, ujenzi utaanza mara moja. Nimhakikishie ni katika kipindi cha mwaka huu. Kuhusu suala la Mheshimiwa Waziri kwenda, naomba nilichukue hili nitamweleza Mheshimiwa Waziri na ninauhakika kabisa atakuwa tayari kufika kule katika uzinduzi wa Minara hiyo.

Na. 154

Utekelezaji wa Shughuli za Mkongo wa Taifa

MHE. MARGARETH A. MKANGA aliuliza:-

Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa ulikusudiwa kurahisisha mawasiliano ya *Internet*, simu za video, upokezi wa taarifa mbalimbali na kadhalika.

- (a) Je, ni lini Mkongo huo utaanza kutumika?
- (b) Je, kwa kuchelewa kuanza kwa shughuli za Mkongo, Serikali haioni kuwa Tanzania inazidi kuwa na gharama kubwa za mawasiliano ambayo sio bora?
- (c) Je, Serikali imejiandaaje katika kuwawezesha wananchi jinsi ya kunufaika na Matumizi ya Mkongo huo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU YA RAIS alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolijia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Margaret A. Mkanga, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano tayari umeshaanza kutumika tangu Mwezi July, 2010. Hadi kufikia Mwezi Machi, Mwaka huu (2013), Makampuni Saba ya Mawasiliano (*Telecom Operators*) ya hapa nchini yameunganishwa kwenye Mkongo wa Taifa kwa

ajili ya kutoa huduma zao kwa wateja. Aidha, Kampuni ya Simu ya *MTL* ya Malawi, *UCOM* ya Burundi, *MTN* ya Rwanda, na kampuni ya Simu ya *MTN* na *Airtel* za Zambia zinatumia huduma ya Mkongo wa Taifa wa mawasiliano kwa ajili ya mawasiliano ya Kimataifa.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa ujumla kutumika kwa Mkongo huu kumesaidia sana katika kushusha għarama za mawasiliano. Kwa mfano, katika għarama za kusafirisha masafa (*transport charges*) zimeshuka kwa asilimia 99 kutoka Dola za Kimarekani 20,000.00 kwa mwezi kwa umbali wa Kilomita 1,000.00 kwa mwendo kasi ya 2 *megabits per second* mwaka 2009 hadi kufikia Dola za Kimarekani 160.00 kwa mwezi kuanzia mwaka 2011 na huduma za *internet* zimeshuka kutoka shilingi 36,000/= kwa *Gigabyte (GB)* moja (2009) hadi shilingi 9000/=kwa *GB* moja (2013), sawa na kushuka kwa asilimia 75.

(c) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoelezea hapo awali, wananchi tayari wameanza kunufaika kwa kushuka għarama za mawasiliano. Aidha, Serikali inaendelea na jitihada za kuzihamasisha Taasisi mbalimbali ambazo bado hazijajunganisha katika Mkongo ziweze kuijunganisha ili ziweze kunufaika na faida zitokanazo na Mkongo. Aidha, changamoto kubwa iliyopo kwa hivi sasa ni uwezo mdogo wa kifedha uliopo katika Wizara, Idara, Vyuo, Mashule, Hospitali na Taasisi nyngi nchini hususan za umma zikiwemo Halmashauri za Miji na Wilaya wa kuijunganisha kwenye Mkongo. Hii imepunguza kasi ya kuijunganisha. Awamu ya tano ya Mradi inalenga kusaidia kutatua tatizo hili kwa kuijunganisha Wizara, Idara, Vyuo, Mashule, Hospitali na Taasisi nyngi nchini hususan za umma kwenye Mkongo.

(d) Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwahimiza watoa huduma za mawasiliano nchini kutumia fursa hii ya uwepo wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ili wajiunganishe na wautumie kikamilifu (*Fully Utilize*) katika kutimiza lengo la Serikali la kuwapatia wananchi huduma bora, za uhakika na kwa għarama nafuu kwa maendeleo ya Taifa letu.

SPIKA: Mheshimiwa Mkanga swali la nyongeza.

MHE. MARGARETH A. MKANGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi, pamoja na majibu mazuri kutoka kwa Naibu Waziri, nilikuwa nataka kufahamu, hiyo awamu ya tano itaanza lini?

Endapo awamu ya tano itaanza baadaye kidogo. Je, Serikali inaonaje hizi Taasisi ambazo kifedha zinashindwa kuunganishwa kwa haraka, wakaunganishwa kama mkopo halafu wakalipa kidogokidogo?

SPIKA: Ahsante umeuliza vizuri maswali mafupi, Mheshimiwa Naibu Waziri na wewe ujibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU YA RAIS: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolijia, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Margareth A. Mkanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awamu ya Tano itaanza mara tu *Tenderitakapotangazwa* na Wazabuni kupatikana. Sasa hivi documents za *Tender* zinatengenezwa na nina uhakika itaanza mara moja baada ya hilo kuwa limekamilika. Kuhusu mpango wa namna gani watu ambaao hawana fedha waweze kukopeshwa, hili tayari linafanyika, kwa hivyo, tushawishi tu Makampuni au Halimashauri ambazo zinaweza kukopeshwa halafu baadaye zikawa zinalipa kidogo kidogo ziweze kuwasiliana na *TTCL* na zitaunganishwa kwenye Mkongo. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante, muda wa maswali umekwisha. Nilitangaza mwanzoni, tunayo *Supplementary Order Paper* na ninaomba m-note hiyo, imegawiwa sasa.

Halafu la pili Waheshimiwa Wabunge maswali yetu tukiwa tunayafuliza mafupi na wanaojibu wakajibu kwa kifupi. Yale yaliyoandikwa wengine wanasema wameandika *page* moja lakini maandiko madogo sawa na *page* tatu, matokeo yake sasa hampati maswali ya *supplementary* mengi kwa

6 MEI, 2013

sababu hiyo. Kwa hiyo, muulize maswali kwa kifupi, mjibu kwa kifupi, tunaweza kuwa na *dialogue* nzuri sana asubuhi, lakini kwa mtindo huu basi atauliza mwenye swali na kuishia hapo.

Tuna matangazo ya kazi. Kaimu Mwenyekiti Kamati ya Bunge ya Miundombinu, Mheshimiwa Prof. Juma Kapuya, ameomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa saba mchana, watakuwa na kikao katika Ukumbi Namba 231.

Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, yeye ni Mwenyekiti wa APNAC Tanzania, ameomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati Tendaji ya APNAC kuwa leo tarehe 6 Mei, 2013 watakuwa na kikao chao ukumbi Namba 227. Kwa hiyo, wote wanaohusika muendelee. (*Makofî*)

KAULI ZA MAWAZIRI

**Mlipuko Katika Kanisa Katoliki la Mtakatifu Joseph,
Parokia ya Olasiti, Arusha**

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 49(1) ya Kanuni za kudumu za Bunge toleo la Aprili, 2013, naomba kuwasilisha taarifa ya awali kuhusu tukio la mlipuko uliotokea katika Kanisa Katoliki la Mtakatifu Joseph, Parokia ya Olasiti, Jijini Arusha tarehe 5 Mei, 2013, saa 4.30 Asubuhi.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 5 Mei, 2013, saa 4.30 Asubuhi, kulitokea mlipuko katika Kanisa la Katoliki la Mtakatifu Joseph Mfanyakazi, Parokia ya Olasiti, Jijini Arusha. Mlipuko huo uliotokea muda mfupi baada ya kuanza kwa Ibada ya uzunduzi wa Parokia hiyo.

Mgeni Rasmi katika uzinduzi huo alikuwa ni Balozi wa Vatican Nchini na Mjumbe wa Baba Mtakatifu, Askofu Francisco Mantecillo. Padilla. Aidha alikuwepo mwenyeji wake Askofu Josephat Lebulu wa Jimbo kuu Katoliki la Arusha.

Mheshimiwa Spika, wakati Mgeni Rasmi akiwa ametoka nje ya Kanisa akijiandaa kukata utepe kama ishara ya uzinduzi, mtu mmoja alirusha kitu kuelekea eneo kulikokuwa na mkusanyiko wa watu ambapo baada ya kutua, kilitokea kishindo na mlipuko mkubwa, mlipuko huo ulisababisha taharuki mionganoni mwa Waumini na kusababisha watu kukimbia ovyo.

Mheshimiwa Spika, katika tukio hilo, watu wawili wamefariki dunia, ambapo Regina Longino Kulusei, Mwarusha, umri wa miaka 45, Mkazi wa Olasiti, alifariki dunia siku ya tukio wakati akipatiwa matibabu katika Hospitali ya *Mount Meru* na majeruhi mwингine, James Gabriel umri wa miaka 16, amefariki dunia usiku wa kuamukia leo. Aidha, watu 58 wamejeruhiwa, watatu kati yao ni mahututi.

Mheshimiwa Spika, Majeruhi 38 walikimbizwa Hospitali ya *Mount Meru* kupatiwa matibabu, 16 walikimbizwa Hospitali ya St. Joseph, mmoja alipelekwa Hospitali ya Selian na majeruhi mwингine alipelekwa katika Hospitali ya Dr. Wanjala, katika eneo la Mianzini.

Natumia fursa hii kutoa pole kwa wafiwa, uongozi wa Kanisa Katoliki, wakazi wa Arusha na Watanzania wote kwa tukio hili la kinyama. Aidha nawaombea majeruhi wote wa tuko hilo wapone haraka.

Mheshimiwa Spika, Viongozi wa Dini na Serikali waliohuduria Ibada hiyo hawakupata madhara yoyote kufuatia mlipuko huo, baada ya tukio hilo, Jeshi la Polisi Mkoa wa Arusha lilipopata tu taarifa ya tukio hilo wallimarisha ulinzi kwa kuongeza idadi ya Askari katika eneo hilo.

Aidha, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa ikiongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mheshimiwa Magesa Mlongo walifika eneo la tukio na kufanya tathimini ya hali ilivyo na kuelekea hatua za kuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uzito wa tukio hilo kitaifa na kimataifa, Makamu wa Rais, Mheshimiwa

Dkt. Mohamed Gharib Bilal, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa Pereira Ame Silima, na *Inspector General* wa Polisi Said Mwema, walikwenda Arusha na walitembelea eneo la tukio, waliwatembelea majeruhi na kuelekeza hatua za ziada za kuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, uchunguzi wa awali unaonyesha kuwa mlipuko huo ni bomu, uchunguzi wa kubaini aina ya bomu lilitotumika unaendelea kufanywa na Jeshi la Polisi na Wataalam kutoka Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Hadi sasa watuhumiwa sita wanashilihiwa na jeshi la Polisi, mionganon mwayo ni Victor Calisti Ambrose mwenye umuri wa miaka 20, dereva wa Bodaboda, mkazi wa kwa Mrombo Arusha, ambaye anatuhumiwa kwa kurusha bomu hilo. Watuhumiwa wengine watano waliokamatwa ni raia wanne wa kigeni na Mtanzania mmoja ambao wanashikiliwa kwa mahojiano.

Mheshimiwa Spika, siku za karibuni kumekuwepo na jitihada kubwa sana za watu wachache wasioitakia mema nchi yetu kutaka kupandikiza chuki za kidini miongoni wa Watanzania na kuleta mapigano na mauaji miongoni mwa Watanzania. Sina shaka kuwa shambulio la Arusha ni sehemu ya mikakati hiyo miovu. Nataka niwahakikishie Watanzania kuwa Serikali haitavumilia hata kidogo mbegu hizi za kidini na za chuki miongoni mwa Watanzania kuendelea kupandikizwa, tutachukua hatua kali bila huruma kuzikandamiza njama hizi. (*Makof!*)

Tutachukua hatua kali kwa mtu ye yeyote bila kujali hadhi na nafasi yake katika jamii, Amani yetu kwanza, Taifa letu kwanza. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kukamatwa watuhumiwa hao, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, wametoa maelekezo kwa vyombo vyya ulinzi na usalama ambapo tayari *Inspector General* wa Polisi kwa kushirikiana na Wakuu wengine wa vyombo vyya ulinzi na usalama, wameunda kikosi kazi maalum ili kuchunguza tukio hilo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kokote Duniani, tukio la kushtukiza, linalosikitisha na kuhuzunisha kama hili linapotokea, wananchi wote huungana na kuwa wamoja kama Taifa na kulaani wahusika na kuwafariji waathirika wa tukio hilo. (*Makof*)

Nchini Marekani, mgombea mmoja wa Urais wakati wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2012, alishutumu Serikali kutokana na tukio la kulipuliwa kwa Ubalozi wa Marekani Nchini Libya, ni wazi kuwa mgombea huyu alichukua tatizo lile kama ajenda ya kunufaika kisiasa. Hata hivyo, alishutumiwa vikali na Wamarekani wenzake kwa kuelezwaa kuwa ni mtu mwenye kukosa kabisa misingi ya uaminifu na uzalendo kwa Taifa lake. (*Makof*)

Wenyewe kwa Kingereza walisema *Fundamental dishonest*, Serikali inasikitiswa sana na wanasiasa wa aina hii, ambao wanajitokeza nchini na kutafuta umaarufu wa kisiasa kwa gharama ya maisha ya Watanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, wanasiasa na viongozi wote, lazima wajiepushe na kutoa kauli zinazochochea ubaguzi wa kidini, mifarakano ya kijamii na chuki mionganii mwa Watanzania. Serikali isilaumiwe kwa hatua kali za kisheria itakazochua dhidi ya viongozi wa aina hii ambao maslahi yao ni muhimu zaidi kuliko maisha ya Watanzania. (*Makof*)

Maslahi yao ni muhimu kuliko utulivu wa Watanzania, na maslahi yao ni muhimu kuliko umoja wa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Serikali, naungana na Watanzania wenzangu kulaani wahusika wote wa tukio hilo, walioshiriki kwa njia yoyote ile. Aidha Serikali kwa nguvu zake zote itahakikisha kuwa watuhumiwa wote waliohusika na kushiriki kwa namna yoyote katika tukio hili, wanasaakwa popote walipo na kufikishwa katika vyombo vyanya sheria.

Tunawataka viongozi wa kisiasa, kidini na wananchi wote kwa ujumla, kila mmoja kwa nafasi yake kuwajibika ili kuhakikisha kuwa nchi yetu inaendelea kuwa kisiwa cha amani na utulivu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nawasihi Watanzania wawe watulivu wakati vyombo vya dola vikiwasaka waliohusika na shambulio hilo, kila mwenye taarifa za kuwezesha kukamatwa wahalifu hao, atoe taarifa hizo kwa jeshi la polisi. Aidha nawaoba Watanzania wote, wa dini zote, imani zote, itikadi zote, tuendelee kukataa vitendo vya uvunjifu wa amani katika nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana, Katibu!

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali Mwaka 2013/2014 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

SPIKA: Mheshimiwa Mtoa Hoja, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

MHE. MOSE J. MACHALI: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Hakuna Mwongozo sasa hivi, hakuna lilitotokea la mwongozo ni kupoteza muda. Silipendi kabisa, naomba ukae, Mheshimiwa mtoa hoja endelea.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia taarifa iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia muda nilio nao kuwasilisha hoja hii sitasoma neno kwa neno, lakini naomba hotuba yangu kama ilivyo katika kitabu cha hotuba iingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kutumia fursa hii kutoa masikitiko yangu kwa familia na wananchi kwa ujumla kutokana na vifo, ulemavu, upotevu na uharibifu wa mali na miundombinu vilivyosababishwa na ajali za barabarani, majini, kuperomoka kwa majengo na vifusi, vurugu na fujo katika mwaka mzima wa 2012.

Aidha, nawapa pole ndugu na jamaa wa marehemu waliopoteza maisha yao katika matukio hayo. Namwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Anna Margareth Abdallah, Mbunge Viti Maalum kwa kuyachambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Naishukuru pia Kamati hiyo kwa maelekezo na ushauri wao wenye lengo la kuboresha utendaji kazi wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake alioitoa mapema katika mkutano huu wa Bunge ambayo imetoe mwelekeo wa kazi za Serikali kwa ujumla katika mwaka wa fedha wa 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya msingi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ni kulinda usalama wa raia na mali zao, kuhifadhi na kuwarekebisha wafungwa, kutekeleza Programu ya Huduma kwa Jamii, kudhibiti uingiaji na utokaji nchini wa raia na wageni, kutoa huduma za zimamoto na uokoaji, kuwashudumia wakimbizi waliopo nchini, na kutoa vitambulisho vya Taifa.

Majukumu haya yanatekelezwa kupitia Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Idara ya Huduma kwa Jamii, Idara ya Uhamiaji, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Idara ya Wakimbizi na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Hali ya Uhalifu. Kama inavyofahamika kwamba wajibu wa kwanza wa Serikali ni kulinda usalama wa raia na mali zao. Umuhimu wa amani na utulivu kama msingi mkuu ambao umejengwa nchini na waasisi wa Taifa letu na mchango wake katika ustawi wa nchi yetu kiuchumi, kijamii na kisiasa umeendelea kuzingatiwa.

Kwa upande wake, Jeshi la Polisi limeendelea kutekeleza kikamilifu jukumu lake la kulinda na kudumisha amani na utulivu nchini kwa kubaini, kuzuia na kutanzua vitendo vya uhalifu, migogoro, vurugu, fujo na ukiukwaji wa Sheria za Usalama Barabarani.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2012 makosa ya jinai makubwa na madogo 566,702 yaliripotiwa katika vituo vya Polisi ikillinganishwa na makosa 564,716 yaliyoripotiwa katika kipindi kama hiki mwaka 2011. Idadi ya makosa imeongezeka kwa asilimia 0.3. Tazama Jedwali Na.1. Ongezeko hilo limechangiwa na kuongezeka kwa makosa madogo kutokana na ushirikishwaji wa wananchi katika vita dhidi ya uhalifu na kuongezeka kwa wigo wa doria na misako ya Polisi Mijini na Vijiji.

Mheshimiwa Spika, makosa makubwa ya jinai yamegawanyika katika makundi matatu ambayo ni makosa dhidi ya binadamu, makosa ya kuwania mali na makosa dhidi ya maadili ya jamii. Idadi ya makosa makubwa ya jinai yaliyoripotiwa katika vituo vya polisi imepungua kutoka 76,052 mwaka 2011 hadi 72,765 mwaka 2012 ikiwa ni sawa na upungufu wa asilimia 4.3.

Mafanikio ya kupungua idadi ya makosa makubwa ya jinai yanatokana na utekelezaji wa mikakati ya Jeshi la Polisi ya kuimarisha doria, misako na operesheni maalum, ushirikishwaji wa wananchi katika mapambano dhidi ya uhalifu, ushirikiano wa Jeshi la Polisi na vyombo vingine vya dola ndani ya nchi na ushirikiano wa Jeshi la Polisi na majeshi mengine ya Polisi kikanda na kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Usalama Barabarani. Pamoja na mikakati ya Jeshi la Polisi ya kuzuia na kudhibiti ajali za barabarani, ajali hizi zimeendelea kusababisha vifo, majeraha na ulemavu wa kudumu kwa wananchi pamoja na upotevu na uharibifu wa mali za wananchi, Taasisi na Serikali kwa ujumla. Katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2012 makosa makubwa ya usalama barabarani 23,604 yaliripotiwa katika vituo vya Polisi ambapo watu 4,062 walipoteza maisha na wengine 20,037 kujeruhwa ikilinganishwa na makosa makubwa 24,078 yallyoripotiwa katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2011 ambapo watu 4,013 walifariki na wengine 20,917 kujeruhwa. Idadi ya makosa ilipungua kwa asilimia 1.9.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na wadau wengine kama *SUMATRA, TBS, TANROADS* na Shule za Udereva zillizosajiliwa limeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuzuia na kudhibiti ajali za barabarani zikiwemo kutoa elimu ya kuzingatia Sheria za Usalama Barabarani kwa watumiaji wa barabara, kushirikisha wadau wa usalama barabarani katika kuhuisha mikakati ya kupunguza ajali za barabarani, kuendeleza doria za masafa mafupi na marefu katika kusimamia Sheria za Usalama Barabarani, kufanya ukaguzi wa magari, kutumia kamera za kutambua madereva wanaoendesha kwa mwendo kasi bila kuzingatia alama za usalama barabarani, kuendelea kusimamia zoezi la utoaji wa leseni mpya, kuwahamasisha wasafiri kutoa mapema taarifa za madereva wanaokiuka Sheria za Usalama Barabarani na kuwahamasisha wamiliki wa Mabasi kubandika kwenye Mabasi yao namba za simu za viongozi wa Polisi Usalama Barabarani.

Kwa ujumla Jeshi la Polisi linaendelea kutekeleza maoni ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yaliyoainishwa katika *Performance Audit Report on the Management of Traffic Inspections and Speed Limits in Tanzania* ya mwaka 2012. Taarifa hii inalitaka Jeshi la Polisi lijikite zaidi katika kuzuia na kudhibiti vyanzo vya ajali za barabarani vya mwendokasi, ulevi, uzembe wa madereva na kuzidisha abiria na mizigo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vitendo vya uvunjifu wa amani, vurugu na fujo; mnamo tarehe 15/02/2013, Mawaziri tisa kutoka Wizara za Katiba na Sheria; Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto; Kilimo, Chakula na Ushirika; Nishati na Madini; Elimu na Mafunzo ya Ufundji; Mambo ya Ndani ya Nchi pia Ofisi ya Rais, Utawala Bora na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa walihudhuria warsha ilioandaliwa na Jeshi la Polisi iliyofanyika hapa Dodoma kuhusu mipango ya Serikali katika kudumisha usalama nchini.

Mheshimiwa Spika, Warsha hiyo ilitanguliwa na mukutano mkuu wa mwaka wa Maafisa Waandamizi wa Jeshi la Polisi uliofanyika kuanzia tarehe 12 – 14 Februari, 2013 uliokuwa na kauli mbiu isemayo: "Tujenge Uwezo wa Jamii na Polisi Kukabiliana na Vurugu kwa Kuimarisha Utii wa Sheria Bila Shuruti".

Mheshimiwa Spika, kufanyika kwa warsha hiyo ya Mawaziri kulitokana na kuendelea kuwepo kwa vitendo vya vurugu, fujo na uvunjifu wa amani vinavyotokana na migogoro ya kijamii katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, vurugu za kisiasa zilizotokea Arusha, Mwanza, Mbeya, Mtwara, Morogoro, Singida na Iringa; migogoro ya ardhi iliyotokea Babati, Madale - Dar es Salaam, Sumbawanga, Ngorongoro, Rufiji na Kilosa; migogoro ya kidini iliyotokea Zanzibar, Mbeya, Temeke, Geita na mgogoro kuhusu uwekezaji katika sekta ya gesi Mkoani Mtwara, ni kati ya matukio mengi yanayoendelea kutokeea nchini.

Mheshimiwa Spika, katika matukio hayo ya vurugu, fujo na uvunjifu wa amani, watu kadhaa wamepoteza maisha wakiwemo Askari Polisi, wananchi mbalimbali wamejeruhiwa na umefanyika uharibifu wa miundombinu, mazingira na mali za Serikali na watu binafsi.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni kumejitokeza vurugu za udini ambapo zipo kesi 16 zilizohusisha jumla ya

watuhumiwa 195. Kesi 13 tayari zimefikishwa Mahakamani na kesi tatu upelelezi bado unaendelea. Athari za vurugu za udini ni pamoja na uvunjifu wa amani. Serikali imejpanga vyema kuona kuwa hali hiyo haiendelei na hajirudii tena kwa ustawi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, matukio haya inawezekana yameacha makovu ya chuki za kiitkadi na hisia za kulipiza kisasi miongoni mwa waathirika. Jeshi la Polisi limejizatiti kukabiliana na vitendo hivi vya fujo, vurugu na uvunjifu wa amani kwani vikiachwa viendelee uchumi wa nchi utadorora kutokana na ushiriki hafifu wa wananchi kwenye shughuli za maendeleo unaosababishwa na hofu inayojengeka katika jamii ya Watanzania na wawekezaji wa ndani na nje kutokana na nchi kuelekea kupoteza sifa yake ya kuwa ni Kisiwa cha Amani.

Mheshimiwa Spika, naungana na Watanzania wenzangu kulaani vitendo vyote vya fujo na vurugu vilivyosababisha uvunjifu wa amani. Nawakemea vikali wale wote walioshiriki, kuwezesha, kufadhili, kuhamasisha, kuchochea na kushawishi jamii kushiriki katika vitendo vilivyosababisha vurugu hizo na hata umwagaji wa damu. Natoa pole kwa wahanga wote wa vurugu hizo. Hatua za kisheria kwa watuhumiwa zinaendelea kuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii pia kuliomba Bunge lako Tukufu liendelee kuunga mkono kwa vitendo utekelezaji wa Programu ya Maboresho ya Jeshi la Polisi. Programu hii pamoja na mambo mengine, imelenga kuligeuza Jeshi la Polisi kuwa la kisasa, lenye watendaji wenye weledi na linaloshirikiana na jamii katika kubaini, kuzuia, kudhibiti na kukabili vitendo vya uhalfu, fujo na vurugu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Mawaziri wenzangu waliohudhuria warsha ilioandaliwa na Jeshi la Polisi hapa Mjini Dodoma mwezi Februari 2013 kwa kutoa Tamko la Dodoma lililokubali kusimamia na kutekeleza mipango ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu ya kuimarisha ulinzi na usalama nchini kwa:-

- (i) Kuliweka suala la usalama kuwa ni moja ya vipaumbele vya Taifa;
- (ii) Kutenga fedha za kutosha kuliwezesha Jeshi la Polisi kumudu kikamilifu wajibu wake wa kuhakikisha usalama wa raia na mali zao;
- (iii) Kutambua kwamba kila Wizara ni mdau katika suala la usalama na inayo wajibu wa kuepusha migogoro inayozalisha vurugu;
- (iv) Kufanya tathmini ya maeneo ambayo ni vyanzo vya migogoro na kutafuta njia ya kuzuia/kutanzua migogoro hiyo. Kuimarisha/kuhuisha mifumo ya usimamizi wa sheria na uwajibikaji wa kila Idara ya Serikali;
- (v) Kujenga ubia wa kiutendaji baina ya Wizara wanazoziongoza na vyombo vya ulinzi na usalama katika kubaini vyanzo vya migogoro na kuweka mikakati ya pamoja ya kuzuia na kutanzua migogoro hiyo;
- (vi) Kuliwezesha Jeshi la Polisi kwa rasilimali vifaa na miundombini pindi Mikoa mipyä inapoanzishwa; na
- (vii) Kurekebisha haraka na kwa vipaumbele upungufu wa kisera, kisheria na kikanuni unaoweza kuchangia mianya ya kusababisha migogoro ya kijamii.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya utekelezaji wa malengo ya llani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 katika kipindi cha 2012/2013. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ina malengo 10 ya kutekeleza yanayotokana na llani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010. Taarifa ya utekelezaji wa malengo hayo kwa mwaka 2012/2013, ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, lengo la kwanza ni kuendeleza mapambano dhidi ya biashara ya dawa za kulevyia. Katika kipindi cha Julai, 2012 hadi Februari, 2013, Jeshi la Polisi

liliwahamasisha na kushirikiana na wananchi katika Ulinzi Shirikishi ili kudhibiti uhalifu ukiwemo uingizaji, usambazaji na matumizi ya dawa za kulevyatika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, ushirikiano wa wananchi na vyombo vingine vya dola uliliwezesha Jeshi la Polisi kuwakamata watuhumiwa 546 wakiwa na jumla ya kilo 33.299 za dawa za kulevyatza viwandani ambapo *Cocaine* ni kilo 14.209, *Heroin* kilo 13.073 na *Mandrax* kilo 6.017.

Mheshimiwa Spika, aidha, watuhumiwa 6,730 walikamatwa na kilo 37,704.201 za dawa za kulevyatza mashambani ambapo *bhangi* ni kilo 26,938.445 na mirungi kilo 10,765.756. Jumla ya ekari 211 za mashamba ya *bhangi* zilitketezwa katika Kanda Maalum ya Kipolisi ya Tarime/Rorya na Mkoani Tanga.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi litaendelea kushirikiana na wananchi kupata taarifa za waingizaji, wasafirishaji na watumiaji wa dawa za kulevyat. Pia litaendelea kubaini mtandao wa wahalifu wa ndani na nje ya nchi unaojihusisha na uingizaji na usambazaji wa dawa za kulevyatnchini kwa kushirikiana na Shirika la Polisi la Kimataifa (*INTERPOL*) kupata taarifa za kiintelijensia kuhusu wasafirishaji wa dawa za kulevyat.

Kikosi Kazi cha Kitaifa cha Vyombo vya Ulinzi na Usalama cha kupambana na biashara ya dawa za kulevyat kitaendelea kuimarishtwa kwa kukiongezea rasilimali watu na vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, lengo la pili, ni kupunguza msongamano wa wafungwa na mahabusu katika Magereza. Tatizo la msongamano wa wafungwa na mahabusu bado ni kubwa licha ya hatua mbalimbali zinazochukuliwa katika kukabiliana nalo.

Mheshimiwa Spika, kulingana na takwimu, msongamano Magerezani kwa kiwango kikubwa unasababishwa na uwepo wa mahabusu wengi. Tarehe 1

Februari, 2013 idadi ya wafungwa na mahabusu waliokuwepo Magerezani ilifikia 34,355. Kati ya hao wafungwa walikuwa 16,330 na mahabusu 18,025.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2012 hadi Februari, 2013 jumla ya wafungwa 387 walikuwa wanatumikia kifungo cha nje kwa kutumia kanuni za kifungo cha nje za mwaka 1968.

Mheshimiwa Spika, vile vile wafungwa 903 waliachiliwa na Mahakama ili kutumikia kifungo cha nje, chini ya Sheria ya Huduma kwa Jamii kwa kipindi cha Julai, 2012 hadi Februari, 2013. Aidha, wafungwa 3,814 walifaidika na msamaha wa Rais uliotolewa tarehe 9 Desemba, 2012 wakati wa sherehe za kuadhimisha miaka 51 ya Uhuru wa Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, hatua zingine zinazochukuliwa ili kupunguza msongamano ni pamoja na kuundwa kwa Jukwaa la Haki Jinai, chini ya Uenyekiti wa Mkurugenzi wa Mashtaka ambapo wajumbe wengine ni Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza na Mahakama. Jukumu la msingi la jukwaa hilo ni kuimarisha utoaji wa haki nchini.

Mheshimiwa Spika, lengo la tatu, ni kuimarisha na kuboresha mfumo wa upelelezi wa makosa ya jinali ili kurahisisha uendelezaji wa kesi Mahakamani. Kwa kutumia vyuo vya Taaluma ya Polisi vya Moshi na Kidatu, kati ya Julai 2012 hadi Februari 2013, Jeshi la Polisi limetoa mafunzo ya Intelijensia na mbinu za kisasa za upelelezi kwa wapelelezi 328. Wapelelezi 22 walipata mafunzo katika nchi za Marekani, Misri, Nigeria na Botswana.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi pia limepata vifaa vya kisasa kwa ajili ya kufanya uchunguzi wa kisayansi katika maabara iliyopo Makao Makuu ya Polisi. Vifaa hivyo vitaimarisha ung'amuzi wa wahalifu, ukaguzi na ukusanyaji wa vielelezo na ushahidi kwenye matukio makubwa ya uhalifu.

Mheshimiwa Spika, aidha, mchakato wa kuikabidhi Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kazi za kuendesha mashtaka Mahakamani umeendelea. Hadi sasa mchakato huo umekamilika katika Mahakama za Hakimu Mkazi na Mahakama za Wilaya katika Mikoa 22 ya Kipolisi Tanzania Bara na Mikoa mitano ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, lengo la nne, ni kuanzisha mpango wa kuwapatia askari nyumba bora za kuishi. Kutokana na mahitaji makubwa ya rasilimali fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za makazi ya askari nchi nzima, Jeshi la Polisi limeanza utekelezaji wa mpango wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi (*PPP*) ili kupunguza ukubwa wa tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, kwa kuanzia Jeshi la Polisi limeingia ubia wa kujengewa nyumba 350 katika Mkao wa Polisi Kinondoni kuanzia mwaka wa fedha wa 2013/2014. Utaratibu uliofuatwa katika Mkao wa Kinondoni utatumika kupunguza tatizo la makazi ya askari katika Mikoa yote nchini.

Mheshimiwa Spika, Mkakati wa muda mrefu ni kujenga nyumba za gharama nafuu kwa kutumia Shirika la Uzalishaji Mali (*Corporation Sole*) la Jeshi la Polisi ambalo uanzishwaji wake utakamilika hivi karibuni. Kwa sasa tumekamilisha ujenzi wa maghorofa 90 yaliyotoa nafasi ya makazi bora kwa askari 360 pamoja na familia zao. Jeshi la Polisi litaendelea kutumia fedha za bajeti ya maendeleo kujenga nyumba za askari kadri uwezo utakavyoruhusu.

Mheshimiwa Spika, lengo la tano ni kujenga vituo vya Polisi katika kila Tarafa nchini. Mikakati ya kupunguza tatizo la makazi itatumika pia kupeleka huduma ya polisi karibu na wananchi kwa kujenga Vituo vya Polisi katika kila Tarafa. Kutokana na mahitaji makubwa ya rasilimali, fedha kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Polisi, Jeshi la Polisi litatumia Shirika la Uzalishaji Mali litakaloanzishwa na mfumo wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi kujenga vituo vya Tarafa kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Jeshi la Polisi litaendeleza

utekelezaji wa Polisi Jamii kwa kuwatumia Wakaguzi 526 wa Tarafa na askari Kata kutoa huduma za Polisi kwa kutumia vituo vilivyopo karibu na Tarafa zisizo na Vituo vya Polisi hasa maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, lengo la sita, ni kuwapatia wananchi mafunzo ya Ulinzi Shirikishi ili wawe tayari kujilinda katika maeneo yao. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imeanzisha kampeni mahsus ya kuhamasisha Wizara, Idara na Taasisi mbalimbali za Serikali kuzingatia ukweli kwamba zinao wajibu wa kujenga miundombinu ya amani katika ngazi za Mikoa, Wilaya, Tarafa na Kata kwa kutumia sheria na taratibu zilizopo.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi limeendelea kuwatumia Wakaguzi wa Tarafa/Jimbo na Askari Kata/Shehia kuwaelimisha wananchi kwamba, kila mmoja anawajibika kwa ulinzi wake binafsi, familia yake, jirani yake na jamii kwa ujumla tofauti na fikra potofu za baadhi ya watu kwamba, usalama wa raia na mali zao ni jukumu la Jeshi la Polisi na viongozi wa Serikali pekee.

Mheshimiwa Spika, lengo la saba, ni kuimarisha mafunzo ya askari wa vyombo vya ulinzi na usalama. Katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2012 askari 12,276 kutoka Polisi, Magereza, Zimamoto na Uokoaji na Uhamiaji wamepatiwa mafunzo katika fani mbalimbali ambapo Polisi ni 9,407, Magereza 2,413, Zimamoto na Uokoaji 72 na Uhamiaji 384. Mwaka 2013/2014, mafunzo yatatolewa kwa jumla ya askari 32,957 ambapo Polisi ni 30,000, Magereza 2,307 na Uhamiaji 650.

Mheshimiwa Spika, lengo la nane, ni kuimarisha uzalishaji wa mbegu bora za kilimo katika maeneo ya Magereza. Katika mwaka 2012/2013, Jeshi la Magereza kwa kushirikiana na Wakala wa Mbegu za Kilimo nchini katika Mikoa ya Arusha, Dodoma, Manyara, Lindi, Iringa, Mbeya, Kilimanjaro na Morogoro na vile vile kwa kushirikiana na Kampuni ya *Highland Seed Growers Limited* na *TANSEED*

katika Mikoa ya Rukwa, Ruvuma na Kigoma kwa ujumla imelima hekta 990.2 za mashamba ya mbegu bora za kilimo na matarajio ni kuvuna tani 2,000 za mbegu bora.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Jeshi la Magereza linatarajia kuhudumia hekta 3,175 za mazao mbalimbali kwa mategemeo ya kupata mavuno ya tani 4,500 iwapo hali ya hewa itakuwa nzuri.

Mheshimiwa Spika, lengo la tisa ni kutoa vitambulisho vya Taifa. Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (*NIDA*) ina jukumu la kusimamia mfumo wa utambuzi na usajili wa watu pamoja na utoaji wa vitambulisho vya Taifa kwa Watanzania, wageni wakaazi na wakimbizi wanaostahili. Huu ni mfumo mpya ambao utakuwa na manufaa kwa Taifa katika nyanja za kiuchumi, kijamii na kiusalama.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete alizindua mfumo wa utambuzi na usajili wa watu hapo tarehe 7 Februari, 2013, Jijini Dar es Salaam. Tukio la uzinduzi liliambatana na Mheshimiwa Rais kukabidhiwa kitambulisho cha kwanza cha Taifa katika historia ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, hili ni jambo jema linalohitaji Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa nchini kupongezwa. Aidha, vitambulisho vilitolewa pia kwa vikundi mbalimbali vinavyowakilisha jamii na viongozi Wakuu wa Kitaifa wakiwemo Marais wastaafu, Mawaziri Wakuu wastaafu, Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, hatua inayofuata ni kuendelea kutoa vitambulisho vya Taifa kwa wafanyakazi wa Wizara, Idara na Wakala wa Serikali wa Mkoa wa Dar es Salaam na Zanzibar pamoja na vyombo vya ulinzi na usalama wapatao

290,000, wakaazi 220,000 wa Wilaya ya Kilombero Mkoani Morogoro, wakaazi 2,159,182 wa Mkoa wa Dar es Salaam na wakaazi 165,825 wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwataarifu Watanzania wote kupitia Bunge lako Tukufu kwamba zoezi la utoaji wa vitambulisho vya Taifa ni endelevu ambalo litafanyika katika Mikoa na Wilaya zote za Tanzania Bara na Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kwa vile zoezi hili haliendeshwi kwa kuzingatia misingi ya itikadi za kisasa, kidini au kikabila, natoa rai kwamba, sote tuweke mbele suala la uzalendo na kutoa ushirikiano wa dhati kwa *NIDA* katika kufanikisha utoaji wa vitambulisho hivi kwa maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, lengo la kumi, ni kuimarisha Vikosi vya Zimamoto na Uokoaji vyenye wataalam na zana za kisasa ili kukabiliana na majanga ya moto. Katika kipindi cha mwezi Julai hadi Desemba 2012 askari wa Zimamoto na Uokoaji 72 wamepatiwa mafunzo. Kati yao 12 wamepatiwa mafunzo nje ya nchi ya uokozi kwenye maji (7) na majengo marefu (5) na askari 60 wamepatiwa mafunzo ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Jeshi pia limepata msaada kutoka Ujerumani wa kompyuta 100 na vifaa vya kinga ya moto. Ili kusogeza huduma za zimamoto na uokoaji karibu na wananchi, ujenzi wa kituo cha Zimamoto na Uokoaji eneo la Mwenge, Dar es Salaam unaendelea.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2012/2013 na malengo ya mwaka 2013/2014. Katika mwaka 2012/2013, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ilipangija kukusanya mapato ya sh. 96,449,327,801/=. Hadi tarehe 28 Februari, 2013, Wizara ilikuwa imekusanya sh. 76,990,955,792/=, sawa na asilimia 79.8 ya lengo la mwaka.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Wizara ina lengo la kukusanya mapato ya sh. 145,024,760,000/=. Nguvu zaidi zitaelekezwa katika kuziba mianya ya uvujaji wa

mapato hususan katika kuimarisha na kuboresha matumizi ya benki kwa ajili ya kufanya malipo ya huduma zitolewazo na taasisi za Wizara.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara iliidhinishiwa kutumia sh. 555,540,268,000/= kwa ajili ya bajeti ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Februari, 2013 jumla ya sh. 337,534,661,068/= zilikuwa zimetumika sawa na asilimia 60.8 ya bajeti ya mwaka mzima kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sh. 178,838,875,099/= zimetumika kulipia mishahara, Matumizi Mengineyo yalikuwa ni kiasi cha sh. 148,977,021,516/= na fedha za maendeleo zilikuwa kiasi cha sh. 9,718,764,453. Katika mwaka 2013/2014, Wizara imetengewa sh. 741,131,711,000/= kwa ajili ya bajeti ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi; kama niliviotangulia kusema hapo awali kwamba amani, utulivu na usalama wa nchi yetu ni mihimili mikuu ya maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa kwa wananchi wetu. Kuongezeka kwa tishio la uhalifu, fujo, migogoro na kuzorota kwa usalama wa raia huathiri mfumo mzima wa ustawi wa nchi katika maeneo hayo matatu na kwa ujumla hudhoofisha nguvu za wananchi katika kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi Tanzania ndilo lenye jukumu la kuhakikisha amani, utulivu na usalama vinakuwepo wakati wote kwa kuweka mazingira salama kwa wananchi, kuendesha shughuli za kujiletea maendeleo yao na wakati huo huo kuvutia wawekezaji wa ndani na nje, kuwekeza mitaji yao katika sekta za kiuchumi kwa faida ya maendeleo ya nchi yetu. Pamoja na ukweli huo, mafanikio ya hatua za Polisi yanategemea mashirikiano ya jamii na mtu mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, kuzuia na kudhibiti vitendo vya uhalifu na ajali za barabarani. Katika mwaka 2012/2013, Jeshi

la Polisi liliendelea kutekeleza jukumu lake la kisheria la kuhakikisha usalama, amani na utulivu vinakuwepo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto zilizojitokeza, Jeshi la Polisi lilifanikiwa kwa kiasi kikubwa katika kuwalinda wananchi na mali zao, kusimamia utii wa sheria za nchi, kuzuia makosa ya jinai na usalama barabarani, kupeleleza makosa ya jinai, kuwakamata na kuwafikisha Mahakamani watuhumiwa wa makosa ya jinai na makosa ya usalama barabarani.

Mheshimiwa Spika, mafanikio haya yanathibitishwa na kupungua kwa makosa makubwa ya jinai yakiwemo mauaji na unyang'anyi wa kutumia silaha kwa kiwango cha asilimia 4.3 na kupungua kwa ajali za barabarani kwa asilimia 1.9.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Jeshi la Polisi limejipanga kuimarisha doria, misako na operesheni maalum ili kupunguza matishio ya uhalifu, makosa makubwa ya jinai na ajali za barabarani kwa kiwango cha asilimia kumi.

Mheshimiwa Spika, Programu ya Maboresho ya Jeshi la Polisi. Katika mwaka 2012/2013, Jeshi la Polisi liliendelea kutumia fedha za bajeti zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kuimarisha mifumo ya kubaini, kuzuia na kutanzua uhalifu na makosa ya usalama barabarani na kuongeza matumizi ya TEHAMA katika kazi za Polisi.

Mheshimiwa Spika, pia Jeshi la Polisi liliendelea kuimarisha mifumo ya menejimenti ya rasilimali watu na ustawi wa askari kijamii na kiuchumi, kuandaa mikakati mipya ya kupunguza tatizo la uhaba na uchakavu wa kambi na vituo vya Polisi, kupunguza tatizo la uhaba wa vitendea kazi hususan magari na pikipiki na kuhamasisha wananchi na wadau wa usalama wa raia kuhusu Ulinzi Shirikishi na Utii wa Sheria Bila Shuruti.

Mheshimiwa Spika, napenda kulifahamisha Bunge

Iako Tukufu kuwa, kama sehemu ya utekelezaji wa Programu ya Maboresho, Jeshi la Polisi limeanza utekelezaji wa mfumo wa kupima kiwango cha ufanisi wa Maafisa, Wakaguzi na askari kwa kutumia mkataba wa utendaji (*Performance Contract*) uliosainiwa kati ya mtendaji mmoja mmoja na kiongozi wake wa kazi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Jeshi la Polisi litapima ufanisi wa utendaji kwa ngazi ya Mkoa/Kikosi, Wilaya, Tarafa/Jimbo na Kata/Shehia na litaendelea kutekeleza malengo na shabaha zilizomo katika maeneo saba ya maboresho kama yalivyo dhinishwa na Baraza la Mawaziri mnamo tarehe 31 Machi, 2011.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa kupunguza uhalifu unaotumiwa pia na majeshi mengine ya Polisi duniani umelisa idia Jeshi la Polisi nchini kubaini, kuzuia na kudhibiti uhalifu na wahalifu kwa kiwango kikubwa katika mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, Mkakati huo unaelekeza mbinu na hatua zinazotakiwa kuchukuliwa kabla uhalifu haujatendeka, baada ya uhalifu kutendeka, mshtakiwa anapofikishwa Mahakamani na ufuutiliaji wa wahalifu wa kawaida na wahalifu wazoefu baada ya kumalizika kwa kesi zao Mahakamani. Matumizi ya mbinu hizi yanahusisha ushirikiano wa karibu kati ya Jeshi la Polisi na vyombo vinavyounda Jukwaa la Haki Jinai pamoja na raia wema.

Mheshimiwa Spika, mionganoni mwa mbinu zinazotumika kuzuia uhalifu kabla haujatendeka ni pamoja na kutambua maeneo hatarishi ambayo uhalifu hutendeka mara kwa mara na kuongeza doria ya askari Polisi na vikundi vyta ulinzi shirkishi katika maeneo hayo na kufuatilia nyendo za wahalifu wazoefu mara wanapomaliza kutumikia adhabu gerezani.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Jeshi la

Polisi litaendelea kutumia mkakati wa kupunguza uhalifu ili kila Mkoa wa Kipolisi ufikie shabaha ya kupunguza uhalifu kwa asilimia kumi.

Mheshimiwa Spika, mauaji ya wazee na vikongwe kwa imani za kishirikina. Kumekuwa na wimbi la mauaji ya wazee na vikongwe hasa katika Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Tabora, Mbeya, Rukwa, Iringa na Singida.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2011 hadi 2012, takwimu za Jeshi la Polisi zinaonesha kwamba jumla ya wazee na vikongwe 1,271 waliuawa katika Mikoa hiyo kutokana na imani za kishirikina. Kati ya idadi hiyo, wanaume walikuwa 532 sawa na asilimia 41.9 na wanawake 739 sawa na asilimia 58.1. Serikali inalaani kwa nguvu zake zote mauaji haya ya wazee na imani za kishirikina katika karne hii ya 21.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na hali hiyo, Jeshi la Polisi limeweka mikakati ifuatayo:-

(i) Kuendelea kuwahamasisha wananchi kutekeleza kwa vitendo falsafa ya Polisi Jamii na Ulinzi Shirikishi kama mkakati mkuu wa kuzuia uhalifu katika maeneo wanayoishi;

(ii) Kuendelea kushirikiana na raia wema, Mamlaka za Serikali za Mitaa na taasisi zinazoratibu shughuli za waganga wa jadi kuwabaini, kuwakamata na kuwafikisha Mahakamani waganga wanaothibitika kupiga ramli za uchochezi na kusababisha mauaji ya wazee na vikongwe;

(iii) Kuendelea kushirikiana na raia wema na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwabaini, kuwakamata na kuwafikisha Mahakamani wahalifu wanaokodishwa kufanya mauaji ya wazee na vikongwe;

(iv) Kuendelea kutumia taarifa za kiintelijensia kuwabaini, kuwakamata na kuwafikisha Mahakamani

wanaotuhumiwa kutoa fedha kwa waganga wa jadi kwa lengo la kuambiwa waliowaua ndugu zao au kupewa mbinu na masharti ya kupata utajiri wa haraka;

(v) Kuendelea kukiimarisha Kitengo cha Intelijensia cha Jeshi la Polisi kwa rasilimali watu na vitendea kazi kuanzia ngazi ya Makao Makuu hadi ngazi ya Kata/Shehia ili kujenga uwezo wa kupata mapema taarifa za uhalifu Mijini na Vijiijini; na

(vi) Kuendelea kutumia Vikosi Kazi vya Kitaifa, Mikoa na Wilaya kuendesha operesheni maalum za kuzuia na kudhibiti ongezeko la mauaji ya wazee na vikongwe katika Mikoa iliyokithiri kwa mauaji hayo.

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa Watanzania wote kushirikiana na Serikali kukomesha mauaji, hofu na unyanyasajji kwa wazee.

Mheshimiwa Spika, Huduma za Polisi katika Tarafa/Jimbo, Kata/Shehia na Maeneo Maalum ya Uwekezaji. Idadi ya watu na mahitaji ya huduma ya usalama wa raia na mali zao yanazidi kuongezeka kila mwaka hususan kwenye ngazi ya Tarafa/Jimbo, Kata/Shehia na maeneo mapya ya makazi na uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Jeshi la Polisi lilinunua pikipiki 564 kwa ajili ya kuimarisha utendaji kazi wa Wakaguzi wa Tarafa kwa Tanzania Bara na Majimbo kwa Zanzibar. Aidha, vitengo vipyta vilivyoanzishwa Makao Makuu ya Polisi kwa ajili ya kuratibu usalama katika migodi, ulinzi wa mazingira na usalama wa watalii vilianza kazi rasmi kwa kupatiwa watendaji hadi ngazi ya Kituo cha Polisi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Jeshi la Polisi litaongeza idadi ya askari katika Kata/Shehia ambazo ni tishio kwa uhalifu na kununua pikipiki kwa ajili ya kuimarisha doria na misako katika Kata/Shehia hizo.

Mheshimiwa Spika, kuongeza matumizi ya *TEHAMA*

katika kazi za Polisi. Mabadiliko ya mbinu za kutenda uhalifu na maendeleo ya Sayansi na Teknolojia duniani ni changamoto kwa Jeshi la Polisi hivyo matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ni ya lazima ili kuongeza uwezo wa Jeshi la Polisi kubaini na kutanzua uhalifu nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Jeshi la Polisi limeajiri wataalam 355 wa fani ya *TEHAMA* ambao wanaendelea na mafunzo ya awali ya uaskari katika Chuo cha Taaluma ya Polisi Moshi. Mfumo wa kisasa wa kuchukua alama za vidole za watuhumiwa (*Automated Fingerprints Information System - AFIS*) umeendelea kusimikwa katika vituo vya Polisi.

Mheshimiwa Spika, aidha, Mkandarasi atakayesimika mfumo wa ufuatilaji wa washtakiwa (*Offender Management Information System - OMIS*) ameanza kazi za awali katika Mkoa wa Dar es Salaam na Makao Makuu ya Idara ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Jeshi la Polisi litawapanga askari wapya wenye fani ya *TEHAMA* kufanya kazi katika Mikoa yote nchini na litaendelea kutekeleza awamu zinazofuata za miradi ya *AFIS* na *OMIS* kwa mujibu wa mikataba na uwezo wa kibajeti.

Mheshimiwa Spika, Jukwaa la Haki Jinai; katika mwaka 2012/2013, ushirikiano wa kuitendaji kati ya Jeshi la Polisi na taasisi nyingine zinazounda Jukwaa la Haki Jinai ambazo ni Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Jeshi la Magereza na Mahakama uliendelea kuimarka. Viongozi wa Taasisi hizo walishiriki katika Mkutano Mkuu wa Maafisa Waandamizi wa Polisi uliofanyika Mjini Dodoma mwezi Februari 2013 na kuweka mikakati ya pamoja ya kuimarisha utoaji wa haki hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi lilijikita katika eneo la kuongeza ufanisi katika upelelezi wa makosa ya jinai na hivyo kufanikiwa kuongeza kiwango cha washtakiwa kupatikana na hatia kutoka asilimia tano mwaka 2011 hadi

asilimia 11.6 mwaka 2012. Katika mwaka 2013/2014, Jeshi la Polisi litaanza rasmi kutumia mitihani ya kupima ujuzi ili kujenga na kuongeza weledi wa askari wake katika fani za Intelijensia na upelelezi.

Mheshimiwa Spika, udhibiti wa uzagaaji wa silaha ndogondogo; Jeshi la Polisi liliendelea kuweka alama maalum katika silaha ndogo ndogo zinazomilikiwa na taasisi za Serikali, makampuni na watu binafsi kwa lengo la kudhibiti uzagaaji wa silaha na matumizi ya silaha hizo katika uhalifu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2012 hadi Februari, 2013, jumla ya silaha 15,003 zimebekewa alama hiyo, hivyo, kufanya jumla ya silaha 52,607 zilizowekewa alama hiyo tangu zoezi hili liliopoanza mwaka 2009. Hadi sasa zoezi la kuweka alama kwenye silaha limefanyika katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Dodoma, Tanga, Dar es Salaam, Morogoro, Tabora, Manyara, Singida, Mwanza, Shinyanga, Kagera na Mara.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ambazo silaha zao zimebekewa alama maalum ni pamoja na Tanzania *National Parks Authority (TANAPA)*, *Barrick Gold*, *Bank of Tanzania (BoT)*, *Grumet Games Reserves* na *Ngorongoro Conservation Area Authority (NCAA)*. Katika mwaka 2013/2014, zoezi hilo litaendelea kutekelezwa na sheria mpya ya kusimamia na kudhibiti umiliki na utumiaji wa silaha za kiraia inatarajiwaa kuanza kutumika.

Mheshimiwa Spika, ushirikiano wa Polisi Kikanda na Kimataifa. Katika mwaka 2012/2013, Jeshi la Polisi liliishiriki katika mafunzo, ubadilishanaji wa taarifa za kiintelijensia, operesheni za kikanda na lilikuwa mwenyeji wa vikao vya Kamati na Mkutano Mkuu wa Shirikisho la Wakuu wa Polisi wa nchi za Kusini mwa Afrika (*SARPCCO*) ambavyo vilifanyika Zanzibar na Dar es Salaam mwezi Septemba 2012 na Machi, 2013.

Mheshimiwa Spika, kwa mpangilio huo, Jeshi la Polisi liliendelea kushirikiana na Mashirika ya Polisi ya Kikanda na

Kimataifa katika kubaini, kuzuia na kutanzua uhalifu hapa nchini. Mashirika hayo ni pamoja na Shirikisho la Polisi la Kimataifa – *Interpol*, Shirikisho la Polisi la Nchi za Afrika Mashariki na Pembe ya Afrika – *EAPCCO* na Shirikisho la Polisi la Nchi za Kusini mwa Afrika *SARPCCO*.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Jeshi la Polisi litaendelea kushirikiana na majeshi mengine ya Polisi Kikanda na Kimataifa ili kuimarisha udhibiti wa makosa yanayovuka mipaka ukiwemo ugaidi, uharamia, biashara ya dawa za kulevyta, biashara haramu ya kusafirisha binadamu, uhamiaji haramu, wizi wa magari, wizi wa kutumia mitandao ya *TEHAMA*, bidhaa bandia, biashara haramu ya silaha na uchafuzi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, kuimarisha mifumo ya menejimenti ya rasilimaliwatu; katika mwaka 2012/2013, jumla ya askari 3,024 walajiriwa na 5,637 wa vyeo mbalimbali walihudhuria mafunzo na kupandishwa vyeo. Mafunzo ya upandishwaji vyeo yalifanyika kama ifuatavyo:-

Uofisa (200), Ugaguzi mdogo (597), *RSM* (47), Sajini Taji (404), Sajini (882) na Koplo (3,502). Aidha, Inspeksa Jenerali wa Polisi alihamisha Maafisa, Wakaguzi na askari wapatao 540 kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utendaji katika komandi za Jeshi la Polisi nchini na kuziba nafasi zilizoachwa wazi kutokana na Maafisa na askari kwenda nje ya nchi kushiriki katika Ulinzi wa Amani.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Jeshi la Polisi litaajiri askari wapya 3,000 na kuwapandisha vyeo, jumla ya askari 7,110 wakiwemo *NCO* wenye elimu ya shahada ya kwanza na shahada ya uzamili. Pia Jeshi la Polisi litaendelea kuwaruhusu Maafisa, Wakaguzi na askari kufanya mitihani maalum inayowawezesha kushiriki katika Operesheni za Ulinzi wa Amani ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, jumla ya Maafisa watano wamesimamishwa kazi, 12 mashtaka ya

kijeshi yanaendelea dhidi yao na wengine 28 wameandikiwa barua za kujieleza kwa nini wasishtakiwe kijeshi kutokana na makosa mbalimbali ya kinidhamu.

Mheshimiwa Spika, ushughulikiaji wa malalamiko; Jeshi la Polisi limeendelea kupokea na kushughulikia malalamiko ya wananchi dhidi ya watendaji wachache wanaojihusisha na vitendo vya ukiukwaji wa maadili ikiwemo kuomba na kupokea rushwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012 malalamiko yaliyopokelewa yalikuwa 314 ikilinganishwa na malalamiko 340 yaliyopokelewa mwaka 2011. Malalamiko ya wananchi dhidi ya Jeshi la Polisi yalikuwa 193 na 121 yalikuwa ni madai ya askari kuhusu stahiki zao mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, malalamiko 213 kati ya 314 yamejibwa na kupatiwa ufumbuzi. Kutokana na ushughulikiaji wa malalamiko mbalimbali ya ukiukwaji wa maadili askari 99 walishtakiwa kijeshi na kufukuzwa kazi na mwingine mmoja amesimamishwa kazi kutokana na kukiuka maadili ya ajira ndani ya Jeshi la Polisi, hali iliyosababisha askari wanafunzi 95 kutopokelewa kuanza mafunzo katika Chuo cha Polisi Moshi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho askari 13 walitunukiwa sifa na zawadi ya jumla ya sh. 7,540,000/= kwa kukataa kupokea rushwa. Askari hao ni wa Mikoa ya Iringa, Kilimanjaro, Lindi, Manyara, Rukwa, Shinyanga, Temeke na Kaskazini Pemba.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Jeshi la Polisi litaendelea kusimamia nidhamu na maadili ya Maafisa, Wakaguzi na askari wake ikiwa ni pamoja na kutoa ufumbuzi wa haraka wa malalamiko ya wananchi dhidi ya Jeshi la Polisi. Jeshi litaendelea pia kutekeleza Programu ya Kupambana na Rushwa nchini inayofadhiliwa na Shirika la Misaada la Uingereza (*DFID*).

Mheshimiwa Spika, kuimarisha miundombinu na

vitendea kazi vya Polisi; Katika mwaka 2012/2013, Jeshi la Polisi liliendeleza ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Idara ya Upelelezi Dar es Salaam, kuanza hatua za awali za kusimika mfumo wa *OMIS* na kukamilisha awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mradi wa kuimarisha usalama wa mizigo na huduma zinazosafirishwa kuititia barabara kuu za Tanzania hususan barabara kuu ya Dar es Salaam hadi Rusumo.

Mheshimiwa Spika, Miradi ya maendeleo yenye thamani ya shilingi bilioni 10.1 haikuendelezwa kutokana na ufinyu wa bajeti ya maendeleo. Aidha, taratibu za kisheria za kuanzisha Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Polisi (*Police Force Corporation Sole*) zimekamilika.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Jeshi la Polisi litaendeleza ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Idara ya Upelelezi, Kituo cha Polisi Vikoktoni, kukamilisha ujenzi wa nyumba za askari katika Mikoa ya Mwanza, Kagera, Mara na Iringa na kuendeleza miradi ya *AFIS* na *OMIS*. Kuhusu vitendea kazi Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inakamilisha taratibu za kupata magari ya aina mbalimbali kwa ajili ya kazi za Jeshi la Polisi kuititia ushirikiano uliopo kati ya Tanzania na Serikali ya Watu wa China na India.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Magereza; usafirishaji wa Mahabusu kwenda Mahakamani na kurudi Magerezani. Jukumu la kuwasindikiza mahabusu kwenda Mahakamani na kurudi Gerezani linaendelea kutekelezwa katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani. Hivi karibuni jukumu hili limeanza kutekelezwa katika Mkoa wa Arusha na Mkoa wa Dodoma katika Wilaya tatu za Dodoma Mjini, Dodoma Vijijini na Mpwapwa.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu umeonesha mafanikio katika suala zima la kupunguza msongamano wa mahabusu Magerezani kwa sababu mahabusu hufikishwa Mahakamani kwa tarehe walizopangiwa na Mahakama ambapo wengine huachiliwa kwa dhamana au kesi zao kufutwa na nyininge kumalizika kwa mujibu wa sheria. Lengo

la mwaka 2013/2014, ni kutekeleza jukumu hili katika Wilaya za Mkoa wa Dodoma zitakazokuwa zimesalia na kuanza katika Mkoa wa Mwanza.

Mheshimiwa Spika, Programu za urekebishaji wa wafungwa. Mradi wa uendeshaji wa shughuli za wafungwa kwa kutumia mtandao wa kompyuta kwa awamu ya pili unaendelea baada ya awamu ya kwanza kukamilika. Utekelezaji wa awamu ya pili umeanza kwa kusimika miundombinu katika Magereza ya Butimba – Mwanza, Uyui - Tabora na ofisi za Magereza katika Mikoa hiyo.

Mheshimiwa Spika, kazi kama hiyo inatarajiwu kufanyika katika ofisi ya Magereza Mikoa wa Dodoma, Gereza Kuu la Isanga na Msalato. Kwa ujumla mfumo huu umesaidia kujenga uwezo wa Jeshi la Magereza katika upatikanaji wa taarifa za wahalifu zilizo sahihi na kwa wakati, kujua maendeleo na mwenendo mzima wa wahalifu katika maeneo mbalimbali yaliyounganishwa katika mfumo huu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Jeshi la Magereza litaendelea na awamu ya pili ya utekelezaji wa mpango huu kwa Mikoa mingine mitatu ambayo itaanzia na vituo vya Magereza Makuu ya Ruanda - Mbeya, Maweni – Tanga na Arusha kisha kumalizia ofisi za Magereza katika Mikoa ya Mbeya, Tanga na Arusha.

Mheshimiwa Spika, ajira na mafunzo; kibali cha kuajiri askari wapya 1,000 kimepatikana na mchakato wa ajira umeanza. Jumla ya watumishi 2,413 wamepatiwa mafunzo. Katika mwaka 2013/2014, Jeshi la Magereza linatarajia kuajiri askari wapya 1,020 na watumishi raia 15 wa fani mbalimbali na kuwapatia mafunzo watumishi 520 nje ya Vyuo vya Jeshi la Magereza na askari 1,787 ndani ya vyuo vya Jeshi.

Mheshimiwa Spika, uimarishaji wa magereza yenye ulinzi mkali. Ukarabati na uboreshaji wa majengo na miundombinu ya Magereza yenye ulinzi mkali umefanyika na unaendelea katika Gereza la Butimba sehemu za wanawake, kiwanda na mahabusu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, ukarabati wa majengo na miundombinu utaendelea chini ya Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria nchini (*LSRP*) katika Sehemu ya Wanawake ya Magereza ya Ruanda – Mbeya, Karanga – Kilimanjaro, Musoma – Mara, Isanga – Dodoma na Lilungu – Mtwara.

Mheshimiwa Spika, upanuzi, ukamilishaji, ukarabati na ujenzi wa mabweni ya Wafungwa. Kazi ya ujenzi wa mabweni ya wafungwa katika Gereza la Wilaya ya Chato unaendelea. Ukarabati wa ukuta wa ngome, upanuzi wa sehemu ya wanawake na kuezeka upya mabweni ya wafungwa iliendelea katika Magereza ya Kilwa na Bukoba.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, lengo ni kuanza kazi ya ukarabati wa mabweni ya wafungwa katika Gereza la Mahabusu Sumbawanga na kuendeleza ujenzi wa mabweni mapya katika Gereza la Mkusa – Pwani.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Ofisi za Wakuu wa Magereza wa Mikoa. Katika mwaka 2012/2013, Jeshi la Magereza limeendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa Ofisi ya Magereza, Mkoa wa Singida na ujenzi wa Ofisi ya Magereza, Mkoa wa Dar es Salaam. Katika mwaka 2013/2014, Jeshi litakamilisha ujenzi wa Ofisi ya Magereza, Mkoa wa Singida, kuendeleza ujenzi wa Ofisi ya Magereza, Mkoa wa Dar es Salaam na kuanza ujenzi wa Ofisi ya Magereza, Mkoa wa Tanga.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya nishati mbadala magerezani; katika kukabiliana na changamoto zinazotokana na matumizi makubwa ya kuni Magerezani na hivyo kuwepo na tishio la uharibifu wa mazingira, Jeshi la Magereza limeendelea kuchukua hatua za kuanza kutumia gesi asilia (*natural gas*), gesi itokanayo na tungamotaka (*biogas*) na makaa ya mawe kama nishati mbadala kwa kupikia chakula cha wafungwa Magerezani.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa gesi itokanayo na

tungamotaka katika Gereza la Ukonga umekamilika na umeanza kutumika. Matumizi ya makaa ya mawe yanaendelea katika Magereza ya Mkoa wa Mbeya. Kwa sasa Jeshi la Magereza lipo katika mchakato wa kutumia majiko yanayotumia kuni kidogo ambayo yameanza kutumika katika Gereza Karanga – Moshi na Ilagala – Kigoma. Matarajio ni kueneza matumizi ya nishati hii katika Magereza mengine yenye matumizi makubwa ya kuni kadri uwezo wa fedha utakavyoruhusu.

Mheshimiwa Spika, ujenzi na ukamilishaji wa nyumba za askari. Jeshi la Magereza limekamilisha ujenzi wa jengo la ghorofa la kuishi askari Mkoani Iringa na limeanza kutumika. Aidha, Jeshi linaendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa nyumba zilizojengwa kwa njia ya ubunifu katika Magereza ya Ngara, Kasulu, King'ang'a, Mwanga, Masasi, Ngudu, Kenegole, Nzega na Kambi ya Bugorola.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Jeshi la Magereza litaendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa nyumba katika Magereza ya Butimba, Karanga na Mugumu. Aidha, nyumba zilizojengwa kwa ubunifu wa askari ambazo zipo katika hatua mbalimbali, pia zitaendelea kupewa kipaumbele katika ukamilishaji wake.

Mheshimiwa Spika, uimarishaji wa mifumo ya Majisafi na Majitaka. Magereza yaliyo mengi yanakabiliwa na tatizo la ukosefu wa maji na uchakavu wa miundombinu ya majisafi na majitaka ambayo pia inaelemewa na tatizo kubwa la msongamano wa wafungwa na mahabusu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, ujenzi wa miundombinu ya majisafi umeendelea katika Gereza Isupilo, Iringa na ujenzi wa mfumo wa majitaka unaendelea katika Gereza Mkwaya, Mbinga. Katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, lengo ni kukarabati mfumo wa majitaka na kuboresha mfumo wa majisafi katika Gereza Kuu Isanga.

Mheshimiwa Spika, kilimo cha umwagiliaji. Jeshi la

Magereza liliendelea na mchakato wa ujenzi wa miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji katika Gereza la Idete – Morogoro. Hatua mbalimbali za kufanya tathmini ya athari za mazingira na usanifu wa michoro kwa ajili ya mradi huo zimekamilika. Aidha, taratibu za kumpata Mkandarasi wa ujenzi zinaendelea. Katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Jeshi la Magereza litaanza mchakato wa mradi wa umwagiliaji katika Gereza Kitengule, Kagera uwezo wa fedha ukiruhusu.

Mheshimiwa Spika, ununuzi wa magari na zana za kilimo. Katika kutekeleza bajeti ya mwaka 2012/2013, Jeshi la Magereza halikuweza kununua matrekta kutokana na ukosefu wa fedha. Malengo kwa mwaka 2013/2014, ni kuendelea kuyafanyia matengenezo matrekta yaliyopo pamoja na zana zake.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika kuboresha huduma ya usafiri na usafirishaji Magerezani, Jeshi la Magereza linatarajia kununua magari madogo matatu kwa ajili ya shughuli za utawala.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Magereza limeendelea na uzalishaji wa bidhaa zitokanazo na viwanda vidogo vidogo kwa kutengeneza samani za ofisi na bidhaa za ngozi kwa ajili ya taasisi na Idara za Serikali na watu binafsi. Kwa upande wa kilimo, eneo la ekari 6,400 limelimwa kwa matarajio ya kuvuna tani 8,640 za mazao mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, vile vile Shirika kupitia Kikosi Ujenzi cha Magereza limeendelea kufanya kazi za ujenzi wa majengo ya taasisi za Serikali na watu binafsi. Kazi hizo ni pamoja na ujenzi wa uazio wa Makao Makuu ya Wizara ya Maliasili na Utalii, ukarabati wa majengo ya Idara ya Uhamiaji Mkoani Tanga, ujenzi wa *Rest House* ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na ujenzi wa mfumo wa majitaka, Baraza la Mitihani la Taifa.

Mheshimiwa Spika, matarajio ya mwaka 2013/2014, ni kuongeza shughuli za uzalishaji kupitia miradi ya kilimo,

mifugo na kutumia ipasavyo soko la samani za ofisi, bidhaa za ngozi na shughuli za ujenzi ambalo linaendelea kupanuka.

Mheshimiwa Spika, Programu ya huduma kwa jamii ilianza rasmi mwaka 2005 kama adhabu mbadala ya kifungo gerezani. Hivi sasa programu hii inatekelezwa katika Mikoa 16 ya Tanzania Bara ambayo ni Dar es Salaam, Mwanza, Mtwara, Dodoma, Mbeya, Kilimanjaro, Tanga, Arusha, Iringa, Kagera, Mara, Shinyanga, Ruvuma, Pwani, Geita na Morogoro. Katika kipindi cha Julai, 2012 hadi Februari, 2013 jumla ya wafungwa 903 wamefaidika na programu hii.

Mheshimiwa Spika, wafungwa hao hutumikia vifungo vyao nje ya magereza kwa kufanya kazi bila ya malipo katika taasisi za umma. Changamoto kubwa ya programu hii ni Mikoa mingine kushindwa kunufaika nayo kutokana na ufinyu wa bajeti, uhaba wa Maofisa wa Probesheni na baadhi ya Mahakimu kujikita katika kutoa adhabu ya kifungo gerezani badala ya kutumia adhabu mbadala.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Uhamiaji ina jukumu la kudhibiti uingiaji, utokaji na ukaaji wa wageni na pia kuwawezesha raia wa Tanzania kupata hati za kusafiria. Aidha, Idara hii ndio inayoratibu mchakato wa maombi ya uraia wa Tanzania kwa wageni.

Mheshimiwa Spika, hali ya ulinzi na usalama mipakani; katika kipindi cha Julai, 2012 hadi Februari, 2013 Idara iliendelea kutoa huduma katika mipaka kwa wageni wanaoingia na kutoka nchini. Katika kipindi hicho, jumla ya wageni 801,676 wалиingia na wengine 729,078 walitoka.

Mheshimiwa Spika, kiujumla hali ya mipaka ni shwari na idadi ya Wasomali na Waethiopia wanaosafirishwa kwenda Kusini mwa Afrika kwa makundi imepungua kufikia 627 mwaka 2012 ikilinganishwa na 1,424 katika kipindi kama hiki mwaka 2011. Aidha, huduma zilizotolewa na Idara ya Uhamiaji.

Mheshimiwa Spika, tatizo la wahamiaji haramu; Idara

ya Uhamiaji imeendelea kupambana na tatizo la wahamiaji haramu nchini. Tatizo hili linatokana na sababu za kihistoria kama kuwepo kwa masalia ya wapigania uhuru wa Nchi za Kusini mwa Afrika, wakimbizi hususan wale wa muda mrefu walitoroka toka makambi ya wakimbizi pamoja na kundi la wahamiaji haramu hususan kutoka nchi za Pembe ya Afrika kama Somalia, Ethiopia na Eritrea, ambalo lilianza kujitokeza mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, kundi hili la raia toka Pembe ya Afrika linakuwa kubwa kutokana na mtandao wa usafirishaji unaoendesha biashara haramu ya binadamu. Mtandao huo huanzia nchi wanazotoka hadi kule wanakoelekea Kusini mwa Afrika kupitia hapa nchini na kuendesha biashara hii kwa kupata kipato.

Mheshimiwa Spika, kundi hili linawajumuisha wahanga wa biashara haramu ya usafirishaji binadamu (*victims of human trafficking*) na raia wa kigeni wanaohiari wenyewe kusafirishwa na mawakala haramu kuelekea nchi nyingine bila kufuata taratibu zilizowekwa (*smuggled persons*). Makundi yote haya kwa ujumla yanatengeneza kundi moja la wahamiaji haramu ambalo kwa sasa ni tatizo la Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2012 hadi Februari, 2013 Idara ya Uhamiaji illendelea kufanya doria na misako yenye lengo la kudhibiti wahamiaji haramu nchini ambapo jumla wahamiaji haramu 2,319 walikamatwa na kuchukuliwa hatua mbalimbali za kisheria, ikilinganishwa na wahamiaji haramu 5,603 waliokamatwa katika kipindi kama hiki mwaka jana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wahamiaji walitoroka na masalia ya wapigania uhuru pamoja na wakimbizi walitoroka makambini, Serikali imeamua kwa kuushirikisha uongozi wa Mikoa husika kufanya operesheni ya kuwabaini na kuwaondosha wahamiaji haramu hao.

Mheshimiwa Spika, Mikoa ambayo itahusika na zoezi hilo ni Kagera, Kigoma, Rukwa na Mara kwa upande wa

Kaskazini na Magharibi mwa nchi yetu. Operesheni hii pia itafanyika katika Mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma kwa upande wa Kusini.

Mheshimiwa Spika, katika kupambana na tatizo linalokua la usafirishaji wa binadamu, Serikali imebainisha biashara hii kuwa ni moja ya uhalifu mkubwa wa Kimataifa (*Serious Crime*). Serikali imeanzisha Kikosi Kazi kinachopambana na wasafirishaji wa biashara hii haramu. Hadi sasa Serikali imekamata na kutaifisha vyombo vya usafiri vinavyotumiwa na wasafishaji hao.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tatizo hili linazigusa nchi mbalimbali katika ukanda wanakotoka, wanakopitia na kule wanakoishia wahamiaji haramu, Serikali imefanya juhud ya kuwa na vikao vya pamoja na nchi hizo ili kutengeneza mikakati itakayowezesha kupata suluhisho la pamoja katika kukabiliana na tatizo la wahamiaji haramu.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Uhamiaji pia imeendelea kukabiliana na tatizo hili kwa kufanya yafuatayo:-

Kuendelea kushirikiana na nchi jirani kwa kufanya mikutano ya ujirani mwema ya mara kwa mara pamoja na kuingia makubaliano ya kufanya misako na kupeana taarifa ya biashara haramu ya binadamu na wahuksika kuchukuliwa hatua, kuendelea na zoezi la kuwaorodhesha wahamiaji walowezi ili kuwatambua na kuwa na kumbukumbu sahihi.

Kushirikisha wadau wengine wa masuala ya Uhamiaji katika zoezi la kuwaondosha nchini wahamiaji haramu waliokamatwa, kuendeleza mfumo wa Maafisa Uhamiaji Kata kwa lengo la kushirikiana kwa karibu zaidi na jamii katika kutekeleza sheria ya Serikali za Mitaa ya kumtaka kila mwenyeji kutoa taarifa ya mgeni yeoyote anayeingia au kuishi mahali popote ugenini na kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu madhara ya kuwahifadhi na kuwapa kazi wahamiaji haramu bila kuwa na vibali halali.

Mheshimiwa Spika, vibali mbalimbali vilivyotolewa

kwa wageni. Idara imetoea vibali kwa wageni wawekezaji, wageni waliopata ajira katika makampuni na wageni wengine walioingia nchini kwa malengo mbalimbali. Jumla ya wageni 12,878 walipewa hati za ukaazi kwa mchangano ufuatao:- daraja "A" 1,191, daraja "B" 7,037, daraja "C" 2,571, hati za ufuasi 297 na hati za msamaha 1,782. Hati za msamaha ni vibali vya kuishi vinavyotolewa kwa wageni bila malipo yoyote.

Mheshimiwa Spika, wageni hao ni wale wanaofanya kazi katika Taasisi za Kimataifa zilizoko nchini (*International Organizations*), Wawakilishi wa nchi pamoja na wafanyakazi katika Ofisi za Balozi mbalimbali hapa nchini pamoja na wategemezi wao, wanafunzi toka nchi wanachama wa Jumuia ya Afrika Mashariki na nchi nyingine, pamoja na wageni toka nchi Washirika wa Maendeleo wanaofanya kazi katika Mashirika ya Umma, Asasi za Kiserikali au katika sekta mbalimbali Serikalini.

Mheshimiwa Spika, hati za kusafiria; Idara imetoea jumla ya hati za kusafiria 31,347 kwa Watanzania waliotaka kusafiri nje ya nchi kwa madhumuni mbalimbali. Kati ya hati hizo 30,202 ni za kawaida, 818 za Afrika Mashariki, 212 za Kibalozi na 115 za kiutumishi. Aidha, kukua kwa hali ya utandawazi kumesababisha kubadilika kwa teknolojia ya udhibiti wa pasipoti na hati nyingine za safari.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mabadiliko hayo, Idara ya Uhamiaji imeanza mchakato wa kupata mitambo mipya ya kuchapisha hati za safari itakayokuwa na uwezo wa kutoa hati zenye *Biometric Features* ili kuepuka tatizo la pasipoti za Tanzania kughushwa kirahisi.

Mheshimiwa Spika, wageni waliopatiwa uraia wa Tanzania; katika kipindi cha Julai, 2012 hadi Februari, 2013 wageni 64 walipatiwa uraia. Wageni waliopata uraia ni wa kutoka India (27), Kenya (7), Uingereza (2), Pakistani (5), Somalia (1), Japan (1), Lebanon (6), Malawi (1), Burundi (6), Rwanda (1), Uganda (4), DRC (1), China (1) na Umoja wa Falme za Kiarabu (1). Hivi sasa Wizara ya Mambo ya Ndani

ya Nchi inaendelea kuandaa Sera ya Uhamiaji na Uraia ili kushughulikia masuala ya uhamiaji na uraia nchini kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Watanzania waliopatiwa uraia wa Mataifa mengine. Katika kipindi hiki Watanzania 37 walipata uraia wa Mataifa mengine kama ifuatavyo:- Uingereza (1), Ujeruman (9), Norway (14), Uganda (2), Uholanzi (1), Denmark (3), Namibia (5) na Zambia (2) hivyo kupoteza haki ya kuwa raia wa Tanzania kwa mujibu wa Sheria ya Uraia Na. 6 ya mwaka 1995.

Mheshimiwa Spika, Wasomali waliovuliwa uraia; Serikali imekuwa ikiwapa raia wa kigeni uraia wa Tanzania wageni wakaazi walioomba na kukubaliwa baada ya kukidhi vigezo vilivyowekwa kwa mujibu wa sheria ya uraia. Hata hivyo, kutohana na baadhi yao kutokuwa waaminifu, kama Waziri mwenye dhamana kwa mamlaka niliyonayo chini ya kifungu Na. 15(1) cha Sheria ya Uraia Na. 6 ya mwaka 1995, nilifuta uraia wa Tanzania kwa watu 102, raia wa Somalia (wakimbizi) walikuwa wamepewa uraia wa Tanzania kwa tajnisi baada ya kuthibitika kwamba, waliwasilisha taarifa na vielelezo visivyo kuwa sahihi wakati wanaomba uraia.

Mheshimiwa Spika, hivyo kuanzia tarehe 6 Julai, 2012 wahusika wote walipoteza uraia wa Tanzania na wanatakiwa kuishi nchini kwa mujibu wa Sheria ya Uhamiaji Na. 7 ya mwaka 1995 na Sheria ya Wakimbizi Na. 8 ya mwaka 1998.

Mheshimiwa Spika, ajira na mafunzo. Watumishi wapya 52 wameajiriwa na wengine 385 walioko kazini wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi na mrefu. Kati yao tisa wamepata mafunzo ya muda mfupi nje ya nchi, mmoja mafunzo ya muda mrefu nje ya nchi, 324 wamepata mafunzo ya muda mfupi ndani ya nchi na 51 walipatiwa mafunzo ya muda mrefu ndani ya nchi. Katika mwaka 2013/2014, Idara inatarajia kutoa mafunzo kwa watumishi 650 waliopo kazini.

Mheshimiwa Spika, vyombo vyatuzi; Idara imenunua jumla ya magari 34 ambapo magari 10 ni aina ya

Toyota Landcruiser Hardtop na 24 Toyota Hilux Pickup. Aidha, imenunua mabasi madogo matatu (3) na pikipiki 100. Katika mwaka 2013/2014, Idara ya Uhamiaji inatarajia kununua magari 12, pikipiki 56, boti za doria tano na lori moja. Vyombo hivi vya usafiri vitasaidia kuimarisha shughuli za misako na doria dhidi ya wahamiaji haramu katika sehemu mbalimbali nchini zikiwemo zile za mipakani.

Mheshimiwa Spika, majengo ya ofisi; Idara imekamilisha ujenzi wa ofisi za Uhamiaji katika Mikoa ya Shinyanga na Morogoro. Aidha, ujenzi wa ofisi za Uhamiaji katika Mikoa ya Ruvuma na Manyara unaendelea na mchakato wa kuwapata Wakandarasi wa ujenzi wa ofisi za Uhamiaji katika Mikoa ya Pwani, Lindi na Singida umeanza.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, Idara inatarajia kuanza ujenzi wa ofisi mpya katika Mikoa ya Mtwara na Geita, ofisi ya Wilaya ya Ifakara, Mkoani Morogoro na Kituo cha Kirongwe, Mkoani Mara. Idara pia itaendelea na ukarabati wa ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Mbeya.

Mheshimiwa Spika, makazi ya askari; katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Idara imenunua maghorofa mawili Mkoani Tabora kwa ajili ya makazi ya askari yenye uwezo wa kuishi familia 12 pamoja na nyumba tano za Maafisa Uhamiaji zenye uwezo wa kuishi familia tano. Aidha, ujenzi wa nyumba tano za viongozi wa Idara ya Uhamiaji Makao Makuu unaendelea Mtoni Kijichi – Dar es Salam. Katika mwaka 2013/2014, Idara itaanza ujenzi wa nyumba za askari Kisongo Jijini Arusha na Chakechake, Pemba.

Mheshimiwa Spika, Idara imekamilisha ukarabati wa nyumba za askari Igoma - Mwanza na pia ukarabati unaendelea katika vituo vya Horohoro – Tanga, Borogonja – Mara, Tunduma – Mbeya, Tanga Mjini, Dodoma Mjini na mabweni ya Chuo cha Uhamiaji cha Kikanda Moshi. Katika mwaka 2013/2014, Idara inatarajia kufanya ukarabati wa nyumba za askari zilizoko Mtoni Kijichi – Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, mapambano dhidi ya VVU/

UKIMWI; Idara ya Uhamiaji imeendelea kutoa elimu pamoja na kuwahudumia watumishi wanaoishi na VVU/UKIMWI kwa lengo la kupunguza maambukizo mapya ya UKIMWI mahali pa kazi na kwa familia za askari. Aidha, Idara imesambaza vipeperushi katika vituo vya kuingilia nchini vinavyolenga kutoa elimu juu ya maambukizo ya VVU na UKIMWI pamoja na athari zake.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Zimamoto na Ukoaji; katika kutekeleza majukumu yake, limeendelea kuokoa maisha na mali kwenye majanga ya moto na majanga mengineyo yanayolikumba Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majukumu haya ya msingi, katika kipindi cha Julai, 2012 hadi Februari, 2013, jumla ya maeneo 5,149 yalifanyiwa ukaguzi wa kinga na tahadhari ya moto. Pia jumla ya magari makubwa na madogo 6,455,447 yalikaguliwa. Huduma hii inatolewa kwa mujibu wa Sheria ya Zimamoto na Uokoaji Na. 14 ya mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limefanikiwa kuwapatia mafunzo askari 72, ndani ya nchi askari 60 na nje ya nchi 12. Katika mwaka 2013/2014, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji litaendelea na zoezi la ukaguzi wa kinga na tahadhari ya moto, kuendelea kutoa elimu juu ya kinga na tahadhari ya moto kwenye maeneo mbalimbali, na litaendelea kuimarisha huduma zake kwa kujenga vituo vya Zimamoto na Uokoaji kwenye maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Wakimbizi; Serikali iliendelea na jitihada mbalimbali zenye lengo la kulipatia ufumbuzi wa kudumu tatizo la kuwepo maelfu ya wakimbizi hapa nchini, ambao baadhi yao walikuwa wanasita kurejea kwenye nchi zao za asili pamoja na kuwa hali ya usalama katika nchi hizo ilikuwa imeimarika vya kutosha.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na tatizo hilo niliwavua hadhi ya ukimbizi, kwa mujibu wa sheria, wakimbizi

wa Burundi wapatao 38,000 na kuwataka kurejea kwenye nchi yao ya asili na wale ambao wangekataa kutekeleza agizo hilo wangechukuliwa hatua.

Mheshimiwa Spika, uamuzi huo uliwezesha raia wa Burundi wapatao 35,000 waliokuwa wanaishi kwenye kambi ya Mtabila Wilayani Kasulu, Mkoani Kigoma kurejea nchini Burundi kwa kusaidiwa na Mashirika ya Umoja wa Mataifa ya UNHCR na *International Organization for Migration (IOM)* na kuwezesha kambi hiyo kufungwa rasmi tarehe 31/12/2012, kama tulivyolahidi Bunge katika bajeti iliyopita. Hivi sasa UNHCR wanafanya ukarabati wa miundombinu ya kambi hiyo ili eneo la kambi likabidhiwe rasmi kwa uongozi wa Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Spika, baada ya kufunga kambi ya Mtabila, kwa sasa Tanzania inayo kambi moja tu ya Nyarugusu, Wilayani Kasulu ambayo inahifadhi wakimbizi kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC). Pamoja na kwamba hali ya usalama katika Majimbo ya Kivu Kaskazini na Kusini nchini DRC ambako wakimbizi hao wanatoka bado sio ya kuridhisha. Tunaamini kuwa yapo baadhi ya maeneo katika Majimbo hayo ambayo hali ya usalama inaridhisha ambapo wakimbizi wa DRC wanaweza kuanza kurejea huko.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hali hiyo, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Tanzania inakusudia kuitisha Kikao cha Pande Tatu kitakachojumuisha Serikali ya Tanzania, Serikali ya DRC na UNHCR ili kukubaliana namna ya kuwapa fursa wakimbizi wanaotoka maeneo ya Kivu Kaskazini na Kusini kurejea nchini kwao bila ya kikwazo chochote. Aidha, katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2012 wakimbizi 96 wa DRC walirejea kwao. Lengo pia ni kuwezesha wakimbizi wote wa kambi ya Nyarugusu kurejea kwao na kambi hiyo kufungwa.

Mheshimiwa Spika, vile vile Serikali imeendelea na mchakato wa kutoa uraia kwa wakimbizi wa Somalia wa

makazi ya Chogo yaliyopo Wilayani Handeni ambao wametimiza sifa na masharti yaliyowekwa. Lengo ni kufunga makazi hayo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada hizo zilizofanya idadi ya wakimbizi kupungua, Tanzania imeendelea kuwahifadhi wakimbizi ambapo takwimu zinaonesha kuwa hadi tarehe 31 Desemba, 2012 ilikuwa inahifadhi jumla ya wakimbizi 100,489 wakiwemo Warundi 35,343, Wakongo 63,330, Wasomali 1,574 na 242 wakimbizi wa Mataifa mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, lipo kundi maalum la wakimbizi wa Burundi wapatao 162,000 walioingia nchini mwaka 1972 ambao wanaishi kwenye makazi ya Katumba na Mishamo, Mkoani Katavi na Ulyankulu, Mkoani Tabora ambapo Serikali ipo kwenye mchakato maalum wa kupata ufumbuzi wa kudumu wa hadhi yao.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (*NIDA*) imeajiri watumishi 89, imenunua vitendea kazi muhimu vya ofisi vikiwemo vifaa vya elektroniki na kuendelea na ukarabati wa ofisi katika Mkoa wa Dar es Salaam na Zanzibar. Aidha, NIDA imempata Mkandarasi wa kujenga ofisi za utambuzi na usajili za Wilaya zote nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/2014, NIDA itaendelea na zoezi la utambuzi na usajili wa watu, kuajiri watumishi 542, kununua magari 20, kuendelea kuweka mfumo wa mawasiliano kati ya ofisi za Wilaya na Makao Makuu ya NIDA, kuendelea na uboreshaji wa upanuzi wa Makao Makuu ya *NIDA* na kukamilisha mchakato wa kutunga Sheria ya Usajili na Utambuzi wa Watu.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa ahadi zilizotolewa na Serikali Bungeni katika mwaka 2012/2013, umezingatiwa katika hotuba hii katika eneo la III -Taarifa ya utekelezaji wa malengo ya llani ya Uchaguzi na la IV - Mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, ahadi hizo zipo katika maeneo ya vitendea kazi, ajira na mafunzo, misako na doria, ujenzi na ukarabati wa ofisi, vituo, nyumba na magereza, zoezi la utambuzi na usajili wa watu, kuwarejesha wakimbizi kwao na kuweka alama maalum katika silaha zinazomilikiwa na taasisi za Serikali, makampuni na watu binafsi.

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani zangu za dhati kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Anna Margaret Abdallah, Mbunge Viti Maalum, kwa kuyapitia na kuyachambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Maelekezo na ushauri wa Kamati hiyo utaisaidia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, shukrani za pekee nazitoa kwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Pereira Ame Silima, Mbunge wa Chumbuni; Katibu Mkuu, Ndugu Mbarak Abdulwakil; Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Mwamini Malemi; Inspekta Jenerali wa Polisi, Ndugu Saidi Mwema; Kamishna Jenerali wa Magereza, Ndugu John Minja; Kamishna Jenerali wa Zimamoto na Uokoaji, Ndugu Pius Nyambacha na Kamishna Mkuu wa Uhamiaji, Ndugu Magnus Ulungi.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa, Ndugu Dickson Maimu; Mkurugenzi wa Wakimbizi, Ndugu Judith Mtawali; Mkurugenzi wa Huduma kwa Jamii, Ndugu Fidelis Mboya; Wakuu wote wa Idara na Vitengo, Makamanda, askari pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, ambao wamefanikisha maandalizi ya hotuba hii na pia kwa kusaidia kufanikisha majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, nachukua pia fursa hii kuwashukuru nchi wahisani ikiwemo China, Marekani, Ujerumani, Misri, Botswana, Nigeria na taasisi za *INTERPOL, IOM, EU, UNHCR, DFID, UNICEF, WFP, Hanns Seidel Foundation*

na *Pharm Access* pamoja na wadau wengine wote kwa misaada yao ambayo imeongeza uwezo wa kiutendaji katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ingawa sio mwisho kwa umuhimu, nawashukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete na Makamu wa Rais, Dkt. Mohamed Gharib Bilal kwa maelekezo yao mbalimbali na Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, Waziri Mkuu kwa kuhimiza utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipitishe Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2013/2014 ya sh. 741,131,711,000/= kwa ajili ya bajeti ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo.

Kati ya makadirio hayo, sh. 578,284,694,000/= ni za matumizi ya kawaida ambapo sh. 271,572,291,000/= ni matumizi mengineyo na mishahara sh. 306,712,403,000/=. Makadirio ya sh. 162,847,017,000/= ni kwa ajili ya mipango ya maendeleo. Mchanganuo ni kama ifuatavyo:-

Fungu 14 - Jeshi la Zimamoto na Uokoaji: matumizi mengineyo ni sh. 18,610,590,000/=. mishahara sh. 1,812,194,000/= na fungu la maendeleo halikutengewa fedha. Jumla ni sh. 20,422,784,000/=.

Fungu 28 - Jeshi la Polisi: matumizi mengineyo sh. 149,600,221,000/=. mishahara sh. 205,663,241,000/= na fungu la maendeleo sh. 8,980,451,000/=. Jumla yake ni sh.364,243,913,000/=.

Fungu 29 - Jeshi la Magereza: matumizi mengineyo sh. 53,510,022,000/=. mishahara sh. 72,758,378,000/= na maendeleo sh. 2,666,566,000. Jumla ni sh. 128,934,966,000/=.

Fungu 51 - Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi:

matumizi mengineyo sh. 2,107,467,000/=, mishahara sh. 2,711,513,000/= na fungu la maendeleo halikutengewa fedha. Jumla ni sh. 4,818,980,000/=.

Fungu 93 - Idara ya Uhamiaji: matumizi mengineyo sh. 47,743,991,000/=, mishahara sh. 23,767,077,000/ na maendeleo sh. 151,200,000,000/=. Jumla ni sh. 222,711,068,000/=.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuniskiliza.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:
Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

SPIKA: Hoja hiyo imeungwa mkono. Sasa nitamwita Mwenyekiti ambaye Kamati yake ilishughulikia Wizara hii, kwa niaba yake Mheshimiwa Masele.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE (K.n.y. MHE. ANNA MARGARETH ABDALLAH - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ULINZI NA USALAMA): Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni Na 99(9) na 117(11), Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili 2013, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inahusisha Mafungu sita, Fungu 51 – Wizara ya Mambo ya Ndani; Fungu 93-Idara ya Uhamiaji; Fungu 28 – Jeshi la Polisi; Fungu 29 - Jeshi la Magereza na Fungu 14 – Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ilikutana tarehe 26 Machi, 2013 hadi tarehe 5 Aprili, 2013 na kupitia taarifa ya utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani, kwa Mwaka 2012/2013 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2013/2014. Katika kikao hicho, Waziri alieleza kuhusu utekelezaji wa maoni na ushauri wa iliyokuwa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa mwaka fedha 2012/2013. Wakati wa Kuchambua Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa fedha 2012/2013, iliyokuwa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ilitoa maoni na ushauri katika maeneo mbalimbali. Napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kuwa ushauri wa Kamati hiyo ulizingatiwa na kufanyiwa kazi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kupunguza msongamano wa Wafungwa na Mahabusu Magerezani. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na:-

(i) Kutolewa elimu kwa jamii kuhusu haki ya dhamana kwa Watuhumiwa.

(ii) Kamati za Kusukuma kesi (*Case Flow Management Committee*) zilifanya kazi zake za kusukuma kesi zilizokaa muda mrefu mahakamani.

(iii) Jeshi la Magereza linaifahamisha Mahakama Kuu kila mwezi idadi ya Mahabusu waliokaa Gerezani zaidi ya siku 60.

(iv) Serikali imeunda Kikosi Kazi chini ya Uenyekiti wa Mkurugenzi wa Mashtaka ili kushughulikia tatizo la msongamano Magerezani na kutoa mapendeleko ya hatua za kuchukuliwa.

(v) Mheshimiwa Rais alitoa msamaha kwa wafungwa 3,814 tarehe 9 Desemba, 2012. Aidha, tarehe 26 Aprili, alitoa tena msamaha kwa wafungwa 4,000.

(vi) Kupitia utaratibu wa *extra mural labour*, wafungwa 387 walipewa Kifungo cha nje na wafungwa 818 waliachiliwa kwa Sheria ya Huduma kwa Jamii.

Mheshimiwa Spika, pili, Serikali ilimarishe Jeshi la Magereza katika uzalishaji na utekelezaji wa majukumu mengine kwa kulipatia vitendea kazi vya Kisasa. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na Jeshi la Magereza kuanzisha mashamba mapya 17 katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Iringa, Mbeya, Rukwa, Ruvuma na Kigoma.

Mheshimiwa Spika, tatu, Serikali iifanyie kazi changamoto za Idara ya Uhamiaji kukosa mawasiliano madhubuti ya mtandao wa kompyuta unaouunganisha Makao Makuu ya Uhamiaji, Dar es Salaam, Ofisi Kuu – Zanzibar, Mikoa, Wilaya na Vituo vya Mipakani.

Mheshimiwa Spika, hatua zilizochukuliwa ni pamoja kuweka Mfumo wa Mawasiliano ya *Internet* kuunganisha Ofisi za Uhamiaji Mikoani na baadhi ya Vituo vya mipakani (*Boarder Posts*) umeanzishwa. Katika mfumo huo, njia ya kuwasiliana kwa *e-mail* na mtandao wa njia binafsi na salama wa kupitishia taarifa za aina mbalimbali – *Virtual Private Network (VPN)* *hutumika*.

Mheshimiwa Spika, nne, Idara ya Uhamiaji iwezeshwe kukabiliana na changamoto ya uhaba na uchakavu wa majengo na vitendea kazi na kuimarisha misako na doria. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na:-

- (i) Kukamilisha upanuzi wa Ofisi Kuu Zanzibar.
- (ii) Kukamilisha Ujenzi wa Ofisi za Uhamiaji katika Mikoa ya Shinyanga na Morogoro.
- (iii) Kuendeleza Ujenzi wa Ofisi za Uhamiaji katika Mikoa ya Ruvuma na Manyara.
- (iv) Kukarabati Ofisi ya Mkoa Rukwa na Nyumba za Watumishi.

(v) Kuendeleza Ukarabati wa nyumba za Makazi katika Mkoa wa Pwani na Kituo cha Sirari.

Mheshimiwa Spika, tano, Idara ya Uhamiaji iimarishe misako na doria. Yafutayo yamefanyika:-

(i) Ili kufanikisha misako na doria, mchakato wa ununuzi wa magari 34, pikipiki 100 na Mabasi matatu (3) umekamilika. Vyombo hivyo vya usafiri vitasaidia kupunguza uhaba wa vitendea kazi katika kuendesha misako na doria.

(ii) Kazi ya upembuzi yakinifu imeanza ili kupata mfumo bora wa utoaji wa huduma za vibali vya wageni kupitia mfumo wa Kieletroniki (*e-immigration*). Mfumo huu utasaidia kudhibiti uingiaji na utokaji wa wageni nchini.

Mheshimiwa Spika, sita, kuhusu kasi ya kukamillisha Sera ya Uhamiaji. Rasimu ya mwisho ya sera ya Uhamiaji, iliyozingatia maoni ya mwisho ya Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, imeperekwa Zanzibar kwa uhakiki wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, saba, katika mwaka wa Fedha 2013/2014, Serikali iongeze fedha za maendeleo kwa Fungu 14 – Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Kwa masikitiko makubwa, Kamati imebaini kuwa Serikali haijatenga fedha za maendeleo kwa ajili ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa mwaka wa Fedha 2012/2013 na 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, nane, uandaliwe utaratibu mzuri wa kuliwezesha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kufanya ukaguzi wa tahadhari na kinga ya moto kwa majengo yote ili kuzuia matukio ya moto. Taarifa ilionesa kuwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linaendelea kutoa ushauri kuhusu uwekaji wa vifaa vya kuzimia moto na elimu ya matumizi ya vifaa hivyo ili kudhibiti matukio ya moto. Aidha, utaratibu wa kufanya ukaguzi wa tahadhari ya kinga ya moto katika nyumba za mijini umeendela kufanyika.

Mheshimiwa Spika, tisa, uwekwe utaratibu wa kuzitaka

Taasisi zote zenyе mkusanyiko mkubwa wa watu kuhakikisha kuwa watumishi wake wanapata mafunzo ya Zimamoto na Uokoaji. Kamati ilijulishwa kuwa Jeshi la Zimamoto na uokoaji limeendelea kutoa elimu kwa Taasisi mbalimbali ili kusaidia kupunguza matukio ya moto. Aidha, Jeshi linaendelea kutoa elimu kwa umma kupitia vyombo vy ya habari.

Mheshimiwa Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati, baada ya kupitia taarifa ya utekelezaji na kuchambua makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Kamati inatoa maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mambo ya Ndani, Fungu 51:-

(i) Kutokana na uhaba wa ofisi za kufanya kazi, Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ilianzisha mradi wa ujenzi wa jengo la Makao Makuu na kukamilisha mradi huo katika mwaka wa Fedha 2011/2012. Baada ya kukamilika, Serikali iliamua jengo hilo litumiwe na Tume ya Mabadiliko ya Katiba. Hata hivyo, Serikali inapaswa kuamua deni la Sh. 666,056,704.00 linalotokana na hati namba 25 na deni la mwisho la mkandarasi (*retention*) la Sh. 608,324,057.00 litakavyolipwa, kwani katika mwaka wa fedha 2013/2014, mradi huu haujatengewa fedha za maendeleo. Ikumbukwe kuwa Serikali inapoteza fedha nyingi kutokana na adhabu ya kutokulipa kwa wakati fedha za wakandarasi wa miradi mbalimbali.

(ii) Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Sheria ya Huduma kwa Jamii Na. 6 ya Mwaka 2002, wahalifu wanaohukumiwa adhabu ya kifungo kisichozidi miaka mitatu wanapaswa kutumikia adhabu hiyo nje ya Magereza. Sheria hii inatakiwa kufanya kazi katika Mikoa yote ya Tanzania Bara, lakini hivi sasa inafanya kazi katika Mikoa 16. Idara hii licha ya kukabiliwa na changamoto nyingi katika kutekeleza majukumu yake katika hiyo Mikoa hiyo 16, Idara inatakiwa sasa kuanza kazi katika Mikoa iliyosalia.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa kiasi cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya kutekeleza jukumu hilo kwa mwaka wa fedha 2013/2014 hakitoshi kufanikisha jukumu hilo. Kamati inashauri Serikali iangalie uwezekano wa kuongeza bajeti itakayowezesha utaratibu wa kutumikia adhabu nje ya magereza kwa Mikoa yote Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi – Fungu 28:-

(i) Kamati inalipongeza Jeshi la Polisi kwa kufanya kazi zao kwa weledi japo katika mazingira magumu na changamoto nydingi. Miongoni mwa changamoto hizo zilizo dhahiri zaidi ni pamoja na bajeti isiyokidhi mahitaji hususan katika matumizi mengineyo. Katika majadiliano na Wizara ya Mambo ya Ndani, Kamati ilijulishwa wastani wa chini wa mahitaji ya Matumizi mengineyo (*OC*) kuendesha Mkoa mpya mmoja wa Kipolisi ni sh. 500,000,000.00.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati unaonesha kuwa kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Fungu 28 la Jeshi la Polisi lilitengewa na kuidhinishiwa sh. 133,600,221,000.00 wakati ambapo Mikoa ya Kipolisi ilikuwa 28 tu. Katika mwaka 2013/2014, fungu hilo limetengewa sh 149,600,221,000.00 kwa ajili ya Mikoa ya Kipolisi 33 iliyopo kwa sasa. Mikoa mipyä ya kipolisi ambayo imepatiwa kifungu (*Sub-Vote*) katika mwaka 2013/2014 ni Geita, Katavi, Njombe na Simiyu.

(ii) Mheshimiwa Spika, ili kuliwezesha Jeshi la Polisi kumudu majukumu yake ipasavyo, Jeshi hili liwezeshwé zaidi kifedha na vifaa kwa lengo la kuliwezesha kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake.

(iii) Mheshimiwa Spika, Askari Polisi anapokuwa kazini kwa saa 24 anatakiwa kupata mlo uliokamilika kuanzia asubuhi hadi jioni ili aweze kumudu kikamilifu majukumu ya ulinzi na usalama wa raia na mali zao. Utafiti uliofanyika kuhusu bei za vyakula katika soko kwa sasa unaonesha kwamba, kiasi cha fedha kinachotakiwa kwa mlo wa askari kwa siku ni Sh. 10,000.00 na kiwango cha chini ni sh. 7,500.00 wakati kiwango kinachotolewa kwa sasa ni sh. 5,000.00. Kamati

inashauri kuwa Serikali iangalie uwezekano wa kuongeza kiwango cha posho ya chakula kufikia angalau Sh. 7,500.00 kwa siku.

(iv) Mheshimiwa Spika, katika siku za hivi karibuni umezuka mtindo wa vikundi nya watu, Vyama nya Siasa au Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kufanya maandamano bila utaratibu wa kueleweka na hivyo kusababisha usumbu mionganoni mwa jamii ikiwa ni pamoja na shughuli za kijamii kusimama. Kamati inatambua haki ya kikatiba ya vikundi mbalimbali kujumuika bila kuvunja sheria. Hata hivyo, ni maoni ya Kamati kuwa Serikali iandae Muswada wa Sheria utakaoweka utaratibu wa kuandamana, siku za kuandamana, maeneo mahsus ya kukusanyika pamoja na muda wa kuandanma ili yejote anayependa kufanya hivyo, akamilishe haki yake hiyo pasipo kuingilia uhuru wa mtu mwingine. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Idara ya Uhamiaji Fungu 93:-

(i) Idara ya Uhamiaji ni moja ya Idara za Serikali zinazokusanya maduhuli ya Serikali. Bajeti ya matumizi mengineyo ya Idara hii hutegemea kwa asilimia mia moja gawio (*retention*) kutoka maoteo ya mapato kwa mwaka. Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Fungu 93 linategemea kukusanya jumla ya sh. 90,004,519,000.00 kiasi ambacho ni ongezeko la asilimia 29 ikilinganishwa na makadirio ya mapato kwa mwaka 2012/2013 ya sh. 70,003,523,000.00.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Idara ya Uhamiaji imetengewa gawio la asilimia 61. Hata hivyo, gawio hilo limepunguzwa hadi asilimia 47 kiasi ambacho ni sh. 42,743,991,000.00. Badiliko hilo litasababisha upungufu wa sh. 14,236,023,000.00 na hivyo kusababisha maeneo mengi kuathirika.

Mheshimiwa Spika, kutokana na athari hizo, Kamati inaishauri Serikali kuirudishia Idara ya Uhamiaji gawio la asilimia 61 kama ilivyokuwa mwanzo ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato na kusaidia miradi ya maendeleo waliyonayo.

(ii) Mheshimiwa Spika, moja ya majukumu ya Idara hii ni kuendesha operesheni maalum ya kuwaondosha wahamiaji haramu katika Mikoa ya mipakani. Mikoa hii inakabiliwa na idadi kubwa ya wahamiaji haramu kuititia nchi jirani. Kamati inashauri kuwa Serikali iangalie uwezekano wa kuiongezea fedha Idara hii ili kujengea uwezo wa kukabiliana na wimbi la wahamiaji haramu.

(iii) Mheshimiwa Spika, Kamati imepata Taarifa kwamba baadhi ya Vituo nje ya nchi kama vile Milano na Venice vilivyo nchini Italy, Nice nchini Ufaransa, Japan (Seksheni ya Australia) na kadhalika hawatumii mashine za *Visa Stickers* pamoja na kwamba mashine hizo wanazo na hivyo kuendelea na mfumo wa zamani wa kupiga mihuri kwenye hati za kusafiria. Kamati inaitaka Serikali kuchukua hatua za haraka na kuelekeza vituo vyote vitumie mashine za *Visa Stickers* kwani kutotumia mashine hizo kunainyima Serikali mapato inayostahili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa, lengo la Mamlaka hii ni kukamilisha zoezi la utoaji wa vitambulisho kabla ya mwisho wa mwaka 2014 ili vitambulisho hivyo viweze kusaidia Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika kuwatambua Watanzania wanaostahili kupiga kura.

Mheshimiwa Spika, ili lengo hilo litimizwe, Mamlaka inahitaji vifaa 5000 aina ya *Mobile enrollment unit (Biometric)* dhidi ya 200 ilivyonyavyo kwa sasa vinavyotumika kuchukua alama za kibaiolojia, yaani picha, alama za vidole na saini. Hata hivyo, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Mamlaka imetengewa kiasi cha sh. 151,200,000,000.00 ikilinganishwa na mahitaji halisi ya sh. 270,000,000,000.00. Ili kukamilisha zoezi muhimu la utoaji wa vitambulisho vya Taifa kabla ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, Kamati inaiomba Serikali kuongeza fedha zaidi katika kifungu 6501.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji - Fungu 14:-

(i) Ujenzi wa ofisi za Makao Makuu ya Jeshi la

Zimamoto na Uokoaji ulianza Agosti, 2010 na kutarajiwa kukamilika Novemba, 2011. Mradi huu ultarajiwa kugharimu jumla ya sh. 5,168,139,053.62. Hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa, katika mwaka wa fedha 2011/2012, 2012/2013 na hata 2013/2014, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji halikutengewa kabisa fedha za Miradi ya maendeleo, hivyo kupelekea kuchelewa kukamilika kwa Mradi huu.

Kwa kuzingatia kwamba mradi ni wa muda mrefu na kwa kuzingatia maelezo ya Waziri wa Fedha kwamba vipaumbele vya ulipaji madeni kwenye bajeti ya 2013/2014 vitazingatia madeni yaliyozalishwa kwa mwaka 2012/2013 na miaka ya nyuma, Kamati inashauri kuwa Jeshi la zimamoto na uokoaji liwezeshwe kukamilisha mradi huo.

(ii) Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa Fedha 2013/2014 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji walitegemea kupewa sh. 24,745,672,000.00 ambayo ni 70% ya sh. 35,350,960,000.00 kama makadirio ya Makusanyo kwa mwaka huo. Hata hivyo, Kamati imeelezwa kwamba, gawio hilo limepunguzwa hadi kufikia asilimia 49. Mategemeo ya Uhamiaji sasa ni Sh. 16,547,790,000.00 na hivyo kuwasababishia upungufu wa Sh. 8,197,882,000.00.

Kwa kuzingatia kwamba, Jeshi hili halijapewa fedha za maendeleo kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo na kwa kuzingatia kwamba fedha hizi ndizo zinazotumika kugharamia shughuli za uendeshaji pamoja na miradi ya maendeleo, Kamati inashauri kuwa, Serikali irudishe gawio la asilimia 70 kwa Fungu 14 ili kutekeleza malengo waliyojipangia hasa kukamilisha Jengo la Makao Makuu ya Zimamoto na Uokoaji.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kwamba Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ni sawa na majeshi mengine ambayo hayachukuliwi kama Idara za kuongeza mapato Serikalini, Serikali inatakiwa kuangalia uwezekano na umuhimu wa kurudisha gawio la asilimia mia moja kwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa miaka ijayo. Aidha, kwa kuwa Mkoa wa Dar es Salaam ndio uko katika hatari kubwa (*risk*) ya kukumbwa na majanga, Kamati inaiomba Serikali kuongeza fedha zaidi

katika Fungu 14 na hivyo kuwezesha ununuzi wa vifaa ambavyo vitasaidia shughuli za kuzima moto na uokozi hasa kwa Mkoa wa Dar es Salaam.

(iii) Mheshimiwa Spika, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limekuwa linafanya kazi katika mazingira magumu na pasipokuwa na vifaa vya kufanya kazi na hivyo kutotekeleza majukumu yao ipasavyo. Mfano mzuri ni tukio lilitotokea tarehe 29 Machi, 2013 Jijini Dar es Salaam ambapo jengo la ghorofa 16 liliporomoka. Jeshi la Zimamoto na Uokoaji halikuweza kutekeleza jukumu lake la uokozi kutokana na ukosefu wa vifaa vya kufanya kazi hiyo, badala yake nao walibaki kuwa watazamaji.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Magereza – Fungu 29:

(i) Kamati ilijulishwa kuwa kiasi kilichotengwa kwa mwaka wa fedha 2013/2014 kwa ajili ya gharama za chakula kwa wafungwa ni Sh. 8,240,219,000.00 sawa na sh. 500/= kwa mlo wa mfungwa mmoja kwa siku. Kiasi hiki ni kidogo mno. Kwa maoni ya Kamati, huu ni ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu.

Katika hali hiyo, mfungwa anapata adhabu mbili, moja ni adhabu ya kufungwa na nytingine ni adhabu ya kukosa chakula cha kutosha. Kamati ilielezwu kuwa, kiasi kilichokubaliwa kwa mlo wa mfungwa mmoja kwa siku ni sh. 3,000/=. Kamati inapendekeza kwamba kiasi hicho kiongezwe hadi kufikia angalau sh. 3,000/= kwa siku.

(ii) Mheshimiwa Spika, Kamati inaiomba Serikali itekeleza Sheria ya Huduma kwa Jamii na Sheria ya Majaribio na Ujenzi wa Tabia ambazo zinatoa nafasi kwa wahalifu wanaohukumiwa adhabu ya kifungo kisichozidi miaka mitatu kutumikia adhabu zao nje ya Magereza ili kupunguza gharama za kuwalisha Magerezani.

(iii) Mheshimiwa Spika, Kamati inaishukuru Serikali kwa kuanzisha maeneo mapya ya utawala ili kusogezza huduma kwa wananchi. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali

kujitahidi kujenga Vituo vya Polisi, Magereza na Mahakama katika maeneo hayo mapya hususan katika Wilaya na Mikoa mipyä inayoanzishwa kwani moja ya sababu kubwa ya msongamano wa mahabusu na wafungwa ni kukosekana kwa Magereza katika Wilaya mpyä na hivyo kulazimika kusafirisha wafungwa na mahabusu kwenda Wilaya nyingine na kusababisha gharama zaidi kwa Serikali.

(iv) Mheshimiwa Spika, Kamati imefuatilia na kubaini kwamba, kutotekeliza kwa Sheria ya *Parole* ni moja ya sababu nyingine inayosababisha msongamano wa mahabusu na wafungwa Magerezani. Kamati inaishauri Serikali kuharakisha mchakato wa kuleta Bungeni marekebisho ya sheria hiyo ili kupanua wigo (Kifungu cha 4 cha Sheria ya *Parole Board Act No. 25* na kufanyiwa marekebisho mwaka 2002) (*Act No. 5/2002*) na kuwahuishisha wafungwa wengi zaldi.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa jumla, wakati Kamati ilipokuwa inachambua bajeti za Wizara inazozisimamia ilibaini kuwa vyombo vya dola havishirikiani ipasavyo katika kutekeleza majukumu yake na katika kutumia nyenzo zilizopo. Kwa mfano, katika jukumu la ulinzi na doria majini, karibu vyombo vyote vya Ulinzi na Usalama kama vile Polisi, Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Kamandi ya Majini (*NAVY*), Uhamiaji na hata Uvuvi, vyote vinafanya doria majini na wote wana bajeti au maombi ya ununuzi wa boti za doria na mafuta.

Mheshimiwa Spika, Kamati inajuliza ni kwa nini vyombo vyote hivi visiunganishe nguvu na kuwa na ununuzi wa pamoja wa boti za doria au kutumia boti zilizopo za Jeshi la Wanamaji na wengine wakachangia mafuta? Kamati inaishauri Serikali kuangalia kwa makini suala hili na kuona ni jinsi gani nyenzo za doria zinaweza kutumiwa na wote badala ya mashindano ya kununua nyenzo hizo zinazofanana.

Mheshimiwa Spika, kwa kuhitimisha, napenda kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa nafasi hii muhimu kuwasilisha Maoni ya Kamati yangu. Aidha, napenda

kumshukuru kwa dhati, Mheshimiwa Emmanuel Nchimbi, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Mheshimiwa Pereira Ame Silima, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Makatibu Wakuu, Wakuu wa Taasisi, Idara, Vitengo na Maafisa wote, kwa maelezo yao ya kina na ushirikiano walioutoa wakati wote Kamati tulipochambua Makadirio ya Wizara hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Wabunge wote wanaonisikiliza na kipekee Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama pamoja na Sekretarieti yake, kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, uzoefu wao wa muda mrefu katika masuala mbalimbali kuhusu Sekta za Ulinzi na Usalama, umesaldia kufanikisha kazi hii kwa ufanisi. Aldha, napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa Taarifa hii inakamilika kwa wakati uliopangwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu, lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante. Sasa nimwite Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara hii.

MHE. VINCENT J. NYERERE – MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kutohana na muda nitaomba hotuba hii yote iingizwe na Idara ya Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*) kama iliviyowasilishwa mezani.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013; napenda

kuchukua fursa hii kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayoongozwa na CHADEMA, kuhusu mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya 2012/2013 na Makadirio ya Mapato na Matumizi katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, kufuatia shambulio la bomu katika Kanisa Katoliki, Kigango cha Olasiti, Jimbo Kuu Katoliki la Arusha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa salamu za rambirambi na pole nydingi kwa Kanisa Katoliki nchini na kwa familia za marehemu na majeruhi wa shambulio hilo. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inalaani kwa nguvu zote kitendo hicho cha kigaidi dhidi ya raia wasio na hatia waliokuwa katika ibada ya kumwabudu Mungu.

Mheshimiwa Spika, hii ni changamoto kubwa kwa Serikali ya CCM ambayo mara zote imekuwa ikishindwa kuzuia matukio ya kihalifu dhidi ya raia na mali zao, lakini imekuwa hodari kuzuia ukuaji wa demokrasia nchini kwa kuvikandamiza Vyama vya Upinzani na hasa CHADEMA. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani, inataka kuikumbusha Serikali na wananchi wote kwamba tarehe 24 Oktoba, 2012 Katibu wa BAKWATA, Mkoa wa Arusha Shekhe Abdulkarim Jonjo alilipuliwa kwa bomu nyumbani kwake eneo la Esso, Mjini Arusha na taarifa za uchunguzi wa tukio hilo bado hazifahamiki.

Mheshimiwa Spika, aidha, mwezi Novemba, 2012, Katibu wa Mufti wa Zanzibar, Sheik Fadhil Soraga, alimwagiwa tindikali na watu wasiojulikana na bado hakuna za uchunguzi juu ya watu waliohusika na uhalifu huo.

Mheshimiwa Spika, muda mfupi baadaye, Makanisa yalichomwa moto huko Zanzibar na Dar es Salaam na watu wasiojulikana na mpaka leo hakuna taarifa ya kuwashughulikia waliohusika na uhalifu huo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, jaribio lilitoshindwa la kumuua

Padre Ambrose Mkenda wa Kanisa Katoliki Zanzibar liliofanywa na watu wasiojulikana pia, ukichanganya na matukio ya kuchoma moto Makanisa na kushambuliwa kwa viongozi wengine wa dini tayari ilishatoa picha kwamba, viongozi wa dini na taasisi zao wanalengwa na mashambulizi ya kigaidi.

Mheshimiwa Spika, tukio la kuuawa kwa kupigwa risasi kwa Padre Evarist Mushi wa Kanisa Katoliki, Zanzibar tarehe 13 Februari, 2013 tayari Serikali ilikuwa inajua kwamba viongozi wa dini wanawindwa na magaidi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua ni kwa nini Serikali haikutoa ulinzi kwa viongozi wa dini wakati tayari ilijua kuwa viongozi wa dini ni walengwa wa mashambulio ya kigaidi?

Mheshimiwa Spika, baada ya mashambulio hayo kwa viongozi wa dini na Makanisa, Serikali ilijua kwamba, kuna makundi ya watu (magaidi) yanalenga Makanisa ili kuyachoma moto. Serikali haikutoa ulinzi kwa Makanisa, matokeo yake jana tarehe 5 Mei, 2013 Kanisa limelipuliwa kwa bomu huko Arusha.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua ni kwa nini mpaka leo Serikali haijatoa ulinzi kwa Makanisa ilhali inafahamu kwamba Makanisa yanalengwa na mashambulizi ya kigaidi? Aidha, Kambi Rasmi inataka Serikali itoe maelezo katika Bunge hili, inahitaji watu wangapi wauawe ndipo ichukue hatua?

Mheshimiwa Spika, ni hivi karibuni tu tarehe 22 Aprili, 2013, Jeshi la Polisi lilitoa angalizo kwamba, kuna dalili za kuibuka kwa *Al Qaeda* na *Al Shabab* nchini. Hata hivyo, mwezi mmoja haujapita, Kanisa limelipuliwa kwa bomu, Kambi Rasmi ya Upinzani inaliuliza Jeshi la Polisi, kama walikuwa na taarifa za kiintelijsancia kuhusu Ugaidi mbona hawakuchukua tahadhari?

Mheshimiwa Spika, kutokana na matukio haya ya

kigaidi yanayoendelea kushamiri katika nchi yetu na Serikali ikiwepo na kunya maza kimya bila kuchukua hatua za makusudi za kuyakomesha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili na wananchi wote kwa ujumla kama ina uhalali wa kuendelea kutawala ikiwa imeshindwa kuzuia matukio ya Kigaidi kama haya na ikiwa pia imeshindwa kuwachukulia hatua wale waliohusika na vitendo vya kigaidi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutafakari kwa kina jinsi ambavyo Serikali haithamini tena uhai na utu wa Mtanzania kwa kuangalia matukio ya mauaji na unyanyasaji wa kiimani ambaao una malengo ya moja kwa moja ya kuvunja amani na utulivu wa nchi yetu, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayoongozwa na CHADEMA, imeona kwamba, kuna haja ya kutafakari tena kama Taifa uzito wa jambo hili kwa kuwa ni muhimu kwa mustakabali wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, aidha Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kuchukua nafasi hii kuionya Serikali kuacha kufanya mzaha na amani ya nchi yetu, kwani kwa kutoshughulikia wahalifu wanaoivunja amani yetu ni sawasawa na kuivuja amani yenye moja kwa moja.

Kwa kutambua umuhimu wa amani na utulivu katika maendeleo ya Taifa, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kipindi hiki, itajielekeza kwenye mambo machache ya msingi ambayo ambayo yanatakiwa kufanyiwa kazi ili kujenga mustakabali bora wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayoongozwa na CHADEMA inapenda wananchi wote wajue kwamba, kamwe haitakaa kimya kwa udhalimu wowote dhidi ya raia wa Tanzania. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa angalizo kwa Serikali na wananchi wote kwamba, kama hatutasmama kidete kama Taifa kupinga kwa nguvu zote matukio yoyote yenye kuhatarisha usalama na uhai wa raia wa Taifa letu, kuna hatari kubwa ya matukio

haya kuzoleka na kuonekana kuwa ni ya kawaida. Hali hiyo itakapotokea, basi nchi itaingia katika machafuko makubwa kwani sheria za nchi zitakuwa zimeshindwa kuweka utaratibu katika nchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu haki ya kufanya mikutano ya siasa; kwa mujibu wa kifungu cha 4 cha Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge, Na. 3 ya mwaka 1988 (*The Parliamentary Immunities, Powers and Privileges Act*) Mbunge ana haki na uhuru wa kufanya mikutano ya hadhara katika Jimbo lake na mamlaka zote za Serikali zinazohusika zina wajibu wa kuwezesha mikutano hiyo kufanyika.

Mheshimiwa Spika, Iakini kwa masikitiko makubwa vyombo vya dola hasa Polisi imekuwa ikizuia kufanyika kwa mikutano hiyo na Spika wa Bunge ambaye kimsingi anatakiwa kuhakikisha kuwa Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge inaheshimiwa amekaa kimya wakati haki na madaraka ya Bunge yanadhulumiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Wabunge waliozuiliwa kufanya mikutano na wananchi wao ni pamoja na Mheshimiwa John Mnyika, Mheshimiwa Tundu Lissu, Mheshimiwa Meshack Opulukwa, Mheshimiwa Ezekia Wenje, Mheshimiwa Said Arfi, Mheshimimiwa Magdalena Sakaya na Mheshimiwa Godbless Lema.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua kama kuna sera inayokataza Wabunge wa Upinzani kufanya mikutano na wananchi katika Majimbo yao. Kama hakuna sera, ni kwa nini Serikali inawazuia Wabunge kufanya mikutano na wananchi wao?

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa, Chama cha Siasa kilichopata usajili wa kudumu, kina haki ya kufanya mikutano ya siasa na kupatiwa ulinzi kwa mikutano hiyo na Jeshi la Polisi. Hata hivyo, Jeshi la Polisi limeonesha upendeleo mkubwa kwa namna linavyoshughulikia mikutano ya Vyama vya Siasa vya Upinzani na ile inayofanywa na CCM.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, wakati Sheria ya Vyama vya Siasa inataka Vyama vya Siasa vitoe taarifa kwa Kamanda wa Polisi wa Wilaya na kwa kiasi kikubwa Makamanda wa Polisi wa Wilaya wamekuwa wakiruhusu mikutano hiyo, lakini kumekuwa na tabia ya Makamanda wa Polisi wa Mikoa kuingilia masuala ya mikutano ya vyama ambayo hayawahu kisheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya Kamati ya Dkt. Emmanuel Nchimbi, chini ya uongozi wa Jaji Ihema, iliyotolewa tarehe 9 Oktoba, 2012, nanukuu: "Kuwepo kwa zuijua mikutano ya siasa ya CHADEMA, mkoani Iringa wakati wa zoezi la sensa ya watu na makazi linathibitishwa na amri ya utendaji (*Operation Order*) ya Kamanda wa Polisi Mkoa (SAC Michael Kamuhanda) ya tarehe 1 Septemba, 2012.

Mheshimiwa Spika, uhalali wa amri au zuijua hili ulithibitishwa pia na Msajili wa Vyama vya Siasa nchini katika barua yake yenye Kumb. Na. DA.112/123/01/34 ya tarehe 28 Agosti, 2010 na wakati wa mahojiano na Kamati ya Uchunguzi tarehe 22 Septemba, 2012."

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, uhalali wa kauli hii umehojiwa na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Katika taarifa yake ya tarehe 10 Oktoba, 2012; Tume ya Haki za Binadamu ilisema yafuatayo: "Ili pawepo na utawala bora mamlaka zote za Serikali ni lazima zifuate utawala wa sheria.

Uchunguzi umebaini kuwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Iringa, Michael Kamuhanda, tarehe 2 Septemba, 2012 katika utekelezaji wa majukumu yake alikiuka Sheria ya Vyama vya Siasa (*Cap 258 RE. 2002*) kifungu cha 11(a) na (b) na Sheria ya Polisi (Sura ya 322) kwa kuingilia kazi za *OCD* wa Mufindi na kutoa amri ya kuzuia shughuli za CHADEMA wakati yeeye hakuwa *Officer In-charge* wa Polisi wa eneo husika.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, amri aliyoitoa haikuwa halali kwa kuwa ilitolewa na mtu ambaye hakuwa na mamlaka kisheria kutoa amri hiyo. Haya ni matumizi mabaya ya mamlaka, hivyo ni ukiukwaji wa misingi ya

utawala bora. Aidha, hatua ya Msajili wa Vyama vya Siasa, Mheshimiwa John Tendwa kuwaandikia barua viongozi wa Vyama vya Siasa kuwataka kusitisha shughuli zao kwa sababu ya sensa ilikiuka misingi ya utawala bora kwani maelekezo yaliyotolewa ndani ya barua hizo yanakinzana na Sheria ya Takwimu Na. 1 ya mwaka 2002 inayotoa fursa kwa wananchi kuendelea na kazi zao wakati wa sense, pia ni kinyume na sheria ya Vyama vya Siasa (*Cap. 258 RE. 2002*) kifungu cha 11 (a) na (b) inayotoa fursa kwa Vyama vya Siasa kufanya shughuli zake bila kuingiliwa.”

Mheshimiwa Spika, aidha, katika mapendekezo yake, Tume ya Haki za Binadamu ilisema yafuatayo, naomba kunukuu:

“Kuhusiana na polisi na Msajili wa Vyama vya Siasa; Jeshi la Polisi na Msajili wa Vyama vya Siasa waepuke kufanya maamuzi au matendo yanayoibua hisia za ubaguzi au upendeleo mionganoni mwa jamii wakati wanapotekeleza majukumu yao ya kisheria. Mfano, Jeshi la Polisi lilizua mikutano ya CHADEMA kwa sababu ya sensa wakati huo huo Chama cha Mapinduzi (CCM) walikuwa wakifanya uzinduzi wa Kampeni huko Zanzibar. Aidha, rai ya Msajili wa Vyama vya Siasa haikuzingatiwa kwa upande wa CCM Zanzibar, huku CHADEMA wakishurutishwa na Polisi kutii rai hiyo”. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe kauli mbele ya Bunge hili kama inakubaliana na taarifa ya Tume ya Haki za Binadamu. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ilieleze Bunge hili hatua ilizochukua kama zipo dhidi ya Makamanda wa Polisi wa Mikoa ambao wamekuwa wakiingilia mikutano ya Vyama vya Siasa ambayo imekabidhiwa kisheria kwa Makamanda wa Polisi wa Wilaya.

Mheshimiwa Spika, mashinikizo ya Wakuu wa Mikoa, Wilaya na Mawaziri uliikera hata Kamati ya Jaji Ihema iliyoteuliwa na Waziri wa Mambo ya Ndani mwenyewe. Kwa

mfano, katika mapendekezo yake, Kamati ilisema yafuatayo kuhusiana na CCM kutumiwa na kulitumia Jeshi la Polisi kwa manufaa yake, naomba kunukuu:

"Muundo uliopo wa Jeshi la Polisi uangaliwe upya kisheria ili kuziba mianya inayotoa nafasi kwa wanasiasa kulitumia Jeshi hilo kwa manufaa ya kisiasa. Nafasi za Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa kiutendaji ziangaliwe upya ili zisitumike na mhusika kwa ajili ya manufaa ya kisiasa". Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo haya yanakwenda sambamba na kauli aliyoitaoa Mwenyekiti wa CCM Taifa, Dkt. Jakaya Kikwete alipokuwa akihutubia mikutano wa Halmashauri Kuu ya CCM, Dodoma kwamba CCM isitegemee Jeshi la Polisi kujibu hoja za Wapinzani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaliasa Jeshi la Polisi liache kazi za siasa na badala yake wazingatiesheria na taratibu zinazowaongoza ili kurejesha imani ya jamii kwa jeshi hilo ambayo kwa sasa inakaribia kutoweka kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwa miaka mingi CCM na viongozi wake imekuwa ikivikejeli vyama vya Upinzani kwa kuviiita vyama vya msimu. Kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita, CHADEMA kimethibitisha kuwa si chama cha msimu kwa kufanya mikutano na maandamano kwa wingi kuliko Vyama vingine vya siasa. Matokeo yake sasa CCM na Serikali yake wanakula njama ya kuzuia Vyama vya Upinzani kufanya mikutano ya siasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani, imeona mapendekezo yaliyoandaliwa na Msajili wa Vyama vya siasa, ambayo lengo lake ni kupiga marufuku mikutano ya Vyama vya Siasa wakati ambao sio wa kampeni za uchaguzi. Kwa mapendekezo haya, haki ya Vyama vya Siasa kufanya shughuli za kisiasa itakuwa imeuawa na Serikali hii ya CCM kwa kumtumia Msajili wa Vyama.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo haya ya Msajili wa

Vyama vya Siasa ambayo lengo lake ni kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Vyama vya Siasa ambayo yakikubaliwa yatapelekea kupiga marufuku mikutano ya siasa yanatokana na shinikizo la CCM na yana lengo la kuidhibiti CHADEMA.

Mheshimiwa Spika, hii ni kwa sababu, Taarifa ya Kamati ya Jaji Ihema iliyoundwa na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Dkt. Nchimbi inasema hivi: "Kasi ya CHADEMA kuendesha mikutano katika sehemu mbalimbali hapa nchini kwa ajili ya kujimarisha kichama, imepokewa kwa hisia tofauti na Vyama vingine vya Siasa.

Wakati kuna makundi ya watu katika jamii wakidhani kuwa hiyo ni haki yao kama Chama cha Siasa kinachotaka kukua na kukubalika kisiasa, wengine wanaona mikutano hiyo ya hadhara ya CHADEMA kama ni kuwapunguzia muda wa kufanya shughuli zao za maendeleo hasa baada ya kipindi cha uchaguzi kumalizika.

Katibu Mkuu wa CCM, Wilson Mukama alishauri kufanyiwa marekebisho Sheria ya Vyama vya Siasa, Namba 5 ya mwaka 1992 itakayoweka wazi shughuli za Vyama vya Siasa baada ya Uchaguzi Mkuu. Alisisitiza kuwa shughuli za siasa baada ya Uchaguzi Mkuu zihamie Bungeni kwa wanasiasa kuhoji mipango ya maendeleo ya Serikali na matumizi ya rasilimali za nchi na wananchi waachwe wachape kazi zao za maendeleo". Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa aliyekuwa Katibu Mkuu wa CCM ndio uliochukuliwa na kufanyiwa kazi na Msajili wa Vyama vya Siasa. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali itoe kauli mbele ya Bunge hili juu ya hatua zozote kama zipo za kutekeleza mapendekezo haya ya Kamati ya Jaji Ihema.

Mheshimiwa Spika, haki ya kufanya mikutano ya siasa na mikutano mingine yoyote na kwa wakati wowote, inatambuliwa na kulindwa na Katiba yetu. Ibara ya 20(1) ya Katiba yetu inasema: "Kila mtu anao uhuru wa kukutana na

watu wengine kwa hiari yake na kwa amani, kuchanganyika, kushirikiana na watu wengine na kwa ajili hiyo kutoa mawazo yake hadharani na kuanzisha na kujunga na vyama au mashirika yaliyoanzishwa kwa madhumuni ya kuhifadhi au kuendeleza imani au maslahi yake au maslahi mengineyo".

Mheshimiwa Spika, Uhuru huu haujawekewa masharti ya muda au wakati wa kukutana au kuchanganyika na watu kwa wakati au kipindi fulani. Kwa hiyo, mapendekezo ya Msajili wa Vyama vya Siasa ya kupiga marufuku mikutano ya siasa kwa nyakati zisizokuwa za kampeni za uchaguzi yanakwenda kinyume na Katiba na hayakubaliki.

Mheshimiwa Spika, ni ajabu ilioje kwamba, wakati nchi nyingine jirani yetu zinapanua demokrasia kwa kupanua haki ya kufanya mikutano na maandamano, Serikali hii ya CCM inapendekeza kuminya demokrasia kwa kudhibiti na kufifisha haki hizo.

Mheshimiwa Spika, hii inafanyika wakati Taifa likiwa kwenye mchakato wa kuandika Katiba mpya. Jirani zetu wa Kenya katika Katiba yao mpya ya mwaka 2010 wameamua kufanya ifuatavyo katika ibara ya 37 ya Katiba yao: "Kila mtu ana haki, kwa amani na bila kuwa na silaha kukutana, kuandamana, kufunga njia au eneo au jingo (*to picket*) na kupelekea malalamiko katika mamlaka za umma".

Mheshimiwa Spika, marafiki zetu wa Zimbabwe, baada ya miaka mingi ya utawala wa kiimla wa ZANU-PF nao wamepata Katiba mpya iliyopitishwa mwezi Februari mwaka huu na Katiba yao inasema yafuatayo katika Ibara ya 58(1) na 59: "Kila mtu ana haki ya uhuru wa kukutana na kuchanganyika na haki ya kutokutana na kuchanganyika na wengine. Aidha, kila mtu ana haki ya kuandamana na kuwasilisha malalamiko lakini haki hizi zitatekelezwa kwa amani".

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, masharti pekee ya haki ya kukutana, kuandamana na kuchanganyika na watu wengine katika Jamhuri ya Kenya na Zimbabwe ni

kwamba, maandamano au mikutano hiyo ifanyike kwa amani. Badala ya kujifunza kwa wenzetu wanaopanua haki Serikali hii ya CCM inatuelekeza njia nyingine ya kuminya na kufifisha haki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, maslahi na stahili za Askari Polisi; mara zote Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikitetea maslahi bora na mazingira mazuri ya kazi kwa watumishi wa Serikali na hata wa sekta binafsi ili kuwapa motisha watumishi, jambo ambalo huongeza tija katika uzalishaji na hatimaye kukuza uchumi.

Mheshimiwa Spika, katika maboresho ya maslahi na stahili mbalimbali kwa watumishi wa Serikali, Askari wa Jeshi la Polisi wamekuwa wakiachwa nyuma sana. Tumeshuhudia posho zkipanda maradufu kwa kada nyingine za watumishi Serikalini huku fedha za kujikimu kwa Askari wa Jeshi la Polisi na Magereza zikiwa pale pale licha ya gharama za maisha kupanda kila kukicha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwamba, kitendo cha gharama za maisha kupanda huku mishahara na stahili nyingine za askari kubaki katika kiwango kile kile cha zamani ndicho kinachofanya askari wetu kuingia tamaa ya kupokea rushwa na kutoa vitisho kwa raia ili kujipatia kipato cha ziada kunusuru maisha yao na wategemezi wao.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Jeshi la Polisi, linafanya kazi zinazoshabihiana na Jeshi la Wananchi na kwa kuwa Askari wa Jeshi la Polisi wanahitaji chakula kama vile ambavyo Jeshi la Wananchi wanahitaji ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuongeza posho ya chakula (*Ration allowance*) kwa Askari wa Jeshi la Polisi ili angalau posho hiyo ishabihiane na posho ya Jeshi la Wananchi ambayo kwa sasa ni sh. 7,500/= kwa siku kwa akari mmoja.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba posho hii ya shilingi 7,500 kwa Jeshi la Wananchi haitoshi, kutokana na

kupanda kwa gharama za maisha, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuiboresha ili majeshi yetu yaweze kukabiliana na ugumu wa maisha.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kabisa kwamba, jambo hili linawezekana kama tukipunguza posho mbalimbali ambazo si za lazima (*discretionary allowances*). Itakumbukwa kwamba, wakati wa bajeti ya Wizara ya Maji, Mheshimiwa Spika alisema kwamba, fedha iliyoongezwa katika bajeti ya maji ya shilingi bilioni 181 haikutoka kwingine isipokuwa posho mbalimbali.

Kwa hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kabisa kwamba ikiwa Serikali hii ya CCM itajibana kidogo na kujiondolea posho zisizo za lazima, sio tu kwamba, Polisi watapata *ration allowance* tunayopendekeza ya sh. 7,500, bali pia fedha hizo zinaweza kuelekezwa pia kwenye ujenzi wa nyumba za Polisi na Magereza na hivyo Polisi wakawa na nyumba nzuri na maisha yao yakawa ya staha zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Serikali kuboresha posho ya chakula kwa askari wa Jeshi la Polisi na Magereza kama tulivyopendekeza ili waweze kukabiliana na ugumu wa maisha.

Mheshimiwa Spika, umri wa kustaafu kwa Maafisa wa Polisi na Magereza. Kati ya marekebisho ya sheria mbalimbali iliyofanyika katika Bunge liliopita, ilikuwa ni kuongeza umri wa kustaafu kwa Askari Polisi na Magereza kutoka miaka 50 kwenda 55 na kutoka miaka 55 kwenda 60.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na ukimya juu ya utekelezaji wa sheria hiyo, kwa upande wa Serikali na hivyo kuwaacha Maafisa wa Polisi na Magereza wanatakiwa kustaafu njia panda kwa kutojua wafuate utaratibu wa zamani wa kustaafu au wasubiri utekelezaji wa sheria hii mpya.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa mwongozo kwa Maafisa wa Polisi na Magereza wanaotakiwa kustaafu juu ya sheria ya kufuata.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kujiendeleza kimasomo nje ya kituo cha kazi kwa Maafisa wa Polisi na Magereza. Kwa mujibu wa *General Service Order (GSO)* na sheria nydingine za kazi, mtu akiajiriwa kwa mara ya kwanza (*first appointment*) na akataka kujiendeleza kimasomo nje ya kituo chake cha kazi anatakiwa kukaa kazini kwa muda wa miaka miwili au mitatu ndipo aweze kuomba ruhusa ya kwenda masomoni.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Magereza wamechakachua sheria na kujiwekea utaratibu wao kwamba, ili askari aweze kupata kibali cha kwenda masomoni ni mpaka akae miaka sita, yaani aende likizo mbili ndipo aombe kibali cha kwenda masomoni.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona huo ni urasimu usio na tija na ni kulidumaza Jeshi la Magereza kwani kwa utaratibu huo wengi watakata tamaa ya kujiendeleza kielimu na kwa maana hiyo ufanisi wao katika jeshi utakuwa unapungua. Aidha, kwa kuzingatia ugumu wa kupata nafasi (*admission*) katika vyuo, ambapo mtu anaweza kuomba na kukosa nafasi hata kwa miaka miwili mfululizo, kama masharti yataendelea kuwa, Askari akae kazini miaka sita ndipo aombe nafasi, kuna uwezekano ikamchukua Askari hata miaka kumi kabla hajapata nafasi ya kusoma na akija kupata umri wake unaweza ukawa umekwenda sana kiasi cha kuathiri masomo yake.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuliagiza Jeshi la Magereza, kufuta haraka sana masharti hayo ya kukaa kazini miaka sita ndipo askari apate fursa ya kujiendeleza kimasomo kwani hauna tija hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, hali duni ya maisha kwa Askari Magereza. Askari Magereza wanaishi katika mazingira magumu kiasi ambacho wanashindwa kufanya kazi zao kwa

ufanisi. Askari hawa wanashinda mashambani na maeneo ya kazi kusimamia wafungwa, wanakesha magerezani kuwalinda wafungwa wakati wafungwa wamelala na wanapopata muda wa kupumzika, hakuna mahali pazuri pa kupumzika, nyumba zao zipo katika hali duni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kusema kweli wanaishi maisha magumu na wanajiona kuwa wao ndio wafungwa kuliko wafungwa wenyewe. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kujibana kama ilivyojibana kwenye bajeti ya Wizara ya Maji ili kujenga nyumba za Askari Magereza na kuboresha makazi yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hali ya Magereza na msongamano wa wafungwa. Mfumo wetu wa Magereza unakabiliwa na msongamano mkubwa wa wafungwa na mahabusu. Kwa mujibu wa Kamishna wa Jeshi la Magereza nchini, idadi ya wafungwa na mahabusu hapa nchini ni 36,365 ambapo wafungwa ni 18,452 na mahabusu ni 17,913 na uwezo wa hifadhi Magerezani ni nafasi 29,552.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa mujibu wa tovuti ya Wizara ya Mambo ya Ndani, Magereza yana uwezo wa kuhifadhi wafungwa na mahabusu 22,669, lakini kwa sasa inatunza zaidi ya wafungwa na 45,000, kiwango ambacho kimezidi kwa zaidi ya asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, pamoja na takwimu hizi kuwa tofauti, ukweli ni kwamba, magereza yamefurika. Lakini pia tofauti ya idadi iliyotolewa na Kamishna wa Jeshi la Magereza na ile ya tovuti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, ni uthibitisho kwamba, hata Serikali haijui kuna wafungwa wangapi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili, ni kitu gani kinachosababisha msongamano mkubwa hivi katika Magereza yetu. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Mahakama kutoa adhabu

ya vifungo vya nje na faini na kazi mbalimbali katika jamii kama njia mojawapo ya kupunguza msongamano wa na wafungwa Magerezani.

Mheshimiwa Spika, hali duni ya lishe na afya kwa Wafungwa na Mahabusu. Fedha inayotolewa na Serikali kwa mlo wa mfungwa mmoja ni sh. 577/= tu ambayo ni sawa na bei ya chupa ndogo moja tu ya maji. Huu ni ukiukwaji mkubwa wa haki msingi za binadamu, kwa maana kutompa mtu chakula cha kutosha maana yake unamtakia kifo. Hii ina maana kwamba, haki ya kuishi ambayo ni ya Kikatiba inakiukwa na Serikali kwa kutoa kiwango ambacho hakimtoshi mtu kuishi.

Mheshimiwa Spika, wafungwa na mahabusu nchini wanakosa huduma muhimu za kibinadamu ikiwemo mlo kamili, matibabu na maji. Viwango vya chakula cha wafungwa Magerezani vimewekwa kwa mujibu wa Kanuni za Magereza za mwaka 1968, kifungu cha 23(1) zilizotungwa kwa mujibu wa Sheria ya Magereza (*Prisons Act* ya Mwaka 1967).

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni hizo, wafungwa wanatakiwa kula milo miwili: (asubuhi kifungua kinywa gramu 450 ambazo ni sawa na gramu 150 za unga wa uji na gramu 300 za vitafunwa. Mchana wanapata gramu 500 ambazo ni mlo miwili ambayo ni gramu 250 za mchana na usiku gramu 250 ambazo hutolewa kwa pamoja). Licha ya mlo huu kuwa hautoshi, lakini pia umekuwa hauna makundi yote ya lishe.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuongeza kiasi cha fedha ya mlo kwa mfungwa ili kiendane na gharama halisi za maisha kwa sasa. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inataki kujua ni kwa nini wafungwa wapewe chakula mara mbili tu wakati kiafya mtu anatakiwa kupata mlo mara tatu kwa siku? Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji ni kwa nini wafungwa wanalazimishwa kulala saa kumi jioni badala ya saa mbili usiku baada ya mlo wa jioni? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwapa wafungwa milo mitatu (yaani kifungua kinywa, chakula cha mchana na chakula cha jioni) kwa awamu tatu na sio kuwapa chakula cha mchana na cha jioni kwa pamoja, kwani kwa kufanya hivyo ni kuwatesa wafungwa kwa makusudi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kubadili muda wa kulala wafungwa kutoka saa kumi jioni hadi saa mbili usiku ili waishi kama binadamu wengine. Kitendo cha wafungwa kutokuwa huru tayari ni adhabu ya kutosha, kuongeza adhabu nytingine zisizo rasmi kama vile kupata milo miwili tu na kulazimishwa kulala saa kumi jioni ni ukiukwaji wa haki za binadamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani pia inataka kujua kama kuna huduma maalum za lishe, matibabu na malazi kwa waathirika wa UKIMWI, wajawazito na akinamama wanyonyeshao Magerezani.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 13(6)(d) na (e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inakataza kumdhaliilisha mtu au kumpa adhabu za kumtweza utu wake. Mfumo wa upakuaji unaofanywa na askari Magezeza dhidi ya wafungwa na mahabusu bila shaka ni wa kiudhalilishaji.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani haipingi wafungwa au mahabusu kupekuliwa au kukaguliwa mara waingiapo gerezani, lakini angalau upakuaji huo uwe wa faragha kuliko ilivyo sasa hivi ambapo wafungwa na mahabusu huvuliwa nguo mbele ya kadarnasi na kulazimishwa kuinama wakiwa utupu ili kuhakiki kama hawajaficha chochote kwenye sehemu zao za siri bila kujali hata tofauti ya umri wa wafungwa na mahabusu wenyewe. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwatendea wafungwa na mahabusu kama binadamu na sio kama wanyama.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Kumekuwepo na ukusanyaji wa fedha wa lazima kutoka kwa

wafanyabiashara kwa ajili ya zimamoto bila kujua kama fedha hizo ni kwa ajili ya malipo ya ada, vifaa vyta kuzimia moto au huduma nyingine. Fedha hizo zimekuwa zikitozwa kwa kutumia nguvu bila kuwapa raia elimu ya kutosha juu ya matumizi ya fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua kiasi cha sh. 30,000/= hadi 300,000/= kinachotozwa na Jeshi la Zima Moto bila kutoa kifaa cha kuzima moto (*fire extinguisher*) ni kwa madhumuni yapi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inakemea tabia ya Serikali kuweka nguvu kubwa zaidi kununua vifaa vyta kuumiza na kuangamiza watu badala ya kununua vifaa vyta uokoaji wa maisha ya watu. Nasema hivi kwa kuwa pingu za kuwafunga na mabomu ya kuwapiga wana CHADEMA na rala wanaodai haki zao hayakosekani, lakini kunapotoka ajali ya moto au maghorofa kuperomoka, au meli kuzama watu hufa na Serikali kubaki na kisingizio cha kuchefua, cha ukosefu wa fedha za kununulia vifaa vyta uokoaji. (*Makof*)

Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuliimarisha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa kununua vifaa vyta kutosha na kuwapatia mafunzo ya uokoaji maafisa wa jeshi hilo ili liweze kukabiliana na maafa mbalimbali yanayotokea hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, uonevu unaofanywa na askari wa vyeo vyta juu dhidi ya wadogo. Kumekuwa na tabia ya Askari wenye vyeo vyta juu kuwanyanyasa askari wa vyeo vyta chini, jambo ambalo linawakatisha tamaa askari hao kufanya kazi kwa moyo. Unyanyasaji huo unafanywa kwa makusudi ili kuwaziba midomo Askari wa vyeo vyta chini wasihoji kuhusu haki na stahili zao wawapo kazini.

Mheshimiwa Spika, unyanyasaji huo umechukua sura mpya baada ya askari wa kada ya chini kusingiziwa kuwa ni vichaa ili tu kubatilisha ukweli wanaousema kuhusu utendaji mbovu na ubadhirifu unaofanywa na mabosi wao.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, *PC Mesiaki Samson Na. E.6767* wa *Central Police*, Arusha alisingiziwa kuwa ni kichaa na *SPMushumbusi* wa Makao Makuu ya Polisi, Dar es Salaam aliyekuwa Arusha kusikiliza matatizo ya Polisi wa vyeo vya chini na kutoa amri *PC Mesiaki Samason* kwenda kupimwa maradhi ya akili katika Hospitali ya *Mount Meru* Arusha kutokana na kuhoji watu wasio na sifa kupelekwa kusomea nyota wakati wenye sifa wanaachwa.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inalaani tukio hilo kwani ni la kiudhalilishaji kwa kuwa *PC Samson Mesiaki* hakukutwa na maradhi yoyote ya akili na hajawahi kuwa na historia ya maradhi ya akili. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, tangu hapo askari huyu ameendelea kunyanyaswa na mabosi wake mpaka anashindwa kufanya kazi kwa kuwa hapewi ushirikiano wowote. Kambi Rasmi ya Upinzani, inamtaka Waziri wa Mambo ya Ndani kuingilia kati suala hilo na kutafuta ukweli kwani inaonekana kuwa kupigwa vita kwa askari huyu ni kutokana na kuwa na taarifa za utendaji mbaya wa wakubwa zake na ndio maana wanatafuta njia za kumfanya aonekane ni kichaa ili taarifa alizonazo zisitiliwe maanani.

Mheshimiwa Spika, kuporomoka kwa maadili ya kazi ya Jeshi la Polisi na jinsi Jeshi hilo linavyotumiwa kutimiza maslahi ya kisiasa ya viongozi. Ni wazi kwamba, maadili ya kazi katika Jeshi la Polisi yameporomoka kwa kiwango kikubwa sana hasa baada ya kuanzishwa kwa siasa ya Vama Vingi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika matukio mengi, Jeshi la Polisi limeonekana wazi kabisa kutoshughulikia uhalifu nchini (na kwa maana hiyo kutowalinda raia na mali zao) na badala yake kutumia nguvu kubwa kupita kiasi katika kuzuia mikutano na maandamano halali ya CHADEMA yanayolenga kutoa elimu ya uraia na kuwafungua watu kifikra na kimtzamko kuhusu ushiriki wao katika siasa na maendeleo ya nchi yao.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la polisi kwa sasa linaonekana kuacha maadili ya kazi na kujielekeza kukinusuru Chama cha Mapinduzi kinachoelekea kushindwa badala ya kunusuru heshima yake ambayo imekuwa ikipotea siku hadi siku mbele ya jamii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa hivi Jeshi la Polisi limekuwa likifanya kazi kwa mashinikizo na maelekezo ya wanasiaya badala ya kuzingatia sheria na taratibu zinazoliongoza. Mashinikizo hayo yamesababisha watu wasio na hatia kubambikiwa kesi ili kutimiza maslahi ya kisiasa ili kukomoa Wapinzani wanaopiga kelele kudai haki za wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakati Jeshi la Polisi linawashtaki Wabunge wa Upinzani kwa makosa ya kutunga, limeshindwa kuwachukulia hatua Wabunge wa CCM waliofanya makosa ya jinai hadharani. Kwa mfano, sheria ya makosa ya jinai inakataza mtu kutembea na silaha hadharani kwa namna itakayotishia watu, lakini Mheshimiwa Ismail Aden Rage alifanya hivyo na kupigwa picha na vyombo vya habari, lakini hakuchukuliwa hatua hadi sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha, Mheshimiwa Rage alimshambulia na kumpiga mwanachama wa CHADEMA hapa Dodoma baada ya kuzuiwa na kijana huyo kung'oa bendera ya CHADEMA, akapigwa picha katika hekahuka za kumpiga kijana huyo lakini bado yupo ilhali Polisi waliona tukio alilolifanya.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani ina taarifa kwamba, Jeshi la Polisi limeshakamilisha uchunguzi wa matukio ya Mheshimiwa Rage, lakini wanashindwa kumkamata na kumpeleka Mahakamani kutokana na mashinikizo kutoka kwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Dkt. Rehema Nchimbi na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Dkt. Emmanuel Nchimbi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutenda haki sawa kwa wote ili kudumisha misingi ya

utawala wa sheria. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe kauli juu ya hatua inazokusudia kuchukua dhidi ya kiongozi huyu anayefanya makosa ya jinai hadharani.

Mheshimiwa Spika, kuwindwa kwa Waandishi wa Habari. Waandishi wa Habari sasa nao ni kundi maalum linalolengwa na mashambulizi kutokana na kazi yao ya kufichua maovu katika jamii na hasa ya viongozi. Kwa mfano, katika tukio la kuuawa kwa Mwandishi mmoja huko Iringa, taarifa ya *MCT* ya Oktoba, 2012 inasema kwamba: "Wanahabari waliokuwepo kwenye mkutano huo wanakiri kwamba, marehemu alikuwa ndiye mwandishi pekee aliyemuuliza *RPC* maswali magumu kiasi cha kumkera kiongozi huyo wa Jeshi la Polisi".

Mheshimiwa Spika, kati ya maswali allyouliza marehemu ni: "Kwa nini Chama Tawala CCM kiko huru kufanya mikutano ya kisiasa, wakati Chama cha CHADEMA kinawekewa vikwazo na Polisi kila wakati?" Aidha, baada ya mkutano huo wa waandishi wakati wanahabari wakitoka kwenye ofisi za Mkoa za Polisi, baadhi ya Polisi ambaa utambuzi wao haukuhamika mara moja waliwaonya wasiende Nyololo kwa ajili ya kukusanya habari za shughuli za kisiasa za CHADEMA kutokana na uwezekano wa kutokea kwa hali hatarishi.

Mheshimiwa Spika, vilevile kwa mujibu wa taarifa hiyo: "Baada ya mkutano wa Waandishi wa Habari wa asubuhi katika ofisi za *RPC*, waandishi waliokuwepo wanakumbuka kuwa askari mmoja mpelelezi alimfuata marehemu na kumwambia: "Ina maana gani kwenda Nyololo kuandika habari za shughuli za CHADEMA ambazo zinaweza kuishia na kifo chako?"

Mheshimiwa Spika, uthibitisho kwamba, Serikali ya CCM na Jeshi la Polisi wamekuwa wanawalenga Waandishi wa Habari kwa makusudi kunathibitishwa na kauli ya Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai aliyoitoa tarehe

5 Septemba, 2012. Kwa mujibu wa taarifa ya Pamoja ya *MCT* na *TEF, DCI* Manumba alisema yafuatayo: “....matukio ya aina hii yapo na yataendelea kuwepo”

Mheshimiwa Spika, kauli ya *DC/Manumba* imerudiwa tena na Mkuu wa Mkoa wa Arusha Magessa Mulongo tarehe 1 Mei, 2012. “Unapoingia katika mkakati wa kumdhaliilisha kiongozi wa Serikali unaiweka roho yako rehani.... kuweni makini.”

Mheshimiwa Spika, matamshi ya *DCI Manumba* na Magessa Mulongo ni matendo ya kigaidi kwa mujibu wa Sheria ya Ugaidi 2002. Kifungu cha 4(3) (a), (b) na (l) vinafafanua matendo ya kigaidi kuwa ni pamoja na vitisho vinavyohusu mtu kusababishiwa maumivu au majeraha makubwa kimwili, kuhatarisha maisha ya mtu na vinavyohusu usalama wa umma ambavyo vimelengwa au ambavyo kwa hulka au muktadha wake vinaonekana vimelengwa kutishia umma au sehemu ya umma.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, kauli ya *DCI Manumba* kwamba, mauaji ya waandishi yamekuwepo na yataendelea kuwepo na kauli ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Magessa Mulongo kwamba waandishi wanaofuutilia nyendo za viongozi wa Serikali wanaweka roho zao rehani ni matendo ya kigaidi. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua ni kwa nini *DCI Manumba* na Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Magesa Mulongo hawajakamatwa na kufunguliwa mashtaka ya ugaidi?

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (*NIDA*); wazo la kuwa na vitambulisho vya Utaifa lilibuliwa kwa mara ya kwanza mwaka 1986 katika kikao cha Kamati ya Intelejesia ya Pamoja (*Inter – State Intelligence Committee*) ambapo Viongozi Wakuu wa Nchi za Kenya, Uganda, Zambia na Tanzania walihudhuria. Katika kutekeleza azimio hilo, Kikao cha Baraza la Mawaziri Na. 3/85 cha mwaka 1985 kiliamua kwamba kuwe na usajili wa raia na wasio raia.

Mheshimiwa Spika, azimio hili lilitekelezwa kwa

kutungwa kwa Sheria ya Kusajili na Kutambua Watu Na.11 ya mwaka 1986. (*The Registration and Identification of Persons Act, No.11/86 1986*). Hata hivyo, Serikali haikuwa na uwezo wa kuendelea na shughuli za vitambulisho, kwa sababu ya gharama za maandalizi na utekelezaji wa program hiyo.

Mheshimiwa Spika, pia kwa wakati huo hakukuwa na mpango wa mweleko (*road map*) na gharama za shughuli hiyo hazikuwa zinajulikana. Wakati huo wote huo, Serikali ya Chama cha Mapinduzi (CCM) haikujishughulisha hata kidogo na suala la Vitambulisho vya Taifa mpaka mwaka 2006 ilipoingia mkataba wa kufanya upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako tangu wakati huo limekuwa likitenga pesa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli hiyo muhimu, lakini *NIDA* imekuwa ikitekeleza shughuli hiyo kwa kasi ya kinyonga na hivyo pesa zinazotengwa haziakisi ufanisi wala mafanikio ya utekelezaji wa shughuli hiyo. Mathalani tangu wakati huo hakuna raia wa kawaida aliyepewa kitambulisho ukiondoa watumishi wachache wa umma na watu wengine wachache. Zoezi la majaribio (*pilot study*) lililofanyika Dar es Salaam limeishia hewani na wananchi hawajui hatua gani inafuata.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji mambo yafuatayo:-

(1) Ni kiasi gani cha fedha kimeshatumiwa na *NIDA* tangu mwaka 2006 hadi leo na matumizi hayo yamekuwa na tija kiasi gani (*value for money*) kwa kuwa hatuoni maendeleo mazuri ya utoaji wa vitambulisho vya Taifa?

(2) Ni lini wananchi wote wa Tanzania watakuwa wamepata vitambulisho vya Taifa?

Mheshimiwa Spika, Vitambulisho vya Taifa ambavyo Waheshimiwa Wabunge na watumishi wengine wa umma wamepewa vina taarifa chache na havina taarifa nyingi muhimu, mathalani, hakuna taarifa ya kundi la damu, aina ya kazi, anuani ya makazi, tofauti na vitambulisho vya

Mataifa mengine, tofauti hata na vya ndugu zetu wa Zanzibar ambaao vitambulisho vyao vina taarifa zaidi kumhusu mwenye kitambulisho. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuweka taarifa zaidi zinazomhusu raia katika vitambulisho vya Taifa.

Mheshimiwa Spika, kuzagaa kwa silaha na matukio ya kijambazi; mara kadhaa kumetokea matukio ya kihalifu katika maeneo mbalimbali hapa nchini na silaha zinazotumika katika matukio hayo ni silaha nzito za kivita. Hata hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani ilishatoa angalizo mara kadhaa juu ya uwezekano wa kuzagaa kwa silaha kutokana na wahamiaji haramu na makampuni binafsi ya kigeni kuajiri walini wao wenyewe na kutumia silaha zao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika mapendekezo ya Kambi Rasmi ya Upinzani ilikuwa ni kwamba, Serikali Ichukue hatua ya kuimarisha ulinzi zaidi mipakani ili kudhibiti wimbi la wahamiaji haramu kutoka nchi jirani, kudhibiti wafugaji kutoka nchi jirani wanaoingia nchini kwetu bila utaratibu kutafuta malisho ya mifugo yao na kuyazuia makampuni ya kigeni kutumia walini na silaha zao wenyewe na badala yake makampuni hayo yapewe ulinzi na vyombo ya dola vya hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza bunge kwamba, imefikia hatua gani katika kutekeleza mapendekezo ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ili kuliepusha Taifa kukumbwa na matukio ya kijambazi kutokana na kuzagaa kwa silaha kiholela?

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni pia inaitaka Serikali kuwa makini sana inapotoa uraia kwa wakimbizi hapa nchini kwa kuwa kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wananchi kutoka maeneo yenye makambi ya wakimbizi kwamba, wakimbizi wamekuwa wakijihuisha na vitendo vya kihalifu vya uporaji na unyanganyi wa kutumia silaha. Hivyo uraia utolewe kwa kuzingatia uadilifu na pia ujuzi au utaalalm alionao mtu anayeomba uraia wa Tanzania na sio kutoa uraia kiholela.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo awali, nchi yetu imekumbwa na tatizo kubwa la kuzagaa kwa silaha haramu jambo ambalo linatishia amani na utuliu wa nchi yetu. Kama hatua za haraka na madhubuti hazitaweza kuchukuliwa mapema hali itakuwa mbaya hasa ikizingatiwa kuwa baadhi ya nchi ambazo tumepakana nazo, hali yao ya usalama sio nzuri na hairidhishi na hasa ikizingatiwa kuwa kwa kipindi cha mwaka mmoja wa 2012 silaha 889 zilikamatwa na risasi 10,210 zikiingizwa nchini kinyume cha sheria.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani, inataka kujua kuna mkakati gani madhubuti wa kukabiliana na wimbi hili la uingizwaji wa silaha haramu hapa nchini na hasa ikizingatiwa kuwa silaha hizi zinatumwa na wahalifu kwa ajili ya kuendesha vitendo vya kihalifu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, biashara ya dawa za kulevyta nchini; takwimu za Jeshi la Polisi zinaonesha kuwa matukio ya kukamatwa kwa dawa za kulevyta hapa nchini ni makubwa sana na kiwango kinachokamatwa kinaongezeka mwaka hadi mwaka. Kwa mfano, kwa mwaka 2012 kilo 55,499 za madawa aina ya *heroin, cocaine, mandrax* na *morphine* zilikamatwa ikilinganishwa na kilo 17,776 zilizokamatwa mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, takwimu hizi sio nzuri hata kidogo kwani kiwango hiki ni kikubwa sana na hasa ikizingatiwa kuwa hizi ni tani 55 na nusu zilizokamatwa. Bado kuna kiwango kingine ambacho hakikukamatwa, hivyo nchi yetu ipo kwenye hatari kubwa ya Taifa kuangamia kutokana na matumizi ya madawa ya kulevyta.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani, inaitaka Serikali kutoa maelezo ni kwa nini madawa ya kulevyta yanaongezeka wakati kuna sheria kali za kudhibiti biashara ya madawa ya kulevyta?

Mheshimiwa Spika, wimbi la mauaji na unyanyasaji wa raia bila hatua kuchukuliwa. Kwa mujibu wa ripoti ya Haki

za Binadamu Tazania 2012, idadi ya watu waliouawa Tanzania kinyume cha sheria (*extra judicial killings*) toka mwaka 2003 hadi 2012 ni 246. Mchanganuo wa mauaji hayo kwa kila mwaka ni kama ifuatavyo:-

MWAKA	IDADI
2003	22
2004	7
2005	36
2006	37
2007	26
2008	6
2009	10
2010	52
2011	25
2012	31

Mheshimiwa Spika tukirejea mauaji yenyeye sura ya kisiasa yaliyofanywa na Polisi katika mikutano halali ya siasa ya CHADEMA huko Arusha, Morogoro na Nyololo, Iringa ambayo Serikali hii ya CCM imeamua kwa dhati kabisa kuyafumbia macho licha ya Tume mbalimbali za uchunguzi kuthibitisha kuhusika kwa vyombo vya Dola katika mauaji hayo, Kambi Rasmi ya Upinzani inashawishika kuamini kwamba, sasa Serikali hii ya CCM imeamua kusimamia mauaji ya raia wasio na hatia hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, tuna kila sababu ya kuamini hivyo kwa kuwa hatuoni hatua za makusudi zikichukuliwa dhidi ya

maafisa wa Polisi waliofanya mauaji hayo na hasa kwa aliyekuwa Kamanda wa Polisi, Mkoa wa Iringa Michael Kamuhanda ambaye ripoti za uchunguzi zilithibitisha bila shaka yoyote kwamba alihuksika na mauaji ya Nyololo, Iringa.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa tamko mbele ya Bunge hili kuhusu hatua zinazochukuliwa dhidi ya aliyekuwa Kamanda wa Polisi, Mkoa wa Iringa, Michael Kamuhanda na maafisa wengine wa Polisi waliohusika na mauaji ya raia wasio na hatia hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kuna kila dalili kwamba Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, chini ya uongozi wa Dkt. Emmanuel Nchimbi, imeshindwa kabisa kusimamia utendaji kazi wa Jeshi la Polisi na kwa maana hiyo imeshindwa kusimamia usalama wa raia na mali zao ikiwa ni jukumu lake la msingi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani imefikia hitimisho hili kwa sababu hivi karibuni pia kumetokea mauaji ya kutisha katika mkoa wa Mara hasa katika Wilaya za Butiama na Musoma Mjini ambapo watu wengi wanauawa kinyama kwa kukatwa vichwa na wauaji kuondoka na vichwa na viungo vingine vya marehemu huku wakiacha familia zao na wategemezi wao sio tu na majonzi, bali pia na hofu kuu juu ya mauaji hayo kwani hawajui ni nani atakayeua wa siku inayofuata.

Mheshimiwa Spika, hii ni kwa sababu mauaji yamekuwa yakiongezeka siku hadi siku na bila Serikali na Jeshi lake la Polisi kuonesha umahiri wake wa kuzuia mauaji haya kama inavyoonesha umahiri huo kwenye kuzuia mikutano halali ya CHADEMA.

Mheshimiwa Spika, sambamba na matukio haya ya mauaji ya kutisha, miaka ya hivi karibuni pia kulizuka wimbi la mauaji ya walemaru wa ngozi hapa nchini na wengine kukatwa viungo vya mili yao wakiwa hai jambo ambalo lilizua hofu kubwa sana miongoni mwa familia nyingi zilizokwua na watu wenye ulemavu wa ngozi.

Mheshimiwa Spika, jambo la kutisha zaidi ni kwamba, hata askari wetu wenye jukumu la kuwalinda raia na mali zao, nao pia wanauawa katika mazingira ya kutatanisha. Itakumbukwa kwamba huko Zanzibar na Ngara, Kagera kuna Polisi waliuawa na pia hivi karibuni aliyekuwa Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoani Mwanza naye aliuawa katika mazingira ya kutatanisha.

Mheshimiwa Spika, katika mazingira kama haya ni nani anayeweza kushawishika kwamba Serikali, kwa maana ya Wizara ya Mambo ya Ndani, imefaulu katika kutekeleza majukumu yake?

Mheshimiwa Spika, uhalifu mwingine unaofanywa dhidi ya binadamu hapa nchini ni ule wa kuchoma nyumba za wananchi unaofanywa na vyombo vy'a dola kwa sababu zisizo na uzito kabisa. Kitendo cha kuchoma nyumba za wakazi wa Kijiji cha Mpago katika Kata ya Kaniha, Wilayani Biharamulo na Kata ya Rutoro, Wilayani Muleba, Mkoani Kagera kwa madai kwamba wanakijiji hao wamevamia eneo la hifadhi ya Taifa na Vitalu vilivyogawiwa kwa mwekezaji na *NARCO* kwa mtiririko huo, ni cha kinyama na ni kinyume kabisa na haki za binadamu.

Mheshimiwa Spika, jambo la kushangaza ni kwamba, eneo hilo linalodaiwa kuwa ni la hifadhi lina miundombinu ya barabara, mashule na hospitali zilizojengwa na Serikali ikiwa ni ushahidi kwamba, ni eneo la makazi.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya familia zilizochomewa nyumba zao zimepotea kusikojulikana na mpaka sasa haifahamiki kama wamekuwa au wapo hai. Katika unyanyasaji unaofanywa katika Kata ya Rutoro, Wilayani Muleba ni kwamba, wananchi wanauawa kwa kupigwa risasi na watendaji wa vitalu vy'a mwekezaji ambao ni Wanyarwanda.

Mheshimiwa Spika, badala ya wahalifu hawa kushughulikiwa na Polisi, kinyume chake ni kwamba *RCO* wa Mkoa wa Kagera amekula njama na mwekezaji na kuwasaliti

wananchi na kuwabambikia kesi ya mauaji Diwani wa Kata ya Rutoro, Mtendaji wa Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji, Bwana Kahatano.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa kauli rasmi mbele ya Bunge hili kama imeruhusu wawekezaji kuwaua wananchi kwa kuwapiga risasi. Pili, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua ni kwa nini viongozi wanaowatetea wananchi wanabambikiwa kesi za mauaji ili kumlinda mwekezaji?

Mheshimiwa Spika, Ajali za barabarani na rushwa kwa Askari wa Usalama Barabarani. Kwa mujibu wa Ripoti ya Haki za Binadamu 2012, ajali za barabarani zinashika nafasi ya pili nchini kwa kusabisha vifo baada ya Malaria. Sababu zilizotajwa na ripoti hiyo kusababisha ajali ni rushwa iliyotawala kwa Askari Polisi wa barabarani ambao muda mwingi wanajishughulisha zaidi kuomba rushwa kwa madereva huku ajali zikiendelea kutokea. Aidha, uendeshaji wa hovyo wa madereva na mwendokasi vimetajwa na ripoti hiyo kama visababishi vyaa ajali.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa majibu mbele ya Bunge hili Askari wa Usalama barabarani wanasaidiaje kupunguza ajali za barabarani?

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2012/2013; Mnamo mwaka 2012/2013, Jeshi la Polisi lilitengewa jumla ya shilingi bilioni 335.605 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na fedha za Maendeleo, mpaka mwezi Februari, 2013 jumla ya shilingi bilioni 232.750 tu ndio zilikuwa zimetolewa ikiwa ni sawa na asilimia 69.3 ya fedha zilizokuwa zimetengwa. Aidha, hakukuwa na kiasi chochote cha fedha kilichokuwa kimetolewa na Hazina kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na fedha kutokutolewa kwa wakati, lipo tatizo kubwa la baadhi ya vikosi, Mikoa na Wilaya kutokupata fedha kwa wakati ama chini ya kiwango kilichoidhinishwa na Bunge kama ifuatavyo:-

Fungu 28, kifungu 2002 - *Police Marine* waliidhinishiwa shilingi milioni 767.2 ila mpaka Februari walikuwa wamepokea kiasi cha shilingi milioni 147.438 tu. Kifungu 2006 - Polisi Anga (*Airwing*) waliidhinishiwa shilingi bilioni 1.777 ila mpaka Februari, 2013 walikuwa wamepokea kiasi cha shilingi milioni 95.364 tu. Kifungu 2008 - FFU waliidhinishiwa kiasi cha shilingi milioni 818.030 ila mpaka Februari 2013 walikuwa wamepokea kiasi cha shilingi milioni 147.365 tu.

Mheshimiwa Spika, kifungu 2009 - Polisi wa Usalama Barabarani waliidhinishiwa kiasi cha shilingi milioni 161.455 na mpaka Februari, 2013 walikuwa wamepokea kiasi cha shilingi milioni 78.354 tu. Kifungu 2012 - Kanda Maalum ya Dar es Salaam iliidhinishiwa shilingi bilioni 1.012 mpaka mwezi Februari ilikuwa imepokea kiasi cha shilingi milioni 153.425 tu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mwenendo huu wa Jeshi la Polisi kutokupewa fedha kwa wakati, hali ni ya tofauti sana ukienda kwenye Kitengo cha Upelelezi (*CID*) kifungu 7001, ambacho walikuwa wameidhinishiwa shilingi bilioni 6.191, ila mpaka mwezi Februari 2013 walikuwa wametumia kiasi cha shilingi bilioni 12.359 yaani nyongeza ya zaidi ya asilimia 100 ya kiwango kilichokuwa kimeidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kitengo hicho kutumia fedha nyinyi kiasi hicho, lakini randama ya Wizara inaonesha kuwa upelelezi wa makosa makubwa ya jinai 72,765 ulifanyika na ni kesi 32,775 tu ndio zilifikishwa Mahakamani na washtakiwa waliokutwa na hatia ni asilimia 11.6 tu ya kesi zote zilizofikishwa Mahakamani. Pia ni askari 511 tu ndio waliweza kupata mafunzo ya Intelijensia na Upelelezi kwa mwaka huo wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani, inataka kupata majibu kuhusiana na masuala yafuatayo:-

(i) Ni kwa nini fedha kwa ajili ya matumizi kwenye vikosi vyta Polisi mwenendo wake umekuwa ni wa kusuasua sana kwenye mwaka wa fedha uliopita, hasa kwenye Mikoa na Wilaya nchini?

(ii) Je, kiasi cha bakaa iliyokuwa bado haijatolewa kitaweza kutolewa ifikapo mwishoni mwa mwaka huu wa fedha?

(iii) Je, ni kwa nini mpaka mwezi Februari hapakuwa na fedha yoyote iliyokuwa imetolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambayo ilipaswa kufanywa na Jeshi la Polisi?

(iv) Ni kwa nini Kitengo cha Upetelezi (*C/D*) kilitumia zaidi ya kiasi cha fedha ambacho kilikuwa kimeidhinishwa na Bunge, wakati kiwango cha makosa yaliyoweza kupelelezwa na uwiano wa washtakiwa kutiwa nguvuni Mahakamani haviendani au ndio kusema hapakuwa na ushahidi kutokana na watu kubambikiwa kesi?

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Magereza; mwaka wa fedha 2012/2013, Fungu 29 - Jeshi hili lilitengewa jumla ya shilingi bilioni 114.358 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na kiasi cha shilingi bilioni 1.555 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi mwezi Februari, 2013 fedha iliyokuwa imetolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ilikuwa ni kiasi cha shilingi bilioni 76.517 na fedha kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ilikuwa kiasi cha shilingi milioni 327.000 tu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mwenendo huu wa fedha, ni dhahiri kuwa, Jeshi la Magereza limeshindwa kupata fedha kwa ajili ya kuboresha Magereza yetu, na hata kukarabati nyumba, ofisi na makazi ya Askari Magereza kote nchini. Hivyo, kuendelea kufanya maisha ya mahabusu, wafungwa na Askari Magereza kuendelea kuwa mabaya na wakiendelea kupata mateso kutokana na kukosekana na miundombinu thabitii kwenye Magereza yetu.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inasikitishwa sana na hali hii ya Magereza kutokutengewa fedha na hata zikitengewa huwa hawapewi kwa wakati na sasa Jeshi hili limegeuka na kuwa mdaiwa sugu, kwani mpaka Februari,

2013 jumla ya madeni yote walikuwa wanadaiwa kiasi cha shilingi bilioni 35.330 na kiasi hicho kilikuwa kimegawanyika kama ifuatavyo:-

Bilioni 12.547 ni madeni ya Askari Magereza, bilioni 18.838 ni madeni ya wazabuni waliota huduma mbalimbali kwa ajili ya wafungwa Magerezani na shilingi bilioni 3.994 ni madeni kwa ajili ya umeme na maji.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mwenendo huu wa fedha kidogo kutengwa kwa ajili ya Magereza imepelekea kuwa na msongamano mkubwa sana kwenye Magereza yetu hapa nchini na kwa sasa uwezo wa Magereza yetu ni kuwa na wafungwa 29,552, ila mpaka tarehe 1 Februari, 2013 walikuwepo wafungwa 34,355. Hali hii Kambi Rasmi ya Upinzani haikubaliani nayo kwani ni kinyume na haki za binadamu na kamwe hatutakuwa tayari kubariki vitendo vya uvunjaji wa haki za binadamu wa aina yoyote.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lipo katika Fungu 14 na katika mwaka wa fedha 2012/2013, zilitengwa jumla ya shilingi bilioni 16.967 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na hazikutengwa fedha zozote kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo zilizokuwa zimetengwa kwa mwaka huo wa fedha. Aidha, hadi mwezi Februari 2013, ni asilimia 40 tu ya fedha ambazo zilikuwa zimetengwa ndio zilikuwa zimetolewa na Hazina.

Mheshimiwa Spika, kutokana na serikali kutotoa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa wakati kwa ajili ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kumesababisha madhara mbalimbali kama vile kushindwa kununua vitendea kazi mbalimbali kama vile madawa ya kuzima moto, magari ya zimamoto, kutoa mafunzo kwa ajili ya Askari wa Zimamoto na kushindwa kujenga vituo vipyta vya Zimamoto.

Mheshimiwa Spika, aidha, kutokana na hali hiyo, Jeshi hili limeshindwa kukabiliana na majanga ya moto yanayotokea hapa nchini kama vile kushindwa kuzima moto kwenye maeneo mbalimbali, kushindwa kukabiliana na

maafa kama kuperomoka kwa ghorofa Dar es Salaam, kutokana na kukosekana kwa vifaa vyta kisasa kwa ajili ya kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani, inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa Jeshi hili sasa linapewa kipaumbele ili liweze kukabiliana na maafa mbalimbali ya moto yanayotokea hapa nchini na kuweza kuokoa mali za wananchi ambazo zimekuwa zikiteketeta.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani 2013/2014. Miradi ya Maendeleo mwaka 2013/2014; kwa mujibu wa randama iliyowasilishwa na Wizara, Fungu 28 limetengewa jumla ya sh. 8,980,451,000/= kwa ajili ya miradi ya Maendeleo na katika mgawo huo ni kuwa kiasi cha shilingi bilioni tano ndio fedha za ndani na zilizosalia ni utegemezi kutoka kwa wahisani/wafadhilli.

Mheshimiwa Spika, jambo la kusikitisha ni kuwa pamodzi na matatizo lukuki yanayolikumba Jeshi la Polisi bado Serikali haja ya kuongeza fedha za kutosha kwa ajili ya miradi ya maendeleo ili kuweza kukabiliana na changamoto zinazolikumba Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, hakuna fedha zilizotengwa kwa mwaka huu wa fedha kwa ajili ya kuimarishe doria baharini (kifungu 6108), hakuna fedha kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya Polisi (*rehabilitation of police building*, kifungu 6303) na fedha iliyotengwa kwa ajili ya kujenga ofisi na makazi ya askari wetu ni shilingi bilioni mbili tu (kifungu 6302), vile vile hakuna fedha kwa ajili ya kununua vifaa vyta mawasiliano kama magari kwa ajili ya kuhakikisha kuwa doria inaimarishwa.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani, haikubaliani na mgawanyo huu wa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo na tunaitaka Serikali kutenga fedha kwa ajili ya makazi ya Polisi, ukarabati wa vituo na sero za Polisi pamodzi na fedha kwa ajili ya fulana za kuzuia risasi ili kuwalinda askari wetu pindi wanapokuwa wakipambana na wahalifu. Serikali

imewaaahidi sana Polisi kuhusu makazi bora, sasa sio muda wa ahadi tena ila uwe muda wa kutekeleza ahadi hizo kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, ni haki ya Kikatiba ya kila raia wa Tanzania kulindwa yeye na mali yake na kuishi kwa uhuru na amani katika nchi yetu. Kwa kuwa watu ndio msingi wa Taifa lolote lile duniani, wajibu wa kwanza kabisa wa Serikali yoyote ni kuwalinda watu na mali zao.

Mheshimiwa Spika, wananchi huuza uhuru wao kwa kuipa Serikali mamlaka na madaraka yote kumiliki vyombo vyote vya Dola ili iwalipe wananchi ulinzi na usalama. Kwa hiyo, kama Serikali imepewa mamlaka yote na wananchi na inashindwa kutimiza jukumu lake la msingi la kuwalinda wananchi na mali zao, kwa vyovyote vile Serikali ya namna hiyo haina uhalali wa kuendelea kutawala.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ijitazame upya na kuona kama ina uhalali wa kuendelea kutawala ilhali kuna matukio makubwa ya kigaidi na kijambazi yanayofanywa dhidi ya raia wasio na hatia bila hatua madhubuti za kukomesha uhalifu huo kuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasikitishwa kuona Serikali ikiwadhulumu wananchi kwa kuendelea kukaa kimya juu ya mambo mengi yasiofaa yanayoendelea kutokea katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, hivyo Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa wito kwa wananchi wote kupima utendaji wa Serikali hii ya CCM na kama hawaridhishwi na utendaji wa Serikali, basi wachukue hatua kwa kuchagua Serikali mbadala itakayoongozwa na CHADEMA ifikapo 2015.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mazoea ya Serikali kubeza hoja za Kambi Rasmi ya Upinzani, lakini ukweli unabaki pale pale na pia wito kwa wananchi wote waendelee

kutuunga mkono kwa kuwa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inayoongozwa na CHADEMA imedhamiria na imejipanga vizuri kutwaa madaraka ya Dola ifikapo 2015.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kuwasilisha. (*Makof!*)

SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge kwa muda huu tulionao, natangaza watakaochangia. Namwita Mheshimiwa Godfrey Zambi atafuatiwa na Mheshimiwa Jaku Hashimu Ayoub, Mheshimiwa Esther Matiko, Mheshimiwa Mustapha Akunaay, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa James Lembeli Mheshimiwa Sabreena Sungura na Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, Mheshimiwa Amina Clement na Mheshimiwa Aliko Kibona. Mheshimiwa Godfrey Zambi!

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi kuwa mchangaiji wa kwanza kufuatia hotuba iliyowasilishwa na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Dkt. Nchimbi.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nianze kwa kumpongeza sana Waziri pamoja na Jeshi la Polisi, Magereza, Zimamoto na Mambo ya Ndani kwa kazi nzuri ambayo wanafanya katika nchi yetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, ujisikiliza Hotuba ya Kambi ya Upinzani ya CHADEMA, siamini kama ni Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, lakini ni ya CHADEMA kwamba, Jeshi la Polisi limekuwa linaitetea Serikali ya Chama cha Mapinduzi, sijui limekuwa linafanya kwa Chama cha Mapinduzi, lakini ni ukweli ambao hauwezi kipingika kwamba, Serikali iliyoko madarakani ni Serikali ya Chama cha Mapinduzi na kwa maana hiyo Serikali hiyo ina jukumu la kuhakikisha kwamba Watanzania hawa pamoja na mali zao wanangaliwa vizuri na Jeshi letu la Polisi.

Mheshimiwa Spika, naomba nimweleze Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi pamoja na *IGP* wasonge

mbele, wafanye kazi. Msitegemewe kusifiwa na Chama kingine chochote cha Upinzani maana nia yao eti sijui kama itawezekana, ni kuchukua nchi. Sasa lazima wawaseme vibaya Watanzania wakate tamaa. Naomba niseme Jeshi la Magereza, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi songa mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kuna Mwandishi mmoja aliwahi kusema hivi na naomba niseme kwa lugha yake aliyosema: "*I have learned that to ignore the facts does not change the facts.*" Anasema kuukataa ukweli hakuondoi ukweli. Hiyo ni tafsiri yangu. Lakini ni ukweli kwamba, Jeshi la Polisi limekuwa linafanya kazi kwa maslahi ya Watanzania pamoja na wananchi wote wa nchi hii bila kujali itikadi za Vyama vyaa Siasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini Wapinzani wanataka Jeshi la Polisi liimbe nyimbo zao, haiwezekani hata siku moja. Mfanye michezo mnavyotaka, mwandamane wakati wote, mtukane viongozi, Jeshi la Polisi liendelee kuwachekea, haiwezekani. Ikifika wakati huo Jeshi la Polisi litaonekana la ajabu sana kama haliwezi likaangalia kwamba, haki za Watanzania wote zinalindwa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naomba viongozi wasikatishwe tamaa waendelee mbele wasonge mbele na Watanzania wote wenye nia njema wanaona kabisa Jeshi la Polisi na majeshi yote yanafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kumekuwa na hali ya uvunjifu wa amani kama alivyosema Waziri wa Mambo ya Ndani na Wizara hii ningesema kwamba, imekuwa na uvumilivu wa ajabu sana, lakini kubwa zaidi Mheshimiwa Rais amekuwa mvumilivu sana.

Mheshimiwa Spika, katika nchi ambazo Rais angekuwa mkali, nadhani Upinzani sijui kama ungekuwa kwenye hali iliyopo leo. Ukweli ni kwamba, Rais wetu ni mpole.

Maana Rais huyu ametukanwa amenyamaza, amedhalilishiwa amenyamaza na Wapinzani wanaona sawasawa.

Mheshimiwa Spika, nadhani tumsifu Rais kwa uvumilivu huo, lakini kimsingi Wapinzani wanataka kufanya kazi vibaya na Taifa hili lisitawalike ili waweze kutawala. Nadhani hali hii Serikali ya Chama cha Mapinduzi, Waziri Mkuu yupo, Waziri wa Mambo ya Ndani yupo *IGPyupo*, hatuvezi kuivumilia hata kidogo lazima tuone kwamba, wanafanya kazi sawasawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niseme jambo moja linalohusu Wilaya ya Mbozi. Mwaka 2007/2008, nilisema hapa Bungeni kwamba, Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Mbozi pale Vwawa kiko katika hali mbaya sana. *IGP*ameshawahi kuwa *RPC* kule Mbeya, anakifahamu kituo hiki, kiko barabarani, ni cha miaka ya 1960. Kiko kwenye hali mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2007/2008, niliposema, jibu la Serikali lilikuwa kwamba, kiko kwenye mpango wa miaka mitano, tangu wakati huo kituo hicho ambacho kina hali mbaya sana hakijawahi kukarabatiwa kwa namna yoyote ile, tofauti na ahadi ya Serikali kwamba, kiko kwenye mpango wa miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, bajeti tunayoipitisha ni ya mwaka 2013/2014, bado kituo kile hakijawahi kuchukuliwa hatua yoyote kwa maana ya ukarabati. Naomba Waziri awaeleze Wanambozi kwamba, kituo kile baada ya ahadi waliyopewa mwaka 2007/2008, sas kitakarabatiwa lini au kitajengwa lini?

Mheshimiwa Spika, nyumba za Askari Polisi pale Vwawa zinatia aibu, wanaziba nguo, wanaziba magunia na mtu yoyote anayepita kwa sababu nyumba zipo kituoni, zinatia aibu sana. Naomba Serikali ilifanyie kazi jambo hili kwa ukaribu sana na ni vizuri pia ningepata taarifa ya Waziri kwamba anapanga kuchukua hatua gani.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kidogo suala la

Magereza. Magereza wamekuwa wanajishughulisha na kazi nydingi sana katika nchi yetu, kubwa ikiwa ni pamoja na utengenezaji wa samani za maofisini, lakini pia na shughuli za kilimo. Naomba nizungumzie suala la utengenezaji wa samani.

Mheshimiwa Spika, wakati wote na kwa sehemu kubwa, Serikali inaaagiza samani kutoka nje ya nchi. Lakini tunaacha Jeshi la Magereza ambalo kwa sehemu kubwa linatengeneza vifaa hivi kwa uzuri sana. Naomba tuishauri Serikali, badala ya kuendelea kutumia pesa nydingi sana kwa ajili ya kuagiza samani nje mpaka leo, kazi hii ifanywe na Magereza. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, fedha za Watanzania zatabaki nchini na nikupongeze wewe mwenyewe kwa kusema kwamba, samani zote za ofisi za Wabunge zitatengenezwa na Jeshi la Magereza. Kwa hiyo Bunge tumeonesha njia na naomba na taasisi nydinge zote za Serikali zioneshe njia kwa maana ya kuagiza samani za ofisi katika Jeshi letu la Magereza ili tuweze kuliwezesha na kwa maana hiyo Serikali iweze kuokoa pesa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa. Tumeanza kupata vitambulisho vya Utalifa, lakini kasi ambayo inaendelea sasa ni ndogo sana. Naomba Serikali kwa makusudi kabisa iongeze pesa kwa ajili ya Mamlaka hii ya utengenezaji wa vitambulisho ili vitambulisho hivi vitengenezwe kwa muda mfupi inavyostahili.

Mheshimiwa Spika, Wabunge tumeshapata vitambulisho lakini kimsingi hata familia zetu hazijapata vitambulisho, Watanzania wengi kule vijijini hawajapata vitambulisho. Hatujui vitapatikana lini kama utaratibu wa utoaji wa fedha kwa ajili ya Mamlaka hii utakuwa ulivyo leo. Kwa hiyo, naomba suala hili liwe la kasi ili upatikanaji wa vitambulisho uweze kuwa wa mapema inavyowezekana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo napenda

nizungumze, ni suala la usalama barabarani. Kwanza niwapongeze Polisi wa Usalama wa Barabarani, wanafanya kazi nzuri pamoja na kasoro zinazojitokeza, lakini kimsingi wanajitahidi. Nataka kuamini kwamba, kusingekuwa na watu wa usalama barabarani, nadhani huko barabarani kungekuwa na vioja vikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, jambo ambalo linanisikitisha na tumezungumza mara kadhaa hapa Bungeni, magari yakiharibika barabarani, mawe yanawekwa na miti mikubwa inakatwa, inawekwa barabarani. Magari yale yakishatengenezwa yakiondoka, miti ile inabaki barabarani.

Mheshimiwa Spika, siku moja nilinusrika kupata ajali kwa sababu nilikuwa naendesha usiku na watu wameweka miti barabarani, unafika hapa na hapa unagundua kwamba kuna miti, lakini mbele hakuna hiyo gari iliyoharibika. Watu wameondoka baada ya kutengeneza gari lao na miti imebaki barabarani.

Mheshimiwa Spika, sasa niliombe sana Jeshi la Polisi na kwa sababu wanakuwa barabarani, magari yanapoharibika yakanatengenezwa, basi takataka zinazowekwa barabarani ziondolewe. Lakini watu wote wenye magari wanaelekezwa kuwa na alama ambazo zinaashiria kwamba mtu amepata tatizo barabarani. Sasa badala ya kuweka zile alama sisi tunaweka miti na mawe, hali hii ni ya hatari sana.

Mheshimiwa Spika, naamini kuna watu wameshapata ajali kwa sababu ya magogo pamoja na miti ambayo inawekwa barabarani. Naomba hali hiyo irekebishwe, vinginevyo itatuletea tabu sana.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nizungumzie suala la Zimamoto. Jeshi la Zimamoto limepata lawama sana kwamba halifanyi kazi vizuri. Lakini ni ukweli usiopingika kwamba, zana ambazo Jeshi la Zimamoto linazo bado ni duni, bado ni chache na hatuwezi kufika katika maeneo mengi.

Mheshimiwa Spika, tusilaumu tu, lakini tuangalie je, wana zana za kutosha kuwawezesha kufanya kazi? Vyovyote vile hawana hizo zana za kutosha. Kwa hiyo, naomba Serikali chini ya Wizara hii ihakikishe kwamba, wanapatiwa zana za kutosha ili waweze kufanya kazi zao vizuri na kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ni kwa Jeshi la Uhamiaji. Jeshi la Uhamiaji limekuwa linapata lawama kwamba, watu ambao si raia wa Tanzania wameingia kwenye mipaka yetu na hasa ukanda wa kaskazini ambako kumekuwa na lawama kubwa sana. Jeshi hili limelaumiwa kwa maana ya kwamba, linaingia kwenye mikataba michafu, baadhi ya watu sio waaminifu ndani ya Jeshi hili, wanalipaka matope Jeshi zima la uhamiaji kwamba, wanakula rushwa na kuruhusu watu kuingia nchini.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Wizara ya Mambo ya Ndani, ihakikishe kwamba Jeshi la Uhamiaji hasa mipakani linafanya kazi kwa uadilifu mkubwa ili kuzuia wahamiaji haramu katika nchi yetu. Kwa maana hiyo, tunaweza tukafanya nchi yetu isitawalike na kukawa na machafuko katika nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niendelee kuishauri Wizara ya Mambo ya Ndani iendelee kufanya kazi kwa uadilifu kama ambavyo inafanya sasa. Mambo mengine yaliyopo ni changamoto ambayo Serikali ya CCM ni sikivu na itaendelea kuzitatua kwa kadri ya hali ya pesa inavyoruhusu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Vita Kawawa atafuatiwa na Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa kuwa mtu wa pili kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Mambo ya Ndani. Kwanza kabisa Waswahili wanasesma "Mdomo huponza Kichwa."

Sasa kuna kauli zilisemwa nchini kwamba, itahakikishwa nchi hii isitawalike. Kwa hiyo, haya mambo yanayotokea tuna wasiwasi nayo na hali ya mdomo uliotamka uko nyuma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa nirudi katika hotuba yangu, ajali za barabarani ni moja ya suala kubwa katika jamii yetu kiusalama, kiafya na kiuchumi. Hali ya usalama barabarani imekuwa ikizirota na hii inahatarishwa na kila magari yanavyoongezeka.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa inaaniszisha mipango mbalimbali katika kujaribu kupunguza tatizo la usalama barabarani. Moja ya mipango hiyo ilikuwa ni utoaji wa leseni mpya ambazo zitasaidia kupata taarifa zote za madereva waendeshao magari nchini ambayo iligharamiwa na madereva wenyewe na Serikali. Pia mipango ya miradi mingine mbalimbali kama vile ya kudhibiti mwendo barabarani.

Mheshimiwa Spika, lakini takwimu zinaonesha jumla ya idadi ya ajali zimeongezeka kutoka mwaka 2000 mpaka 2008 kwa asilimia 42. Yaani mwaka 2000 ajali zilikuwa 14,500 mpaka mwaka 2008 ajali zimeongezeka kufikia ajali 20600. Pia idadi ya watu waliofariki katika ajali hizi wamefikia asilimia 67.

Mheshimiwa Spika, mbali na kupoteza maisha ya watu wetu, pia zinaathiri kwa kiasi kikubwa uchumi na wahanga wa familia zilizoondokewa na watu wao.

Mheshimiwa Spika, sasa kutohana na takwimu hizi za Polisi ambazo zinasema asilimia 75 ya ajali hizi zinachangiwa na makosa ya kibinadamu. Makosa haya ya kibinadamu yako mengi, kuna uzembe wa dereva, lakini pia kuna uzembe wa wenyе magari kutoyafanyia matengenezo ya mara kwa mara au *service* maga yao.

Mheshimiwa Spika, tulianzisha leseni mpya na sababu mojawapo ni kutambua makosa ya madereva. Swali langu

kwa Serikali na Jeshi la Polisi, je, leseni hizi mpya mpaka sasa wana rekodi ya kiasi gani ya kutambua makosa ya madereva yaliyofanywa, ili mwisho wa siku dereva aweze kuadhibiwa kwa makosa ambayo anayarudiarudia kila mara?

Mheshimiwa Spika, lazima kuwe na kumbukumbu ambazo mtazifutilia kwa wavunja Sheria barabarani; awe dereva wa Waziri, awe dereva wa Mbunge, awe dereva wa malori, wa mabasi ya watu binafsi, wote wafuatiliwe kwa kumbukumbu ya makosa watakayofanya na Jeshi la Polisi litakazoziveka katika kumbukumbu zenu.

Mheshimiwa Spika, suala la pili, Polisi haina uwezo wa kukagua magari, uzima wake kiundani. Kazi ya Polisi kuangalia matairini, kadi za gari, leseni na vipima mwendo pekee haitoshi kwa usalama barabarani. Ushauri wangu lazima Serikali ilete Sheria ya kusaidia kazi ya ukaguzi wa magari, malori na mabasi na utoaji wa *certificate* ya kuruhusu gari kuingia barabarani kutokana na uzima wake.

Mheshimiwa Spika, nashauri kazi hii ifanywe na *garages* binafsi zitakazotambuliwa rasmi na Serikali kwa mfumo wa *PPP* ili kila baada ya kilomita kadhaa malori, mabasi na magari yanayosafiri mara kwa mara yaweze kwenda *garage* kufanyiwa matengenezo na kubadilishwa baadhi ya vipuri. Hii itatusaidia sana kupunguza ajali barabarani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, malori na mabasi mengi ni mitumba lazima yakaguliwe kwa lazima na hii *compulsory vehicle inspection* itasaidia pia pato kwa Serikali na kuimarisha usalama barabarani.

Mheshimiwa Spika, jambo llingine, tulipofanya maamuzi kuruhusu pikipiki kuwa moja ya usafiri utakaosaidia kutoa huduma Mijini na Vijiji tulikuwa pia na maana ya ajira kwa vijana walio wengi katika kariba hii wanaoendesha pikipiki.

Mheshimiwa Spika, pikipiki zimetusaidia sana vijana wetu wameweza kupata ajira. Lakini ndiyo imekuja kuonekana pia kuwa inasaidia sana kukuza uchumi wa vijana wetu au kufanya uchumi wa familia zinazopata pato lake kwa mara moja kwa mwaka, baada ya kuuza mazao yao hununua pikipiki, na inafanya familia hizo kuwa wanapata pato la kila siku na kusaidia familia zao.

Mheshimiwa Spika, pikipiki zimekuwa zikisaidia sana kwetu vijiji kubeba wagonjwa na nyingine mpaka zinabeba maiti. Lakini pia kupeleka mazao sokoni. Sasa tunaomba, kwa kuwa jambo hili la pikipiki maeneo yetu ya vijiji limekuja kwa kasi sana, kunakuwa na makosa mengine siyo ya makusudi, ni ya kutokufahamu tu kwa waendesha pikipiki.

Sasa tunaomba basi, Serikali kuwaelimisha waendesha pikipiki kwa Vijiji na katika Kata zetu za Vijiji kama zinavyofanyika Mijini ili waweze kufahamu sheria ya vyombo hivi vya moto. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tusiachie baadhi ya vijana wetu Askari Polisi kuona ndiyo mradi wa kupatia fedha kwa kuwanyanya waendesha pikipiki za vijiji. Ana kosa, hana kosa akisimamishwa anatakiwa kutoa fedha bila risiti. Hili ni tatizo kubwa sana ambalo linaleta chuki baina ya waendesha pikipiki vijiji kwetu na Jeshi letu la Polisi. Kwa hiyo, tunaomba sana Jeshi letu la Polisi litoe elimu kwa vijana wetu hawa, lakini pia liweze kusaidia vijana wetu waweze kuendeleza uchumi wa nchi yao, uchumi wa vipato vyao na familia zao.

Mheshimiwa Spika, ni hayo. Naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Matiko na Mheshimiwa Mustapha Akunaay ajiandae.

MHE.JAKU HASHIM AYOUB: Mheshimiwa Spika, kabla ya yote, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeweza kuniwezesha kusimama hapa na kuvuta pumzi yake.

SPIKA: Sina uhakika kama unasikia huko!

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Kabla ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu aliyoinezesha kusimama hapa na kuniazima pumzi yake.

Mheshimiwa Spika, vilevile nitakuwa siyo mwinci wa fadhlila kama sitakushukuru wewe kwa kunipa fursa hii adimu kwangu mimi. Vilevile nataka nitoe pole kwa wananchi wa Arusha kwa mtihani walioupata, ni mtihani wetu sote, niwatakie majeruhi afya njema na waweze kupona haraka. Baada ya hapo nampongeza Mheshimiwa *IGP*kwa kazi nzuri aliyoionesha tokea kuingia kwake kwa kuweza kupunguza uhalifu wa kutumia silaha za moto. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia kuingia kwake kumeleta maendeleo makubwa kwa kipindi hiki na kutokuvamiwa kwa benki. Kila baada ya muda mabenki yalikuwa yanavamiwa na kuchukuliwa pesa. Takwimu zinaonyesha kwamba Januari hadi Desemba, 2012 na pia Januari hadi Aprili, 2013 uhalifu umepungua kwa 4.3% kutokana na jumla ya matukio makubwa ya jinai 72,765 yaliyori potiwa Polisi. Kutoka kipindi cha Januari hadi Desemba, 2012 kuna matukio 76,052 ikiwa ni sawa na pungufu ya matukio 3287 kwa sawa na 4.3%.

Mheshimiwa Spika, sina sababu ya kutolipongeza Jeshi la Polisi kwa kazi nzito waliyoifanya pamoja na ukosefu wa vitendea kazi katika mazingira magumu Polisi wanayofanya.

Mheshimiwa Spika, ama mpaka sasa hivi sijamjua mrithi wa /GP ni nani kutokana na utulivu wake, usikivu wake na utendaji wake wa kazi. Kuhusu mpango wa kuboresha Jeshi la Polisi kwa umuhimu mkubwa, Serikali ni lazima iipe uzito mpango huu kwa sababu una umuhimu mkubwa katika kupambana na vitendo nya uhalifu.

Mheshimiwa Spika, nigosie suala la Haki za Binadamu kwa wafungwa na Mahabusu. Hapa napata masikitiko makubwa kwamba limekuwa halizingatiwi kwa vile bado wananyimwa haki na uhuru wa mawazo kinyume na kifungu cha 18 cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977 ya Tanzania ambayo inaeleza: "*Kila mtu ana uhuru wa kutoa maoni na kueleza.*"

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoka hapo, nieleze kuhusu usalama wa Viongozi wetu Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Usalama wa Viongozi wetu hasa Makamu wa Kwanza wa Rais na Makamu wa Pili wa Rais. Gari wanazozitumia kwa ajili ya *escort* haziridhishi. Naomba Serikali itafute gari mpya katika ku-*escorts*. Gari zile wakati mwingine tunashuhudia zinasimama njiani, haziwezi kupita kwenye mashimo. Usalama wa Viongozi wetu umekuwa mdogo kwa gari mbili za *escort* kwa Mheshimiwa Makamu wa Kwanza wa Rais na Makamu wa Pili wa Rais, yaani vimulimuli hivi, maarufu tunaviita visakina.

Mheshimiwa Spika, nikitoka hapo, nije katika kesi za watoto za uzalilishaji hasa katika Zanzibar kuna kesi 127 zilitofunguliwa mwaka 2012, na kesi 66 zilitopatiwa ufumbuzi, kesi tatu Mahakama na Mkurugenzi wa Mkurugenzi wa kesi za Jinai alikuwa na masikitiko sana kuhusu utendaji wa kazi wa Polisi. Kesi zimetupwa, watoto wananyanyasika; nahitaji maelezo hapa ni kesi tatu zilitopatiwa hukumu. Sijui kuna Askari gani mabingwa kule wanaopeleleza kesi hizi. Naomba itolewe taaluma kwa Askari Polisi wa Upelelezi wakapewa ujuzi nije na ndani ya nchi. Kumekuwa na kilio kikubwa kesi 127 na tatu tu ndizo zilitopata ufumbuzi na nyiningine kutupwa nije.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, nije katika chombo kimoja muhimu cha *DNA*. Zanzibar chombo hicho kimekuwa hakipatikani kwa muda mrefu sasa. Sijui Serikali kuititia Wizara ya Mambo ya Ndani ina mpango gani kupeleka chombo hiki.

Mheshimiwa Spika, nije na kilio cha mwisho kwa kumalizia. Makazi duni ya Polisi Unguja na Pemba sehemu ya Madungu na sehemu ya Ziwanu maarufu panaaitwa Bomani. Nyumba zile tokea Ukoloni mpaka hii leo hazijafanyiwa matengenezo, enzi za Said Khalifa. Chumba kimoja wanaishi mtu na mkewe. Sehemu ya faragha haipatikani, na cha kusikitisha zaidi, banda la choo liko nje kabisa, maana hata mtu akitoka na kanga unajua shughuli inayokwenda kufanyika. Ni jambo la kusitikisha sana. (*Kicheko/Makofi*)

Kuna barabara za ndani (*feeder roads*) zimechimbika kupita kiasi, kiasi kwamba hazihitaji hata bajeti, na kuna hatari ya Askari kupoteza miguu yao wakiingia usiku mle.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, kuna Polisi wa Zanzibar wanakaribia miezi mitatu hawajapata mishahara yao. Sijui ni sababu gani! Waliambiwa akaunti zao zimekosewa na watu wameshafanya kazi miezi mitatu, wana familia zao na wanategemea kipato chao. Kwa muda mrefu wamehangaiwa wakaombwa akaunti zao hazionekani. Hii nitahitaji maelezo.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, kuna ubani ultolewa sijui kama ni amri ya Polisi au vipi! Wafiwa wanachangishwa fedha, ile maiti mpaka inaoza hizo fedha hazijawahidi kupatikana kwa mwaka mmoja. Naomba hili lingefutwa.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo hayo, nasubiri maelezo zaidi nipate kuunga hoja mkono. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa Esther Matiko na Mheshimiwa Mustapha Akunaay, dakika tano, tano.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza kabisa, napenda kuunga mkono hotuba ya Kambi ya Upinzani na naiomba Serikali iyachukulie yote yaliyoandikwa kwa uzito wake na iyafanyie kazi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nazungumzia kuhusu msongamano wa Mahabusu na Wafungwa katika Magereza yetu nchini. Msongamano wa Mahabusu na Wafungwa kwa kiasi kikubwa unasababishwa na ubambikwaji wa kesi kwa raia wetu wa Tanzania. Hii inatokana kwa njia moja au nyingine labda kutokujibika kwa Maaskari wetu au kukosa maadili.

Kwa *research* ndogo niliyofanya, unakuta raia wetu hawa wanabambikwa kesi nyingine ni za kisiasa kutaka kudhoofisha kazi ya upinzani, nyingine ni kutokana na mahusiano ya kijamili na upungufu wa Polisi, labda unakuta akimbambika mtu kesi, *then atamwomba fedha au rushwa na yeye akikosa kumpa, anaandikiwa kesi kubwa zaidi ya armed robbery au murder*. Nyingine pia unakuta Polisi labda kampenda msichana au mwanamke, na kesi hizi zipo anaamua kumbambikiza kesi mume wake au *partner* wake na kumwandikia kesi isiyo ya maana na hii hupelekeea msongamano. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, lakini kwa zile kesi ambazo ni za halali, ambazo zinakuwa Mahabusu wanapelekwa kule, tungependa basi Serikali wawe wanatoa dhamana. Maana kuna kesi nyingine zina dhamana lakini unakuta hawapewi dhamana na wanaendelea kulundikana mahabusu. Vilevile hata imependekezwa kwenye hotuba ya Kambi ya Upinzani kuwepo na vifungo vya nje ambavyo vinaweza kuambatana na *fine* au kupewa kazi mbalimbali za kijamii.

Ningependa kuzungumzia pia unyanyasaji wa raia na mauaji yanayofanywa na Jeshi la Polisi. Nimekuwa nikilizungumzia hili nadhani kwa kiasi kikubwa sana tangu nimeingia katika Bunge hili. Kuna mauji makubwa sana yanafanyika Tanzania na kwa kesi, nita-*cite* kesi ya Mkoani kwangu Mara.

Kwa mfano, tarehe 2/2/2009 kuna kijana mmoja anaitwa Paschal Mwita alipigwa risasi ya mgongoni akiwa shambani anavuna mahindi katika Kijiji cha Magoto, Wilayani Tarime. Yule Askari akaenda kituo cha Nyawamwaga na kuripoti kwamba amemjeruhi mguuni kwa bahati mbaya wakati amempiga risasi mgongoni. Aliyejuwa Mkuu wa Wilaya kipindi hicho Wilaya ya Tarime, Mheshimiwa Kolimba, alikwenda mpaka kwa mzee huyo ambaye ni mlemavu, Mzee Paschal Rioba akaelezea kuwa ni kweli kuwa Askari huyo amefanya tukio lile na akaahidi kuwa Serikali itamchukulia hatua za kisheria.

Mheshimiwa Spika, wakampa fedha Sh. 20,000/= yule Mzee wakatengeneza jeneza, wakanunua mchele gunia, wakanunua na mafuta debe moja na kilo 25 za sukari, lakini pia walikwenda mbali, kwamba kwasababu yule mzee ni mlemavu na alikuwa na mtoto mmoja tu wakaahidi kwamba watakwenda kumhudumia kwasababu walikuwa akimtegemea yule kijana. Lakini mpaka leo cha ajabu hawajamhudumia yule Mzee na badala yake wamegeuza kwamba yule Askari hakutenda lile kosa.

Mheshimiwa Spika, napenda Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi ambayo inajinasibu kwamba inawajali raia, kwanza kabisa wawachukulie Sheria Maaskari ambao wanakwenda kinyume na maadili na kuendelea kuua raia wetu. Pili watekeleze wajibu wanaoutoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna mauaji mengi yanayoendelea na nimeshaleta kesi hii mpaka kwako ya wananchi wa Serengeti...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa Mzungumzaji)*

SPIKA: Ahsante. Muda umekwisha. Dakika tano, Mheshimiwa Akunaay.

MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Awali kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha nisimame mbele ya Bunge hili ili nitoe hotuba hii fupi. Pili, nawatolea salamu za pole wakazi wa Mjini wa Arusha kwa mtihani walioupata jana.

Mheshimiwa Spika, naanza na suala la maslahi ya Askari wote wa Mambo ya Ndani, makazi yao ni mabovu na mishahara ni midogo. Polisi wanapata taabu sana kupandishwa vyeo hata kuingia katika nyota ya kwanza hasa wale waliokuwa na shahada, kuna upendeleo mkubwa katika kupandishwa madaraja.

La pili, kutokana na muda, nitazungumza kuhusu vitendea kazi nya Polisi. Polisi hawana makazi mazuri, kama alivyoeleza mzungumzaji mmoja aliyepita, hali yao ni mbaya, naomba Serikali lwatazame, hasa magari. Nikichukulia mfano katika Wilaya yangu ya Mbulu, magari ni mabovu na Polisi wanasukuma magari. Watu waliokamatwa ndiyo wanasaidia kusukuma magari. Sasa ni Jeshi gani hili?

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri wa Mambo ya Ndani wakati wa kujumuisha aniambie gari ambalo alilitoa *Inspector General* kwa kituo cha Haidom katika Wilaya ya Mbulu liliishia wapi? Maana Dar es Salaam liliondoka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Usalama Barabarani; magari mengi yanapokamatwa na Polisi barabarani yanajazwa *Police Station* bila sababu yoyote. Aliye na kosa ni dereva, siyo gari. Sasa magari kujazwa Polisi, inaashiria kwamba magari hayo yamezuiliwa kwa *coupon*, yaani inatakiwa kitu kitoke ili yale magari yaachiwe.

Jambo la pili, kuhusu magari na Usalama Barabarani ni matumizi ya *traffic notification*. Polisi wanawaadhibu watu barabarani kwa kuwapa adhabu kwa makosa ambayo yanakuwa *shocked pale pale*, yaani yanatafutwa kwenye gari. Inatakiwa mtu anapoendesha gari, klabla hajasimamishwa na kuulizwa makosa, ajue awali kabisa anakwenda kuulizwa kosa gani. Imekuwa ni mtindo sasa wa

kutumia *traffic notification* kama mapato kwa Mapolisi. Kwa hili, watanisamehe.

Mheshimiwa Spika, tunaliheshimu sana Jeshi la Polisi, lakini Jeshi la Polisi linatumiwa vibaya sana na Wakuu wa Wilaya ambao wanashindwa kufanya kazi zao, wanawaamrisha vibaya. Sisi tunajua Polisi wanafanya kazi kwa *General Police Orders* ambao Mkuu wao Mkubwa ni *Inspector General*. Lakini sasa kuna ma-*Inspector General*/wa *Police* ambao wanapatikana katika kila Wilaya. Mkuu wa Wilaya akishindwa kazi zake, anataka kutembelea Kijiji fulani anachukua Jeshi la Polisi na kuwapigisha wananchi gwaride. Tunaomba jambo hili likome na Askari wafanye kazi kwa amri kama Sheria inavyotaka.

Mheshimiwa Spika, lingine ni mafunzo kwa Askari. Sheria zinabadilika mara kwa mara, tunaomba ili weledi wao uwe kama ni Askari wa leo, wafundishwe na komputa, lugha mbalimbali na waheshimu watu. Pia siyo kila mtu anayefika *Police Station* ni mhalifu. Maana unaweza kufika wewe ni mlalamikaji pale Polisi, halafu unaambiwa kaa chini! Sasa hajulikani kuwa nani hapa ni mlalamikaji na nani hapa ni mtuhumiwa?

Pili, tunaomba pale Polisi kuwe *counters* mbalimbali. *Counter* ya malalamiko na *counter* ya hawa watu walioshtakiwa. Siku nydingine mtu anayelalamika anaweza kulundikwa ndani bila sababu.

Mheshimiwa Spika, kabla muda haujawkwisha, naomba Polisi wazingatie haki ya binadamu katika kuwakamata watu na kuwatia ndani bila kuwapa dhamana. Kosa dogo tu, watu wamegombea mpaka wa ardhi, mtu anawekwa ndani masaa matatu, manne. Baadaye wanaambiwa nendeni mkapatane. Hili ni kinyume na haki za binadamu na mashauri ya ardhi kwanza hayhusiani na Polisi, ni mambo ya Mahakama za Madai.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Askari wa Magereza, tunawashukuru kidogo wameanza kuwatunza wafungwa,

lakini tunaomba sasa na wao wapewe elimu juu ya haki za binadamu ili wawatunze wale watu waliovunja Sheria, lakini waelewe kamba bado utu wao uko palepale. Wakitoka pale wanakuwa binadamu wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, naungana na Kambi ya Upinzani waliposema ni mara ngapi wanapata mlo kwa siku? Mtu kula mara moja kwa siku unamdhoofisha kiafya. Lakini huyu mtu anazalisha, na mashamba mengi ya Magereza yanazalishwa na wafungwa na wana-*subsidise* mapato yao.

Mheshimiwa Spika, nashukuru. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Ritta Kabati, atafuatiwa na Mheshimiwa Sabreena Sungura na Mheshimiwa Joseph Mbilinyi ajiandae.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, lakini nianze kwa kumpongeza Mbunge mwenzangu Mheshimiwa Aeshi kwa kushinda kesi yake pale Sumbawanga Mjini. Kidumu Chama cha Mapinduzi! (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo hii nitachangia kama Askari mwenye Namba AKC 4317, ambaye nimehitimu pale K. J. Msange Kituo Namba 23 chini ya Kiongozo Meja Mkalawa. Niwaambie kuwa changamoto zao zote nimeziwasilisha kwa maandishi, maana walikuwa na wasiwasi kuwa pengine hazijawafikia Serikali.

Mheshimiwa Spika, nitaanza mchango wangu kwa kulaani vikali kwa baadhi ya viongozi wa kisiasa nchini kwanza kuhamasisha wananchi kuvunja Sheria za nchi hii, wakati wao pia wanashiriki kutunga Sheria hizo na kusababisha Askari kutumia nguvu kubwa; kuwatukana Viongozi Wakuu wa nchi hii na kuwajengea chuki; kutukana Wabunge wa Viti Maalum katika majukwaa yao wakati wakijua kuwa na sisi ni Wabunge ambaao tumechaguliwa na tuna haki Kisheria; kuhamasisha vitendo vyta mauaji ya viongozi wa kidini na kuchoma

nyumba za ibada na tukio la jana lilitotokea kule Arusha.
(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya laana hizo, sasa nijielekeze moja kwa moja katika Wizara ya Mambo ya Ndani. Wizara hii imetengewa bajeti ndogo sana ukilinganisha na changamoto nydingi ambazo inakabiliana nazo.

Mheshimiwa Spika, Askari wa Jeshi hili wana matatizo makubwa sana. Wanaishi katika makazi duni, kila mwaka tumekuwa tukichangia na kila anayesimama kuchangia anachangia kuhusu makazi duni anayoishi Askari Polisi, vifaa vingi vya kazi wanavyovitumia Askari Polisi ni duni. Hakuna bajeti ya kutosha katika mafuta. Tumeshudia sisi wenye kazi vituo vingi matukio yanatokea hawana mafuta, wanashindwa hata kutimiza wajibu wao. Vile vile upandishwaji wa vyeo kwao ni tatizo kubwa. Pia kupata nafasi kwenda kusoma ni tatizo katika Jeshi hili na Askari wanacheleweshewa mafao wanapostaafu.

Mheshimiwa Spika, vile vile magari ya Askari ni mabovu. Suala hili la magari mabovu linanisikitisha, kwa sababu utaona katika Vituo hivi vya Polisi kwa mfano pale Kiheza *Line*, kuna magari sana mabovu na yamekaa pale kwa muda mrefu yanaharibika. Ukiuliza tatizo ni nini unaambiwa ni kibali. Sasa hiki kibali kinatolewa wapi? Ni bora yakauzwa kama chuma chakavu ili yaweze kuongeza pato kwenye Jeshi hili kuliko magari yamekaa miaka na miaka mpaka yanaharibikia pale kwenye vile vituo. Nitaomba kupata majibu wakati Waziri anajibu hoja hizi.

Mhehsimiwa Spika, labda nijielekeze kuhusiana na suala la makazi ya Polisi hasa katika Mkoa wetu wa Iringa. Mkoa wetu wa Iringa kwa kweli kama nilivyosema na nilishachangia toka huko mwanzo kwamba Askari wale wanaishi kwenye makazi mabovu sana kiasi kwamba hata akina mama wale na watoto wanapata shida, miundombinu katika nyumba zao ni mbaya sana, wanapata magonjwa. Vilevile ukienda katika Wilaya ya Mufindi, tatizo lipo pale pale. Ukienda Wilaya ya Kilolo mpaka leo bado hakujajengwa

Makao Makuu ya Polisi katika Makao Makuu ya Wilaya kwa sababu Kituo cha Kilolo kipo kama kilomita 70 kutoka Makao Makuu ya Wilaya. Hili ni tatizo kubwa kwa wananchi wanaoishi Kilolo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vilevile nizungumzie vitu nya Polisi. Vituo nya Polisi pia ni tatizo katika Mkoa wetu, kwa sababu utakuta vituo vingi sana havijajengwa, watu wanapata shida sana kupata hiyo huduma. Kwa mfano, watu wanatoka Kihesa, Kigonzile na Mkimbizi, hakuna Kituo cha Polisi mpaka uende kituo kikubwa.

Vilevile ukienda hata Mikoani na Wilaya zote vituo viko mbali na wananchi. Naomba Jeshi hili ijitahidi kuongeza pesa katika Mkoa wetu wa Iringa ili vite vituo viweze kujengwa.

Mheshimiwa Spika, lakini naomba nitoe pongezi kwa Kamanda wetu wa kikosi *RPC Kamhanda*, ameweza kuhamasisha sana ujengaji wa vituo. Kwa mfano, kuna Kituo cha Idodi amehamasisha wananchi wameanza kujenga, Kituo cha Ifunda na ameweza pia kujenga hata dawati la kijinsia. Tumejengewa kituo kizuri sana ambacho nafikiri utakapokuja kitakuwa ni kituo cha mfano katika nchi nzima. Ni kituo kizuri sana! Kwa hiyo, nampongeza na niwapongeze wananchi wote wa Iringa ambao wamejitahidi kulichangia Jeshi letu katika Mkoa wetu. Naomba Serikali sasa ijitahidi kuongeza kwa sababu bado hivi vituo havijakwisha ambavyo nguvu ya wananchi imetumika.

Mheshimiwa Spika, naomba niende moja kwa moja katika Jeshi la Zimamoto. Kwanza, nashukuru kwamba sasa hivi tuna Makamanda wa Mikoa, lakini tatizo liko pale pale kwamba Kamanda amekuja kuripoti, hana Ofisi. Kwa mfano, Yule aliyopo Iringa tunamshukuru amehamasisha Ofisi ya Kituo cha Zimamoto, ameweza kukaa pale lakini bado anatakiwa apate Ofisi yake.

Vilevile kuna tatizo kubwa sana la magari ya Zimamoto. Iringa sasa hivi Mji umekua na vite vite ukienda Mufindi tuna msitu. Ule msitu ni rasilimali kubwa sana ya pato

la nchi hii. Lakini pale hakuna gari. Kuna matukio yamekuwa yakinkeo mara kwa mara ya moto. Sasa gari inayokwenda kuzima moto katika msitu ule, linatoka Iringa Mjini. Sasa hivi barabara inatengenezwa, hebu *just imagine* hili gari litafika saa ngapi? Si litakuta moto umeshakolea?

Mheshimiwa Spika, vile vile ukienda *Nduli Airport*, hakuna gari la kuzima moto. Je, ajali ikitokea, mtafanyaje wakati ndege imeungua, hakuna gari; sasa mtaanza kuunda tena Kamati? Si mtakuwa mnapotiza pesa wakati tatizo tayari lipo? Kwanini msiweke gari la Zimamoto katika uwanja wetu wa ndege?

Mheshimiwa Spika, pia niende moja kwa moja katika Jeshi la Magereza. Jeshi la Magereza halikadhalika, matatizo yapo palepale! Lakini niwapongeze kwamba mmeanza kujenga jengo moja ambalo limechukua baadhi ya Askari, nami nilikuwepo wakati wa ufugazi, lakini bado tatizo lipo pale pale. Askari wengi wanaishi nje ya nyuma za Magereza. Kwa hiyo, tunaomba zile nyumba ziboreshwe na ziendelee kujengwa kwa wingi ili Askari wasipate matatizo makubwa.

Mheshimiwa Spika, lakini tatizo lipo pia kwenye Magereza la watoto wadogo kuchanganyika na watu wazima. Tatizo hili tumekuwa tukilizungumzia mara kwa mara kwamba watoto wetu wanapochanganyika na watu wazima kwenye Magereza, tunawajengea nini? Hawa si ndiyo wanaokuja kuwa baadaye majambazi sugu?

Naomba suala hili liangaliwe na tuweke mkakati wa kuhakikisha kwamba tunajenga bweni la watoto katika kila Gereza ili wasichanganyike na watu wazima.

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna msongamano mkubwa sana wa Wafungwa. Nafikiri tatizo kubwa, hata pale kwetu sio wafungwa, ila mahabusu. Kwa sababu kuna wafungwa 300 na mahabusu 700. Kwa hiyo, tunaomba pia kesi ziendeshwe kwa haraka ili kuendelea kusaidia kusiwepo na msongamano.

Mheshimiwa Spika, pia kunahitajika ujenzi wa Magereza. Gereza la Mgagao tunaishukuru Serikali kwamba sasa hivi kimekuwa kituo cha elimu. Lakini sasa kutahitajika kujengwa Gereza lingine, kutahitajika pia kujengwa nyumba nyingine kwa ajili ya Askari. Kwa hiyo, tunaomba Mkoa wa Iringa uangaliwe kupewa fungu kubwa. Nilikuwa naangalia katika kitabu cha maendeleo naona zimetengwa tu pesa kidogo kwa ajili ya kujenga nyumba nyumba tu, lakini sijaona kama Magereza wametengewa kitu chochote, wakati kuna changamoto kubwa sana katika Jeshi hili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Sabreena Sungura, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Mbilinyi dakika tano kila mmoja.

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii ya kuchangia. Kwanza kabisa, naunga mkono hotuba ya Kambi ya Upinzani. (*Makofii*)

Pili, ningependa Watanzania wote na Viongozi wajue kwamba Mkoa wa Kigoma ni Mkoa wa Upinzani, ndio maana katika Majimbo nane, Majimbo Matano ni Majimbo ya Upinzani. Lakini kumekuwa na Kasumba ya raia wa Kigoma kila siku kubambikiwa kwamba ni Warundi ama ni Wakongo.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni nchi kubwa. Wenzetu wa Mtwara na Lindi wamepakana na Msumbiji, lakini hatujawahi kusikia watu wa Mtwara na Lindi wakiambiwa ni watu wa Msumbiji. Wenzetu wa Mkoa wa Mbeya wamepakana na Zambia na Malawi, lakini hatujawahi kuambiwa watu wa Mbeya ni Wamalawi ama Wazambia. Wenzetu wa Arusha wamepakana na Kenya na maeneo mengine nchini mengi, lakini *issue* imekuwa ni Kigoma. Kuna nini? Kwa sababu ni wapinzani! Kesi za kubambikiwa kila siku!

Mheshimiwa Spika, leo hii naongea hapa, Diwani wa CHADEMA yupo ndani, Wenyeviti wa Mitaa wapo ndani, kila mtu anayeoonekana ni mpinzani, basi anaonekana ni mhalifu

Kigoma, anaonekana ni Mkongo anaonekana ni Mrundi. Watu wa Kigoma wamechoka na dharau hii. Kama hali hii itaendelea, watu wa Kigoma wanasema Kigoma haitatawalika. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ningependa kumuusia ndugu yangu Mwenyekiti wa Mkoa wa Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Kigoma aache kumtumia *RPC* kuharibu amani ya Kigoma. Yeye alikuwa Mpinzani, alifanya siasa zake kwa uhuru na uwazi mpaka alivyoamua kuja Chana cha Mapinduzi, atuache Wapinzani wa Kigoma tufanye siasa zetu kwa uhuru na amani. Watu wa Kigoma wanasema kwamba wao waachwe kufanywa ni raia wa daraja la pili. Waonekane ni Watanzania na wawe na uhuru wa kuchagua Vyama wanavyovitaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni kuhusu vituo vya Polisi. Tumekuwa na uhaba mkubwa wa Vituo vya Polisi. Tunasema nchi yetu ina wahamiaji haramu; sasa hivi tunasikia milipuko, kama wahamiaji haramu wanaingia, mabomu ya milipuko yataingia, silaha kali zitaingia; tunachukua hatua gani? Leo hii naongea hapa, unapotoka Uvinza mpaka Kigoma Mjini kilomita 80 kuna mageti matano yana Askari. Yote hii ni kuwapa kero wauza mahindi, wauza mihogo, wauza maharage, lakini ukanda wa Ziwa una zaidi ya kilomita 700 hakuna hata kituo kimoja cha Polisi ili kulinda amani ya nchi hii?

Mheshimiwa Spika, ndugu yangu Mheshimiwa Kafulila asubuhi hapa alisema Chama cha Mapinduzi kina Ofisi karibia kila eneo nchi hili; hivi hamwonni kwamba ni busara ya kawaida Ofisi hizi za Chama cha Mapinduzi basi kwa sababu ya uzalendo, tuzifanye ziwe Vituo vya Polisi ili kulinda amani ya nchi hii? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nafikiri itakuwa ni jambo la busara sana ndugu zangu wa Chama cha Mapinduzi kama tutaweka uzalendo wa wananchi mbele na maslahi ya Vyama baadaye. Nitawapongeza sana kwa hilo kama litafanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu nyumba za Askari; ukiangalia kwenye kitabu cha hotuba ya Waziri husika kwenye taarifa ya utekelezaji wa malengo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 katika kipindi cha mwaka 2012/2013, tunaambiwa kwamba, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ina malengo 10 ya kutekeleza yanayotokana na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010. Taarifa ya utekelezaji wa malengo hayo kwa mwaka 2012/2013 ni kama ifuatavyo:-

Katika malengo hayo kumi tunaoneshwa kabisa, lengo la nne ni kuanzisha mpango wa kuapatia Askari nyumba bora za kuishi. Lakini mpaka leo hii Askari wetu wengi bado wanaishi kwenye makazi na raia. Leo hii Askari anapanga nyumba uraiani, baba mwenye nyumba anakuwa mhalifu, ama anaamua kuuza gongo; hivi Askari huyu kweli atawezekumshughullikia mwenye nyumba wake? Hii inakuwa ni ngumu. Kwa hiyo, tunavyosema kwamba tunatekeleza Ilani ya CCM ndugu zangu, tutekeleze kwa vitendo. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Joseph Mbilinyi.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Spika ahsante. Mimi kwenye Wizara ya Mambo ya Ndani kila mwaka ninapopata nafasi ya kuchangia huwa napenda kutoa ushauri.

Mheshimiwa Spika, ningeanza kutoa ushauri wangu kwa Waziri japokuwa ametoka lakini Naibu wake atampa salamu. Tulitarajia afike humu ndani kama Waziri mwenye dhamana atuambie au afunguke kwamba tumsaidie vipi kwa mawazo, akina Mzee Mrema wapo watamsaidia kwamba tufanye nini ili nchi iwe salama badala ya kuingia humu ndani kupiga siasa, afunguke achukue ushauri kama alivyochukua ushauri katika suala la vazi la Taifa alipokuwa Wizara ya Utamaduni ambalo halijakamilika, lakini *at least* alijaribu kuchukua ushauri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna mzee mmoja *RCO Mstaafu*, alikuja ofisini kwangu Mbeya akaniambia kwamba, Mheshimiwa ukienda Bungeni, toa ushauri Jeshi la Polisi livunjwe liundwe upya. Alisema ilishawahili kutokea hivyo miaka ya 1980 sisi tukiwa vijana na Jeshi likafumuliwa na ndio katika ujana wangu nikapata fursa ya kuwa *RCO* na kutoa mawazo mapya kwenye Jeshi.

Mheshimiwa Spika, tuache tabia ya kuongeza mikataba. Sijui nani amestaafu, mkataba wa miaka mingapi, unakuta vyeo vinapandana mpaka vinavuruga *chain of command*. Unakuta mtu alikuwa *OCD* Wilaya fulani, anapelekwa Mkoani, anakwenda kuwa mshauri wa *RPC*. Sasa *OCD* wa ile Wilaya pale Mjini anakuwa anashindwa kujua nafasi yake ni ipi, *OCDMstaafu* anapokuwa katika eneo husika. Kwa sababu anamheshimu kama *RPC*.

Kwa hiyo, mimi naamini kama Bungeni kuna vijana Wabunge makini, pia kwenye Jeshi la Polisi kuna Vijana makini na wenye uzalendo na weledi, wapewe sasa fursa walete mawazo mapya; kwa sababu Jeshi letu la Polisi *unfortunately*, lina *elements* za kikoloni, lilikuwa na mfumo wa Chama kimoja, kazi kubwa ikiwa ni kulinda watawala. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, *RC* wa Arusha anatumwa Askari wakamkamate Mbunge, wanaruka ukuta kwa sababu amezomewa. Sasa yule *RC* wamengemhamishia Mbeya, nafikiri sijui Lema ameshindwa kufanya nini! Wangemhamishia Mbeya aje amchomoe Mbunge usiku kama mhalifu, wakati Askari hao 100 wapo nyumbani, wananchi 100,000 wangekuwa nyumbani kwa Mkuu wa Mkoa. Kwa sababu haiti maana yoyote, Askari 100 wanakwenda kumkamata Mbunge ambaye sio mhalifu, kwa sababu Mkuu wa Mkoa amezomewa, wakati mwananchi, raia akipiga simu anavamiwa kwenye kioski chake au *grocery* yake, Polisi wanasema hatuna Askari, Polisi wanasema hatuna gari; gari likiwepo, wanasema hatuna mafuta! Hii kwa kweli kuna kila sababu kwamba Jeshi la Polisi linatakiwa lifumuliwe na lianzé upya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo la msingi kwa niaba ya wana Mbeya ni kwamba, Mahakama ilihukumu kwamba Jeshi la Polisi lilihusika na mauaji ya kijana mwanafunzi Michael Sikupya wa Shule ya Sekondari Mbeya. Nakala ya hukumu tunayo, lakini mpaka leo tunataka kujua ni nani alichukuliwa hatua katika Jeshi la Polisi kwa kuhusika na mauaji yale? Kwanini Serikali sasa isione aibu na kuilipa fidia familia ya Mzee Sikupya ambayo kila siku tunawasiliana na unamwona yule mzee kwa niaba ya familia yake kwamba machozi hayajawahi kufitika mpaka leo, bado wanalia ili kufunga ile hatma ya mtoto wao. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nakubaliana kabisa na suala la Katiba Mpya kwamba Mawaziri wasiwe wanasiasa, wawe watu wenyewe weledi, wachaguliwe kutokana na taaluma zao za Wizara husika, badala ya kuwa na Mawaziri ambao wanakuja katika masuala *serious*. (*Makof!*)

MBUNGE FULANI: Wanaleta utani!

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Viongozi wa dini wanauawa, watu wanakuja humu ndani wanaleta siasa. Hampi hata *credit* Mbunge ambaye alihamasisha uchangiaji damu katika suala la Arudha, Mheshimiwa Lema na Mheshimiwa Nassari wamehamasisha suala la watu kuchangia damu mpaka benki ya damu ikakosa sehemu ya kuweka damu. Hasemwi katika mchango wake, Waziri anapiga tu siasa pale ndugu yangu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, ni hayo tu, nashukuru sana. (*Makof!*)

SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe.

MHE. KIDAWA HAMID SALEHE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nami naungana na wenzangu kuwapa pole ndugu zetu wa Arusha waliofikwa na matatizo yale jana na

ninaamini vyombo vya dola vipo, wahalifu wale watafikishwa katika vyombo vya sheria na haki itatendeka.

Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuunga mkono hoja asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, Jeshi letu la Polisi linafanya kazi nzuri ya kutulinda sisi raia na mali zetu, wanatufanya tunalala kwa amani wakati wao wako nje wanazunguka kutulinda. Kwa hiyo, tuna kila sababu ya kuwapongeza.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi linafanya kazi katika mazingira magumu. Moja ni kwamba bajeti yao tunaona ni ndogo sana ya kuwawezesha kufanya kazi zao kama wanavyojipangia.

Mheshimiwa Spika, nimeangalia fungu 28 nimejumlisha mishahara pamoja na OCnigawanya na 41,000 ya Jeshi la Polisi, nimekuta ni hela ndogo sana inapatikana. Ile hela Shilingi milioni kama 8.8 ukigawanya kwa miezi 12 kwa mwaka, unakuta kwa kila Askari mmoja wa Polisi ana average ya Sh. 720,000/= tu kwa mwezi.Hii ni bajeti ndogo sana. Naomba kwa mwaka unaofuata, Serikali ifikirie kuongeza bajeti kwa Jeshi letu la Polisi ili waweze kufanya kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Spika, mafuta lita nne kwa gari ni mafuta kidogo sana ya kuwawezesha hawa Askari wetu kufanya kazi zao kama wanavyojipangia. Wanahitajika katika matukio mbalimbali. Watalaumiwa sana kuwa wanaitwa lakini hawafiki, na wakifika, kwa mafuta ya lita nne, amefika katika eneo mafuta yamemalizika. Amemkamata mhalifu, amemtia pingu, atampelekaje kituoni? Gari imekwisha mafuta, ina maana wanajamii pale wachangishane kutia gari la Polisi mafuta! Hiki ni kitendo cha aibu. Naomba Serikali iangalie hayo.

Mheshimiwa Spika, amani ni kila kitu. Amani ni maisha, amani ni maendeleo ya kiuchumi na maendeleo ya kijamii. Kwa hiyo, kila Mtanzania ni lazima awe Polisi kwa upande

wake kwa kuweza kulinda amani ya nchi yetu. Kama siyo hivyo, nchi yetu itatetereka, itaharibika, na tutraigawa nchi yetu vipande vipande. Kila mmoja asimamie kulinda amani tukishirikiana na Jeshi letu la Polisi na vyombo vingine vya dola.

Mheshimiwa Spika, nawaomba Jeshi la Polisi kwamba wajaribu kuzima cheche kabla moto haujawaka. Kuna matokeo mengine yanaonesha mapema dalili za kuvunjika amani. Lakini wanapuuzia, nikisema wanazembea itakuwa siyo neno zuri. Lakini wanachelewa kuyafanyia kazi hatimaye mpaka inatokea matukio makubwa kabisa. Mfano, ni tatizo lilitotokea Zanzibar; sizungumzii kesi ambayo iko Mahakamani, lakini ni mfano tu.

Mheshimiwa Spika, kuna dalili zilitokea za kauli za hapa na pale ambazo siyo nzuri. Lakini Polisi wakawa wamechelewa mpaka hatimaye watu wakafa, barabara zimeharibiwa, miradi ya Watanzania wenzetu imevunja, baadaye wamekuja kufanya kazi tayari imekuwa ni *too late*. Kwa hiyo, tunaomba Jeshi la Polisi, wamepewa *mandate* kabisa, wana *authority* ya kushughulikia mambo haya, kwa hiyo, wajaribu mapema iwezekanavyo kuyadhibiti kabla hasara hajitokea.

Mheshimiwa Spika, uhalifu wa kutumia silaha za moto kwa upande wa Zanzibar. Hili ni jambo ambalo limezidi nguvu au kasi katika miaka hii ya karibuni. Miaka ya zamani tulikuwa na wahalifu wapo, lakini wakitumia mapanga, mashoka na wanavunja milango na kuingia ndani kwa jiwe linaloitwa Fatuma. Jiwe zito, wanasukuma mlango, wanaingia ndani. Lakini sasa hivi kumeongezeka matendo ya kutumia silaha za moto.

Mheshimiwa Spika, kule Zanzibar Sheria zetu hazituruhusu kumiliki silaha, lakini silaha zimekuwa zinaingia ndani kupitia, siyo bandari rasmi, kupitia bandari za vichochoroni na bandari za njia ya panya. Kwa hiyo, wananchi ni lazima waelimishwe kwa njia zote, kila mmoja awe ni Askari Jamii kuangalia chombo gani kimeingia kupitia

njia ya panya na mtu gani ambaye ni mgeni ameingia kule. Lazima mambo haya yakitokea watoe taarifa ili watu wale waweze kufuatiliwa.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile vyombo nya doria viongezwe kwa sababu, muda umebadilika, uhalifu umeongezeka. Tunasema bajeti ndogo, lakini iongezwe kufikiria vitu kama hivi; maboti ya doria, wawe wanazunguka hapa na pale waweze kusaidia ulinzi wa nchi yetu. Lakini na wanajamii waelimishwe kwa kila Kijiji, wapewe ile taaluma ya Polisi Jamii kila mmoja awe anamwangalia mwenzake.

Mheshimiwa Spika, lakini isitoshe kwa vile kule Zanzibar wanaomiliki silaha ni Askari tu, Serikali iangalie utaratibu maalum wa kufanya uchunguzi na utafiti wa kuona ni nani anamiliki silaha? Pengine labda na wananchi wakiambiwa kila mmoja amchunguze mwenzake, tunaweza tukajua ni nani wana hizi silaha ambazo wameziingiza kwa njia ya panya? Ingawa sasa hivi kuna utaratibu wahalifu wakiingia wanazikata-kata zile silaha, kwa hiyo, inakuwa ni vigumu. Lakini inawezekana vilevile kugunduliwa.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kuna uhalifu wa aina mbalimbali, uhalifu mpya, sayansi na teknolojia imechukua hatua za juu. Kwa hiyo, Wanajeshi wetu nao wawekwe tayari kwa kupewa mafunzo ya kupambana na uhalifu huu mpya unaojitokeza. Wapatiwe silaha za kisasa, vifaa nya kisasa nya kufanya kazi na magari. Karibu bajeti hii ya tatu, sijaona kama kuna bajeti ya kununua magari. Kule upande wa Zanzibar hawajanunua magari, na magari yaliyokuwepo yamechakaa, fedha za ukarabati wa magari zinakuwa ni chache. Vilevile ukarabati wa nyumba; nyumba zao ni mbovu sana. Naomba wajengewe nyumba mpya, lakini na kukarabati zilizokuwepo. Mwenzangu amezungumza kwamba pale Ziwani hali ni mbaya na ni kweli hali ni mbaya, sisi ndio tuko kule tunajua.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Polisi cha Mkokotoni, tuliuliza swali hapa tukaambiwa kinajengwa, na ni kweli kimejengwa. Lakini Mkandarasi hajalipwa hadi leo. Fedha

zimetengwa karibu Shilingi milioni 400 katika bajeti ya mwaka huu inayomalizika, lakini Mkandarasi hajalipwa na kuna madeni mengi ya namna hii. Serikali, iangalie utaratibu tuepukane na aibu hii ya kudaiwadaiwa. Kama fedha zimetengwa, zitolewe basi zifanye kazi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Polisi Jamii, inafanya kazi nzuri na ndiyo maana katika Mitaa yetu, katika vijiji vyetu, hali iko shwari, uhalifu umepungua. Kwa hiyo, kwa ujumla wake naendelea kulipongeza Jeshi la Polisi, lifanye kazi na kila Mtanzania aelimishwe awe Polisi kwa upande wake kumwangalia jirani yake anafanya nini. Vinginevyo, itakuwa ndiyo wale wahalifu wanaingia, badala ya kuwaripoti tunawasaidia. Kama mimi nina *taxis*, basi mhalifu nimeshajua ameingiza silaha, namkodisha gari yangu, na nimeshaelewa kuwa yule ni mhalifu, lakini kwa vile na mie atanipatia chochote, siendi kumripoti. Ikiwa hali itaendelea namna hii, tutakuwa hatuendi vizuri katika nchi yetu na tutaumia.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana.

SPIKA: Ahsante. Sasa niwaite wasemaji wa mwisho; Mheshimiwa David Silinde na Mheshimiwa Tundu Lissu.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii. Nianze moja kwa moja na hoja.

Mheshimiwa Spika, silaha pekee itakayoliokoa Jeshi hili ama itakayoliokoa Taifa hili ni kusema ukweli. Tusiposema ukweli, tunaendelea kuliangamiza hili Taifa. Leo Taifa linakabiliwa na vurugu za kidini, vurugu ambazo kila mwananchi anajua; lakini Serikali, imekuwa ikileta taarifa tofauti.

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba, Jeshi la Polisi kupitia Kitengo cha Upelelezi, ninahisi wazi kabisa, wanamdanganya Mheshimiwa Waziri na wanamdanganya

Mheshimiwa Rais. Vurugu za kidini kama za namna hii zilizotokea hata Arusha jana, katika eneo la Tunduma zilipotokea, Mkuu wa Jeshi la Polisi, kwa maana ya *RPC* pamoja na Mkuu wa Mkoa, wao walikuja wakasema suala hili ni suala la kisiasa, kitu ambacho siyo sahihi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, leo ukiunda Tume ikafuatilie matatizo haya kwa wananchi, moja kwa moja wananchi watakwambia vurugu za kidini zimeanzishwa na Viongozi, sisi wenyewe. Mwaka 2005 Taifa zima liliambiwa *CUF* ni Chama cha kidini, *CUF* ni Chama cha kigaidi, Waislamu moja kwa moja. Leo hakuna Kiongozi yejote wa Serikali, Jeshi la Polisi lilisema, hakuna Kiongozi wa Serikali, hakuna Rais wala Waziri husika aliyesema kabisa kwamba, *CUF* siyo Chama cha Kiislamu, *CUF* siyo Chama cha kigaidi. Hakuna mwenye uwezo! Kwa hiyo, *source* zinaeleweka wazi na hakuna ambaye yuko tayari kulitamka hili mbele ya Umma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hii ni aibu kwa Taifa, hii ni aibu kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Huku kote ni kwa sababu ya kukosa maono kwa Viongozi. Unapokuwa Kiongozi, unapaswa kuwa na maono. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mimi ningeona sasa kulikuwa na haja, watu wamependekeza sana Jeshi livunjwe; siyo tu livunjwe na kuundwa upya, bali kiwe ni Kitengo ndani ya Jeshi la Wananchi, ambako kuna nidhamu, kuna utili na kuna uzalendo vilevile. Hii inawezekana. Kwa sababu, nchi nydingi duniani sasa hivi Jeshi linakuwa moja. Inakuwa ni Kitengo tu kama *JKT*. Jeshi la Polisi linaweza, kwa sababu kuendelea kuacha hivi ni matatizo mengi. Kwa hiyo, kuna haja ya kuangalia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile tujulize, Waziri katoa Kauli ambayo sasa inaendana na hotuba ya leo, kataja mtuhumiwa mmoja, watuhumiwa wengine watano wako wapi? Tutajiwe kwa sababu ni wazi. Hao raia wa wanenye wa kigeni ambao wanahusika na kutaka Balozi wa Papa kulipuliwa, ni akina nani? Huyo Mtanzania mwingine ni akina nani? Tunataka tuambiwe ukweli kutibu Taifa hili, kwa sababu

kinyume na hapo, tunaendelea kuliangamiza hili Taifa. Hili tulieleze wazi kabisa kwamba, Taifa limekuwa likidanganywa; propaganda, uwongo, taarifa za upande mmoja. Watu wanataka kuridhisha watawala. Lakini tutaendelea kuridhisha mpaka lini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna haja kama Bunge, kama Taifa tuamue kuwa na lugha moja kwamba, sasa imefikia hatua. Tusiposema leo, nakwambia miaka mitano ijayo maafa yake yatakuwa mara tatu kuliko leo. Lazima tuseme leo tupate tiba ya tatizo hili kwa wakati uliopo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno hayo, nizungumze tu la mwisho. Jeshi la Polisi limeoza, Jeshi la Polisi limekithiri kwa rushwa, Jeshi la Polisi linabambikia wananchi kesi kweli kweli! Vijjjini watu wanalia kila siku! Kwa nini liwe Jeshi moja? Hatusikil Uhamiaji. Uhamiaji wana matatizo, lakini siyo mengi. Lakini Jeshi la Polisi limekithiri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sisi tunasema hatuwezi kuogopa kufa kwa sababu kufa ni wajibu na kila mwananchi atakufa. Hatuwezi kuogopa kuwasema kwa sababu tusipowasema nyinyi tunaliangamiza hili Taifa. *Enough is enough!* Tufikie mahali sasa tuchukue hatua. Kwa sababu tukisema sasa wananchi waamue, hayo yatakuwa ni mapinduzi dhidi ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunasema kama Serikali inasikia na iyasikie haya. Maandiko yanasema: "Zama za mwisho zitakapofika, wenye macho hawataona." Sasa naona kweli mwisho wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Kina macho, hakioni! Maandiko yanasema: "Watakuwa na masikio na hawatasikia." Wana masikio, hawasakii! Sasa unakuwa na Serikali ya namna gani? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, tunayasema, kila mtu anajua nyekundu ni nyekundu na nyeusi ni nyeusi. Lakini mnataka kubadilisha kwamba nyekundu sasa inakuwa nyeusi. Serikali ya Chama cha Mapinduzi haisikii, Serikali ya Chama cha Mapinduzi haioni, Serikali ya Chama cha Mapinduzi wala

hata kunusa hainusi! Jamani, mbona kila mtu anajua? Tafakarini, chukueni hatua. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Tundu Lissu, ambaye atakuwa msemaji wa mwisho mchana huu, dakika tano.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Spika, Mwandishi wa Kimarekani, William Rivers Pitt, aliandika kitabu miaka mitano iliyopita alichokiita, "Ukimya Ndiyo Uchochezi Mkubwa." Yaani *Silence is The Greatest Sedition*. Yaliyotokea Arusha jana ni matokeo ya ukimya wa Serikali; ni matokeo ya uchochezi wa Serikali. Zanzibar, Padre ameuawa; ni matokeo ya ukimya wa Serikali, ni matokeo ya uchochezi wa Serikali. Padre alipigwa risasi akajeruhiwa, Makanisa yamechomwa moto, watu wamepigwa kwa sababu Serikali imenyamazia uchochezi wa waziwazi wa chuki za kidini katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa utaratibu wa Kisheria wa Tanzania, ili ufanye Mkutano wa hadhara wa aina yoyote, inabidi utoe taarifa kwa Polisi, kwa *OC*D. Nchi hii kwa miaka mingi sasa inashuhudia miadhara ya kidini inayoeneza chuki waziwazi za kidini.

Kuna vituo vya redio na magazeti yanatangaza mchana kweupe chuki za kidini. Propaganda inaenezwa kwamba nchi hii inaendeshwa kwa Mfumo wa Ukristo. Kwa hiyo, Makanisa yanakuwa *targeted*, Serikali, kimya! Matokeo haya tunayoyaona, tunavuna mavuno ya ukimya na uchochezi wa Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali imeituhumu *CUF* mchana kweupe. Mkuu wa Jeshi la Polisi, anakwenda kwenye *Television* anasema, hiki ni Chama cha Kiislamu, cha Waislamu wenye Itikadi kali; Serikali imekaa kimya kwa sababu, inashabikia mambo ya aina hii. Tusishangae haya yanayotokea. Ni matokeo ya uchochezi wa Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *CCM* mwaka 2005 iliweka kwenye llani yake ahadi kwa Waislamu kwamba itawalet ea Mahakama ya Kadhi. Ilipoleta kelele, *CCM* hiyo hiyo ikageuka na kusema aah, ni Maaskofu wanaokataa Mahakama ya Kadhi. Haikuwaliza Maaskofu kama wanataka llani ya *CCM* iwe na Mahakama ya Kadhi. *CCM* imepalilia mbegu za mgogoro wa kidini. Serikali yake imenyamazia uchochezi wa kidini. Kinachotokea sasa hivi ni mavuno ya uchochezi huo.. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wa kuhusika; tumeambiwa hapa tusilalamike kwa sababu hatutakuwa wazalendo. Tunahitaji kulalamika na kumwambia Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi - Mheshimiwa Nchimbi, huu ni wakati wa kujiuzulu, umeshindwa kazi. Kama huwezi ukajiuzulu, huna uadilifu wa kujiuzulu, ni wakati wa kufukuzwa kazi. Tumwambie Inspeksa Jeneral - Said Mwema, huu ni wakati wa kujiuzulu kwa sababu umeshindwa kazi. Kama huwezi kujiuzulu ufukuzwe kazi. Huu ni wakati wa kuwajibishana. Huu ni wakati wa kusema kweli kwa sababu *silence is the greatest sedition.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *CCM* hii na Serikali yake na Usalama wa Taifa, mnaendekeza siasa za ukabila. *CHADEMA* Chama cha Wachaga, *CHADEMA* Chama cha Kaskazini, *CHADEMA* Chama cha Wakatoliki, *CHADEMA* Chama cha Wakristo, leo Makanisa yanachomwa kwa sababu yenu. Leo Mapadre wanauawa kwa sababu ya *CCM*. Ni wakati wa kuwajibika, siyo wakati wa kupiga chenga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mtuambie ilikuwaje? Tangu lini *CUF* kiliacha kuwa Chama cha Waislamu wa siasa kali? Tuambieni, tangu lini *CHADEMA* kimeacha kuwa Chama cha Wakatoliki? Tuambieni! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, yanayotokea hapa ni matokeo ya uchafu huu. Chama kinaposhindwa kujenga uhalali kwa wananchi... (*Makofi*)

(*Hapa kengele ililia kushairia kwisha kwa
muda wa Mzungumzaji*)

SPIKA: Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, muda uliobakia hautoshi kumpa nafasi mchangiaji mwengine. Mchana watakuwepo akina Mheshimiwa James Lembeli, Mheshimiwa Amina Clement, Mheshimiwa Aliko Kibona, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo na wengine watatajwa baadaye.

Nimepewa niwakumbushe kwamba, watu wa *NIDA*, hawa wanaohusika na Vitambulisho, wapo katika maeneo yetu hapo nje, wanaomba Waheshimiwa Wabunge wale ambao hawajachukua vitambulisho vyao, wataanza kutoa vitambulisho kuanzia leo tarehe 6 mpaka tarehe 8. Naomba tusikilizane! Hii inawahusu ninyi wote. Vitambulisho vinatakiwa kuchukuliwa kuanzia leo tarehe 6 mpaka tarehe 8. Kwa hiyo, naomba wanaohusika waweze kushughulikia suala hilo.

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge, mpaka saa 11.00 jioni.

(*Saa 6.55 mchana Bunge lilitishwa
mpaka saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilitrudia*)

Mwenyekiti (Mhe. Mussa Z. Azzan) *Alikalia Kiti*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mahojiano. Mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Lembeli, na Mheshimiwa Amina Clement, Mheshimiwa Aliko Kibona na Mheshimiwa Beatrice Shelukindo, wajiandae.

MHE. AMINA CLEMENT ANDREW: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika hoja hii. Kwanza, napenda kuchukua fursa hii kuwapa pole wale wote waliofikwa na maafa yaliyotokea jana kule Arusha. Lakini la pili, napenda kuwaasa Watanzania wenzangu wote; jamani, amani, amani, amani Watanzania wenzangu tunaichezea. Amani

hii ikitutoka siyo rahisi kuirudisha. Nawaombeni sana Watanzania wenzangu tuilinde, tuinyenyekie! Amani haipatikani dukani, wala haiuzwi popote kwenye *Supermarket*, amani tunayo wenyewe ndani ya nyoyo zetu na ndani ya nafsi zetu. Nakuombeni Watanzania wenzangu, amani hii ikitutoka tutaangamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kurudi kwenye hoja. Kwanza, napenda kuwapongeza Jeshi letu la Polisi kwa kazi zao nzuri wanazozifanya. Lakini wakati huo huo napenda kuwapa pole kwa kazi ngumu. Askari wetu wanafanya kazi kwenye mazingira magumu; kwanza vitendea kazi vya Askari wetu havitoshelezi kadiri ya kazi zao wanazofanya kila siku masaa 24, Askari wetu kwanza hawana *uniform*, utamkuta Askari kwa muda wa kipindi cha miaka miwili mpaka mitatu ana *uniform* mbili tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri alisikie hili, wakati wa majumuisho atupatie majibu yatakayoturidhisha sote Watanzania ili wafanyakazi hawa wasifanye kazi kwenye mazingira magumu. Wafanyakazi hawana viatu na viatu ni kitu muhimu kwa sababu wanatembea saa zote maporini, kila mahali usiku kucha, kwa hiyo, naomba hili la *uniform* Mheshimiwa Waziri alifuatilie sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini napenda kuelekea kule Zanzibar katika Wilaya yangu ya kipolisi. Katika Wilaya yangu ya Kipolisi kuna vituo zaidi ya nane, lakini hakuna usafiri. Usafiri hautoshi kabisa! Vituo zaidi ya nane vikubwa, kuna gari tatu tu ambazo gari hizo zinazunguka mpaka mwisho. Kwanza, gari zenyewe kila siku ukizilizia ni mbovu, hazina hata muda wa kufanyiwa *service*. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, kule Kituo cha Dunga, Kiboje hakuna hata pikipiki; naomba atakapoondoka hapa awafikirie sana kule Zanzibar Wilaya ya katika vituo hivi angalau wapate vitendea kazi ili wapate kufanya kazi zao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naelekeea kwa Askari wetu. Kuna baadhi ya Askari walikwenda Moshi kwenye Kozi ya Ukoplo. Askari hawa hasa kwa upande wa Zanzibar mpaka

leo hawajalipwa hata nauli zao. Hawajapewa mafao yao baada ya kurudi kwenye kozi yao ya Ukoplo. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, Askari hawa maadamu ni haki yao, basi naomba itazamwe na ifikiriwe sana wapewe haki zao, kwa sababu Askari wetu kama tulivyosema wanafanya kazi nzuri, lakini pia wanafanya kazi kwenye mazingira magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Zanzibar kuna Kijiji kimoja kinaitwa Uzing'ambwa. Kijiji hiki kiko nje ya Mji na ni Kisiwa kwa sababu yanapojaa maji Kijijini huku huwezi kufika mpaka upande boti na kule kuna Kituo cha Polisi. Askari hawa huwa hawafanyi kazi zao kwa utaratibu uliopangwa. Wanaweza wengine wakakaa *shift* siku mbili, siku tatu na kwenye kituo kile hakuna nyumba hata moja ya Askari. Naiomba sana Serikali kupitia Wizara ya Ulinzi wafikirie upande ule wa Uzing'ambwa kujenga nyumba za Askari angalau zenye kuweza kukaa familia mbili za Askari ili waweze kufanya kazi zao vizuri, wakati watakapokuwa kule wakae majumbani kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nielekee kwenye kiinua mgongo cha Askari hasa kwa wale Askari wanaopoteza maisha wakiwa bado wako kazini. Askari anapopoteza maisha akiwa kazini, yaani kufariki, Askari hawa warithi wao wanasumbuliwa sana kupata ile mirathi yao kutoka huko walikokuwa wakifanyia kazi.

Naiomba Wizara, naiomba Serikali ilitazame jambo hili kwa kina, pale anapofariki tu Askari, wajue kama huyu mtu kafa, washughulikiwe, wale warithi wasisumbuliwe sana, pia kuhangaika kupita kwa Wabunge wao; Mbunge nisaidie, wakati ile ni haki yao. Mzazi wao alifanya kazi miaka iliyopo, akaonyesha umahiri wake katika kazi yake na pale pana haki yake. Naiomba sana Serikali, anapofariki Askari tu, kiinua mgongo chake kifanyiwe haraka kulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia pale anapokufa tu Askari, kuna sheria ya pesa zile za miezi mitatu, alipwe yule Kizuka angalau za kumsaidia maisha katika kipindi kile kigumu anachokuwa ndani kwenye eda. Pesa zile hazipatikani vizuri,

pesa zile wakati mwengine yule Kizuka anapewa labda mara moja tu, mara nyingine sijui zinakuwa zinaelekea wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nielekee kwenye Mfuko wa Uji. Huu mfuko wa Uji kweli wanaushughulikia wenye Askari. Lakini Askari wale wanakatwa mishahara yao wanakwatwa pesa zile ndani ya mishahara yao. Kwa hiyo, naomba sana wale wanaoshughulikia Mfuko huu wa Uji; mfuko huu unamsaidia Polisi pale anapofikwa na msiba kufiwa na mzazi wake, mtoto wake au na yejote waliokulaliana; naomba sana, binadamu yejote anapofikwa na mitihani, pengine awe na kitu mfukoni, awe hana kitu mfukoni, lakini kinamsaidia kile chake ambacho anacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana pindi Askari anapofikwa na mitihani kama hii, ule mfuko ufanywe haraka haraka kwa sababu zile pesa za uji zipo. Zinakatwa kila mwezi, kwa nini Askari anafika mpaka miezi miwili, mitatu hajapatiwa zile pesa za kumsaidia. Baada ya miezi miwili, mitatu anapewa zile pesa, za nini? Wakati siku aliyoleta na matatizo hajapatiwa zile pesa. Kwa hiyo, naomba sana hizi pesa za Mfuko wa Uji zishughulikiwe ipasavyo pindi anapofikwa, lakini pia hizi pesa kila siku wanapewa Sh. 500,000/= tu. Naomba hizi pesa kadiri maisha yanavyopanda na mambo mengine yanavyoongezeka hizi pesa za Mfuko wa Uji ziongezeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nielekee kwenye uhamisho wa Askari hasa wale Askari ambao wote mke na mume wana ndoa wanafanya kazi ya Uaskari. Askari hawa nawaombea sana, pindi mmojawapo anapopewa uhamisho labda Askari wa kiume (mume) kutoka Zanzibar kwenda kufanya kazi Kigoma au Mikoa mingine yoyote, naomba sana na yule mke naye apewe uhamisho afuatane na mumewe waende pamoja wakafanye kazi kule Mikoani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti zetu, tunapanga kwamba tunataka kupunguza maambukizo mapya ya Ukimwi, tutapiga vipi vita maambukizo mapya wakati tunamchukua Askari (mume) tunampeleka Kigoma,

mwanamke yuko Pemba, kweli hapa tutapunguza maambukizi ya Ukimwi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana wanandoa hawa pindi watakapopangiwa uhamisho, wote wapangiwe Mkoa mmoja au ikiwezekana Mikoa iliyoko karibu angalau waonane japo *weekend*. Mheshimiwa Waziri naomba utakapotoa majibu, naomba nipate jibu la kuniridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa Askari wetu wanafanya kazi saa 24, hali ya maisha, hali ya chakula tunajua sote, kweli Askari kula chakula Sh. 5,000/= haikidhi. Hiyo Sh. 7,500/= tulijosema kwa mtu wa chini pia haikidhi. Naomba sana Mheshimiwa Waziri hili liangaliwe sana. Askari wetu wanakula kama wanavyokula watu wa kawaida. Tunaomba Askari watakapokula vizuri, basi na hata homa za mara kwa mara na mambo ya utaplamlo yatapungua, na Askari hawa wanatakiwa wawe na lishe bora ili wafanye kazi zetu vizuri saa 24.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naelekea kwenye ulinzi shirkishi. Hawa walini shirkishi ni Askari mbadala wanaotusaidia sana katika Miji yetu. Naomba sana hawa walini shirkishi wasaidiwe angalau kwa kupatiwa visemina ili kwanza wajue mipaka ya kazi zao. Mwaka 2012 niliposimama hapa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa Mzungumzaji)*

MHE. AMINA CLEMENT ANDREW: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Amina. Sasa namwita Mheshimiwa Aliko Kibona.

MHE. ALIKO N. KIBONA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Awali ya yote naunga mkono hoja iliyopo mbele yetu. Baada ya kuunga mkono hoja iliyopo mbele yetu, kwanza kabisa, naipongeze Wizara ya Mambo

ya Ndani, Jeshi la Polisi, *IGP* na Viongozi wote kwa kazi nzuri iliyotukuka ambayo wanaendelea kuifanya katika nchi yetu lakini katika mazingira magumu kama wenzangu waliotangulia walivyosema. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze *OCD* wangu pale lleje kwa kupanda cheo. Amenipigia simu anakwenda kule Mtwara Idara ya *Operation Mkao*. Nampongeza, namshukuru *IGPMwema* na wote waliohusika katika kumpandisha cheo *OCD* wangu. Natoa wito kwa Maaskari wengine watakaopangiwa lleje. Karibuni lleje. Ileje kila atakayefika anapoondoka huwa anaondoka na neema ya kupanda cheo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niseme neno moja. Was wahili, Wahenga wetu walisema: "Kauli huumba." Tena waliendelea wakasema: "Mtoto mwimbie wimbo mzuri."

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi viongozi hususan katika Bunge letu, wanasiasa; hasa wanasiasa tumekuwa na kauli, nadhani tumesahau neno la Wahenga lililosema, mtoto mwimbie wimbo mzuri, na kwamba ulimi au kauli huumba. Ukiendelea kumwita mtoto wako mbwa, paka, punda, nyani na maneno kama hayo, Wahenga wanasema, aghalabu mtoto huyo huishia kuwa na tabia za hicho unachomwitia. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu, kadiri tunavyosema nchi hii haitatawalika, kila kunapokucha kauli kama hizi zikiendelea kusemwa kwa muda mrefu, vijana wetu na watoto wetu tunawarithisha vichwani mwao kauli ya nchi haitatawalika na sasa tunaona ishara. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa natoa wito kupitia Bunge lako kwamba angalau turudi nyuma, maana yake nchi isipotawalika, hakuna ambaye atasalimika. Baba wa Taifa wakati akitetea kuwepo kwa Muungano aliwahi kusema, jamani Muungano huu uendelee kuwepo labda msubiri

wengine tufe. Nami nasema, jamani amani hii iendelee kuwepo, tusubiri wengine tukifa ndipo ivurugike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye malipo ya watumishi, hawa Polisi, hasa wakati wa uhamisho. Nimepata habari kwamba watu hawa wanapata shida kubwa sana. Baada ya kuhamishwa, wanakwenda kwenye vituo vipyta kwa muda mrefu, hawawezi kupata malipo yao. Namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa akijumuisha hotuba yake, aseme kidogo kwenye eneo hili ili kuwapa ahueni kwa Askari Polisi wetu, Uhamiaji na kadhalika walioko kwenye vituo mbalimbali hasa huko vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru baadhi ya maeneo kama kule kwangu lleje Askari wamepata gari. Lakini huwezi kuamini, kwa mwezi Kituo cha Polisi kinapata lita 200. Hili ni Jambo la kusikitisha, Polisi wanapoitwa kwamba kuna uhalifu mahali pengine wanaanza kupita Mitaani kuomba mafuta. Jambo hili linawadhalilisha na ndiyo chanzo cha kulidharau Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia Mheshimiwa Waziri aseme kidogo, hapo kuna nini? Atuambie ili tunaporudi kwenye vituo vyetu, tukawaeleze Maaskari wale wanaofanya kazi ngumu kule Wilayani na Mikoani, nini kitajiri baada ya bajeti hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze kuhusu makazi. Kule kwangu lleje upande wa Magereza, Askari ni kama wako nje. Nyumba zimepasuka, kuta zimebomoka, mapaa ya nyumba yameezuliwa, lakini Maaskari wale kwa kweli wanafanya kazi katika mazingira magumu. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa akimalizia hotuba yake hapa, atusaidie ni lini Magereza pale lleje na mahali pengine watapata nyumba za uhakika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumze kidogo kuhusu Uhamiaji. Pale Isongole kuna Ofisi ya Uhamiaji. Ni Ofisi muhimu, wageni kutoka nje wanapita pale, lakini ajabu kwa muda mrefu nyumba ya kupanga Uhamiaji humo humo,

upande raia. Nimekutana na watu mbalimbali wakipita kwenda nchi za Kusini mwa Afrika, wananiuliza, Mheshimiwa Mbunge, hiki ni kitu gani? Naomba sasa Mheshimiwa Waziri anisaidie, atoe kauli; ni lini Serikali itakwenda kujenga Ofisi pale Isongole ambapo ni mpakani, wageni wengi wanapita kwenda nchi za nje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapokwenda safari ,unaweza ukaenda ukafika njia panda. Ukifika njia panda unakuta njia mbili au tatu, huwezi kujua uende ipi. Utachagua njia moja. Ukienda na njia hiyo mwisho utakuta mawe, visiki, utakuta mashimo na kadhalika, ujue umepotea njia hiyo. Ili uweze kufika unapokwenda, shurti urudi pale ulipopotea, pale njia panda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwanzoni tulikuwa na Jeshi letu la Polisi linakwenda likafika njia panda likashika njia inaitwa Polisi Jamii, limekwenda na njia hiyo. Mimi nahisi huko linakokwenda sasa Jeshi la Polisi siko kwenyewe. Linapaswa lirudi njia panda liangalie njia sahihi ni ipi kwa maana ya kufanya tathmini. Kwa sababu huko nyuma tulikuwa tukishuhudia Askari wakiitwa kwenye tukio ambapo mhalifu amepatikana au wahalifu, wahalifu walikuwa wakikimbia. Siku hizi wahalifu wakisikia Polisi wanakuja, wanajiandaa kwa mapambano. Tumeshuhudia Askari wakifika mahali penye tukio, Polisi wanapigwa, Polisi wanashambuliwa, majambazi wanashirikiana wakati mwingine na raia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili linanisikitisha na linawasikitisha watu wengi. Askari wameumizwa, wameuawa, na pale ambapo Askari anauawa, sijasikia wanaharakati na sisi wanasiasa tukilalamika, tukipiga kelele. Lakini pale ambapo raia ameuawa, mimi nimeshuhudia magazeti, vyombo vyta habari, wanaharakati na sisi wanasiasa kwa muda wa zaidi ya mwezi mmoja tukilalamika juu ya raia kuuawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kuna haja sasa Jeshi la Polisi kufanya tathmini, ni wapi lilipochepeku? Askari wanauawa! Namwomba, *IGP* atakuwa ananisikia,

Mheshimiwa Waziri ananisikia, msiogope kufanya tathmini. Fanyeni tathmini ili kujua ni kitu gani kimetokea, kwani vijana wetu wanaauawa. Nadhani kuna mahali tumepotea. Njia tuliyokuwa tukienda, nadhani kuna mahali tumekengeuka. Turudi pale njia panda ili tuweze kushika njia sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Nakushukuru Mheshimiwa Aliko Kibona. Sasa namwita Mheshimiwa James Lembeli!

MHE. JAMES D. LEMBELI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu siku ya leo ninauelekeza kwa Jeshi la Polisi. Kazi ya Polisi ni kulinda na kudumisha amani na utulivu nchini. Kazi hii ni ngumu na inahitaji moyo wa kizalendo, lakini pia uvumilivu wa hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu uhuru wa nchi yetu mwaka 1961, nchi hii imeshuhudia amani ya kudumu na utulivu uliotukuka ukiachia mbali vitendo vya ujambazi hapa na pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka 50 baada ya uhuru, amani ambayo tumekuwa tukiimba na utulivu, taratibu imeanza kupotea. Zipo sababu nyingi, lakini moja ni utandawazi, demokrasia, teknolojia lakini ni ninaloliona hapa sasa hivi ni bajeti ndogo inayotengwa na Serikali kila mwaka kwa ajili ya Jeshi la Polisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema awali ni kwamba Polisi wanafanya kazi zinazohitaji uzalendo. Kazi ya kubeba silaha kutwa nzima, kudhibiti maovu, kulinda mabenki na baadhi ya wakubwa wakati wengine wamelala usingizi au wanastarehe. Ni kazi ambayo inahitaji moyo na uvumilivu wa hali ya juu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Polisi wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Posho kidogo, nyumba wanazoishi ovyo, huduma kama nguo, lishe haviridhishi. Inasikitisha unamkuta Polisi sare yake imeraruka; viatu, amevaa raba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baadhi ya mambo haya kwa hakika yanawakatisha tamaa Polisi. Amani na utulivu haitakuwepo kama Serikali haitatenga pesa za kutosha kwa ajili ya mahitaji ya Jeshi la Polisi nchini. Naiomba Serikali, katika vipaumbele vyake, nilishawahi kusema ndani ya Bunge hili, miaka 60 Serikali iliweka kipaumbele katika Ulinzi wa mipaka yetu, kwa sababu maadui walikuwa nje ya mipaka ya Tanzania. Leo hii maadui hawa hawako nje, wako humuhumu ndani. Kwa hiyo, Serikali iweke kipaumbele katika Jeshi la Polisi, wapewe vitendea kazi na walipwe posho nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu Mheshimiwa Aliko Kibona hapa amesema, nami nafikiri Serikali imeamua (ni maoni yangu), kulibinafsisha Jeshi la Polisi. Nitatoa mfano, Wilayani kwangu Kahama. Kwanza nampongeza sana *OCD* Simba na vijana wake pale Kahama ambao wanafanya kazi katika mazingira magumu sana! Magari ni mawili! Wilaya ina ukubwa wa karibu kilometa za mraba 10,000, mauaji ya vikongwe, ujambazi na kadhalika, lakini Wilaya hii inatengewa lita za mafuta 300 kwa miezi mitatu au mine. Sasa unategemea nini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Polisi linalaumiwa kwa sababu Serikali hailitendei haki. Ukitokea ujambazi mahali fulani, wananchi wanategemea Polisi watafika mara moja. Hawawezi kufika kwa sababu hawana mafuta. Halafu asubuhi Polisi analaumiwa, lakini Polisi sio wa kulaumiwa, bali ilaumiwe Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti hii, mimi nasita kusema kwamba naunga mkono hoja, kwa sababu kule Kahama Askari wale watania mimi siwatendei haki. Haiwezekani lita za mafuta 300 zitumike kwa magari mawili kwa mwezi mmoja katika Wilaya ya Kahama. Askari wetu wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, posho

hawalipwi. Nani yupo tayari kutembea usiku kwenda kukamata majambazi wakati hajui familia yake kesho itakula nini? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, rushwa ndani ya Jeshi la Polisi kwa upande mwingine inachochewa na Serikali kutowapa mishahara mizuri Askari. Rushwa ni *temptation* tu! Mimi nina njaa, mtu anakuja na jambo lake, ana Shilingi milioni tatu hapa, *obviously* atachukua rushwa na atamwambia nenda mbele kwa mbele, ukikamatwa huko, juu yako. Hivyo ndiyo wanavyofanya! Lakini wanafanya kwa sababu malipo yao, mishahara yao, posho zao na mahali pa kulala hapastahili watu kama Polisi. (*Makoff!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano, mimi nilikuwa mtumishi wa Hifadhi ya Taifa. Askari wa Hifadhi ya Taifa, *Sergeant* yule wa cheo cha juu, mshahara wake ni mkubwa kuliko wa *OCD*, kuliko hata wa *RPC*. Posho zao ni nzuri, ndiyo maana leo hii Ujangili ndani ya Hifadhi za Taifa ni tatizo. Majangili hawaingii huko kwa sababu wanajua hawawezi kuhonga, wala kuleta ujanja ujanja.

Kwa hiyo, nilikuwa naiomba Serikali, kwa kweli bajeti nimeiona na sidhani kama inakidhi. Hawa watu wanahitaji kuthaminiwa. Sisi tuko humu ndani, tunalindwa na Polisi, mbwa wanazunguka huko na nini, sisi tumekaa huku kwenye kiyoyozi, wao wanahangaika. Ukimwuliiza yule Askari anayezunguka na mbwa pale mshahara wake, huwezi kuamini. Mimi naiomba Serikali iangalie suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie rushwa ndani ya Jeshi la Polisi, Kitengo cha Usalama Barabarani. Hawa Usalama Barabarani kazi yao ni kusimamisha malori tu na mabasi au chombo chochote cha moto? Mimi nashangaa wiki hii siwaoni Askari wa Usalama Barabarani hapa Ofisi ya Bunge mpaka St. Gasper pale. Walishaweka vituo viwili au vitatu, kila siku na tochi, hapo! Sasa hawapo! Mimi nadhani hawapo kwa sababu baadhi ya wakubwa wa Jeshi la Polisi wanakaa kule St. Gasper.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Askari wa Usalama Barabarani ni kero. Wanachukua rushwa ndogo ndogo mpaka Sh. 500/=. Kazi yao, wakiona *Loriwanasimama* katikati ya barabara. Magari madogo aina ya *Landrover*, *VX* zikipita hawasimamishi! Malori ndiyo yanasisimamishwa kumbe *Landrover* na *VX* ndiyo zinabeba madawa ya kulevyo, pembe za ndovu, wameng'angania malori tu! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujua kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, kazi ya hao jamaa wa Usalama Barabarani ni kusimamisha malori tu, mabasi na magari mengine hapana? Kwa nini wakisimamisha *bus*, wanakimbilia nyuma ya *bus* au mbele? Kwa nini akisimamisha *bushasimami* mlangoni pale kwa abiria, asiingie ndani? Lakini Mheshimiwa Waziri Nchimbi, hivi huwa huwaoni? Pengine huwaoni kwa sababu unaposafiri kwenda Dar es Salaam kunakuwa na taarifa huko barabarani. Kwa hiyo, wanatoka. Lakini kimsingi hii ni kero kubwa. Rushwa ya Sh. 500/=, Sh. 600/=, wanachukua chochote! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wenye maroli wameshajua, wanafahamu Askari walipo, kwa hiyo, kila akisimamishwa, anachofanya ni kutelemsha mkono, chukua, nenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yote hii inasabishwa na Askari wetu kutokuwa na kipato cha kutosha kuweza kubeba familia zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado sijashawishika kuunga mkono hoja, lakini itategemea na ndugu yangu Mheshimiwa Waziri atasema nini kuhusu tatizo la Askari kutokupewa stahili ambazo zitawawezesha kuishi bila kutegemea rushwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushuru. Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana. Sasa namwita Mheshimiwa Betriace Shellukindo, na Mheshimiwa Pindi Chana na Mheshimiwa Yusufu Haji Khamis wajialdae.

MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba nianze na *NIDA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mimi *NIDA* nawapongeza sana kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. Ukweli kabisa kama hufuatilii kwa karibu unaweza ukasema kila aina ya jambo, lakini *NIDA* wanafanya kazi nzuri sana ya utoaji wa vitambulisho. *Issue* hii nakumbuka tangu nikiwa mtumishi wa Serikali miaka ya nyuma huko, ilikuwa inakwenda, inashindikana, wao wameweza. Wanastahili pongezi za kila aina. (*Makofii*)

Pili, niipongeze Serikali kwa jinsi ambavyo wameendelea kutoa fedha kwa ajili ya kazi hii ya vitambulisho. Ni ukweli kabisa kwamba fedha ilikuwa ni ngumu, lakini sasa hivi wametoa fedha nyingi na ahadi tulizonazo ni kwamba wataendelea kutoa fedha. *NIDA* wameomba kwamba wanataka kuwa katika Wilaya zote, na katika mwaka huu wa fedha wameomba Wilaya 40. Mimi niombe kwa pamoja tushirikiane ili tuhakikishe wanapitishwa hizi fedha ili zoezi hili likamilike. Siyo siri, hakuna asiyejua faida yao katika nchi yetu. Nchi nyiningine zote kwa kupitia vitambulisho zimejua idadi ya watu wake na kazi wanazofanya, kwa kuwasaidia maslahi mbalimbali na pia ukusanyaji wa mapato. Kwa hiyo, naomba sana, hiyo kazi nzuri inayoendelea Dar es Salaam na Zanzibar, nilikuwa shahidi, maeneo kadhaa, niliona vijana wa *NIDA* wanapita na sare zao wakiongea na wananchi kuwaelimisha; na mwamko ni mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi niseme tu kwamba kwa wale wanaosema *speed* yao ni ndogo, ni kwa sababu hawafahamu. *Speed* yao siyo ndogo, ni kubwa ukilinganisha na fedha wanazopewa. *Speedy* yao inaendana na fedha. Wakipewa fedha watakamilisha haraka, lakini kwa

sababu hawana fedha za kutosha, ndio maana inakuwa hivyo. Zinatolewa kidogo kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe tahadhari kwa watu wa *NIDA*. Mipakani msitoe vitambulisho mpaka wale Wahamiaji haramu wamefukuzwa, wamehakikiwa na kuondolewa, kwani wako wengi mno kwenye mipaka yetu. Wengine wameshajichanganya hata huku Mijini wamejifunza Kiswahili, utadhani ni Watanzania, lakini sio Watanzania. Kwa hiyo, naomba sana hiyo kazi ifanywe kwa uangalifu zaidi. Lakini narudia tena kuwapongeza nikiomba tushirikiane kuhimiza Serikali kuongeza fedha zoezi hili likamilike mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni wakimbizi. Nachukua fursa hii kuipongeza sana Serikali. Walisema tarehe 31 Desemba wakimbizi wa Mtabila wataondoka. Eneo la Mtabila tulliotembelea pale lina ardhi na rutuba nzuri sana. Kweli tarehe 31 Desemba wamefanikisha, nawapongezeni sana. Wasiwasi wangu ni kwamba *UNHCR* sasa hivi ni miezi mitano bado hawajakabidhi lile eneo. Mimi naomba mharakishe kulichukua, lisije likatokea jambo lingine wakarudi wengine tena. Kwa hiyo, tukazane hapo ili hao watu waweze kwenda, lakini nawapongezeni sana kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Wahamiaji haramu, mimi nashauri kwamba jamani tuwe waangalifu, tuendelee kutoa elimu bila kuchoka na sisi Wabunge kwenye maeneo yetu tuendelee kutoa elimu bila kuchoka. Ukimwona mgeni ambaye haeleweki, humfahamu ametoka wapi, fanya njia yoyote, pita popote ukatoe taarifa. Hata kama ni kwenye Ofisi ya nani nenda. Hata kama siyo Serikali, ukiona utashitakiwa, nenda popote kwa Wazee maarufu, kwenye vyama vyetu mbalimbali ili hawa watu wajulikane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu nilipokea taarifa kutoka kwa wananchi wema kule Rombo. Kuna njia za panya 320, Askari ni wachache na hawana hela za mafuta. Kuna vijana wa bodaboda wanawatoa watu kutoka mpaka wa Tarakea wanawaleta mpaka Himo halafu wanawapeleka Mwanga kituo kinaitwa Kileo. Kwa kila

kichwa ni dola 2000. Wanashirikiana na baadhi ya Polisi na Maafisa Uhamiaji (*Immigration officers*). Kwa hiyo, jamani, ninaomba na hili linajulikana! Siyo hapo tu, ni maeneo mengi, tumeona watu mbalimbali wasio waaminifu kwa maslahi ya ubinafsi wanaleta watu kama hao. Matokeo yake ndiyo kama haya ambayo tunayaona sasa, tunabaki kunyooosheana vidole, kumbe kuna watu wengine kwa makusudi mazima wameamua kufanya mambo yao wanayoyafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu Polisi. Kilio cha Kituo cha Polisi Kilindi, jamani kwa miaka kumi na zaidi sasa hivi Wilaya, bado tuna *post* ambayo hata haina mahabusu. Stoo ndiyo imekuwa mahabusu. Mahabusu wetu inabidi tuwapeleke Handeni kilometra 132, na kama hatuna mafuta, basi hapo inabidi yule ambaye amekwenda kushitaki atoe hela ili angalau Yule mshitakiwa apelekwe mahabusu. Naomba sana Wizara, mmetuahidi mara kadhaa, Wilaya ambazo zimeanza nyuma yetu tayari zimeshapata Vituo vya Polisi. Naomba Kilindi sasa mwiangalie kwa macho ya huruma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niseme tu kwamba mimi natambua kazi kubwa mnayoifanya. Kwa kweli mimi nikisikia Polisi, kwa kweli hata mimi huwa nalaumu wakati mwingine. Lakini nataka kusema kitu kimoja; hivi Mama Shelukindo nikikosea au nikifanya ubadhirifu ina maana wana Kilindi wote wamekosea? (*Makofii*)

Mimi nataka kusema hivi, lazima tuangalie; kusema tu kwamba Jeshi la Polisi limeoza, halifai, ni nini, kwa upande wangu mimi Beatrice; na ninadhani nina haki ya kutoa maoni yangu; kwa upande wangu mimi naona ni kosa kubwa sana! Polisi wachache wakikiuka maadili, siyo wote! Hivi leo Afande Mwema akisema kwa nusu saa, naagiza Maaskari wote nchini kulala, wasifanye kazi waende likizo, patakalika? Maana yake twende tukiangalia. Wachache wasionyeshe kwamba hakuna kazi inayofanyika. Kazi ni kubwa, wengine hatuioni lakini kazi ni kubwa ndiyo maana tunalala, tunaamka

tunazunguka na magari yetu, tuko salama. Pongezi sana Mheshimiwa Mwema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile ukisema Serikali ya CCM, huwa najaribu kutafakari sana. Kwa sababu ukisema Serikali ya CCM, kwangu mimi ni watu wawili watatu au hata kikundi cha watu wachache. Usiseme Serikali ya CCM kwa sababu Serikali ya CCM sera yake, mipango yake yote ni mizuri. Wapo watu wazuri ndani ya CCM, mimi hapa ni mmojawapo ni mtu mwadilifu, sina *scandal!* (*Kicheko/Makofi*)

Wapo wengine wengi, hata viongozi katika nchi hii wapo ambaao ni waadilifu. Kwa hiyo, mimi naomba kama tukisema, tuwe tunasema kabisa kuna watu fulani. Naomba niseme kwamba sisi kwa pamoja tushirikiane, kwa sababu nina imani kabisa waadalifu wapo.

Kwa mfano, kule Kilindi Askari walikuwa wanakwenda kinyume na maadili kabisa, na ilifika mahali hapawezekaniki! Limekuwa siyo Jeshi la usalama, limekuwa Jeshi linalotishia usalama. Nilikwenda Ofisini kwa *Commissioner Mteweve*, nikamwlezea kilio changu. Ndani ya saa 12 alituma afande anaitwa Gimbi yuko Kilindi. Mimi bado niko Dar es Salaam, sijakwenda Kilindi napigiwa simu akaniambia mama naingia Jimboni kwako, nimekuja kushughulikia jambo ulilomwambia Afande Mteweve. Katika wiki moja Askari tisa waliokuwa na tatizo kubwa sana walihamishwa. Jamani, sasa nitasema kweli watu hawa hawafanyi kazi? Mimi binafsi kwa kweli ninachosema Waheshimiwa Wabunge, wale wachache ambaao sio waaminifu washunghulikiwe kwa utaratibu wao. Lakini kwa pamoja tushirikiane. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *rations allowance* ambalo limezungumzwa la Sh. 5,000/=, kwa kweli kwenda kuwa Sh. 7,500/= ni halali kabisa na mimi naafiki na yale masurufu mengine yote yanayotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *traffic* hapa tumeambiwa mwaka 2012 *allowance* walizopewa nchi nzima ni Shilingi milioni 35, mwaka huu wameombewa Shilingi milioni tano.

Hivi tunategemea hiyo ziada wataipata wapi, kama siyo kule njani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka kulikuwa na *OCD* wangu lakini amestaafu, aliyahidi kutuambia kwenye Kikao cha Halmashauri. Tulimwuliza mbona Askari wanaoletwa hapa wote ni *traffic*? Akasema mama, msinilaumu natumia akili yangu. Hawa Askari wamekuja hawana vitanda, hawana magodoro, ndiyo nawasaidia wajikimu. Ndiyo haya yanayotokea sasa hivi. Ninaomba sana hata hawa Askari tunapowalaumu kama anavyosema Mheshimiwa James Lembeli na wengine, tuhakikishe kwamba hawa watu wanapata maslahi stahiki ili waweze kuacha hayo mambo wanayoyafanya.

Vilevile naomba sana, nadhani haya matukio yanayotokea, pamoja na kwamba tunaweza tukasema mambo mengine, lakini mimi pia hapa nilaumu Jeshi la Polisi. Viongozi wa Dini yaani Maskofi na Masheikh, Wakuu wa Dini wamekuwa wakitoa malalamiko, lakini hakuna hatua zinazochukuliwa. Wameleta maandishi, hamwajibu wala hampeleki doria pale. Kama hotuba asubuhi ilivyosema hapa, kuna Masheikh walimwagiwa tindikali lakini hakuna hatua iliyochukuliwa mpaka leo. Mambo mengi yanatendeka. Ukienda hapa hapa Dodoma, tena niwarahisishie pale barabara ya Saba, kuna nyumba za ibada, watu wanajifunza karate pale, hakuna mtu anayeuliza. Maaskari hamjui? Unapita kwenye barabara upande huu bucha ya Mkristo tena kwa jina la Kikristo na huku jina la Kiislamu. Tunaashiria nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani tunaona haya matukio yanavyokwnda. Hebu jaribuni kufanya uchunguzi wenu. Mimi naomba Askari chukueni nafasi yenu, sisi tusukume mpate masurufu yenu, imani yangu kubwa ni kwamba ninyi ni Jeshi imara, ni Jeshi ambalo linafanya kazi zake; changamoto hazikosekani, lakini najua mnawenza mkajidhibiti mkafanya mambo mema zaidi. Sasa tudhihirishieni Watanzania kwamba ninyi mko imara kama alivyo Waziri wenu.

Baada ya kusema hayo, naomba nimalizie kwa kusema, jamani ninaomba sana Jeshi la Polisi, nimepigiwa simu kama saba asubuhi hii baada ya kuambiya nitachangia, wanasema chagueni watu wenye sifa na uwezo wa kuwa Askari. Hilo pia litapunguza tatizo pamoja na fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Ahsante sana. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Beatrice, nakushukuru.

MHE. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kupata fursa hii. Naanza kwa kusema, naunga mkono hoja. Pia naungana na Watanzania wenzangu na Wakristo wenzangu, kutoa pole ya tatizo kubwa lililotokea Arusha, ni majonzi kwa sisi sote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina tatizo kubwa na ajali za barabarani. Mara nyingi kwenye maombi yangu, ninakumbuka makundi mbalimbali ikiwa ni pamoja na watu wanaosafiri, Mungu awasaidie wafike salama na wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la ajali barabarani hususan mabasi, sisi sote unakuta tumepatwa na matatizo ya ndungu au jirani kufariki au amepata ajali ya kiungo. Kwa hiyo, hili limekuwa ni tatizo na nimeshauliza maswali zaidi ya mawili hapa Bungeni kwamba tunafanya nini kujitahidi kupunguza ajali hususan za mabasi ambayo yanabeba watu 80, 90 mpaka 100 kwa wakati mmoja?

Kuna wakati nilikuja na mapendekezo kwamba, naomba tuwe tuna takwimu, ni kampuni gani inayosafirisha watu inapata ajali mara kwa mara isisafirishe watu isafirishe mazao. (*Makofii*)

Kwamba, wameshindwa kusafirisha binadamu, lakini kuna suala la *insurance*, watu wanapata ajali, lazima walipwe *insurance*. Kwa hiyo, haya ni maeneo ambayo nakuja tena kuomba, kuna wakati nililiza katika nchi yetu ni kampuni gani inaongoza kwa kupata ajali, wakajibu vizuri kwa kusema,

hatuna utaratibu wa kuandika jina la kampuni, tunaandika namba ya gari na dereva. Kwa hiyo, ningeomba sana, kampuni zinazosafirisha watu zinajulikana nchini, tujue kampuni gani inayoongoza kwa kupata ajali. Kwa kuwafungia hivyo, tutasaidiana na wale wamiliki wa yale mabasi, zile kampuni, anapokabidhiwa dereva wa basi kwamba ukipata ajali mimi nafungiwa kampuni. Kwa hiyo, kutoka Dar es Salaam kwenda Mbeya, atahakikisha ana madereva watatu wanapokezana. Wengine inawezekana ni usingizi, *long root* na kadhalika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nawapongeza Askari wa Iringa, Makambako na Njombe; wanajitahidi sana kuhakikisha *speed* haiendi kasi na maeneo yale tumedhibiti sana ajali za barabarani. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao Askari wa aina nydingi; Polisi, Magereza, Nevy, FFU, mimi nawasemea wanawake. Naomba wanawake wapewe fursa. Askari hawa wanafanya kazi vizuri, kwa kujitolea na waaminifu, naomba wapatiwe *training*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwa moja kwa kuokoa muda, nakwenda kwenye taarifa. Taarifa ikiwa *tabled* Mezani maana yake lazima watu wawe tayari kwa *critics* na kwa kui-*defend*. Marekani iliyahi kupata tatizo la ajali, *Twin Towers* ilipigwa, lakini *Pentagon* pia ilikuwa nusura ya kupigwa. Sikuwahi kusikia *Democracy* na *Republican* wanaambiwa wajizuru Serikali yao. Kilichofanyika, Wamarekani wale waliungana na kusema tutamsaka aliyefanya hivyo na hatimaye *Al-Qaeeda networks* zote ilikamatwa. (*Makofî*)

Hivi sasa imedhibitiwa ndani ya mipaka ya Marekani. Kwa hiyo, ni wakati sasa umefika, Watanzania tuungane sote kwa pamoja, matukio haya ya ajali, iwe ni mabomu, iwe ni risasi, tuhakikishe hawa watu wanakamatwa na mitandao yao. (*Makofî*)

Tukifanya hivyo kwa kauli moja, hakika jambo hili tutalidhibiti. Ninaomba tutoe rai na Waziri wakati anajibu,

atueleze hapa namna gani tunaweza tukawasiliana. Ninajua kila Mkoa kuna Polisi, zamani tulikuwa tunapiga 999, una taarifa,, Polisi wanapokea. Kama tunaendelea kutumia namba moja Tanzania nzima au kila Mkoa na namba zake, tuweke wazi na tutashirikiana tutawakamata hawa watu na tutahakikisha mitandao hii inamalizika haraka sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii nimeona ina lugha fulani fulani, nimeangalia kwenye Kanuni aa Bunge iko kimya kwenye lugha za uchochezi, kuna lugha za uchochezi, inasema lugha za uongo wadhibitiwe. Naiomba Kamati ya Kanuni, lakini hili ni la Kiti, lugha za uchochezi tunafanyaje?

Pia tukumbushane namna ya kuwa-*address* watu, unaposema Waziri umam-*mention*, Mjumbe wa Halmashauri Kuu, lazima ujiridhishe kama ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu, inawezekana ni Mjumbe wa Kamati Kuu wewe unasema Halmashauri Kuu na Halmashauri Kuu ya wapi, ipo ya Kijiji, ya Tawi na ya Mkoa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jacob Zuma ni Mwenyekiti wa ANC, lakini pia ni *The President*, lazima uwe makini unapom-*address* Jacob Zuma, unam-*address* kama Rais au kama Mwenyekiti wa ANC. Kanuni za Bunge zinatuelekeza namna gani? Otherwise, tutakuwa tunaweka taarifa hapa potofu, hazina *footnotes*, hakuna *reference* na ni taarifa za uongo. (*Makof*)

Any factual assertion lazima iwe na *footnotes*, leo hii Watanzania wanatusikia, unaposema kwa mfano Wilson Mkama ameshauri Sheria ya Vyama vya Siasa irekebishwe ipo ukurasa wa tisa na wakati sheria ya marekebisho na utungaji wa sheria kikatiba ni jukumu la Bunge na wala siyo la Wilson Mkama. Mambo haya lazima tuyaangalie na tuwe makini sana kwenye kupotosha jamii ya Watanzania. Kuna taarifa inasema, Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, Katibu Mkuu lini? Heee! Kwa tarehe zipo unavyonukuu!

Alishauri kufanyika marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa Tanzania. Tuna uhuru wa maoni, kila mtu ana haki

ya kutoa maoni. Katibu Mkuu yeote wa Chama chochote, Vyama 18 viliviyosajiliwa, anaweza kutoa ushauri, lakini jukumu la kutunga na kurekebisha sheria ni la Bunge. Ndiyo kazi yetu sisi hapa, sasa kama Mwananchi katoa maoni tatizo liko wapi? Ibara ya 18, *Freedom of Expression*. Sheria ziangaliwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu utamaduni wa kutaja taja majina ya Viongozi wa Vyama tuuangalie, kwa sababu kadiri siku zinavyokwenda, nakuta leo katajwa kiongozi huyu, anatajwa tuna-*deal* na *personalities*, badala ya ku-*deal* na *issues*. (*Makofi*)

Juzi kuna Bajeti imepita hapa wametajwa Viongozi wa Vyama, *they are not here; right to be heard* iko wapi? *They are having a right to be heard.* Mtu mmoja anamzungumzla mtu mwingine hapewi fursa; Kanuni za Bunge zinasema nini? (*Makofi*)

Kwa hiyo, mimi ni Mwanasheria tena nime-*defend Ph.D.* yangu, naomba kuilinda *professional*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea. Kuna taarifa, kwa mfano inasema, Serikali hii ya CCM inapendekeza kunyima demokrasia kwa kudhibiti na kufifiisha haki zao. (*Makofi*)

Yapo maeneo wamenekuu Katiba ya Kenya na Katiba ya Zimbabwe ukurasa wa 10 kwamba, wao wanatoa fursa ya watu kukutana. Nachelea kusema kwamba, fursa hiyo, sisi tunayo kwenye Katiba yetu, Ibara ya 20, kabla hata ya Katiba mpya. (*Makofi*)

Wamei-*quote*, Ibara ya 20 ya Katiba yetu inasema; kila mtu anao uhuru wa kukutana na watu wengine kwa hiari yake, lakini hapo hapo anaji-*contradict* anasema, inafifiisha demokrasia; demokrasia ipi? Taarifa haina *footnotes, factual assertion*, tunawadanganya Watanzania, ndiyo maana neno la Mungu linasema; watu wangu wanaangamia kwa kukosa

maarifa. Watanzania muwe macho. Ukiambiwa jambo, ongeza na za kwako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba masuala haya yaangaliwe sana, maeneo mengi ambayo nimependekeza ...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji*)

MHE. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Pindi Chana, nakushukuru sana.

MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, naingia moja kwa moja katika hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka yote mitatu tangu kuwa Mbunge, ninaposimama ndani ya Bunge hili, nimekuwa nikielezea juu ya gari la Kituo cha Polisi Nungwi, ambalo limeahidiwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. Mara zote nikisimama katika Bunge hili, nalizungumzia gari hilo. Bajeti iliyopita, Mheshimwa Waziri alikiri kwamba, gari hilo tayari litakabidhiwa Kituo cha Polisi Jimbo la Nungwi, lakini kwa bahati mbaya kwa kuwa kauli ile ilitamkwa ndani ya Bunge hili, napenda kulijulisha Bunge hili Tukufu kwamba, gari lile halikukabidhiwa na Wananchi wote wa Tanzania waliosikia kauli ile, gari lile halijakabidhiwa mpaka leo, halipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, alipokwenda mbele ya Kituo kile cha Polisi hakwenda kwa ajili ya kampeni, alikwenda kama Jemedari Mkuu wa Vikosi vya Ulinzi vya Tanzania. Kwa hiyo, aliahidi ahadi ile si kwamba kampeni, kwa sababu kampeni unaweza ukaahidi lakini kwa matamanio yako tu ili upate usitekeleze chochote. Yeye aliahidi kama wajibu wake kwa

Jeshi lile la Polisi. Ninasikitika mpaka leo gari lile halikupatikana, kituo kile kinafanya kazi katika mazingira magumu. Mji wa Nungwi nimeeleza hapa kwamba ni mkubwa sana, kuna mazingira mbalimbali ya wajanja, watu ambao wanapenda kuvunja sheria. Kwa hiyo, kukosekana gari ni tatizo kubwa, nimepigana kwa juhudini zangu zote lakini inaonesha juhudini zangu zinagonga mwamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo kile mimi binafsi nimeshuhudia, wanachukuliwa watuhumiwa wanapelekwa katika Kituo cha Mkokotoni Mahakamani, basi wanapakiwa ndani ya magari ya abiria wakiwa wamefungwa pingu mikononi! Sijui hii ni sheria au tunafanya tu mambo tunavyotaka wenyewe? Gari la abiria ambalo tunaita chai maharage kwa huku Bara, kule kwetu tunaziita *Hiace* zile, abiria wanakaa upande huu na upande huu wameelekeana, *belt* yake kuna *pipe* moja hili kubwa, gari linapokuwa linakwenda kwa kasi ikifunga *break* mkamate hivi. Leo unamchukua mtuhumiwa umemfungwa pingu, ikifungwa *break* yeye ajitete wapi, ajitete kwa ninilisho! Sheria hizi zinanisikitisha sana. (*Makofii*)

Ndani ya Tanzania utamkuta mtu mwenye gari lake la kifahari la starehe anatakiwa afunge *belt*, yule unamchukua umemfungwa mikono, ajitete kwa jambo gani! *Pipe* iko hapa, ile *pipe* ikifunga *break* ndiyo unakwenda unajizuia hapo, ndiyo *belt* yake gari zile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa inasikitisha, gari lile kama linaingia moto, kama linabinuka au likipata ajari yoyote, yule uliyemchukua na pingu mikononi umemdhilishi, ajitete vipi. Ana njia gani ya kujijitea? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni mazingira magumu, ambapo Jeshi la Polisi linafanya kazi katika mazingira haya magumu. Ndiyo maana tunasimama kidete kwamba, kile Kituo cha Polisi cha Nungwi ni kituo kikubwa sana, kwa sababu Mji wa Nungwi ni mkubwa, angalau hii ahadi aliyoisema Mheshimiwa Rais mwenyewe basi itekelezwe. Ndani ya miaka mitatu imenishinda kabisa na ahadi hii siyo

kwamba imo ndani ya miaka mitatu, mimi nimeikuta ina miaka minne nyuma huko. Hivi sasa ina miaka kama saba. (*Makof!*)

Serikali ya Chama cha Mapinduzi, nani kama CCM hakuna imeshindwa kutekeleza hili! (*Makofi!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni aibu kwelikweli, kwa hiyo, mimi nasema, Mheshimiwa Waziri gari la Kituo cha Polisi lazima litekelezwe kwa sababu ni ahadi ya Rais...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Khamis, nakushukuru, dakika tano, msirukie mambo msiyoyajua. (*Kicheko*)

MHE. RASHID ALI OMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuokoa muda, napenda nijielekeze moja kwa moja katika kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania waliopo katika nchi yetu hii, wanawakilishwa na Wabunge katika Bunge hili tuliloko hapa. Cha kusikitisha, hili ni Bunge lao wenyewe, wapo Watanzania ambao si wanachama wa chama chochote ambao ndiyo wengi, kwa hiyo, kukaa katika Bunge hili tukajadili masuala ya kidini ni kutowatendea haki Watanzania, wakati tupo hapa kwa ajili ya kujadili maendeleo ya Watanzania kuititia Bajeti hii ya Serikali. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ndiyo yenyeye dhamana ya ulinzi na usalama wa Wananchi wake na mali zao. Sasa ni jambo la kushangaza kuwa tutasimamia katika Bunge hili tukalumbana masuala ya kidini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niishauri Serikali, kuititia Jeshi lake la Polisi, iwaandae Jeshi la Polisi kiutaalamu na wawe na ujuzi zaidi wa kuweza kuangalia matukio

ambayo yanatokea mabaya katika nchi yetu, isiwe kukamata huyu au yule bila kueleweka. Wawe ni wajuzi na wasimamie shughuli zao wenyewe bila kuelekezwa na vyombo vingine, yaani Viongozi wa Chama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya uhalifu yanayojitokeza katika maeneo ya nchi yetu, ninaomba sana sisi Wabunge tukae tuyangalile na tuwaachie Jeshi la Polisi liangalile nafasi yake ya kufanya uchunguzi wa kina. Kusiwe na uchochezi baina ya sisi na vyama vyta siasa upande wowote. Masuala haya ndiyo yanayosababisha kuleta vurugu na fujo kwa Watanzania na kupoteza amani na utulivu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo ajabu mambo yanayojitokeza sasa hivi hapa Tanzania Bara, yalikuwa yanajitokeza kila leo katika maeneo yetu ya Tanzania Visiwani (Unguja na Pemba). Ili kuondoa ule ukweli na uhakika unaohitajika kwa watu, yaani kutekeleza sheria za kuwafanya watu waishi kwa amani na utulivu, mambo haya yalikuwa yanajitokeza. Wazanzibari waliwahi kuonewa kwa kunyanyaswa bila kueleweka, eee! Kwa vile Zanzibar Chama cha Upinzani cha *CUF* kilikuwa kina nguvu mpaka Tanzania Bara, kilikuwa kina mwelekeo wa ushindi, zilianza njama za kuleta matatizo kama haya na Chama cha *CUF* kikaanza kuingizwa katika masuala ya udini.

Leo hii yamekuja Tanzania Bara, hili siyo geni kwa Chama cha Mapinduzi. Mimi nataka niwaeleweshe Wabunge wenzangu na Wananchi wa Tanzania waelewe vizuri, wajue ni Chama gani cha kuelekeza nguvu zao na kujunga na kikitakia ushindi kiongoze vizuri. Chama cha Mapinduzi hii ni tabia yake, inapoonekana nguvu zake zimeitungua, hutafuta mbinu mbalimbali mbadala za kudhoofisha nguvu za Vyama vyta Upinzani. (*Makof!*)

Kwa hiyo, nawataka Watanzania wa nchi hii ya Tanganyika, ingawa Zanzibar wanalelewa vizuri sana suala hili siyo geni, wakae wajiandae rasmi, waangalile wasifuate maneno yanayozungumzwa na Vyama vyta Siasa kwa utashi

wanaokusudia wao. Waangalie ni chama gani cha kukifuata. Ninawashauri, Watanzania mrudi katika Chama cha *CUF* ili tuanze upya, mwone maendeleo gani mtakayoyapata katika nchi yenu kwa amani na utulivu. (*Makofi*)

Kwanza, Sera yetu inaelekeza haki sawa kwa wote na wakati huo huo ni Chama ambacho kinajua, kina Kiongozi shupavu ambaye anaweza kuongoza nchi kwa njia zote, kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni, Mheshimiwa Prof. Lipumba. (*Makofi*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Omar, nakushukuru sana.

MHE. RASHID ALI OMAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MHE. ANNA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote, naomba niunge mkono hoja iliyoko mbele yetu. (*Makofi*)

Pili, napenda kulipongeza sana sana Jeshi la Polisi na vyombo vyote vilivyoohusika na kuhakikisha kwamba, hali ya amani inarudia kule Arusha, hasa kwa kuwakamata watuhumiwa wanaodhaniwa kwamba walitenda tendo la uovu. Hili jambo ni la kupongezwa kwa sababu huko nyuma na katika hotuba zetu humu tunailamu Polisi kwamba hili jambo lilitokea mahali fulani hawakuchukua hatua, leo wamechukua hatua si tuwapongeze basi! Tuwaombe kwamba, kuanzia sasa msirudie tena lile la kutokuchukua hatua mapema.

Kwa hiyo, napenda kulipongeza sana Jeshi la Polisi na ninaomba waendelee ili wahalifu wote wafikishwe katika Vyombo vya Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine nasema mtu anapotaka kukutukana hakuchagulii tusi, anaweza akabandikiza maneno yaliyo ya kweli halafu anarejea kusema kitu ambacho anataka kukisema ili huyu anayesemwa aone kama anasemwa.

Nataka niseme kwamba, Sheria ya *The Parliamentary Immunities, Powers and Privileges* ni ya Bungeni kweli na inamruhusu Mbunge huko akifanya mikutano yake ya Kibunge siyo ile inayokumbakumba na Viongozi wote wa chama chake mnafanya *trail*, hapana, Mbunge kwenye Jimbo lake afanye kazi yake kwa usahihi, hii ni sawa. Sasa kumhusisha Spika tena kwa masikitiko yanasesemwa Spika amenyamaza kimya, mikutano ipo huko, Spika anajuwaje kama kule yamempata hayo?

Mimi nasema jamani tuache kumsingizia Spika, kwani humu ndani mnapata nafasi ya kusema mnasema wakati mwingine na mimi namsifu sana Spika anasemwa hivihivi amekaa na anawapa bado nafasi ya kusema na mnatoka hapa mnakwenda kumtukana mpaka huko nje, amewapa nafasi humu ndani. Nasema mnyonge mnyongeni, lakini haki yake mpeni. Kama kulikuwa na huko mikoani kuzuiliwa ni juu yenu, basi angalau mlalamike lakini ye ye atajuwaje huko? Mimi nasema hili sikulipenda la kumlaumu mtu ambaye anawatendea haki humu ndani na anawapa nafasi, lakini kila kitu ambacho kinawashinda mnasema ni Spika. (*Makof!*)

Jambo la pili, nataka kusema kwamba, yale maneno ambayo Mheshimiwa Wilson Mkama anahukumiwa nayo katika kitabu hiki siyo yake, yapo kwenye kitabu cha Mzee Pius Msekwa. Mnakumbuka alipotupa semina tulipoanza Bunge hili aliyasema tena hayo, tulikuwa Dar es Salaam Ubungo Plaza, kama mnasoma zile *papers* alisema tunapomaliza uchaguzi siasa inahamia Bungeni, watu washindane Bungeni kwa sera huko na maneno na kukosoana na kila kitu, alisema hayo. Sasa kwamba, eti ye ye ndiyo kamwomba Msajili abadilishe sheria; jamani tuwe tunaangalia haya maneno.

Nasema hata suala la kuweka pendekezo kwamba tunaomba Serikali iweke pendekezo ilete hapa sheria itakayoweka utaratibu wa kufanya maandamano yametoka kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama. Mheshimiwa mtoa hoja aliyezungumzia upande wa Upinzani ni Mjumbe, tulizungumza tukakubaliana kwamba haiwezekani tangu Jumatatu mpaka Jumamosi watu waruhusiwe kufanya mandamano na mikutano, hapana! Watu walioendelea na tikitaka kujenga nchi hii lazima kuwe na utaratibu wa maandamano, njia za kupita, mahali pa kukutana na kwa muda maalum na siku maalum siyo kila siku, ye ye hakusema alinyamaza kimya, lakini humu ndani wanasema maandamano ni uhuru, siyo uhuru ni fujo, ndiyo!

Uhuru bila nidhamu ni fujo isipokuwa nidhamu bila uhuru ni utumwa, sasa ni lazima tu-*balance* vitu hivi, haiwezekani! Wakati huu wa maandamano tumeona sehemu nyine watu wanaharibiwa mali zao na wanafunga biashara zao, siku ile badala ya kuingiza vijipesa kidogo watu wanajifungia majumbani, haiwezekani, ni lazima tuwe na utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikubaliane na Waheshimiwa Wabunge wenzetu waliozungumzia suala la ufinyu wa bajeti ambao unafanya wakati mwininge Polisi wanashindwa kutimiza wajibu wao. Sisi kwenye Kamati tumeona na tumefanya hesabu, kwa magari waliyonayo na vyombo vyote vya umma walivyonayo ni wastani wa lita nne kwa siku. Kwa hiyo, wakati mwininge lawama hizi siyo zao, watu wanapokwenda Kituo cha Polisi wana shida wanaambiwa hakuna mafuta, ni kweli kabisa; kwa hiyo, tunaiomba Serikali na hili tumelisema kwenye Kamati yetu, tunahitaji Serikali ihakikishe kwamba Polisi inawezeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mapya ya utawala; inasikitisha sana tunapoambiwa hapa kwamba, Wilaya mpya itafunguliwa tunafurahi sana lakini hatuiambii Serikali unapofungua Wilaya mpya hakikisha Vituo vya Polisi vinajengwa, Magereza inajengwa, nyumba za mahabusu zinajengwa pamoja na boma linajengwa. Leo tumemsikia

Mheshimiwa Beatrice Shellukindo amesema kwamba, hakuna faida ya kuanzisha Wilaya kama vyombo vyomba havitaandamana na sehemu ya utawala, hakuna utawala bila chombo cha dola.

Kwa hiyo, hili ni jambo ambalo Serikali lazima iliangularie, unapofungua mkoa mpya na Wilaya mpya, hakikisha vyombo vyote vinavyohusika na dola hiyo vyoma utawala huo vinakuwepo na wala siyo vyema kuchukua bajeti unapeleka kwenye Polisi ili wajenge kituo, chukua bajeti peleka kwenye Magereza ili wajenge Magereza, hapana, ni juu ya yule aliyeamua kuanzisha Wilaya aweke bajeti ya kutosha kuweka yote hayo yanayotakiwa mahali hapo ili pawe mahali pa utawala bora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni Jeshi la Zimamoto. Jeshi la Zimamoto kwa kweli hapa tunaliita Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, lakini utendaji wake wa kazi unapaswa kwenda kijeshijeshi. Mahitaji yao hakuna ya kijeshi, tena jambo la kushangaza ni kwamba, fedha wanazozikusanya ni mapato ya Serikali, badala ya kusema sasa Jeshi lenyewe lijisaidie kununua baadhi ya vitu vinavyotakiwa, Serikali iliachaa asilimia 70 ya makusanyo, sasa wameipunguza yote inafika mpaka inafika asilimia 49, halafu fedha za maendeleo hazipo; sasa watafanyaaje kazi?

Lilipotokea janga la jengo la ghorofa 16 kuperomoka Dar es Salaam, Kamati ilisema kwamba, Askari hawa pamoja na kwamba wana ujuzi mkubwa sana wa uokoaji, lakini walikuwa watazamaji, hawakuwa hata na chombo kimoja cha uokoaji. Chombo kilichokuwa pale ni boza la maji, sasa pale hakukutakiwa maji na ndicho walichokuwa nacho, hawakuwa hata na spana ya kukatia vitu vingine viliviyokuwa vinatakiwa kukatwa! Tunasema hili siyo sahihi na tunawalaumu vijana hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uhamiaji wanafanya kazi kubwa sana. Afadhali siku hizi kidogo, lakini inasikitisha

unapotoka kwenye nchi jirani unaingia kwenye Kituo cha Uhamiaji cha Tanzania, duuh yaani utakuta ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Nakushukuru. Mheshimiwa Mama Anna.

MHE. ANNA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofii)*

MHE. IDDI M. AZZAN: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Naomba niseme kwamba, katika wachangiaji waliozungumza hapa, kuna mmoja alisema kwamba, CCM imepoteza nguvu. Nataka kumwambia tu kwamba, CCM haijapoteza nguvu kwani ipo imara na huyo mchumi wake anayemwona yeye anaafaa kwenye uchaguzi uliopita hata sjui alichukua nafasi ya ngapi, maana hata kwenye nafasi ya pili hakuwemo. Niseme tu kwamba, tumekuja kwa ajili ya Bajeti ya Serikali na kuelezea matatizo yaliyopo Majimboni kwetu. Hapa kwenye Bunge hili siyo mahali pa mkutano wa hadhara wa chama chochote. *(Makofii)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nielekee kwenye lile ambalo limenileta, kwa maana ya kuchangia kwenye Wizara hii ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti zilizopita, nilizungumzia sana kuhusu suala la nyumba za Askari na hasa katika Jimbo langu, nyumba za Polisi Magomeni, Polisi Mabatini, Kijitonyama pamoja na nyumba za Askari Oyster bay. Nyumba ni chakavu mno na zinasikitisha. Nilimwombwa Mheshimiwa Waziri na akakubali kwenda kutembelea nyumba hizo mwaka 2009, lakini mpaka hivi ninavyozungumza, hakuna Waziri aliyekwenda kutembelea nyumba hizo kwa ajili ya kujionea mwenywewe hali halisi ya ubovu wa nyumba hizo; ni aibu! Wamekata vyumba kwenye hanga lile kwa kutumia mifuko ya plastiki na vipande vya

maboksi, halafu hapo anaishi baba, mama na watoto; kwa kweli hili linasikitisha sana.

Naomba tena kwa bajeti hii ambayo tunaipitisha hapa, tuone umuhimu wa kuwajengea Askari wetu nyumba ambazo zinastahili kwa utu wa binadamu kuliko zile ambazo wanaishi hivi sasa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kinondoni ina takriban watu milioni mbili, ina eneo kubwa sana na ninamshukuru sana Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Kinondoni, Kamanda Kenyela, kwa kazi nzuri anayoifanya kwa sababu uhalifu ni mkubwa kupitiliza. Askari waliokuwepo Kinondoni sidhani kama wanazidi 1,200, ni wachache mno ukilinganisha na ukubwa wa eneo na ukilinganisha na wingi wa watu na uhalifu ambao upo katika maeneo hayo. Naomba sana tuone jinsi gani ambavyo tunaweza tukaongeza Askari katika Wilaya ya Kinondoni. Askari 1,200 ninaowazungumzia siyo tu kwamba, wanakwenda kulinda usalama wa raia, lakini haohao ndiyo utakuta wanakwenda kulinda nyumba za viongozi, haohao ndiyo wanaokwenda kulinda kwenye mabenki na haohao ndiyo wanaokwenda kulinda kwenye kumbi za starehe, pia haohao kama kuna mikutano wanakwenda kulinda. Kwa hiyo, utakuta ni wachache mno, ambao wanakabiliana na hali ya ujambazi ambayo imekithiri katika Jiji la Dar es Salaam hususan katika Wilaya ya Kinondoni. Naomba sana, tuone jinsi gani ambavyo tunaweza kuongeza Askari.

Suala la ulinzi shirikishi ambalo tumekuwa tukilitegemea halikufanikiwa kwa kiasi ambacho tulikitarajia. Badala yake sasa tumeona hata wahalifu wanajunga kwenye ulinzi shirikishi na kuleta matatizo. Kuna mfano mdogo tu ambao umetokea Mwanza kwa Kamanda wa Polisi, Mungu amrehemu, Marehemu Baro, alidhani ni Askari wake wa ulinzi shirikishi kumbe ni watu wabaya. Kwa hiyo, suala la ulinzi shirikishi tuliangalie mara mbilimbili kwa nchi.

Mimi nashauri tuhakikishe Askari wanakuwa wengi, lakini yale mambo mengine ambayo Askari wetu

wanayafanya, basi tuangalie ni kikosi gani ambacho kinaweza kwenda kufanya; kwa mfano, ulinzi kwenye nyumba za viongozi wetu na ulinzi kwenye sehemu mbalimbali, basi tuombe hata Kikosi cha Suma JKT, wanacho kikosi cha Askari ambao wangeweza kufanya hiyo kazi badala ya kuwaachia Polisi kuwa wao ndiyo walini wa kila jambo na uchache wao hauwezi kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni wizi ambao umejitokeza hivi sasa kwa kutumia pikipiki za bodaboda. Kweli ni kazi ambayo imekuja kuwasaidia vijana wetu kuweza kujiajiri, lakini wapo watu wabaya ambao wanatumia bodaboda hizo kwa ajili ya mambo mabaya na uhalifu. Dar es Salaam hili ilmekithiri sana, biashara yoyote kama haina mpangilio ni fujo. Kwa hiyo, suala la biashara ya bodaboda halipo kwenye mpangilio na halikuwekewa utaratibu mzuri, matokeo yake imekuwa ni vurugu na ujambazi umeongezeka, watu wanaporwa, watu wanauawa kwa kutumia pikipiki na akishaua ama akishapora akikimbia ni tabu kumpata kwa sababu wanaweza kupenya, wewe mwenye gari huwezi kumfukuza. Kwa hiyo, tuangalie ni jinsi gani ambavyo tunaweza tukawasaidia vijana wetu wa bodaboda wafanye kazi yao vizuri na wakati huohuo tuhakikishe kwamba watu wabaya hawajiingizi kwenye biashara hii. Abiria wanaopanda kwenye bodaboda wako hatarini; kwanza, kwa ajali; na pili, ni huyo dereva wa bodaboda anaaminika kiasi gani kwa sababu wengi wamekwenda kuwadhuru abiria wao. Kwa hiyo, hili tuliangalie kwa umakini mkubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya *RPC* Mkoa wa Kinondoni, mmetupa Mkoa wa Kipolisi, sawa, lakini *RPC* hana ofisi; hivi anafanyaje kazi kwa Mkoa kubwa kama huo? Kwa hiyo, naomba pamoja na nyumba za Askari, lakini tuhakikishe kwamba tunajenga Ofisi ya *RPC* katika Mkoa wetu wa Kinondoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, ni suala la ajali barabarani. Tuna matatizo makubwa sana kwani tunasema UKIMWI unaua sana, lakini mkipiga hesabu

mtakuta ajali ndiyo zinatumaliza sana kuliko hata huo UKIMWI. Kwa hiyo, naomba sana kuhakikisha kwamba kikosi cha usalama barabarani kinapatiwa zana za kisasa, pia kuchukua hatua kwa madereva ambao wanakiuka ama wanavunja sheria. Tumeona hivi sasa madereva wengi wa malori wanapimwa ulevi na wengi wanakutwa wamelewa, lakini sanasana ataambiwa alipe faini ya shilingi 30,000 halafu anaachiwa aendelee na safari. Sasa huyu mlevi unamwachia aendelee na safari kesho si ataendelea kunywa tena? Kwa hiyo, tuone ni jinsi gani tutawadhibiti madereva hao wa malori ambao ni walevi kwa sababu wao ndiyo chanzo kikubwa sana cha ajali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na vibali nya silaha na tunatoa vibali nya silaha lakini niseme tu kwamba, vibali nya silaha sasa hivi mnatoa kiholela mno. Ukipita kwa Mwenyekiti wa Mtaa, sijui Kamati ya Maendeleo ya Kata, wanapitishwa watu ambao hawastahili kumiliki silaha na matokeo yake haohao ndiyo wanaotumia silaha zao ama kukodisha au kufanya uhalifu. Wapo ambao wameshakamatwa wamefanya uhalifu kwa kutumia silaha ambazo wamepewa kihalali. Naomba tuliangalie kwa umakini sana hili, kwa sababu pia mimi niliomba silaha na niliambiwa ili niipate harakaharaka basi nitoe shilingi 700,000 nikawaambia sitoi, tena kwa kuonewa aibu mimi Mbunge nikaambiwa shilingi 400,000, nikasema sitoi namfuata Kenyela kama anaweza kunisaidia anipe na kama hawezi basi.

Ukiwa na shilingi 700,000, ukiitaka silaha sasa hivi utapata kibali cha kumiliki silaha. Kwa hiyo, naomba sana tuangalie utoaji wetu wa vibali nya silaha kuanzia ngazi ya chini kwenye Kata na Wizarani wanaotoa vibali na wao kweli wanafuata utaratibu ama wanatoa kiholela tu. Kama hukutoa chochote utaambiwa vitabu hakuna, subiri na mambo mengine. Kwa hiyo, hili ni tatizo kubwa mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la ajira kwa Askari. Tunahitaji Jeshi letu liajiri Askari wa kutosha, lakini hatutaki tena mchukue Askari kutoka mitaani au mchukue watoto wenu na jamaa zenu, wengine hao ndiyo wanakuwa

vibaka na wengine wanakuwa hawana nidhamu ndani ya Jeshi. Nendeni JKT mkachukue Askari waajiriwe na Jeshi la Polisi. Wapo Askari JKT ambao wamepata mafunzo kwa muda wa miezi sita na wengine mwaka mpaka miaka miwili wanangoja ajira, lakini ajira mnapeana wenyewe kwa wenyewe, jamaa kwa jamaa na wale ambao wamefanya mafunzo haya mnawaacha, matokeo yake mnaajiri Askari goigoi. Wapo Askari hivi sasa Dar es Salaam, Mtwara na Mikoa mingine, akitoka kituoni kwenda nyumbani kwake anavua *uniform* anavaa nguo ya nyumbani anasema anaogopa mtaani; sasa huyo ni Askari?

Mimi nawaomba sana, hili tuliangalie kwa umakini na bahati nzuri Waziri wa Ulinzi ameliona na amelikubali na ninataka *commitment* ya Waziri wa Mambo ya Ndani juu ya kuajiri Askari kutoka JKT badala ya kuchukua Askari kutoka mtaani, mnawapeleka kwenye mafunzo ya mlezi miwili au mitatu mnakuja kuwapa kazi ya upolisi, matokeo yake wanaendeleza mambo mabaya kwa Wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kulipongeza Jeshi la Polisi, Kamanda wa Polisi na Kamanda wangu wa Kinondoni, kwa kazi nzuri wanayoifanya pamoja na uchache wao, wanafanya kazi nzuri. Kamanda Kikosi cha Usalama Barabarani Taifa hana ofisi ya maana ya kufanya kazi zake, lakini naye amekuwa akifanya kazi zake vizuri na anatimiza wajibu wake kadiri inavyotakiwa. Nampongeza sana kwa hilo. Pia naomba tuangalie na Ofisi ya Mkuu wa Usalama Barabarani ili iweze kuboreshwa nayo na ye ye awe na ofisi pamoja na Askari wa kutosha kwa ajili ya kazi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MHE. YAHYA KASSIM ISSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii. Mambo mengi yamekwisha zungumziwa lakini hata hivyo, kuna haja ya kusisitiza kutokana na uzito wa hali halisi ulivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ni kuhusu kipato cha Jeshi la Polisi. Niliiwahi kuuliza katika Bunge hili Tukufu na nikaambiba kwamba, kuna sheria tofauti ambazo zimesababisha Jeshi letu la Polisi kipato hicho kuwa kidogo. Bunge hili tulilopo sasa. Juu ya malalamiko hayo yote, tunaleta hapa marekebisho ya sheria mbalimbali ili kuweza kurekebisha taratibu za kuendeleza taratibu zetu za Bunge hili Tukufu, lakini hili bado halijaweza kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba, kuna haja ya kuangalia sehemu mbalimbali ndani ya Jeshi la Polisi ili tuweze kuwasaidia kuinua kipato katika taratibu mbalimbali. Tutafute vipengele ambavyo vitawasaidia ili waweze kujikimu pamoja na wenzi wao. Hivi sasa taratibu zetu katika ajira, Wananchi au Vijana wanaelewana kwa kazi nyingi kwa sababu mara nyingi wako pamoja. Kwa hiyo, kama hatutaweza kutekeleza hill, mtaona siku zote tutalaumu na kuzungumza hayo hayo na hatutaweza kuleta maendeleo yoyote katika Jeshi letu la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, kuna utaratibu wa kawaida askari wetu wakishatoka depo kuna fedha ambazo wanapewa kwa ajili ya kujikimu na kuanzia maisha yao. Hata hivyo, inanisikitisha kwamba, katika mwaka 2001 watusika hawakupatiwa fedha hizi. Naomba suala hili liangaliwe na kwa kila mwenye kustahili haki yake aweze kupatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni kuhusu kuijendeze kielimu kwa Askari wa Jeshi letu la Polisi. Katika suala hili, vijana wetu wananyimwa fursa kutokana na sababu mbalimbali. Mara nyingi unaambiba labda askari ni wachache au kuna Operesheni Maalum, kwa hiyo, hakuna fursa ya kwenda kusoma. Nchi hii bado tunahitaji wataalam kwa hivyo kuna haja ya kuhakikisha kwamba, vijana wetu wanaotaka kuijendeze na kusoma wanapatiwa fursa bila pingamizi lolote. Jambo zuri zaidi ni kwamba, wao wanachotaka ni kwenda kusoma, hawaombi muwalipie kwani wanajilipia na kujikimu wenyewe. Ajabu ni kwamba, pamoja na dhamira yao hiyo nzuri hawapati fursa hizo.

Tunaomba Serikali irekebishe suala hili ili fursa za vijana wetu kuijendeleza ziweze kupatikana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni fedha za uhamisho. Kwa kweli vijana wengi sana wanalamika. Wakati tunahisi kuna taratibu maalum za uhamisho, kwa mfano, kimkoa, ikiwa hatujitayarisha basi ni bora tusitoe uhamisho kwa askari. Tusubiri hadi tutakapokuwa tumejitayarisha ndipo tuweze kuhamisha askari. Tusihamishe askari kama tunajihisi bado hatuna uwezo, kwa sababu yanakuja malalamiko mengi sana. Kuna askari waliohamishwa mwaka 2007 na hadi hii leo hawajalipwa fedha zao. Kwa hiyo, hili suala tujitahidi sana.

Jambo la hatari zaidi tunalofanya ni kwamba, leo askari anayehamishwa tuseme kutoka Zanzibar kwenda Killmanjaro, anajitegemea hata nauli ya kwenda na kurudi. Hakuna utaratibu wa kwamba labda atarejeshewa fedha alizotumia. Wengi wao wanalamika suala hili. Kwa hiyo, ni vyema tuwe na utaratibu maalum wa jinsi ya kuwasaidia hawa polisi kuondokana na matatizo yote yanayojitokeza. Siyo siku zote tunakuja hapa tunazungumza mambo yale yale, itakuwa ni kupoteza muda tu. Yale tunayozungumza yawewe kurekebishiwa kwani mengine ni madogo madogo sana na hayahitaji fedha nydingi sana kuyarekebisha. Kwa hiyo, naomba na hili lirekebishiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningombaa askari wetu na hasa walioko Zanzibar, imefikia wakati wa kuweka kitengo cha ufuutiliaji. Askari anatoka Zanzibar kufuatilia mambo yake huku Bara na hakuna kinachofanyika. Atapoteza fedha zake, lakini hakuna mafanikio. Hili suala nimeshalizingumza muda mrefu sana. Kwa nini zile sehemu ambazo tunahisi ni kubwa kama vile Mwanza na Zanzibar pale, tusiweke vitengo, kuwe na mtu maalum atakayesimamia mawasiliano na Bara kwa lengo la kuondoa usumbuwa wa askari kuondoka na kwenda kufuatilia mambo yao bila mafanikio yoyote? (*Makofî*)

Wapo wanawake ambao wamefiwa na waume zao wanadai na hakuna kinachopatikana, hata kikipatikana basi

anaambiwa atoe chochote ndipo asaidiwe. Huu siyo utendaji, haya mambo mengine madogo madogo ni lazima tuyarekebishe. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusu uhamiaji. Kwanza kabisa, nampongezae Kamishna kwa jitihada alizofanya, kwa kuonesha uaminifu na imani katika ujenzi wa jengo jipya. Kwa hili kwa kweli ninampongeza sana, Mungu amzidishie ili ajitihadi zaidi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna tatizo ambalo hivi karibuni limejitokeza. Kuna kijana mmoja katika mambo haya haya ya ajira aliniambia kwamba, ameambiwa aandike barua ya ajira na aipeleke Bara. Ninavyokumbuka, zamani kulikuwa na Kitengo au Kamati Maalum pale Zanzibar iliyokuwa inashughulikia maombi ya ajira katika Idara ya Uhamiaji. Hivi sasa mambo yote yanatoka sehemu moja na hili siyo jambo zuri kusema kweli kwani tumeungana. Kule tumeweka viongozi basi ni vyema tuwaamini kwamba watafuata masharti. Utaratibu wa kumtaka mtu wa Zanzibar aandike barua ya maombi ya kazi Bara au shughuli za Idara ya Uhamiaji kufanyika sehemu moja tu, itakuwa hakuna faida ya Muungano. Kama tumekubaliana, basi ni lazima na wale viongozi na watendaji walioko Zanzibar tuwaamini. Hili sipendi niente kulzungumzia tena, ajira zifuate masharti yanayokubalika, Uongozi wa Idara ya Uhamiaji ulioko Zanzibar upewe nafasi ili uweze kufanya maamuzi kama inavyofanyika katika sehemu nydingine. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ule alipokuwepo ndugu Kihamano, mara nyingi alikuwa akitutembelea, tulikuwa tunamjua. Tangu Ndugu Kihamano alipoondoka, leo ukiniuliza kuhusiana na Mkuu wa Uhamiaji simjui. Kwa hiyo, ningeomba tuwe na ushirikiano mzuri, tutembeleane kama ilivyokuwa awali. Nahisi hii itatusaidia sana na tutafanikiwa katika shughuli zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, niseme kwamba, niliwhali kuzungumza kuhusiana na Kituo cha Polisi cha Dunga. Tunangoja mpaka Kituo kile kiwaangukie wale askari ndipo

tukitengeneze! Wapo wahisani tumewapata ambao wamesema watajitlea kwa baadhi ya vifaa. Tunachoomba ni kwamba, wakati vifaa hivyo vinafika, Wizara ichukue hatua kwa kuleta mafundi na ujenzi uanze. Hilo nalisema hapa Bungeni, kwa sababu najua lile jengo la Kituo cha Polisi lisipoanguka na kuua mtu, hakuna hatua yoyote itakayochukuliwa. Lile jengo litakapoanguka tu, tutajikusanya na kuchukua hatua za haraka ili tuweze kujenga. Huu siyo utendaji mzuri. Tujitahidi kuhusiana na ujenzi wa jengo lile, raia mwema aliyechukua hatua za kujenga kituo kile, basi tuna wajibu wa kuona hisani aliyoifanya. Hisani yake kwetu sisi ni kuendeleza pale ambapo pameharibika, hii itatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.
(Makofi)

MWENYEKITI: Nakushukuru Mheshimiwa Kassim. Sasa namwita Mheshimiwa Diana Chilolo, kisha ajiandae Mheshimiwa Dickson Kilufi.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kutoa mchango wangu kwenye Wizara hii ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni katи ya nchi ulimwenguni ambazo bado zipo kwenye nafasi ya kutolewa mfano kuhusu amani. Inasikitisha sana, wapo wachache wanaotaka kuvuruga amani ya nchi hii. Pamoja na jitihada za /GP, bado kuna wachache wanaona baba wa watu hajafanya kazi. Mimi nasema Watanzania walio wengi wanaona juhudи za /GP, anafanya kazi na wale wachache nina hakika watapatikana na kama ilivyotangazwa hapa wamepatikana na wengine wataendelea kukamatwa. Namtaka /GP achape mwendo, afanye kazi, watu wanaobeza juhudи zake, aweke pamba masikioni, asikilize yale yenye maslahi kwa Watanzania walio wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tusidharau wanaosema kwamba, maafa haya yanatokana na vita za kidini. Naomba

bajeti hii ikipita, *IGP* aweke meza hapa hapa Dodoma, aite Mbunge mmoja mmoja awahoji ili wataje wale Viongozi wa Dini ambaao wanaleta maafa haya, inawezekana wanawajua. Wabunge wa CHADEMA wamesema hapa, inawezekana wanawajua. Tusizembee vitu kama hivi, watuambie, wakileta longo longo wawekwe ndani. (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo *message* imekwenda. Sasa naomba Waziri pamoja na Watendaji wote wanisikilize kuhusu kero ambazo ninazo. Mimi na Wananchi wa Mkoa wa Singida tulipongeza sana Serikali ilipogawa baadhi ya Wilaya na zikapatikana Wilaya mpya mbili. Bila kuchelewa, Wilaya hizo mbili tayari Jeshi la Polisi likawa limefungua ofisi zao japo kwa wasiwasi. Ikungi hapo ofisi ilishafunguliwa, *OCD* yupo, *OC-CID* yupo na kazi inafanya, lakini wanafanya kazi kwenye majengo ya maghala ya zamani ya mazao. Ofisi ni *square metersita* na nyumba anayokaa *OCD*iko hivyo hivyo *square meter* sita. Naomba pamoja na dhiki yote ya fedha kidogo mliyopewa, fanyeni kila liwezekenalo mwangalie uwezekano wa kuanza kujenga ofisi hizi katika Wilaya hizi mpya, Wilaya ya Ikungi na Mkalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwajengea ofisi hizo, tukawawekea na makazi ya kuishi, nina hakika vijana wanafanya kazi na watapata moyo wa kufanya kazi zaidi. Ofisi zinawavunja moyo na zinahififisha nguvu ya kazi. Naomba sana Mheshimiwa Waziri, ndugu yangu, atakapokuwa anajibu atuambie sisi wa Ikungi na Mkalama ametufikiraje katika kuanzisha ujenzi wa ofisi hizi za wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niongelee ujenzi wa nyumba. Napongeza sana juhudzi za *IGP*, zimeonekana Dar es Salaam na yale majengo ya ghorofa yanatia moyo. Ninaamini hata askari wa Dar es Salaam sasa wana moyo wa kufanya kazi kwa sababu wanaishi katika maeneo mazuri. Naomba sasa jicho lielekezwe mikoani. Nenda Singida Mjini, *line police* pale, zile nyumba zinasikitisha.

Tumeshasema sana hapa; Mheshimiwa Nchimbi mbona ni hodari sana wa kujenga hoja, huyu Waziri wa Fedha anamshindaje? Mheshimiwa Waziri apeleke greda pale Mjini Singida, abomoe zile nyumba kwani zinaharibu hadhi ya Mji. Mji wa Singida sasa hivi umeshakuwa na unapendeza, lakini unaharibiwa na majengo ya Waziri Nchimbi, kwani yanatia aibu. Tunaomba abomoe yale majengo na ajenge ya ghorofo ili Askari wote wa Polisi wapate nyumba pale. Ninaamini nyumba zikipatikana pale, heshima ya mji wetu itapatikana na askari watapata moyo wa kufanya kazi. Ninaamini hata Wilaya za wenzangu wengi wameshasema, Mheshimiwa Waziri atatusikiliza, kazi ni kwakwe atafute fedha sisi tunahitaji nyumba. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusu vitendea kazi; ni ukweli usiofichika kwamba, kuna askari wanapata shida huko vijijini. Askari anatumwa kwenda kukamata wahalifu vijijini, wako wanaotembea kwa miguu na wapo wanaokwenda kwa baiskeli. Unakuta mikononi hawana hata simu, hivi kule wanakokwenda wakivamiwa inakuwaje? Naomba watu hawa wapewe hata pikipiki ili waweze kufanya kazi zao vizuri. Nina mfano mdogo tu, hapa nje ya Dodoma, kuna Kituo cha Polisi kinaitwa sijui Bambala. Askari hawana kitendea kazi cha aina yoyote.

Nina mwanangu anafanya kazi kule, ameenda mahali unapiga hata simu hapatikani kwa siku mbili, unamwliza mwanangu leo hata hupatikani, simu hupoeki au umefungwa; anasema, mama nilikwenda kukamata mhalifu huko hata mawasiliano hayapo. Sasa huyo mtoto akienda huko peke yake akizidiwa nguvu na wahalifu inakuwaje? Naomba muwatafutie pikipiki, vilevile wapeni hata na *radio call*, angalau mawasiliano yawepo. Yeye anayeenda porini awe na *radio call* na kituo kiwe na *radio call*, ili angalau wawasiliane juu ya kinachoendelea huko vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu Serikali jitahidini kufanya hivyo kwenye vituo vyetu vyaa polisi huko vijijini. Watakuwa wamewasaidia hawa askari kufanya kazi zao vizuri

na vilevile wao kujilinda, kwa sababu hata wao ni binadamu. Sasa hivi mnaona wenyewe askari wanauawa, jambo ambalo halikuwepo. Siku zilizopita jambo hili halikusikika kabisa, lakini sasa hivi linasikika. Kwa hiyo, ni lazima pia muwawekee tahadhari askari wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nzungumzie kuhusu Magereza yetu. Yanafanya kazi nzuri sana ya kilimo na ufgaji. Natolea mfano Gereza la Manyoni, wamelima na hata mkienda pale mtafurahi. Naomba ile Kamati ya Ulinzi na Usalama itembelee Gereza la Manyoni, tabu yao hawana hata trekta moja, wanakodi matrekta. Trekta la kukodi mji mzima wa Manyoni linaweza kuwa moja au mawili. Watu wanapanga foleni, unakuja kulimiwa mvua zikiwa zimeisha. Naliombea Gereza hili la Manyoni kwa makusudi lipewe trekta ili liweze kufanya vizuri kazi zake za kilimo pamoja na ufgaji. Naomba sana askari wanapofanya kazi nzuri washukuriwe na pia wapewe vitendea kazi ili waweze kufanya kazi zao vizuri. Mkuu wa Gereza la Manyoni, anafanya kazi nzuri sana, nampongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee kuhusu suala la UKIMWI kwenye Magereza yetu. Jamani kuna vitendo vya ajabu vinafanyika huko Magerezani, akina baba wanafanya matendo mabaya wao kwa wao. Sasa sijui muanze kupima wafungwa hawa wanapokuwa wanaingia huko magerezaji, sijui vipi, hata sielewi. Naomba itafutwe dawa ya kukomesha matendo machafu ndani ya Magereza, kwa sababu kama watu wameenda kujifunza huko, wakirudi nyumbani na UKIMWI si wataenda kuua akina mama! Hili lipo, tumetembelea Magereza Dar es Salaam, Ukonga huko, wafungwa wenyewe wamejieleza kwamba matendo haya yapo na wanafanya tena hawana kinga zozote. Naomba suala hili la UKIMWI tusilifanyie ajizi kwani linapoteza Utanzania wetu na ni jambo ambalo siyo zuri kabisa. Naomba likomeshwe kwenye Magereza yetu lisiendelee, wanaopatikana na hatia ya jambo hili waongezewe adhabu labda wataacha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee kuhusu wahamiaji haramu. Wahamiaji haramu bado wapo mipakani. Ninaomba sana zoezi la kuwaondoa wahamiaji haramu mipakani lifanywe haraka kabla Vitambulisho vya Taifa havijafika kwenye mikoa ya pembezoni. Zoezi hili likifika huko, msishangae watu ambao siyo Raia wa Tanzania wakapata vitambulisho. Naomba watu hawa waondolewe mapema iwezekanavyo ili zoezi la vitambulisho litakapofika kwenye mikoa hiyo ya mipakani; Kigoma, Kilimanjaro, Mara, Kagera na maeneo mengine, hawa wahamiaji haramu wawe wameondoka ili tusije tukasajili watu ambao siyo Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusu posho za askari; ni ukweli usiofichika posho hizi tayari zimepitwa na wakati, hebu muwafikirie hawa vijana wanaofanya kazingumu. Waongezeeni posho kwani ni ukweli usiofichika polisi wanafanya kazi ngumu. Wameeleza wenzangu hapa, wanatoa uhai wao kwa ajili yetu Watanzania. Posho hizi haziendi na wakati tulionao, maisha yamekuwa juu, kwa hiyo, ni lazima na posho hizi mziangalie zipandishwe kwa kuzingatia gharama za maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. MODESTUS D. KILIFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Wizara hii ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza sana ndugu zetu Askari Polisi kwa kazi nzuri na ngumu wanayoifanya ya kulinda usalama na mali za Raia wa Tanzania. Kazi hii ni ngumu, pasingekuwepo na polisi nina hakika hali isingekuwa hivi ilivyo sasa. Vilevile niwapongeze sana Askari Magereza kwa kazi ngumu wanayoifanya. Kazi ile ni ngumu, inayotaka kujittoa, hivyo inatakiwa iangaliwe sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, niseme kwamba, suala la amani katika nchi yetu sasa linaanza kuingia dosari. Haya matukio yanayotokea nchini mwetu kama lilitokea Arusha, nawapa pole sana wale wote waliopatwa na maafa haya. Mwenyezi Mungu aziweke mahali pema peponi roho za wale waliopoteza maisha.

Ndugu zangu, tatizo hili lisiangaliwe tu kwa wasiwasi. Inawezekana mengine ni ya kwetu humu humu ndani. Tukizama sana kunawenza kukawa kuna nguvu nyingine ya kutoka nje ya nchi yetu kwa maslahi yao binafsi ya kutaka kuona amani ya Tanzania inatoweka. Wakatumia nafasi hiyo ili tugombane wenyewe kwa wenyewe hasa baada ya kugundua kwamba, Watanzania wanapenda amani, hakuna namna nyingine yoyote ya kuwavuruga, sasa tuingie kwenye dini. Tukiwavuruga kwenye dini huku tutafanikiwa.

Kwa hiyo, kuna haja ya kufanya uchunguzi wa kutosha kuangalia hali ambayo si ya kawaida kwa Tanzania. Waislam na Wakristo tumekuwa tukizikana na tukishirikiana kwa mambo mengi, hatukuwa tunabaguana, lakini sasa tunakoelekeea, inaonekana sasa tunaweza tukapoteana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi, kwa mambo ya ndani ya nchi kuna miadhara huwa inaendeshwa; kuna kanda na *CD* huwa zinazungumzia madhehebu mengine. Nadhani tuanzie hapo, tupige marufuku, hakuna mhadhara utakaoruhusiwa kuzungumzia mambo ya dhehebu lingine, na kusiwe na mhadhara wowote wala *CD* yoyote itakayokejeli dhehebu lingine. Haya tukiyaachia yakiendelea ndiyo yanaendelea kujenga uadui na fitina kati ya dhehebu na dhehebu na pengine yanaweza yakatupeleka pabaya na hao wasiotutakia mema wanaingilia hapo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya Jeshi la Polisi inatakiwa kuangaliwa kwa makini sana, makazi yao ni duni mno. Wilaya ya Mbarali, Askari Polisi hawana nyumba, mimi sijui kwa nini Wilaya hii imesahauliwa kiasi hicho. Sasa najiuliza hivi wanalipwa *allowance* ya kukosa nyumba kila mwezi au mshahara wao huo huo ndiyo walipe na kodi ya nyumba?

Sijajua, Wilaya ya Mbarali ina Vituo vya Polisi, lakini vituo vile ukienda kuviona vingine hata havina hadhi vipo katika hali mbaya sana. Tuna Kituo cha Polisi pale Madibira, tuna Kituo cha Polisi pale Chimala, tuna Kituo cha Polisi pale Ingulusi, lakini ni Vituo vya Polisi unaweza ukafikiri ni *station* ndogo tu wakati Mji ule ni muhimu sana, wenye biashara nyingi. Wilaya ya Mbarali ina shughuli nyingi za kibiashara ambazo zinahitaji ulinzi thabiti wa Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya makazi ya Askari Polisi hawa inabidi iangaliwe kwa makini. Mimi bajeti hii siiungi mkono, lazima tufanye mabadiliko iongezewe fedha tuweze kutatua matatizo ya Askari wetu hawa. Kwa kazi ngumu wanayoifanya, mimi nilikuwa napendekeza kuwepo na *allowance* maalum kwa ajili ya shughuli ngumu wanazozifanya Polisi. Hii inawezekana, kama hatutafanya hivyo tutaendelea kuwalaamu. Kazi wanayofanya Askari Polisi ni ngumu sana na ni kazi ambayo inahitaji kujitoa uhai kupambana na majambazi na pengine yanakuwa na silaha, kwa hiyo, siyo kazi ndogo. Sisi wakati huo tunakuwa tumelala majumbani mwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri za Jeshi la Polisi, lakini yapo matatizo madogo madogo. Naomba Uongozi wa Jeshi la Polisi uangalie wale Askari wote wanatia dosari Jeshi hili zuri la Polisi ambalo lipo kwa ajili ya kulinda uhai na usalama wa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajali nyingi barabarani zinapotokea, Askari Polisi hawa hasa Trafiki, wamekuwa wakijitahidi sana. Mimi nawapongeza, inapotokea ajali haipiti muda mrefu wanafika na hii tumeshuhudia kama wasingekuwa hivyo basi hali ingekuwa mbaya zaidi. Kwa hiyo, naomba moyo huo wa kujitoa na kulinda usalama na maisha ya Watanzania uendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini yapo matatizo vilevile inapotokea kwa namna yoyote ile Mwananchi ameuawa na Askari Polisi, sijajua ni hatua zipi stahili ambazo zinapaswa kuchukuliwa. Kumbukumbu yangu inaonesha tarehe 16

Januari, 2011 raia anayeitwa Justin Miamba aliuawa na Askari Polisi pale Ubaruku Mbarali. Justin tangu ameuawa hakuna hatua inayoonekana Jeshi la Polisi au Serikali imechukua dhidi ya yule aliyehusika na hakuna anayejali. Familia ile imebaki hakuna wa kuiangalia, baba amekufa, amebaki mama anaitwa Hatu Mtewa, anahangaika tu hana mtu wa kumwangalia. Wananchi wamejitahidi kumsaidia lakini wamefika mwisho. Sasa tupate ukweli inakuwaje pale Polisi wanapomuua raia na yule Askari Polisi alifyatua risasi ikampiga kichwani kwenye kundi la watu na akafariki pale pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, raia mwingine anayeitwa Hassan Masila naye alijeruhiwa mpaka leo ni mlemavu alipigwa risasi ya mguuni. Sasa inapotokea hivi, Serikali inawasaidiaje wale wahanga? Tunafanya nini kwa yule mtu ambaye alipoteza? Je, angekuwa ni raia amemuua Askari tungenyamaza? Naomba nipate majibu kwa nini Askari anapopoteza maisha ya raia hakuna hatua zinazochukuliwa na hakuna ufuatiliaji wowote?

Tupate majibu na tuone hatima ya Marehemu Justin Miamba kwa familia yake; Serikali inachukua hatua gani? Namna gani huyu mjane pamoja na familia yake atatunzwa na Serikali kwa sababu hakuna mtu wa kumlea tena?

Mheshimiwa Mwenyekiti, matukio kama haya, yamekuwa yakijitokeza mara nydingi, kuna Mwananchi anaitwa Mwigulu Ngulu wa Kijiji cha Kapunga kule Wilayani Mbarali, alijeruhiwa na Mwekezaji wa Kapunga na huyo mtu ni mlemavu mpaka sasa miguu anatembea anavuta tu. Polisi walipelekewa taarifa wakachukua hatua na mimi mwenyewe nikajulishwa kwa maandishi kwamba hatua zinachukuliwa kumsaidia yule Mwananchi, mpaka sasa kuko kimya. Yule Mwananchi amebaki hana msaada hawezikulima tena na wala hawezikufanya chochote. Nataka tupate majibu ni hatua gani zinachukuliwa dhidi ya matatizo haya yanayowakumba Wananchi na wanakabidhiwa Polisi lakini mwisho hauonekani, kesi haiendi mahakamani na wala hakuna hatua zinazochukuliwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hizi ni baadhi ya dosari ambazo tuzirekebisha, Jeshi la Polisi lipo vizuri. Mimi ninawapongeza sana ndugu zangu Askari Polisi na ninawapongeza sana kwa usimamizi mzuri wakati wa Mikutano ya Viongozi. Mimi mwenyewe ni shahidi, kila nilipokwenda nilipewa ulinzi wa kutosha. Namshukuru sana *OCD* wa Mbarali, pamoja na Askari wake, jinsi wanavyopanga vizuri Askari wake kuangalia Wananchi na mali zao na usalama wa mali zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna jambo ambalo linatakiwa kuangalia sana ni kuweka mtandao mzuri kwa hawa ndugu zetu Askari. Wilaya ya Mbarali ni kubwa sana. Ukitoka Madibira kuja Rujewa hapa katikati kuna Kata inaitwa Kata ya Mapongolo, kwenda Madibira ni mbali, kuja Rujewa ni mbali, ikitokea uvamizi wowote maana yake wale watu hawana msaada. Nilikuwa naomba pale kiwepo Kituo cha Polisi ili usalama wa wale Wananchi uweze kuwa wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Kata ya Rwiwa kumekuwa na matukio mengi sana, watu wanaauawa mara kwa mara. Kwa hiyo, ningeomba Serikali ione umuhimu wa kupeleka Kituo cha Polisi kule Rwiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimeseme, kama kuna jambo ambalo sitaunga mkono ni kutokuona bajeti ya Jeshi la Polisi pamoja na Askari Magereza inaongezwa. Pale kwangu Mbarali, nilitoa taarifa kwa Mheshimiwa Waziri kuhusu Gereza la Mbarali. Gereza lile lilijengwa halikwisha, matokeo yake sasa wakubwa na wadogo wote wanalandikwa mahali pamoja na mengine yamezugumzwa humu mambo mabaya. Sasa wale watoto wanalandikwa na watu wazima inakuwaje?

Gereza lile halina umeme, gereza lile maji ni shida, gereza lile ulinzi wake ni mgumu sana. Kulinda gereza ambalo halina umeme ni kazi kubwa. Nimekuwa nikisema mara kwa mara, naomba gereza lile likakamilishwe ili taratibu za kimagereza ziweze kufanyika vizuri. Nafikiri Mheshimiwa Waziri ananisikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba hilo jambo liangaliwe kwa umakini na wale Askari Magereza hawana nyumba, wale Askari Magereza hawana huduma nzuri ya maji, wanafanya kazi ile katika mazingira magumu mno na Serikali ndiyo hiyo. Kwa nini tusiongeze bajeti huduma kama hizo zikaboreshwa ili Askari wetu wafanye kazi katika mazingira mazuri? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitaunga mkono tu pale nitakapopewa majibu ni lini Gereza la Mbarali litakamilishwa vizuri na wale Askari Magereza wataboreshewa makazi yao ili wafanye kazi vizuri na ni lini Askari Polisi wa Mbarali na nchini kote walipo wataboreshewa makazi yao, pamoja na kuwafikiria posho kutokana na mazingira magumu ya kazi wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hayo yote sitapata majibu kwenye majibu ya Mheshimiwa Waziri, basi mimi sitakuwa tayari kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya usalama katika Taifa letu kama nilivyosema inategemea Jeshi la Polisi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Nakushukuru Mheshimiwa Mbunge, ahsante sana.

MHE. MODESTUS D. KILUFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Sasa namwita Mheshimiwa Sylvester Mabumba, ajiandae Mheshimiwa David Kafulila.

MHE. SYLVESTER M. MABUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama muda utanitosha nina mengi lakini naomba nianze na hali ya Usalama kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mnisikilize; hali ya usalama katika nchi yetu ni mbaya na ubaya wake ni kwa sababu ya Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi ambayo inafanya uchunguzi usiokuwa na mwisho. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katibu wa Mufti alimwagiwa *acid* hatujaambiwa nani alihusika, Padri alijeruhiwa hatujaambiwa nani alihusika, Padri akauawa hatujaambiwa nani alihusika na sasa ya Arusha nayo tutaambiwa sijui nani kahusika. Ninaomba kama kweli tunataka CCM ishinde mwaka 2015, lazima uchunguzi ufanywe na ukamilike kwa wakati, haiwezekani ukawa unachunguza jambo moja kwa mlezi, kwa miaka, huwaambii watu wako ambao walikupa ridhaa ya kuongoza wasiwe na hofu.

CCM ambayo Serikali zake hizi mbili ya Muungano na ya Mapinduzi ya Zanzibar ina ridhaa ya watu wengi, asilimia 78, tunaogopa nini kukamata wahalifu? Tusipofanya hivi, nasema kweli mwaka 2015 patakuwa pagumu. Mwenye masikio na anisikie na anayedhani amesimama, aangalie asije akaanguka. Haya ni maneno ya unabii kwenye Biblia, mimi ni Mkristo, maneno haya lazima tuyazingatieve. Tusipoangalia, mimi ninasema kwa dini zote mbili, kwa Waislam na Wakristo, tushikamane tuungane tukate tunapooleka Taifa letu sasa hivi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusifikirie Somalia walianza kama vile walivyo, walianza kama hivi humu ndani, Majeshi yetu kila mmoja ana dini yake, sasa tunapoanza kuvamia Viongozi wa Dini, Taasisi za Dini, ni mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuwe makini, tukio la jana tumeona kwenye TV, umati wote ule umekusanyana pale kwa ajili ya sherehe ya ufunguzi wa Kanisa, anakuja mhalifu ambaye hatujamua bado, lakini ninaamini AG Said Mwema, yeeye si Jeshi la Kikoloni, ni mtaalam, msomi, naamini

ana wataalam atawatumia kuwakamata hao watu waliofanya uhalifu huo. Tuna imani naye kwa sababu kama amewahi kufanya kazi kwenye *Interpol* mtu ambaye hajafundisha, hajasoma, asingekaa kule, atumie nguvu zake zote na utaalam wake kuwakamata hao watu na kuwapeleka katika Vyombo nya Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumza kwa uchungu kuhusu matukio ya sasa, tusije tukaanza kufikiriana huyu kalubuniwa, huyu kafanya nini. Sote tushikamane, tuwe kitu kimoja, tunu ya amani na utulivu ambayo tumeachiwa tunaichezea. Hata hao Wanyarwanda walipouana ni kwa sababu hii. Mimi ninashangaa sana, wakati huu wa Jeshi letu lenye wataalam, unakuta meseji zinatembea za maudhi, za uchochezi, unakuta mihadhara inafanywa, *CDzinatembea*, tunaambiwa wahusika hawafahamiki; maana yake nini?

Tuna imani kubwa na Serikali, Serikali ikunjue makucha yake tusiangularie ni nani amefanya, tunaogopa nini, tusichezee amani yetu. Namwomba Mheshimiwa *IGP* kwa utaalam wake; kwanza, ninamshukuru sana, huwa ninampigia simu mara nydingi na ananisaidia sana upande wa kule Zanzibar, lakini naomba sasa wepesi wake huo aoneshe utaalam wake, tuseme mwisho ni sasa tuisubiri kesho. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijielekeze katika usawa barabarani. Mheshimiwa Waziri ametuambia hapa kwamba, mwaka jana walikuwa Watanzania 4,062, ni watu wengi sana na amesema pia kuna Watanzania 37,000 walijeruhiwa, pia ni watu wengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kama inawezekana, tumeambiwa kuna Kitengo cha TEHAMA, Jeshi la Polisi tumieni *camera kufuatilia* hayo, madereva wazembe, lakini vilevile mhakikishe hao madereva wote wana leseni ambazo ni halali kutoka *NIT* au vyuo ambavyo Jeshi la Polisi linavitambua vizuri. Watanzania 4,000 wamekufa na pengine hao ndiyo walikuwa nguvu kazi yetu na walipa kodi vilevile na ndiyo matumaini katika familia zao; kama Taifa tumefanya

nini? Tumewafidia namna gani hao na hao ambao wamejeruhiwa pengine wamepata ulemavu wa maisha tuna mikakati gani kuwasaidia watu hawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia tuwe makini tusikubali tena, mwakani tukija hapa tuisomewe idadi kubwa kama hii kutokana na ajali za barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana Polisi wetu watimize wajibu wao hata kama tunasema kwamba mishahara yao ni duni, lakini moyo wa uzalendo huwa hauongozwi na mishahara. Naomba maslahi yaboreshwe, lakini moyo wa uzalendo uwe mbele. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niungane na wenzangu waliosema kwamba, tusajiri vijana kwa kuwaokota barabarani, wapitie JKT, wawe na ule moyo wa uzalendo baada ya mafunzo ya JKT waingie Polisi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niende mbio; Jeshi la Polisi lina mkakati ambao unasaidia kubaini, kuzuia, kudhibiti wahalifu na kukamata wahalifu. Mkakati huu naomba upitiwe upya. Kama kweli tuna mkakati huu Jeshi la Polisi haya matukio ya hivi karibuni kwa nini yanajitokeza? Maana yake mlipobaini mlitakiwa tayari mchukue *precaution* kuzuia jambo hilo lisijitokeze. Sasa leo haya yanajitokeza na mkakati tunao. Namwomba Mheshimiwa /GPna Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, washirikiane kuangalia vizuri mkakati huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia naomba nizungumzie kuhamasisha maandamano, Watanzania wakatae maandamano. Wakati huu ni wa kujenga nchi yetu na kujenga uchumi wetu, tunapoandamana bila kikomo maana yake nini? Maana yake hawa watu hawatashughulika na uzalishaji, mwisho wa siku wanajeruhiwa kwa sababu maandamano yaliyo mengi hayana kibali cha polisi. Wananchi wa Tanzania wayakatae maandamano, nawaomba sana ili kuweza kujenga nchi yetu, kujishughulisha na uzalishaji na hivyo kuwa na uhakika na maisha yetu, kwa

familia zetu na hata tunaposema watoto wetu tuwasomeshe, utawasomesha kama utakuwa na uchumi imara wenye kueleweka. Kama ni uchumi wa maandamano kila siku, huwezi kujenga uchumi wako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia kuhusu maslahi sasa ya Jeshi la Polisi. Katika Jimbo langu la Dole tuna kituo kidogo pale Mwembe Mchomeke, kimepandishwa hadhi kuwa Kituo cha Trafiki Wilaya, lakini majengo yake, kwanza, kuna jengo moja namwomba Mheshimiwa Waziri, Kituo cha Mwembemchomeke kijengwe sasa ili Askari wale waweze kufanya kazi katika mazingira mazuri. Pia ofisi ya Mkoa wa Kusini ambayo ipo ndani ya Jimbo la Dole pale Wilaya ya Kati Mwera, majengo yake ni machakavu sana.

Nachelea kushawishi wenzangu tuzuie bajeti mpaka llongezwe fungu katika Jeshi la Polisi ili Jeshi la Polisi liweze kweli kuwa na mazingira mazuri, vifaa vyatutende kazi, tunavyowalaumu kama hawana magari, hawana mafuta, maeneo yao hayaridhishi, hawawezi kufanya kazi nzuri. Naamini Serikali yangu ni sikivu, itaongeza fungu kuangalia katika maeneo ambayo kuna hela nyinji za kutafuna tuache kuwa na bajeti ya utafunaji na ya ulaji tupeleke katika Miradi ya Maendeleo. Jeshi la Polisi wanajitolea sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna askari wetu ambao wanajeruhiwa wakiwa kazini, wengine wanapoteza maisha yao, kama Serikali naomba uwerekwe mpango mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofii*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mabumba, nakushukuru. Sasa namwita Mheshimiwa David Kafulila na Mheshimiwa Dkt. Chami ajiandae.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja

muhimu kabisa katika usalama na uhai wa Taifa lolote Duniani. Awali ya yote, niseme tu kwamba, nawapa pole wafiwa kufuatia tukio la kigaidi mionganini mwa tukio adimu kuwahi kutokea katika historia ya Taifa letu. Tukio ambalo linahusisha mauaji ya raia kwa silaha za kijeshi kama bomu. Hii ni dalili mbaya sana katika Taifa letu; ni dalili kwamba uhakika wa maisha ya watu sasa uko kwenye hatihati.

Hatuwezi kujenga Taifa kwa namna yoyote ile, iwe katika Sekta ya Elimu, Afya, hatuwezi kujenga uchumi, hatuwezi kujenga jambo lolote kama tunaishi kwenye Taifa la wasiwasi. Kazi ya kwanza ya Serikali ni kuhakikisha usalama wa raia wake. Kwenye uchumi tunaambiwa kwamba, *no peace no production*; kwamba, kama hakuna amani watu hawawezi kuzalisha. Najutia kimsingi na nasikitika kuona ya kwamba, kama Watanzania tumeishi katika mazingira ya klimaskini kiwango hiki, tukiwa na amani kwa miaka 50, sipati picha kama amani hii inavurugika, watawala wetu wanaweza wakatufikisha kwenye hali gani. Maana tunakufa kwa magonjwa yanayotibika, tunapoteza maisha pasipo sababu wakati nchi ina amani; je, tukiingia vitani hali itakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili linahitaji maamuzi na tunahitaji Serikali ijenge uwezo wa kufanya maamuzi yake. Naomba Mheshimiwa Waziri na ndugu yangu /GP Saidi Mwema, mfike mahali sasa muamue kwamba, hii ni nchi ambayo watu wanahitaji uhakika wa usalama. Kuna matatizo ya mitafaruku ya kidini, hii ni changamoto kubwa kwenye Taifa hili. Vyombo vya Dola vinapaswa kufanya kazi kwa mujibu wa taratibu na sheria na siyo hisia za kidini. Nasema haya kwa sababu tumefika wakati Jeshi la Polisi linaanza kufanya maamuzi kwa misukumo ya hisia za kidini.

Unafunga redio ya Waislam, unafunga na ya Wakristo *ku-balance*, hatuwezi kuwa na Serikali ya namna hiyo. Tunahitaji kama ni redio ya Waislam imefanya makosa inachukuliwa hatua bila ya kuhitaji *ku-balance* na redio ya Wakristo. Kama redio ya Wakristo imefanya uchochezi, inachukuliwa hatua bila ya umuhimu wa *ku-balance* na

kufunga redio ya dini nyingine. Tukichukua sheria tunaweza tukakomesha tatizo hili, lakini tukiendelea na utaratibu huu wa kufanya maamuzi kwa hofu, hatuwezi kuwa na Serikali ambayo inafanya maamuzi kwa hofu lazima Serikali ifanye maamuzi kwa taratibu na sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ya Mambo ya Ndani ya Nchi ina mambo mengi, lakini mionganoni mwa changamoto ambazo inazo mpaka sasa ni eneo la Magereza. Tuna wafungwa takriban 18,000 mpaka sasa, ni aibu katika namna yoyote ile Serikali kuomba Bunge liidhinishe fedha kwa ajili ya chakula cha Magereza. Katika hali ya kawaida, kama mtapata Wakuu wa Magereza wenye uelewa wa kujua wajibu wao, Magereza ile idadi ya watu peke yake ni mtaji wa kuweza kuzalisha. Nchi hii ina maeneo makubwa ya kilimo, mnashindwaje kutumia teknolojia hata ya jembe la ng'ombe kuwfanya hawa wafungwa waweze kuzalisha?

Ningeomba Mheshimiwa Waziri ni kijana mwenzetu, ninaamini kwamba katika hili sasa imefika muda uoneshe kwamba inawezekana Magereza kujitegemea. Haiwezekani tuendelee kutenga bajeti ya chakula kwa Magereza, lazima Magereza ijitegemee hata kwa jembe la ng'ombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi hili la Polisi lina changamoto nyingi, moja ya changamoto ni uduni wa miundombinu pamoja na zana ambazo wanazitumia. Mimi natoka Kigoma, ni mkoa ambao una ukanda mrefu sana wa mpaka ambao uko wazi wa Ziwa Tanganyika. Eneo lile kwa mapana yake huduma ya Kipolisi ipo chini kuliko eneo lolote katika nchi hii, lakini ni *risk* kubwa kuacha eneo lile wazi bila huduma za Kipolisi.

Nimechangia pia hata kwa maandishi kumwuliza Mheshimiwa Waziri kwa sababu gani *RPC* anatengeneza mageti matano kwenye umbali wa kutoka Uvinza mpaka Kigoma Mjini, kilomita 80 mageti matano, ambayo ni usumbufu kwa akina mama wauza maharage na mahindi; hakuna sababu yoyote ile. Mnaacha kuweka Polisi kwenye

maeneo muhimu ya kiusalama mnaweka kwenye maeneo ambayo ni kwa ajili ya rushwa na usumbufu kwa raia. Kwa hiyo, naomba suala hili la mageti litazamwe kwa uangalifu mkubwa kwa sababu siyo kazi yake kusumbua raia. Sikatai mageti lakini kuna mazingira ambayo yanaonesha kwamba, sasa Polisi hao wanatumika vibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nisisitize kwamba, Mkoa wa Kigoma sasa una changamoto ya kuwa na *RPC* ambaye anaongozwa sijui na vikao vya namna gani, huenda ni vya vichochoroni, anafanya maamuzi ya hovyo kila kukicha. Mimi ni mstaarabu sana na naamini Mheshimiwa Waziri una ustaarabu wa kutosha, hapa kuna kazi ya kuchukua na hatuwezi kuwa na *RPC* ambaye anaongozwa na Mwenyekiti wa CCM pale anasumbua raia, anaweka watu ndani, halwezekani. Ule mkoa una historia ya watu wasiopenda kuonewa, *RPC* huyu anaonesha uonevu, juzi alimweka ndani Diwani wa Upinzani bila sababu yoyote ile. Juzi alifanya uonevu huu, Kigoma ni watu wavumilivu ni watu wastaarabu, lakini hawapendi kuonewa. Watu wa Kigoma wakichoka ule Mkoa hautawaliki tena. Ni busara tu ya Mheshimiwa Zitto, Mheshimiwa Kafulila, Mheshimiwa Machali na akina Mkosamali, Wabunge wa Mkoa wa Kigoma hatutaki ule Mkoa uingie kwenye vurugu, lakini *RPC* yule ni chanzo cha vurugu. Kama ataendelea, tusije tukalaumiana baadaye kwa sababu hatuwezi kuwa na *RPC* ambaye kila kukicha anafanya vitu vya hovyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ya Mambo ya Ndani ya Nchi moja ya changamoto yake kubwa nimesema ni suala zima la Polisi kuwa na vifaa vya kutosha kukabiliana na changamoto za leo. Leo matatizo ya ugaidi yako Dunia nzima, tunaona Marekani Taifa kubwa na bajeti kubwa ya ulinzi kuliko nchi kumi ambazo zinafuatia Duniani, yaani katika nchi kumi zenyet bajeti kubwa ya ulinzi, ukichukua nchi ya pili mpaka ya kumi na moja bado bajeti yake ni pungufu kwa bajeti ya ulinzi ya Marekani kwa Dola za Kimarekani bilioni 86.

Kwa hiyo, unaweza ukaona namna gani ambavyo wana bajeti kubwa, lakini bado wanakabiliwa na matatizo haya ya kigaidi. Kama Taifa kubwa kama Marekani wana changamoto kubwa kiasi hiki katika masuala ya ugaidi, Tanzania tukifanya masihara tukawa na Polisi hawa goigoi, ambao hawapati chakula cha kutosha, wanadhulumiwa, nilikuwa nazungumza na mtaalamu mmoja wa Polisi, kwamba Polisi inadaiwa mpaka simu wana madeni makubwa, malimbikizo ya mishahara wanadai *billions of shillings* hawa Polisi hawawezi kutimiza wajibu wao.

Nakuomba Mheshimiwa Waziri ni wajibu wa Serikali sasa kuweka ajenda ya amani, kuweka ajenda ya Polisi Wizara ya Mambo ya Ndani kuwa ajenda ya juu kuliko yoyote, maana hatutazungumza chochote kama hawa watu wataendelea kuichezea hii nchi. Hii ni nchi kubwa, yenye historia katika Bara la Afrika, ilikuwa inakomboa baadhi ya nchi za Afrika, Msumbiji huko mpaka Zimbabwe. Hii ni nchi ambayo hatuwezi kuwa legelege kiasi kwamba wahuni wachache wanaweza wakawa wanalivuruga Taifa hili. (Makof)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Cyril Chami.

MHE. DKT. CYRIL A. CHAMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Napenda kuchukua fursa hii, kwanza, kusema kwamba, naunga mkono hoja. Pili, napenda nimpongeze sana ndugu yangu, Dkt. Emmanuel Nchimbi, Waziri na Naibu Waziri, Mheshimiwa Pereira Ame Silima, kwa kazi kubwa wanayoifanya. Ni mara nydingi tunakuwa wepesi kulaumu lakini zipo Wizara zenyekiti za lawama tu. Wizara ambazo zina mambo ya uchumi uchumi hivi, fedha fedha hivi, biashara na ambapo mtu anapata fedha pale huwezi kuepuka lawama. Halafu zipo Wizara nydingine ambazo fedha hazionekani moja kwa moja, lakini mtu akipinda sheria kidogo anapata fedha.

Sasa kati ya Wizara hizi, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ni Wizara mojawapo ambayo ni ya lawama tu. Kama mtu atakuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ategemee kupendwsa na watu wote, atakuwa hafahamu kazi yake sawasawa. Kwa sababu wapo watu waadilifu wengi sana katika nchi ya Tanzania na hata katika Bunge lako Tukufu, wako Viongozi wengi sana waadilifu, lakini lazima tukubali ukweli kwamba wapo wahalifu katika nchi yetu. Lazima tukubali kwamba, wapo watu ambaao wanaonekana kwamba ni waadilifu, lakini wanaunga mkono uhalifu nyuma ya pazia. Sasa watu kama hao, hawawezi kumpenda Waziri anayechapa kazi ya kudhibiti uhalifu. Kwa hiyo, Waziri, ndugu yangu Mheshimiwa Nchimbi na Naibu Waziri, Mheshimiwa Pereira Ame Silima, mnapolauwiwa nasema kazeni *boot*, tuko nyuma yenu, tunaona kazi mnayofanya tutawaunga mkono katika kazi hii kubwa ambayo mmepewa na Mheshimiwa Rais. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini namshukuru sana na kumpongeza /GP. Ukitosha vyombo vya habari na ukisikiliza mambo ambayo yanensemwa unaweza ukadhani kwamba /GP labda huyu ni *average performer*. Nataka niseme kwa kweli tunaye /GPambaye atatolewa mifano na vizazi vijavyo kwa jinsi anavyochapa kazi. Mimi nilikuwa muhanga wa tukio la uvamizi ambapo tulivamiwa tukiwa kwenye kikao pale Riverside Dar es Salaam mwaka 2005, kabla Mheshimiwa Kikwete hajawa Rais hapa. Tulivamiwa pale tukapigwa sana, tukanyang'anywa kila kitu, fedha, simu lakini tangu Mheshimiwa Rais Kikwete amemteua /GP Saidi Mwema, mambo yale sijayaona mahali popote. Mkiyaona haya yanafanyika, tusidhani kwamba yanakuja tu yenye kwa kudra za Mwenyezi Mungu, ipo kazi kubwa inafanyika. Mimi nampongeza /GPna nawapongeza Wanausalama wetu kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nataka nizungumzie kuhusu hali hii ya uvunjifu wa amani ambayo imeanza kujitokeza sasa katika nchi yetu, pamoja na kazi kubwa ambayo wanafanya /GPna vijana wake. Mimi nafikiri jambo hili linasababishwa na watu wanaopenda kutumia matatizo

ya Wananchi kujijenga kisasia na kiuchumi na hapa haijalishi kama ni chama chochote, inawezekana wengine Chama Tawala, wengine Upinzani na wengine hawana hata chama, lakini wanajua kwamba wakitumia fursa ya matatizo ya Wananchi wanaweza kujijenga kiuchumi au kisasia au katika jamii na kadhalika. Nataka niseme; kwa mfano, Mwananchi ambaye mshahara wake anaona kwamba hautoshi, ukamwambia kwamba hali ni mbaya kwa sababu ya fulani, unamsema labda Rais au Waziri fulani ama Serikali, atakubali anaonewa. Unapolinganisha na nchi nyingine ya Kiafrika, unapata wapi kigezo cha kusema kwamba hali ni mbaya kwa sababu ya mtu fulani wakati katika nchi nyingine za Kiafrika hali ni mbaya kuliko hapa kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi ambao tunaumiliki ni ule ule ambao unamilikiwa na wenzetu katika nchi za Kiafrika. Wewe unamdanganya Mtanzania unamwambia kwamba wenzetu wa Marekani, Marekani siyo wenzetu kwa maana ya uchumi. Kipato cha Mmarekani dola 40,000 kwa mwaka, kipato cha Mtanzania ni dola 500 kwa mwaka unamwambia huyu Mtanzania kwamba Wamarekani wanapata hiki wanakosa hiki, kwa hiyo basi, tuandamane, tuvunje sheria.

Mimi nadhani tufike mahali kama Watanzania tujue kwamba, mjenga nchi ni Mwananchi na mbomoa nchi ni Mwananchi. Kwamba, itakapotokea tukaingia vitani hapa Tanzania kwa sababu ya watu wanaopenda kujiimarisha kiuchumi au kisasia, kwa hakika hata hao ambao wanachochea nao watakuwa na kilio. Nataka nirudie hapa siyo kama nalenga Chama chochote wala Upinzani wala Chama Tawala, napenda kusema kuwa, Viongozi wowote katika nchi yetu ambao wanatumia fursa hizi, kwa kweli wajue kwamba wanatupeleka pabaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tawala za kidikteta Duniani zilianza hivi hivi kama tunavyoona hapa hivi sasa. Hitler miaka ya 30, yaani mwaka 1930, kule Ujerumanii alitumia fursa hizi hizi za kuwaambia Wananchi unaona Serikali haifanyi hiki na kadhalika, akaanza *mass protest* na Serikali ikakaa kimya tu

ikaacha, kuja kushtuka Hitler ameshakuwa *so powerful*, hakuweza tena kudhibitiwa. Ameiingiza nchi ile ya Ujerumanî katika mfumo wa unazi na unazi umekuja kudhuru Dunia nzima, ndiyo imesababisha Vita ya Pili ya Dunia. Kwa hiyo, naomba tusione jambo hili kama ni jambo dogo.

Nataka nimwombe sana Mheshimiwa Nchimbi na *IGP* Saidi Mwema na wale wengine, kwa kweli endeleeni kudhibiti haya matukio ambayo yanatokea. Watu wanaamua tu kiholela bila ya kujali kama mtapata sifa, pengine mtapata sifa kwa Mungu, lakini siyo katika ulimwengu huu, historia itawahukumu. Tukiangalia hata hapa Rwanda kwa jirani zetu, ilianza hivihivi kama utaniutani tu. Watu wanaanza kusemana hiki na kile, matokeo yake yakawa haya. Katika hili nataka niombe, vyombo vyâ habari vinachochea sana mitafaruku katika jamii. Wakiamua vile vyombo vyâ habari hao hao wanawenza wakarekebisha hali hili na nchi yetu ikawa moja, jamani tuseme kwamba Tanzania kwanza halafu itikadi baadaye au makundi mengine baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, naomba niende kwenye Jimbo langu la Moshi Vijijini na hapa nataka niombe jambo moja tu, Mheshimiwa Waziri nimekuandikia, Kituo cha Polisi Kata ya Okaoni. Wananchi wa Tarafa ya Kibosho kule kwangu Moshi Vijijini waliamua kuchanga fedha wenyewe kwa ajili ya kujenga Kituo cha Polisi ambacho kwa maelezo ambayo nimeyapata kwa *IGP* mwenyewe ni kati ya vituo bora kabisa ambavyo viko vijijini katika nchi yetu ya Tanzania. Wananchi wamechanga karibu shilingi milioni 500, lakini kwa kweli wameshindwa kumalizia kulipa. Hivi sasa Wananchi wale wanadaiwa shilingi milioni 97 kwa sababu mkandarasi aliamua kujenga akamaliza akasema atatudai. Sasa Wananchi wale wamechanga wamefika mahali wamechoka. Mwaka jana nimekuja nikamwomba Waziri wakati ule Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha na *IGP*, wakaniahidi kwamba wangeangalia, baadaye ikaonekana kwamba haikuwezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu nataka niwaombeni sana, Mheshimiwa Nchimbi na Mheshimiwa *IGP*,

kwa sababu kile kituo mwenyewe mlakisimamia ujenzi wake mpaka ukakamilika, hizo shilingi milioni 97 naomba ipatikane tumlipe huyu mkandarasi ili Wananchi wa Moshi Vijijini wakajenge tena vituo vingine vya Polisi ambavyo ni vya mfano kama kilivyo Kituo hiki cha Polisi cha Kata ya Okaoni. Cha pili, ni kwamba, kituo hiki hakina usafiri, kimekaa mlimani na kule mlimani gari liliopo ni bovu, hakuna hata pipipiki. Kuna mfadhibili alitoa pipipiki mbili zimeshaharibika, kwa hiyo, nataka tuangalie namna gani ya kusaidia kituo hiki kwa sababu kinadhibiti eneo lote la Kibosho ambako zamani lilikuwa ndiyo kitovu cha uhalifu katika Jimbo la Moshi Vijijini.

Naomba nimalizie kwa kuzungumzia suala la uhamiaji haramu. Nampongeza Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, kwa kazi kubwa anayofanya kudhibiti wahamiaji haramu ambao wanapitia zile njia za panya ambazo ziko zaidi 300 katika Mkoa wa Kilimanjaro, wengine wanakamatwa lakini wengine hawakamatwi. Kwa hiyo, niseme tu kwamba, kazi kubwa inafanyika lakini nataka niwaombe tujaribu kuangalia sisi kama Watanzania turudishe lile suala la Balozi wa Nyumba Kumi Kumi ambalo liliidharauliwa katika maeneo fulani fulani ya kisiasa. Tujaribu kuona ni namna gani zile Balozi zinafanya kazi bila kujali kama itikadi, kwa sababu zilikuwa zinatambua wahamiaji wanaokuja kwetu. Inabidi ukipata mgeni unakwenda kwa Balozi kuripoti kwamba leo nina mgeni anafahamika. Sasa lile tumeliacha, matokeo yake wameingia watu wengi tu ambao wanakuja kuvuruga na hata tukio la Arusha la jana Mheshimiwa Waziri amesema kwamba, wapo na watu wa nje ambao wameshiriki, ni kwa sababu tumeondoa ule mfumo ambao ulikuwa unasaidia kuwatambua watu wanaokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nataka niiombe Wizara itoe fedha zaidi kwa Polisi Jamii. Nafahamu bajeti ni ndogo, lakini ile Bajeti ya Polisi Jamii lilikuwa inasaidia sana na katika maeneo kama haya, ina mianya watu wanapita kwa wingi kama Kilimanjaro na yale maeneo mengine ya mpakani ambayo wageni wanatumia kupita kuja nchini

mwetu. Naomba nguvu kubwa zaidi ipelekwe kwa maana ya fedha, kuimarisha Polisi Jamii katika maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, kwa mara nyingine naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Dkt. Chami. Mheshimiwa Gosbert Blandes hayupo, nampa nafasi Mheshimiwa Zitto.

MHE. KABWE Z. ZITTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika mjadala huu muhimu sana. Hapa Afrika kulikuwa kuna nchi na bado ipo inaitwa Ivory Coast, ilikuwa inasifika sana kwa amani na utulivu na ilikuwa ni nchi ya kupigwa mfano. Leo hii Ivory Coast imegawanyika vipandevipande. Ukienda leo Ivory Coast unakuta wanaoitwa Ivorite na wanaoitwa wageni ambao wazazi wao walienda Ivory Coast kufanya kazi miaka mingi sana. Pili, katika mgawanyiko huo kuna mgawanyiko mkubwa sana wa kidini kati ya watu wa Ivory Coast wanaotokea Kaskazini na watu wa Ivory Coast wanaotokea Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tuna Sierra Leone, nchi ambayo wageni walikuwa wanakirimiwa katika hali ambayo haijawahi kutokea hapa Duniani. Leo Sierra Leone ina rekodi kubwa sana ya watu wenye ulemavu kwa sababu ya vita ya wenyewe kwa wenyewe. Naomba nichukue nafasi hii, kufuatia matukio ambayo yametokea hivi karibuni na hasa jana na siku zilizopita, ninukuu hotuba ambayo Rais wa Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Benjamin Mkapa, aliitoa katika Bunge hili tarehe 4 Novemba, 1998. Alisema:-

"Mr. Speaker, after three years of my presidency, I can dare to modify the words of a famous Zanzibar Maestro Siti Binti Saad by saying; Tanzania is a good country, let one who wishes to come do so. God has showered blessings on our country. It is a country of unity, peace, love, rejoicing and exceeding generosity. It is a country of people who love equality and justice. Our national unity brings from our frame

believe in equality of human beings before God and before the Law. A unity reinforced by correct policies of nation building. Policies based on the principle of social justice, peace, harmony and development for all. A unity which is extra sensitive to policies, statements, behaviour and actions which may sown seeds of discord hatred and suspicion among Tanzanians."

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitatafsiri, lakini naomba kila Mbunge ajilizile leo iwapo Rais Mkapa tukimpa fursa ya kuja kuhutubia Bunge hili anaweza akayatumia maneno haya tena? Hakuna Mtanzania yEyote anayeweza kuthubutu leo kutumia maneno haya tena, kwa sababu nchi yetu ina nyufa kwa kujua au kwa kutokujua, sisi kama watu ambao tumepewa wajibu na Wananchi wa kuitunza nchi hii na kuipeleka pamoja, tumejikuta tukiingia katika kutoa kauli, maneno na vitendo, ambavyo ni *Irresponsible*, vinavyopelekea kulgawa nchi na yanayotokea sasa ni matumizi ya nyufa hizo. Asubuhi hapa Mheshimiwa Lissu ametoa rekodi ya namna ambavyo wanasiasa wa chama kinachoongoza wamekuwa wakitoa kauli dhidi ya vyama vya upinzani kuhusiana na masuala ya kidini. Wametoa mfano kuhusu Chama cha CUF kilipoitwa Chama cha Waislam, wamekitolea mfano kuhusu CHADEMA kinavyoitwa mpaka sasa Chama cha Wakristo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana ikawa ni rahisi sana tuka-point fingers kwa wenzetu, ni rahisi sana, lakini CUF wakati wanaitwa ni Chama cha Waislam ambao walikuwa hawaitwi ni Chama cha Waislam, hawakunyosha mkono kupinga. Wakati CHADEMA kinaitwa Chama cha Kikristo, ambao hawaitwi hivyo hawakunyosha mkono. Matokeo yake ni nini? Tumejenga hofu kubwa sana katika Taifa na ni lazima wote kama nchi tuseme kwamba hapa tumekosea na tuanze upya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, adui anapokuja kwenye nyumba anaangalia ni wapi ambapo ni rahisi kamba kukatika. Tumeji-expose, tumejiweka wazi, leo mtu anayetaka kuishughulikia Tanzania ata-deal na udini tu, kwa sababu

anajua watanzania hivi sasa wamegawanyika katika misingi hiyo. Jana limetokea tukio Arusha, angalia kwenye mitandao ya kijamii mara moja Watanzania wenyewe kwa wenyewe na ukiangalia majina ya watu wanaojadiliana wanaanza kusemana kwa dini zao; ndio hatari ambayo tumeifikia na anachokitaka adui ni hicho. Atakuja wanaitwa *Agent Provocateur*, watapiga, mtabaki mnagombana ninyi. Tukiruhusu nyufa hizi ziendelee hatutakuwa na Taifa, ni lazima sote kwa pamoja tusimame imara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waislam na Wakristo nchi hii hawana chuki kwa sababu wanaishi pamoja, ni marafiki, ni ndugu na kama ingekuwa kwa mfano Waislam wanawachukia Wakristo, Waislam wangevunja makanisa au wangechoma makanisa au wangewalipua Wakristo. Wakati wa tukio la Mwembechai ndipo ambapo Polisi waliingga msikitini wakaua watu, wanawake wakateswa kwenye Magereza na kadhalika, watu wakakaa miezi mitano gerezani bila kushtakiwa, lakini hapakuwa na matukio yoyote ya namna hii. Waislam na Wakristo wa nchi ni wamoja. Wananchi wetu ni wamoja lakini sisi Viongozi kwa kutoa kauli ambazo ni *very irresponsible* tunawagawa watu wetu na ni lazima tukatae hali hii. Tunafanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima twende mbele. Kwanza, ni lazima sasa Serikali jenge utamaduni wa kufuatilia grievances zote ambazo zinawapata Wananchi bila kujali dini zao. Pili, turuhusu watu kuwa huru kusema. Nimesikia hapa watu wanasema kwamba, maandalmano ni tatizo na kadhalika. Maandalmano siyo tatizo, ukimzuia mtu kuandalama akiweka hasira zake kesho atafanya nini? Atatoka na bomu. Turuhusu *honest discussions* mionganii mwetu kama Wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ni lazima sasa tuseme ya kwamba ni marufuku kuwa na kauli za chuki, *hate speeches*. Kama hatuna vipengele vya kisheria tutunge Sheria, kwa sababu kumekuwa na *hate speeches* nyingi sana katika hii nchi na hakuna hatua ambazo zinachukuliwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dola ihakikishe inajiondoa kabisa kwenye shughuli za uendeshaji wa mambo ya kidini. Kwa mfano, kuna lawama ya muda mrefu sana ya Waislam kuhusu BAKWATA, miaka mingi toka mwaka 1969 wakati Serikali imeunda BAKWATA wanalamika. Leo hii Serikali ikitaka kuzungumza na Waislam inaenda kuwaita BAKWATA. Hawana *legitimacy* ya Waislam, hamtaweza ku-address masuala ya Waislam lakini ni rahisi sana kuweza kuongea na CCT, kwa sababu CCTni chombo ambacho kina uhuru wake. Kwa hiyo, Serikali ijiondoe kwenye uendeshaji wa shughuli za kidini. Hapa ndipo tutakapoweza kuhakikisha kwamba, tunakuwa na nchi moja ambayo ina amani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kusema nchi hii si ya Waislam peke yake, nchi hii si ya Wakristo peke yake, nchi hii si ya CCM au ya CHADEMA, CUF au ya NSSR-Mageuzi au TLP na kadhalika. Nchi hii ni moja, nchi hii ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lazima wote tusimame kuhakikisha tunailinda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nawashukuru wachangiaji wote. Nataka kuweka jambo moja usahihi tu. Moja kazi ya Meza ni kutazama mazungumzo yanayozungumzwa ndani, usahihi wake na ukweli wake. Kuna mmoja wa wachangiaji amediriki kusema kwamba, Serikali hii inafanya maamuzi kwa *ku-balance*, imefungia redio moja ya Waislam na imefungia redio moja ya Wakristo *ku-balance*. Serikali hii haifanyi maamuzi kwa *ku-balance*. Serikali hii inafanya maamuzi kwa usahihi, kwa haki na misingi ya kisheria. (*Makofi*)

Kwa kuwa wachangiaji wote wamekwisha, Meza ndiyo inasema; naliahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(*Saa 1.25 jioni Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Jumanne, Tarehe 7 Mei, 2013 Saa Tatu Asubuhi*)